

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU
UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA
MWAKA WA FEDHA 2007/2008**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Simu ya Upepo: "Ukaguzi" D'Salaam
simu: 255(022)2115157/8
Tanakishi: 255(022)2117527
Tovuti: ocag@nao.go.tz
Tovuti: www.nao.go.tz
Unapojibu tafadhali taja
Kumb.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu
wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Barabara ya Samora /Ohio,
S.L.P. 9080,
DAR ES SALAAM.
26 Machi 2009

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Sanduku la Posta 9120,
IKULU,
Dar es Salaam.

**Yah: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA
MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA
WA FEDHA 2007/2008**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebisha 2005), ninawasilisha kwako ripoti iliyotajwa hapo juu.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za ukaguzi wa mashirika ya umma kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2007, 31 Disemba, 2007 na tarehe 30 Juni 2008.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'L. Utouh'.

Ludovick S.L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

*Imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara namba 143 ya Katiba ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Kazi na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainishwa katika Sheria ya fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (ilivyorekebishwa 2004) iliyobadilishwa na Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008.

Dira ya Ofisi

Kuwa kituo bora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma.

Lengo la Ofisi

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.
Matumizi bora ya rasilimali za umma	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

© Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Serikali. Hata hivyo, baada ya taarifa kuwalishwa Bungeni, taarifa hii inakuwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hautakuwa na kikomo.

DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu kuhusu ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2008. Ripoti hii ni mkusanyiko wa ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika ya Umma zilizofanyika kwa vipindi husika.

Ripoti hii imechambua mambo mbalimbali ambayo yameonekana kwa njia moja au nyingine kuathiri ufanisi na uwajibikaji wa Mashirika hayo katika kufikia malengo yake.

Ripoti hii pia, imelenga kuwapa wadau wetu kama vile Bunge, Serikali Kuu, Wahisani, Asasi za Kijamii, na Umma wa Watanzania kwa ujumla muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2008, pamoja na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa Mashirika na Taasisi hizo.


Kwa kipindi hiki ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la uwajibikaji kwa umma, limekuwa ni jambo muhimu kwa watendaji kutoa taarifa zao za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha na usimamiaji wa mali za umma ndani ya Mashirika na Taasisi za Umma.

Napenda kueleza kuwa ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ili kuhakikisha kuwa kazi yangu inachangia katika maendeleo ya taifa, Ofisi yangu imekuwa ikiboresha mbinu za ukaguzi mara kwa mara ili kuona kuwa matokeo ya kaguzi yanakidhi haja za wadau wetu. Pia, kujenga uwezo wa wakaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni jambo linalopewa kipaumbele ili kuhakikisha wanapata uelewa wa sheria, miongozo, kanuni na matoleo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayofanywa na Taasisi za taaluma ya uhasibu na ukaguzi za kimataifa kama vile "IFAC", "INTOSAI" na nyiginezo ambazo ofisi yangu ni mwanachama.

Ni vyema ikafahamika kwamba, wakati vyombo vyenye dhamana ya usimamizi (Oversight Organs) vina jukumu la kuhakikisha kuwa sheria na taratibu zinafuatwa ndani ya Taasisi za umma, watendaji wakuu wa Taasisi hizo kwa upande wao wana jukumu la kuweka miundo imara ya udhibiti wa ndani na miongozo ili kuhakikisha kwamba sheria na taratibu hizo zinafuatwa.

Juu ya yote, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati za Bunge za usimamizi wa utendaji, Bunge kwa ujumla, wahisani mbalimbali wa shughuli za maendeleo na Benki ya Dunia kwa michango yao katika kufanikisha uwajibikaji katika nchi yetu.



Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
Dar es Salaam,

26 Machi 2009

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za mara kwa mara za kutilia msisitizo kwenye ripoti zangu na hasa ripoti za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2006.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti na waheshimiwa wajumbe wa Kamati za kudumu za Bunge, Wenyeviti na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati za sekta mbalimbali za Bunge kwa kujitolea kwao kujadili mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu za jumla na ripoti mbalimbali zilizotolewa kwenye Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioniwezesha kutimiza wajibu wangu wa kikatiba na kuweza kutoa ripoti yangu kwa wakati. Ni matumaini yangu kwamba kwa vile ripoti hii ya jumla ya Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma inatolewa kwa mara ya pili na kwa wakati unaotakiwa kisheria, itawezesha kujadiliwa na kamati husika kwa wakati ili kutimiza majukumu yao ya usimamizi wa rasilimali za Taifa kwa muda uliopangwa.

Pia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Watendaji Wakuu na wasimamizi wakuu wa rasilimali za Taifa kwa msaada wao mkubwa uliofanikisha kutoa taarifa hii kwa wakati. Vilevile ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Mpigwa Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuharakisha uchapaji wa ripoti hii na hivyo kuifanya itoke na kuweza kusambazwa kwa wadau kwa wakati.

Zaidi ya hayo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani ambao wamekuwa wakitoa msaada kwa Ofisi yangu na hasa zaidi Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden(SNAO), Serikali ya Sweden na wote wanaoitakia

mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa.

Vilevile napenda kuyashukuru Makampuni binafsi 44 ya ukaguzi kwa kufanya kazi ya ukaguzi pamoja na Ofisi yangu. Makampuni hayo yamefanya kazi nzuri na inayofaa kupongezwa na kudumishwa katika kaguzi za baadae za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo.

Ninapenda pia kuwashukuru sana wafanyakazi wa ofisi yangu ambao wamefanya kazi bila kuchoka na kufanikisha utoaji wa ripoti hii. Kujitolea kwao na uvumilivu waliouonyesha umekuwa wa manufaa sana na nawasihi wote waendeleo kuwa na moyo huu wa kujituma kwa siku zijazo.

YALIYOMO

Ukurasa

DIBAJI	vii
SHUKRANI	ix
MUHTASARI	xiii
SURA YA KWANZA	1
Utangulizi na Taarifa za Jumla.....	1
SURA YA PILI.....	7
Misingi na Mwenendo wa Hati za Ukaguzi	7
SURA YA TATU	53
Muhtasari wa Mapendekezo ya Matokeo ya Ukaguzi wa mwaka uliopita ambayo hayajatekelezwa.....	53
SURA YA NNE	77
Usimamizi wa Mapato na Matumizi.....	77
SURA YA TANO	93
MIFUMO Ya Udhhibiti wa Ndani	93
SURA YA SITA.....	99
Tathmini ya Utendaji	99
SURA YA SABA.....	119
Utekelezaji wa Sheria za Kanuni ya Manunuzi.....	119
SURA YA NANE	135
Usimamizi wa Mikataba	135
SURA YA TISA.....	159
Usimamizi wa Rasilimali.....	159
SURA YA KUMI	183
Usimamizi wa Rasilimali Watu	183

SURA YA KUMI NA MOJA.....	189
Utawala Bora.....	189
SURA YA KUMI NA MBILI	201
Matokeo ya Ubinafsishaji.....	201
SURA YA KUMI NA TATU	211
Matokeo ya Kaguzi Maalumu.....	211
SURA YA KUMI NA NNE.....	219
Hitimisho na Mapendekezo	219
VIAMBATANISHO	237

MUHTASARI

Sehemu hii ya ripoti inatoa muhtasari wa matokeo ya mwisho ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba 2007, 31 Disemba 2007 na 30 Juni 2008.

1.0 Kazi Zilizofanyika

Katika kufanya ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma tulizingatia taratibu zifuatazo za kikaguzi:

- Kujadiliana na menejimenti za Mashirika na Taasisi za Umma kuhusu utekelezaji wa utendaji wa shirika kwa kipindi cha mwaka husika;
- Kuitisha na kuhakiki nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kupata uelewa wa shughuli za Taasisi hizo na namna zinavyojiendesha;
- Kuitisha na kukagua taarifa za fedha za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma na nyaraka muhimu zilizotumika kuandaa taarifa hizo kwa kila Taasisi husika;
- Kutumia njia na mbinu nyingine za ukaguzi kama ilivyoidhinishwa kwenye mpango wa ukaguzi;
- Kujadili matokeo ya ukaguzi na kupata majibu ya menejimenti;
- Kujumuisha matokeo ya taarifa mbalimbali za mashirika ya Umma;
- Kupitia majibu ya Serikali juu ya ripoti yangu ya jumla kama yalivyowasilishwa na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa barua yenye kumbukumbu Na.ED/AG/AUDIT GEN/08/VOL./150 ya tarehe 4 Octoba, 2008.

1.1 Hesabu za Mashirika na Taasisi za Umma

Utangulizi

Hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zilikuwa 145, kati ya hizo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliweza kukagua na kutoa ripoti kwa hesabu 101 mpaka

xiii

ripoti hii inapotolewa (Machi, 2009). Hesabu za Mashirika na Taasisi za Umma 44 ziko kwenye hatua mbalimbali za ukaguzi, wakati Taasisi za Umma 19 bado hazijakamilisha utayarishaji wa hesabu na kuzitoa kwa ajili ya ukaguzi.

Hati za Ukaguzi

Hati za ukaguzi zimeonyeshwa kwenye ripoti za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma husika. Katika kipindi cha mwaka husika, hakuna Shirika wala Taasisi ya Umma iliyopata hati chafu.

Aina ya Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi kilichokaguliwa ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo:

Idadi ya Mashirika	Hati zinazoridhisha	Hati zinazoridhisha na zenye masuala ya msisitizo	Hati zenye kasoro
101	80	6	15
100%	79%	6%	15%

1.2 Muhtasari wa Yaliyojitokeza

Naambatanisha muhtasari wa mambo muhimu yaliyojitokeza kama yalivyoonyeshwa kwenye Sura za ripoti hii kama ifuatavyo:

i. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Mwaka Uliopita

Sura hii inatoa muhtasari wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti yangu ya mwaka jana ambayo aidha, utekelezaji wake ulikuwa haujakamilika au haujaanza kabisa wakati tunamalizia kaguzi za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa kipindi hiki.

Nimepokea majibu ya Serikali kupitia kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa barua yenye kumbukumu Na. ED/AG/AUDIT GEN/08/VOL./150 ya tarehe 4/10/2008.

- (ii) **Usimamizi wa Mapato na Matumizi**
Sura hii inalenga kuzungumzia mambo yanayohusu usimamiaji wa mapato na matumizi ya fedha katika Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma ambazo zimeelezwa kwenye taarifa za kaguzi zilizotumwa kwa viongozi wa Taasisi husika (Management letters) kwa vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba, 2007, 31 Disemba, 2007 na 30 Juni, 2008. Mambo yanayolingana au kufanana kwa Taasisi zote yameelezwa kwa pamoja chini ya vichwa vya habari husika.
- (iii) **Mapitio ya Mfumo wa Udhhibiti wa Ndani**
Sura hii inahusu masuala ya udhibiti wa ndani ambayo yalionekana yana umuhimu wa kujumuishwa kwenye ripoti yangu ya mwaka. Udhhibiti wa ndani ni muhimu sana kwa Mashirika na Taasisi za Umma ili kuboresha utendaji wa Mashirika hayo.
- (iv) **Mapitio ya Utendaji**
Sura hii inahusu utendaji wa Mashirika ya Umma kifedha na kiuendeshaji. Utendaji wa kifedha umepimwa kwa kuangalia faida au hasara iliyopatikana kwa kipindi cha mwaka husika. Utendaji wa kiuendeshaji umepimwa kwa kuangalia ni kwa kiasi gani Taasisi imeweza kufikia malengo yake ya msingi.
- (v) **Ufuataji wa Sheria na Kanuni za Manunuzi**
Tanzania imeingia katika mchakato mkubwa wa kurekebisha mfumo wa manunuzi ya umma ambao umepelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2001 na baadae kufutwa na Sheria Na. 21 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na Mamlaka ya Rufaa za Manunuzi ya Umma (PPAA).

Ili kuhakikisha kuwepo kwa uzingatiaji wa kanuni za manunuzi ya Umma, kifungu cha 44 (2) cha Sheria ya Manunuzi kinamtaka kila mkaguzi wa Taasisi ya Umma

aeleze kwenye ripoti yake kama Taasisi husika imezingatia sheria ya manunuzi.

(vi) Usimamizi wa Mikataba

Sura hii inaelezea mapungufu yaliyojitokeza kwenye usimamizi wa sheria za mikataba ambayo yamejitokeza kwenye ripoti za ukaguzi kwa vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba, 2007, 31 Disemba 2007 na 30 Juni 2008. Umuhimu wa ukaguzi wa mikataba umeongezeka zaidi kufuatia kuanzishwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008. Kifungu cha 26 (i) cha sheria hiyo kinampa uwezo Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wowote itakapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

(vii) Usimamizi wa Rasilimali

Sura hii inaangalia usimamizi wa mali za umma unaolenga zaidi kujenga mikakati ya muda mrefu ya usimamizi wa mali ambazo ni muhimu katika kuleta ufanisi wa Mashirika na Taasisi za Umma ili kunufaisha jamii iliyokusudiwa. Msisitizo katika udhibiti wa mali umelenga kudumisha mali hizo kwani ndizo zinazothaminisha Taasisi.

Kinyume na matarajio ya wakaguzi, na kulingana na umuhimu wa utunzaji wa mali, ukaguzi wa mwaka wa fedha 2007/2008 ulibaini baadhi ya mapungufu kwenye udhibiti wa mali za kudumu licha ya ukweli kuwa mapungufu kama hayo yamekuwa yakiripotiwa na Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ripoti zake kwa Taasisi husika.

(viii) Usimamizi wa Rasilimali Watu

Sura hii inaelezea kwa kifupi matokeo ya kaguzi za Mashirika na Taasisi mbalimbali ambazo zimeonyesha mapungufu mkubwa katika kusimamia rasilimali watu.

Upembuzi umebaini kuwa baadhi ya mashirika huajiri watumishi bila kufuata taratibu za ushindani na uwazi kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za ajira. Pia, imebainika

kuwa mashirika mengine hayatunzi taarifa muhimu za watumishi wao.

Maafisa Waajiri wameonekana kutozipa kipao mbele kasoro zilizojitokeza kwenye mfumo wa ajira ambazo zinaweza kusababisha usumbufu kwa wafanyakazi wakati wanapostaafu au kuacha kazi.

Idadi kubwa ya mashirika yameonyesha udhaifu mkubwa katika kupima ufanisi wa watumishi wao.

(ix) Utawala Bora

Sura hii inahusu masuala ya utawala bora ambao unahamasisha Mashirika ya Umma kuwa na ulazima wa kuwa na sera bora za kusimamia rasilimali. Katika kufikia malengo hayo, mashirika yanahitaji kuwa na mifumo ya uendeshaji ambayo itawawezesha kuwepo na udhibiti wa ndani imara unaolenga kuimarisha uwajibikaji, kufuata sheria, kuondoa upotevu unaosababishwa na udanganyifu, wizi, uzembe na utendaji wa kazi usiokuwa makini.

(x) Matokeo ya Ubinafishaji

Sura hii inatoa matokeo ya ubinafsishaji ikiwa ni pamoja na matatizo na mafanikio yaliyojitokeza tangu kuanzishwa kwa zoezi hilo.

Mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990s) Serikali iliamua kubinafsisha baadhi ya Mashirika na kuacha shughuli za kibiashara mikononi mwa Sekta Binafsi. Uamuzi huu ulisababishwa na usimamizi na utendaji mbovu uliopo MASHIRIKA hayo kujiendesha kwa hasara.

Serikali iliamua kujihusisha zaidi na jukumu la kutunga sera na kusimamia utawala unaozingatia sheria, ulinzi na usalama wa raia.

Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilipewa jukumu la kusimamia shughuli nzima ya ubinafsishaji. Hata hivyo Tume ilivunjwa rasmi tarehe 31 Disemba 2007 baada

ya kubinafsisha sehemu kubwa ya Mashirika ya Umma. Tarehe 1 Januari 2008 idadi ya bidhaa/vifaa/rasilimali iliyokuwa imesalia ya Mashirika ya Umma 34 zikiwa katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji zilihamishiwa kwa Shirika Hodhi la Rasilimali za Mashirika ya Umma (CHC).

(xi) Matokeo ya Kaguzi Maalumu

Sheria ya Fedha Na. 6. ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) na iliyobadilishwa na Sehemu ya 36 (1) ya Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 inampa nguvu za kisheria Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi Maalumu.

Kutokana na Jukumu hilo alilopewa kisheria, kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2008, Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi maalumu katika mashirika ya umma matatu; ambayo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Moshi (MUWSA). Hata hivyo, ukaguzi maalumu wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu hautaelezewa kwenye sura hii kutokana na kuchelewa kukamilika kwa ukaguzi huo.

(xii) Hitimisho na Mapendekezo

Kutokana na udhaifu uliogundulika katika kaguzi za Mashirika ya Umma pamoja na hoja za ukaguzi zilizoandikwa katika sura za awali za ripoti hii ninazo sababu za kutosha za kuhitimisha na kutoa mapendekezo kwa Serikali, Bodi za Wakurugenzi na menejimenti za mashirika husika kama ifuatavyo:-

- Serikali, Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuongeza juhudi zaidi katika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya wakaguzi kwa mwaka uliopita ambayo hayakutekelezwa yanatekelezwa.
- Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa ankara za

madai zinaandaliwa na kupelekwa kwa wateja kwa wakati na kuwa mapato sahihi yanakusanywa na kuandikwa kwa usahihi kwenye vitabu vya hesabu na kuimarisha udhibiti wa maduhuli katika kuondoa mianya yote ya ubadhirifu wa fedha za Umma.

- Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa malipo yanaidhinishwa na maafisa wenye dhamana na nyaraka husika zinaambatanishwa pamoja na hati za malipo.
- Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania inapaswa kutoa maelezo ya uhalali wa malipo ya Dola za Kimarekani 4,865,000 zilizolipwa kwa M/s Dowans kwa ajili ya kukodisha ndege maalumu kusafirishia mashine za kuzalishia umeme kuja Dar es Salaam bila ya kuwa na kifungu kwenye mkataba kilichoruhusu malipo hayo.
- Menejimenti ya Benki Kuu Tanzania inapaswa kufanya uchunguzi wa mazingira iliyopelekea jumla ya Shilingi bilioni 7.3 kulipwa kwa wakala wa bima ikiwa ni “Insurance Premiums” kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya makao makuu ya benki hiyo bila ya kuwepo kwa nyaraka sahihi zinazojitosheleza.
- Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari za Mwanza na Nansio zinapaswa kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na Gati binafsi yanakusanywa kikamilifu kusini na kaskazini mwa bandari ya Mwanza na Nansio.
- Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari Makao Makuu Dar es Salaam inapaswa kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya mapato vinatambulika na mapato yote yanakusanywa.
- Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuwa na mifumo ya ndani thabiti na kuhakikisha kuwa inatumika ipasavyo.
- Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa hundi zilizoandikwa kimakosa (Cancelled Cheques) zinatunzwa mahali salama kuepuka kutumiwa vibaya na watumishi wasio waaminifu.
- Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kujenga “entrepreneurial

culture”, kuajiri menejimenti bora na zenye utaalamu unaotakiwa kwenye shirika husika.

- Pia, wizara mama zinapaswa kujenga uwezo wa ndani ili kuweza kusimamia na kufanya tathmini ya utendaji wa mashirika ya umma yaliyoko chini ya Wizara hizo.
- Msajili wa Hazina anapaswa kuimarisha ofisi yake katika suala zima la usimamizi wa Mashirika ya Umma.
- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inapaswa kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi wake katika suala zima la kuingia katika mikataba ya kisheria na suala zima la usimamizi wa mikataba.
- Mawaziri wenye dhamana wanapaswa kuhakikisha Mashirika ya Umma yaliyoko chini yao yanaendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.
- Msajili wa Hazina anapaswa kuhakikisha kuwa mashirika ambayo hayana mtaji wa kutosha yanapatiwa fedha kwa ajili ya kujiendesha na kuajiri watumishi wenye sifa zinazotakiwa.
- Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka zinapaswa kuhakikisha kuwa zinawatambua wateja wake na kuharakisha kazi ya kuwafungia mita kwa lengo la kudhibiti mapato yatokanayo na mauzo ya maji.
- Menejimenti ya Benki Kuu ya Tanzania inapaswa kuandaa sera na miongozo ya kushughulikia na kudhibiti fedha ambazo hazikupatikana kwa njia halali “Money Laundering”
- Menejimenti ya Shirika la Utangazaji inapaswa kuhakikisha kuwa hati za maombi ya matangazo ya kibiashara zinaandaliwa na hakuna tangazo litakalorushwa hewani bila ya nyaraka za awali za kuomba kurushiwa tangazo la biashara.
- Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari inapaswa kuzingatia kifungu 7.4.2 (2) cha mkataba wa ukodishaji na kuendelea kuishauri Serikali kupitia upya mkataba wa TICTS kwa ukodishaji kwa misingi ya utaratibu usiohalili wa mkataba na utendaji kazi mbovu.
- Mashirika ya Umma yanapaswa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na kuonyesha utendaji bora katika

XX

manunuzi ya vifaa, huduma na kazi. Pia, Watendaji Wakuu wanapaswa kuendelea kuboresha na kuweka mifumo thabiti ya ununuzi ili kuhakikisha kuwa suala zima la thamani ya fedha linazingatiwa.

- Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inapaswa kufanya uchunguzi maalumu katika mamlaka ya kudhibiti Mawasiliano (TCRA) kuhusu zabuni ya kupitia muundo wa ofisi, tathmini ya utendaji kazi na kupitia ngazi za mishahara “organisation review, job evaluation, na job grading” ambayo awali ilitangazwa tarehe 16, 17 na 20 Agosti 2007 na kuingia mkataba tarehe 28 Januari 2008 kinyume na mapendekezo ya Kamati ya Tathmini (Evaluation Committee).
- Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inapaswa kufanya uchunguzi na kujiridhisha kuwa uwazi na taratibu za manunuzi zilifuatwa na Menejimenti ya Mfuko wa Huduma za Jamii (NSSF) katika mchakato mzima wa kutathmini na kuingia mkataba wa huduma za ulinzi. Menejimenti ilimuagiza Meneja Mkuu wa Ulinzi kufanya “vetting” ya wazabuni baada ya mapendekezo ya kamati ya kutathmini ambayo bodi ya manunuzi ya Mfuko ilifuata katika kuingia mkataba na Mzabuni M/s Alliance Day and Night.
- Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inapaswa kufanya uchunguzi maalumu katika Shirika la Utangazaji Tanzania kuhusu zabuni mbili za kuongeza ubora wa Studio ya Redio katika jengo jipya la BH, PRT na “Scoop News Studio” liliko TVT Mikocheni kwa gharama ya GBP 53,212 na kutoa huduma ya mtandao kwa gharama ya Sh.172,000,000 aliyopewa Mzabuni M/s P Square Ltd wa Uingereza na M/s WiA Company Ltd”.
- Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania inapaswa kufanya uchunguzi maalumu kuhusu mkataba wa pamoja “joint venture” kati ya M/s Tangerm Ltd ya Dar es Salaam na M/s Techno Combine Construction Ltd kwa ajili ya ujenzi wa “container staking yard katika sehemu lilokuwa jengo la TANESCO kwa gharama ya Sh.4,165,666,875.

- Menejimenti ya Benki Kuu inapaswa kupitia Mkataba uliopo wa kuendeleza ujenzi wa majengo ya makao makuu ya benki hiyo ili kubaini kama bado makubaliano hayo ni halali na benki ijilinde na vihatarishi vya mkataba.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kuthibitisha endapo thamani ya fedha ilipatikana wakati wa utekelezaji wa mkataba wa “Oracle e-business Suite Application and Core Fund Management System Project” kwa kuunda tume ya kufanya uchunguzi.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kuunda tume huru kufanya uchunguzi wa mapungufu yote yaliyojitokeza wakati wa kuuza nyumba za shirika zilizoko eneo la “ADA Estate Kinondoni” kwa lengo la kubaini uhalali wa zoezi zima la kuuza nyumba hizo.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kuthibitisha kuwa thamani ya fedha ilipatikana katika kuuza majengo ya Club Oasis au vinginevyo kuunda tume huru ya kuchunguza uhalali wa mauzo ya majengo hayo.
- Serikali inapaswa kuiwezesha Wizara ya Fedha na Uchumi kuanzisha kitengo maalumu ambacho kitashughulikia na kutathmini uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika ya Umma. Kitengo hicho kitaisaidia Serikali kufanya maamuzi mazuri ya uwekezaji ili kuepuka hasara ambayo inapatikana katika uwekezaji uliokwishaifanyika katika mashirika mbalimbali.
- Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania anapaswa kufikiria kupanua majukumu ya kamati ya bunge ya Mashirika ya Umma (POAC) katika kuhakikisha kuwa inasimamia hesabu za Mashirika na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa.
- Serikali inapaswa kuingia mikataba ya kiutendaji na bodi za wakurugenzi wa Mashirika ya Umma na kuandaa malengo ambayo yatatakiwa kutekelezwa katika kipindi husika ambacho bodi itakuwa madarakani. Kwa hali hiyo bodi za wakurugenzi nazo zitapaswa kuingia mikataba ya kiutendaji na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma ambao pia watatakiwa kuingia mikataba ya kiutendaji na wasaidizi wao.

- Bodi za Wakurugenzi wa mashirika ya umma zinapaswa kuhakikisha watendaji wakuu wa mashirika ya umma wanawajibika zaidi kwa matokeo ya utendaji kazi zao. Bodi za wakurugenzi zipewe mamlaka zaidi ya kuingia mikataba ya kiutendaji (performance contract) na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma baada ya kuainisha malengo ya mwaka ambayo watatakiwa kuyatekeleza. Kwa hali hiyo, kuna haja kuangalia uwezekano wa watendaji wakuu wa mashirika ya Umma kuteuliwa na Bodi za wakurugenzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na wajibu wa kuteua wenye viti wa Bodi za Wakurugenzi.
- Kwa vile Bunge ni chombo cha juu kinachowawakilisha wananchi na kinachosimamia utendaji wa kazi za mashirika ya umma kupitia Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC), na ili kuepuka mgongano wa kimaslahi, napendekeza kuwa wabunge wasiwe wajumbe wa bodi za wakurugenzi za mashirika ya umma kama ilivyoazimiwa kwenye mkutano wa uwajibikaji wa mashirika ya umma “Parastatals Accountability Conference” uliofanyika tarehe 23-24 Januari, 2009.
- Kwa kuzingatia mapendekezo niliyoyatoa kwenye taarifa yangu ya mwaka 2007 kwamba kuongezwa muda wa miaka kumi na tano (15) kwa kampuni ya kushughulikia makontena bandarini (TICTS) kutoka 2010 hadi 2025 haukuwa sahihi na hivyo mkataba unapaswa umalizike kama ulivyokuwa kwenye mkataba wa awali. Mkutano wa uwajibikaji “Parastatals Accountability Conference” uliazimia kuwa mkataba wa TICTS na Mamlaka ya Bandari Tanzania usitishwe rasmi ili aweze kupatikana mwendeshaji mwingine ambaye ana uwezo wa kuendesha shughuli za konteina kwa ufanisi zaidi.
- Menejimenti ya Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO) inapaswa kuhakikisha kuwa linafua umeme kulingana na mpango nyongeza katika muda uliopangwa na pia kutengeneza mtandao wa kusambaza umeme kupeleka katika vituo vilivyokusudiwa.
- Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuligawa mara mbili Shirika la Maendeleo ya Petroli la Tanzania

(TPDC); ambapo shirika moja litashughulika na shughuli za kibiashara na la pili lishughulike na utoaji wa leseni, kufanya ukaguzi na kufanya kazi zaidi za udhibiti. Kwa kipindi cha muda mfupi shirika la TPDC litahitaji kuwezesha kimtaji ili kuliwezesha kutimiza majukumu yake.


- Menejimenti ya Shirika la Maji Dar es Salaam (DAWASCO) inapaswa kuwekeza kwenye uchimbaji wa maji ardhini ili yatumike kwa eneo kubwa la Jiji la Dar es Salaam ambalo halina maji. Pia, Shirika liangalie kupitia upya ankara za maji ili kuiwezesha DAWASCO kulipa gharama zake za uendeshaji. Ankara za maji zirekebishwe kulingana na mfumuko wa bei.
- Wakala wa barabara Tanzania (TANROADs) inapaswa kuhakikisha kuwa inachukua hatua madhubuti kujua kwa nini gharama za utengenezaji wa barabara hapa Tanzania ni kubwa sana ikilinganishwa na sehemu nyingine za bara letu la Afrika. Hii ni pamoja na kubaini kifanyike kitu gani ili kuweza kupunguza gharama hizo na kuangalia faida isiyo ya kawaida ambayo wanapata makandarasi wa ujenzi wa barabara.
- Shirika la ndege la Tanzania (ATCL) linapaswa kuhakikisha kuwa uamuzi wowote utakaofanywa kutokana na mazungumzo yanayoendelea kuhusu ushirikiano wa pamoja (joint venture) uzingatie matakwa ya watumiaji wa ndege. Kama watumiaji wa ndege watapata huduma bora, nafuu na za kuaminika, basi soko la usafiri wa anga halina budi kuwa huria. Pia, Tanzania, bila kuchelewa inapaswa kuthibitisha kuridhia maamuzi ya YAMAUSSOUKRO.
- Bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA) inapaswa kujikita katika kuendeleza uwezo wa mamlaka ili kuweza kutoa huduma bora. Pia, mshikamano na upendo baina ya wafanyakazi, uongozi wa EWURA na Bodi ya Wakurugenzi ni muhimu sana kwa kila mmoja kutimiza majukumu yake yatakayopelekea kuboresha utendaji kazi wa EWURA. Kuboresha utendaji kazi wa EWURA utategemea dira mudhubuti ya Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi na wafanyakazi walio makini.

- Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa fedha zilizolipwa zaidi kwa Wakurugenzi wa Bodi na watumishi wa EWURA zinarejeshwa kwenye akaunti husika.
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapaswa kuhakikisha kuwa safari za mafunzo nje ya nchi kwa wajumbe wa bodi na watumishi wa EWURA zinapangwa kikamilifu na fedha za kugharamia mafunzo hayo zitolewe kulingana na gharama halisi ya mafunzo.
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapaswa kuhakikisha kuwa safari za mafunzo nje ya nchi kwa wajumbe wa bodi na watumishi wa EWURA zinafanywa wakati kuna haja ya mafunzo hayo.
- Orodha ya wafanyabiasha wasio waaminifu ambao wanachanganya petroli/dizeli na mafuta ya taa/maji inapelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kurejesha mapato yaliyopotea kwa njia ya kusamehewa kodi ya mafuta ya taa ambayo baadaye yalitumika kuchanganywa na petroli/dizeli.
- Serikali inapaswa kuanzisha mamlaka madhubuti ambayo itakuwa na majukumu ya kudhibiti utendaji na uendeshaji wa mashirika ya umma katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika kutoa huduma bora kwa jamii.
- Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma zinapaswa kuimarisha Idara za Utumishi na kuhakikisha kwamba taarifa za watumishi zinatunzwa vizuri, ajira za wafanyakazi zinapaswa kuwa za uwazi na za ushindani ili shirika husika liweze kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa.
- Watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma wanapaswa kuboresha mfumo wa kutathmini utendaji wa watumishi katika kufikia malengo ya shirika husika.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kurejea maamuzi yake ya awali ya kumuhamisha aliyekuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa zamani na taratibu zilizotumika kumpata na kumuajiri Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa sasa. Kwa maoni yangu taratibu zilizotumika katika kumuhamisha Mkurugenzi wa zamani na kumuajiri Mkurugenzi wa sasa zilikuwa na

mapungufu makubwa na hakukuwa na uwazi wa zoezi zima.

- Watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma wanapaswa kuwasilisha kwenye mamlaka husika makato yote ya kisheria kama ilivyoelezwa katika sheria husika.
- Raslimali watu ni muhimu sana kwa maendeleo ya shirika, hivyo watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma wanapaswa kuhakikisha kwamba usimamizi wa raslimali watu unapewa kipau mbele ili kusaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa.
- Serikali inatakiwa kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali, kuziba mianya ya ukwepaji kulipa kodi hususani kwenye mafuta ya magari na mitambo, kupunguza misamaha ya kodi na kupanua wigo wa kodi.
- Serikali inapaswa kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima kama vile ilivyoamua kupunguza manunuzi ya magari ya kifahari na kupunguza gharama za semina. Pia, matumizi ya kawaida yanaweza kusimamiwa vizuri zaidi ili mapato yanayokusanywa yatumike kwenye shughuli za maendeleo.
- Maliasili zetu zinatakiwa zisimamiwe vizuri ili kuhakikisha watanzania wananufaika na maliasili zao.
- Serikali inatakiwa kuangalia fursa ambazo hazijatumika vizuri ili kuzitumia katika kuimarisha na kukuza uchumi kwa manufaa ya Watanzania wote. Maeneo hayo ni kama vile:- kuimarisha huduma za bandari ili majirani zetu waweze kuvutiwa na huduma hizo, kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuboresha sekta ya uvuvi.
- Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa sera za kukabiliana na athari zinafahamika kwa watumishi wote.
- Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanapaswa kumiliki, kuwezesha na kueneza ufahamu kwa watumishi katika dhana nzima ya kukabiliana na athari.
- Dhana ya kukabiliana na athari yapaswa kueleweka katika utawala mzima wa Serikali na mashirika yake.

- Kukabiliana na athari kunapaswa kwenda sambamba na matarajio na malengo ya Taasisi husika.
- Athari zinazotokana na uendeshaji wa mashirika zinapaswa kufanyiwa tathmini na kukabiliana nazo; na inajumuisha usimamizi, upembuzi na inaweza kuhusisha majadiliano muhimu na wadau wengine katika kubuni mbinu za kukabiliana na athari.



Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Dar es Salaam,
26 Machi, 2009

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishwaji wa Kazi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Ofisi ya Kikatiba iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005). Katika kifungu kidogo (5) cha ibara hiyo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kufafanuliwa zaidi katika vifungu 30(1) (c) na 37 vya Sheria ya Fedha ya Umma Na.6 ya mwaka 2001 iliyorekebishwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008, inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo, angalau mara moja kwa kila mwaka wa fedha.

Vilevile, kifungu 33 kifungu kidogo (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kuruhusu Kampuni au mtu yeyote mwenye sifa za kuteuliwa kufanya kazi ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hivyo, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inafanya bidii ya kutekeleza jukumu hili la kisheria kwa kuhakikisha kwamba wadau wake wote, na Umma kwa ujumla wanafaidika na huduma za ukaguzi na ripoti za ukaguzi zilizo bora na zinazotolewa kwa wakati.

Kaguzi za hesabu za awali na zile za mwaka hufanywa kulingana na masharti ya viwango vya kimataifa vya ukaguzi (ISA) na viwango vya Asasi kuu za ukaguzi Duniani (INTOSAI), na taratibu na miongozo mbalimbali ambayo

Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali anaona inafaa kulingana na ukaguzi husika.

1.1 Wajibu wa Kisheria wa Kuwasilisha Ripoti

Ibara 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali awe ameshawasilisha ripoti ya mwaka ya ukaguzi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Akishazipokea ripoti hizi, Rais ndiye atakayesababisha na atakayewaamuru wahusika kuziwasilisha Bungeni ripoti hizo katika Kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea ripoti hizo na ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa Bungeni sio zaidi ya siku saba baada ya Kikao cha Bunge kuanza.

1.1.1 Kuwasilisha Taarifa

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya Ibara 143, Ibara ndogo ya (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge (au Naibu wa Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yoyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge.

1.1.2 Mamlaka ya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi ya juu ya ukaguzi wa Hesabu ambayo ina jukumu la kuhakikisha kwamba kuna uwajibikaji unaofaa, matumizi mazuri ya fedha/nidhamu katika matumizi ya fedha na uwazi ndani ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Zaidi ya hayo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina jukumu la kipekee la kutoa ripoti bora katika tarehe inayokubalika kisheria.

Ripoti hizo zinatoa matokeo ya makusanyo ya maduhuli na mchanganuo wa matumizi na masuala ya utawala bora wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo.

Matokeo ya ukaguzi wa hesabu katika ripoti hii yamepelekwa kwa wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo pamoja na Wizara mama zinazohusika

1.2 Wigo na Matumizi ya Viwango katika Kuandaa Hesabu.

1.2.1 Wigo wa Ukaguzi

Ibara 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi na kifungu cha 30(1) (c) cha Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma angalau mara moja kila mwaka wa fedha.

Ripoti hii inahusika na Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30, Juni 2008. Hasa, inahusu mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Septemba, 2007, tarehe 31 Disemba, 2007 na tarehe 30 Juni, 2008. Pia ripoti hii inahusu mapendekezo ya ukaguzi ambayo hayakutekelezwa wakati wa kipindi cha miaka iliyopita.

Nawajibika kufanya ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kama ilivyoielezwa kwenye kifungu Na.37 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 iliyorekebishwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008.

Kwa vile hii ni ripoti yangu ya pili ya jumla juu ya Mashirika na Taasisi nyinginezo nimeweza kutambua

Mashirika yapatayo 164. Juhudi zinaendelea kufanyika kuhakikisha kwamba idadi kamili ya Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma inapatikana toka Mamlaka husika. Taarifa toka kwa Msajili wa Hazina na Wizara Mama za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa kiasi fulani zinatofautiana, kwa hiyo zinahitaji usuluhisho. Ofisi yangu inafanya kazi kubwa ili kuanzisha kumbukumbu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma. Kwa hiyo, orodha iliyopo kwenye Ripoti hii ya Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma siyo kamilifu. Kama kuna miongoni mwa mashirika yaliyoachwa, yanaombwa yajisikie huru kujitokeza kutoa taarifa kuhusu Shirika au Taasisi hiyo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi.

1.2.2 Utumiaji wa Viwango vya Kimataifa

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Asasi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI) na jumua zingine za kimataifa katika taaluma ya ukaguzi. Hivyo tunatumia viwango vilivyotolewa na INTOSAI na Viwango vya Kimataifa vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Hivyo, wakati wa kufanya kaguzi zetu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ina jukumu la pekee la kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu katika matumizi, uwajibikaji na uwazi. Pia ofisi ina jukumu la kutoa Ripoti iliyo bora na kwa wakati unaofaa inayoelezea namna raslimali za taifa zilivyotumika.

1.3 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu

Jukumu la kutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu kwa madhumuni ya ukaguzi ni la Wakurugenzi wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi husika.

Kiwango Na. 1 cha kimataifa cha utayarishaji wa Taarifa za Hesabu na kiwango Na.1 cha kimataifa cha Uhasibu (IAS 1) vinaelezea aina za taarifa za fedha zinazotakiwa kutayarishwa. Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine nchini zinatakiwa kutayarisha hesabu zao kwa

kufuata/kuzingatia viwango vya kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) au viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS) kulingana na hali halisi na majukumu ya Mashirika ya Umma na Taasisi husika. Hii ni kutokana na uamuzi uliofanywa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) na kuungwa mkono na Serikali Julai 2004.

Utengenezaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ni jukumu la kisheria kulingana na matakwa ya Kisheria ya uanzishaji wa Mashirika na Taasisi husika, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 au kifungu 25 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004).

Ripoti za mwaka za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinawawezesha wananchi kupima ufanisi wa utendaji wa Mashirika hayo nakuona kuwa yanawajibika katika kutumia rasimali za Umma. Hesabu zinazowasilishwa kwa wakati ni muhimu katika kuwezesha utoaji ripoti hii.

1.4 Majukumu ya Msajili wa Hazina

Kulingana na Sheria ya Msajili wa Hazina (Treasury Registrar Ordinance Cap .418) na kifungu Na.6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.16 ya mwaka 1983 inayohusu na Mashirika ya Umma, inaeleza kwamba Msajili wa Hazina ana kazi na majukumu ya kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika.

1.5 Muundo wa Kazi ya Ukaguzi

Ripoti inatoa muhtasari wa matokeo ya mwisho ya shughuli za ukaguzi uliofanywa kwa niaba yangu kwa njia ya kuzitumia (Outsourcing) Kampuni binafsi za ukaguzi zilizosajiliwa na Ofisi yangu kwa madhumuni hayo. Ili Ofisi yangu iweze kushughulikia kazi hii kubwa ya kukagua Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo nchini,

nimeamua kutumia uwezo wangu niliopewa Kikatiba, kushirikisha kampuni binafsi za Ukaguzi wa Hesabu katika kukagua baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma. Katika kutimiza jukumu hili, Ofisi yangu aidha ilifanya ukaguzi huu yenyewe au kwa kushirikiana na Kampuni binafsi za ukaguzi. Kaguzi, zinazofanywa na kampuni binafsi za ukaguzi zinatakiwa kufanyiwa uhakiki wa ubora na Ofisi yangu.

Katika mwaka husika, Ofisi yangu iliweza kushirikiana kufanya ukaguzi na Makampuni binafsi ya ukaguzi yaliyosajiliwa nami yapatayo 44.

1.6 Kuwasilisha Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

Kifungu 25 (1) na (2) cha Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 iliyorekebisha na Kifungu 31 cha Sheria ya ya Ukaguzi Na.11 ya mwaka 2008, kinawataka Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kutayarisha hesabu katika kipindi cha Miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha na kuziwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

1.7 Kampuni Binafsi za Ukaguzi

Kifungu cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 37 (5) kinanipa mamlaka ya kuruhusu kampuni au mtu yeyote mwenye sifa za kuteuliwa kama mkaguzi chini ya Sheria ya kusajili Wahasibu na Wakaguzi Na. 33 ya mwaka 1972 kufanya ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kwa niaba yangu na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi huo kwangu kwa ajili ya hatua zaidi. Ofisi yangu kwa sasa inafanya kazi na makampuni binafsi ya ukaguzi yapatayo arobaini na nne (44) kati ya 134 ambayo yamesajiliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kufanya kazi za uhasibu na ukaguzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SURA YA PILI

MISINGI NA MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI

2.0 Utangulizi

Kamusi ya Uhasibu ya 'Oxford' inaeleza hati ya ukaguzi kuwa ni maoni yaliyomo katika ripoti ya wakaguzi. Yanaeleza iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa kwa kutumia sera za uhasibu kwa mujibu wa sheria zinazohusika, kanuni au viwango/misingi ya hesabu za fedha vinavyotumika.

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) maoni ya ukaguzi yanatakiwa kuonyesha vizuri misingi iliyotumika katika kutayarisha hesabu, na kutoa maoni ya Mkaguzi kuonyesha kwamba hesabu zinaonyesha hali halisi iliyopo na kama pia hesabu hizo zimezingatia na kufuata taratibu zinazotakiwa.

Maoni ya ukaguzi yanatolewa na mkaguzi wa hesabu anayejitegea baada ya kufanya ukaguzi kwenye Taasisi au idara kwa nia ya kumpa mtumiaji wa taarifa za Taasisi husika uwezo wa kutoa maamuzi kutokana na maoni ya ukaguzi.

Katika lugha ya kawaida hati ya ukaguzi ni thibitisho kuwa hesabu zilizowasilishwa na kukaguliwa ni sahihi na zinaaminika kwa ajili ya kufanyia maamuzi mbalimbali.

Ni muhimu kuzingatia kwamba hati za ukaguzi wa hesabu sio tathmini wala maoni kuhusu uwezo wa kifedha, utendaji, kuvutia na vigezo vingine vinavyotumika kutathmini Taasisi ili kufikia maamuzi. Suala la kwamba hesabu zilizowasilishwa ni sahihi na hazina makosa ni maoni ya ukaguzi lakini vigezo vingine vya tathmini vimeachwa kwa mtumiaji kuamua.

Maoni ya mkaguzi ni nyenzo muhimu wakati wa kutoa taarifa za fedha kwa watumiaji wa taarifa hizo. Inalenga

kulieleza Bunge na watumiaji wengine kama au la, hesabu za Mashirika ya Umma zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu hapa nchini, pamoja na kuzingatia viwango vinavyotolewa na Taasisi za kimataifa.

2.1 Aina za Hati za Ukaguzi

Kuna aina tano za hati za ukaguzi kila moja ikieleza mazingira tofauti aliyokutana nayo mkaguzi wakati wa ukaguzi. Aina hizo tano (5) ni kama ifuatavyo:-

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati inayoridhisha inajulikana pia kama hati safi. Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kuzingatia viwango vya kimataifa, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa.

2.1.2 Hati Inayoridhisha na Yenye Masuala ya Msisitizo

Hati ya ukaguzi inaweza kurekebisha kwa kuongeza msisitizo wa aya inayotaja suala linaloathiri taarifa za fedha. Kuongeza kwa aya ya msisitizo hakuwezi kuathiri maoni ya ukaguzi. Kwa kawaida, aya hiyo inaongezwa baada ya aya ya maoni, na kwa kawaida inahusu hoja ya kwamba hati inayotolewa si yenye shaka.

Aya ya suala la msisitizo inaambatanishwa wakati kunahitajika uzingatiaji wa haraka kutoka kwa watendaji wakuu na watumiaji wa taarifa za fedha kuwatahadharisha kuhusu masuala hayo yanayohitaji kushughulikiwa haraka, kushindwa kufanya hivyo kutasababisha kutolewa kwa hati yenye shaka katika ukaguzi utakaofuata. Hata hivyo, lengo kuu la suala la msisitizo ni kuleta karibu uelewa wa hali hiyo ndani ya Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati inayoridhisha.

2.1.3 Hati Yenye Kasoro

Aina hii ya hati hutolewa pale Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapokutana na mazingira ya kutokubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi (fundamental) katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye kasoro yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka. Kwa hiyo, itaonyesha kuwa hesabu kwa wastani zinaonyesha vizuri hali ya kifedha isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyochojiwa.

2.1.4 Hati Mbaya (Adverse opinion)

Hati mbaya inatolewa pale Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapona kuwa taarifa za fedha za Shirika au Taasisi ya Umma kwa kiasi kikubwa zina makosa na zikiangaliwa kwa ujumla wake hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na zile zinazotolewa na bodi za taaluma ya uhasibu za kimataifa. Hati hii inaonekana kuwa ni kinyume cha hati inavyoridhisha au hati safi kimsingi ikielezea kwamba taarifa zilizomo kwa kiasi kikubwa si sahihi wala kuaminika kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha na matokeo ya kiutendaji ya shirika au Taasisi ya umma. Maelezo ya hati isiyoridhisha yako bayana inapoelezwa kuwa taarifa za fedha hazifuati viwango vinavyokubalika vya uhasibu na hazitoi taswira halisi ya hali ya kifedha na utendaji wa mkaguliwa.

2.1.5 Mkaguzi Kushindwa Kutoa Maoni (Disclaimer Opinion)

Hati hii hutolewa wakati Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni kuhusiana na hesabu hizo. Katika hali ambayo hati hii inatolewa ni pamoja na kukosa uhuru katika kazi au kunapokuwa na wigo finyu wa kupata taarifa kwa ajili ya

ukaguzi (Audit Scope) ama kwa kukusudia au kutokukusudia ambako kunazuia kazi ya mkaguzi kupata vielelezo vya kutosha.

Kwa mfano, wakati mkaguliwa kwa makusudi anapoficha/anapokataa kutoa taarifa muhimu au kutokutoa vielelezo na taarifa kwa mkaguzi katika maeneo muhimu ya hesabu na kunapokuwa na mashaka makubwa ndani ya Taasisi inayokaguliwa.

2.2 Vigezo vya Kutoa Hati Isiyoridhisha

Sababu za kutoa hati isiyoridhisha zinaangukia kwenye makundi mawili au moja kutegemeana na mazingira ya ukaguzi.

- (a) Wakati kuna mashaka yanayomfanya mkaguzi ashindwe kutoa maoni juu ya taarifa za fedha. Kifungu cha 5 cha Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofafanuliwa kwenye kifungu cha 32(5) cha Sheria Namba 6 ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ambacho kimefutwa na kifungu cha 15 cha Sheria namba 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 imempa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kuona kumbukumbu zote, vitabu, hati za malipo, nyaraka, dhamana, vifaa vya umma vilivyo chini ya uangalizi wa afisa au mtu yeyote aliyepokea fedha au mali za umma. Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anaposhindwa kupata taarifa kamili kuhusu uandaaji wa hesabu au nyaraka na wigo wa ukaguzi kwa kutopata kumbukumbu au taarifa hizo za fedha anaweza kushindwa kutoa maoni yake.
- (b) Wakati mkaguzi anapoweza kutoa maoni yake kwa jambo fulani lakini akatofautiana kimtazamo na menejimenti kuhusu maana inayotolewa kwenye hesabu yaani kutokubaliana kuhusu njia bora za utunzaji kumbukumbu na uzingatiaji wa sheria na kanuni na kutozingatia viwango na kanuni za kitaalamu

za uhasibu zinazotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu au zile zinazotolewa na Taasisi za kimataifa.

Kati ya mambo yaliyoainishwa hapo juu kila moja kati ya hayo litapelekea utoaji wa aina tofauti ya hati za ukaguzi, mbali na hati inayoridhisha kutegemeana na kiwango cha mashaka kinachochukuliwa kuwa cha muhimu na msingi kuweza kupotosha maana iliyotolewa kwenye hesabu kwa ujumla.

Miundo ya utoaji hati mbali na hati inayoridhisha inayotumika katika mazingira mbalimbali ni kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali Lionyeshalo Misingi ya Utoaji Hati za Ukaguzi

Aina ya mazingira	Kubwa lakini si muhimu sana	Kubwa na muhimu sana
Kutokubaliana (Disagreement)	Hati yenye kasoro (Except for -	Hati mbaya (Adverse Opinion)
Mashaka (Uncertainty)	Qualified Opinion)	Kushindwa kutoa maoni (Disclaimer of Opinion)

Jedwali la hapo juu linatoa mwongozo katika utoaji hati za ukaguzi ambalo tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

- (i) Wakati matokeo ya ukaguzi yanapohusu kutokubaliana na:
 - Mambo yenyewe ni makubwa lakini siyo muhimu sana, hati ya ukaguzi itakuwa yenye kasoro (Except for).
 - Mambo yenyewe ni makubwa na ya muhimu sana, hati ya ukaguzi itakuwa mbaya.
- (ii) Wakati matokeo ya ukaguzi ni yenye shaka:
 - Shaka hiyo ni kubwa lakini si ya muhimu sana, hati ya ukaguzi itakuwa yenye shaka (Except for)

- Shaka hiyo ni kubwa na ya muhimu sana, hati ya ukaguzi itakuwa ambayo mkaguzi hawezi kutoa maoni (Disclaimer of Opinion)

Lengo la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kutoa taarifa zenye uwiano sawa wa mtazamo, kuweka mkazo katika mambo ya kimsingi yanayohitaji uangalifu na kuainisha maeneo yanayohitaji maboresho.

Kwa mujibu wa viwango vya ukaguzi, taarifa za ukaguzi zinatoa kwa ujumla uhakika, lakini siyo uhakika kamili. Kulingana na hati za ukaguzi zilizotolewa dhidi ya malengo ya ukaguzi, kiwango cha uhakika kinatolewa kwa kuweka taratibu kiasi kwamba maamuzi ya kitaalamu, hatari ya hitimisho lisilo sahihi linapunguzwa kupitia taratibu kama ukaguzi, uangalizi, uchunguzi, uthibitisho, ukokotoaji, mchanganuo na majadiliano.

Uhakika kamili hauwezi kupatikana kutokana na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufinyu katika utumiaji wa sampuli katika ukaguzi, ufinyu wa asili katika udhibiti wa ndani katika Mashirika na Taasisi za Umma na ukweli kuwa vielelezo vingi vinavyotolewa kwa mkaguzi havimsaidii kutoa hitimisho katika jambo fulani. Kiwango cha uhakika kwa hali fulani kinaweza pia kuathiriwa na usahihi uliomo katika jambo lenyewe.

Ni muhimu kufahamu kuwa hati inayoridhisha haitoi uhakika kuwa hesabu hazina makosa kabisa.

- 2.3 Msimamo wa Hesabu za Mashirika na Taasisi za Umma Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amesainisha Mashirika na Taasisi nyingine za Umma zipatazo 164 kwa kipindi kinachoishia tarehe 30, Juni 2008 ikilinganishwa na Taasisi 158 zilizoainishwa kwenye ripoti ya kipindi kilichoishia tarehe 30, Juni 2007. Hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zilikuwa 145, kati ya hizo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliweza kutoa ripoti kwa hesabu za Taasisi 101 mpaka ripoti hii inapotolewa

(tarehe 26, Machi 2009). Hesabu za Taasisi 44 ziko kwenye hatua mbalimbali za ukaguzi. Watendaji wakuu wa Taasisi za Umma 19 wanaendelea na utayarishaji wa taarifa za mahesabu yao. Hesabu zilizokaguliwa na taarifa za ukaguzi za Taasisi za Umma 101 zimetolewa kwa bodi za wakurugenzi au wadhamini na Wizara mama husika. Kwa muhtasari, maelezo ya hapo juu ni kama ifuatavyo:

Na.	Shirika/Taasisi	Hesabu zilizokaguliwa	Hesabu ambazo kaguzi zinaendelea	Hesabu ambazo hazijaletwa	Jumla
1.	Mamlaka za Maji	18	6	5	29
2.	Bodi za Udhhibiti	19	3	3	25
3.	Vyuo vya Elimu ya Juu	12	9	3	24
4.	Mashirika ya Umma	31	10	1	42
5.	Taasisi za Serikali	21	16	7	44
Jumla		101	44	19	164

2.4 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa Mwaka 2007/2008

Katika mwaka wa ukaguzi unaohusika, aina mbalimbali za hati zilitolewa kwa Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma zilizokaguliwa. Kati ya Mashirika 101 yaliyokaguliwa, Mashirika 80 (79%) yalipata hati zinazoridhisha (Hati safi), wakati mashirika 6 yalipata hati zinazoridhisha zenye masuala ya kutiliwa mkazo, ambayo ni sawa na asilimia sita (6%) ya mashirika yote. Mashirika 15 sawa na asilimia kumi na tano (15%) yalipata hati zenye kasoro (Qualified Opinion). Hakuna Shirika lililopata hati mbaya wala ambapo mkaguzi alishindwa kutoa maoni (Qualified Opinion) kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:-

Na.	Shirika/ Taasisi	Hati inayori- dhisha	Hati zinazori- sha zenye masuala yenye msisitizo	Hati yenye Kasoro	Hati Mbaya	Kushi- ndwa kutoa maoni	Jumla
1.	Mamlaka za Maji	14	1	3	-	-	18
2.	Bodi za Udhibiti	16	1	2	-	-	19
3.	Vyuo vya Elimu ya Juu	9	-	3	-	-	12
4.	Mashirika ya Umma	23	3	5	-	-	31
5.	Taasisi za Serikali	19	-	2	-	-	21
Jumla		80	6	15	-	-	101
Asilimia		79%	6%	15%			100%

Mchanganuo hapo juu ni uthibitisho kuwa hesabu katika Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo unaridhisha. Matokeo ya zoezi la ukaguzi kwa kipindi hiki unachukuliwa kwa ujumla wake kuwa unaridhisha hasa kwa udhibiti wa ndani na usimamizi wa mali za umma.

2.4.1 Hati Zinazoridhisha

Katika mwaka husika Mashirika na Taasisi za Umma 80 zimepata hati zinazoridhisha bila masuala ya msisitizo Mashirika na Taasisi hizo ni kama yafuatayo hapa chini:-

Na.	Jina La Shirika au Taasisi	Aina ya Hati (Maoni)
1.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu Majenzi	Inayoridhisha
2.	Bodi ya Korosho Tanzania	Inayoridhisha
3.	Mfuko wa Amana wa Bima	Inayoridhisha
4.	Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati	Inayoridhisha
5.	Bodi ya Usijali ya Wahandisi	Inayoridhisha
6.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	Inayoridhisha

7.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu	Inayoridhisha
8.	Bodi ya Taifa ya Utunzaji wa Vifaa	Inayoridhisha
9.	Mamlaka ya Kusimamia Manunuzi ya Umma	Inayoridhisha
10.	Bodi ya Sukari Tanzania	Inayoridhisha
11.	Bodi ya Pamba Tanzania	Inayoridhisha
12.	Bodi ya Chai Tanzania	Inayoridhisha
13.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Inayoridhisha
14.	Bodi ya Utalii Tanzania	Inayoridhisha
15.	Bodi ya Pareto Tanzania	Inayoridhisha
16.	Mamlaka ya Soko la Hisa na Mitaji	Inayoridhisha
17.	Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa	Inayoridhisha
18.	Baraza la Kukuza Uchumi Tanzania	Inayoridhisha
19.	Baraza la Taifa la Mazingira	Inayoridhisha
20.	Makumbusho ya Taifa Tanzania	Inayoridhisha
21.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Inayoridhisha
22.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Inayoridhisha
23.	Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT)	Inayoridhisha
24.	Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi	Inayoridhisha
25.	Kituo cha Mikutano cha Kimataifa - Arusha	Inayoridhisha
26.	Soko la Mitaji Dar es salaam	Inayoridhisha
27.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Inayoridhisha
28.	Shirika la Maendeleo la Taifa	Inayoridhisha
29.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Inayoridhisha
30.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Aridhi	Inayoridhisha
31.	Mamlaka ya Hifadhi ya Maeneo Ngorongoro	Inayoridhisha
32.	Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma	Inayoridhisha
33.	Simu 2000 Limited	Inayoridhisha
34.	Shirika la Taifa la Madini	Inayoridhisha
35.	Shirika la Viwango Tanzania	Inayoridhisha
36.	Shirika la Umeme Tanzania	Inayoridhisha
37.	Tanzania Engineering and Manufacturing	Inayoridhisha

	Design Organisation (TEMDO)	
38.	Kampuni ya Mbolea Tanzania	Inayoridhisha
39.	Benki ya Raslimali Tanzania	Inayoridhisha
40.	Shirika la Maendeleo ya Petroli	Inayoridhisha
41.	Benki ya Posta Tanzania	Inayoridhisha
42.	Reli Assets Holding Company	Inayoridhisha
43.	Twiga Bancorp Limited	Inayoridhisha
44.	Chuo Kikuu Cha Ardhi	Inayoridhisha
45.	Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam	Inayoridhisha
46.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Inayoridhisha
47.	Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	Inayoridhisha
48.	Chuo kikuu cha Mzumbe	Inayoridhisha
49.	Shirika la Tija la Taifa	Inayoridhisha
50.	Taasisi ya Taifa ya Sukari	Inayoridhisha
51.	Taasisi ya Elimu Tanzania	Inayoridhisha
52.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	Inayoridhisha
53.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa	Inayoridhisha
54.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya	Inayoridhisha
55.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi	Inayoridhisha
56.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma	Inayoridhisha
57.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza	Inayoridhisha
58.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga	Inayoridhisha
59.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida	Inayoridhisha
60.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea	Inayoridhisha
61.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga	Inayoridhisha
62.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati	Inayoridhisha
63.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro	Inayoridhisha
64.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka	Inayoridhisha

	Bukoba	
65.	Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania	Inayoridhisha
66.	Shirika la Reli Tanzania	Inayoridhisha
67.	Taasisi ya Jamii	Inayoridhisha
68.	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania	Inayoridhisha
69.	Kampuni ya Ranchi za Taifa	Inayoridhisha
70.	Shirika la maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo	Inayoridhisha
71.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	Inayoridhisha
72.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TSHDA)	Inayoridhisha
73.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania	Inayoridhisha
74.	NHC/PPF/IPS Co. Ltd	Inayoridhisha
75.	Ubungo Plaza Co. Ltd	Inayoridhisha
76.	Kituo cha Elimu Kibaha	Inayoridhisha
77.	Tume ya Ushindani ya Biashara (Fair Competition Commission)	Inayoridhisha
78.	Baraza la michezo la Taifa	Inayoridhisha
79.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Inayoridhisha
80.	Baraza la Mitihani Tanzania	Inayoridhisha

2.4.2 Hati Zinazoridhisha Zenye Masuala ya Msisitizo.

Katika mwaka husika Mashirika na Taasisi za Umma 6 zimepata hati zinazoridhisha na masuala ya msisitizo. Masuala ya yaliyojitokeza ni kama yalivyoorodheshwa hapa chini:-

Na.	Jina	Aina ya Hati	Misingi ya kutoa hati inayoridhisha
1.	Shirika la Bima la Taifa	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	<ul style="list-style-type: none"> • Uwezekano ya kutoendelea na biashara (Going concern problems) Mpaka kufikia tarehe 31 Desemba, 2007 madeni ya muda mfupi ya shirika yalikuwa yanazidi mal iza muda mfupi kwa shilingi 47,657,784,000. Hali hii

			<p>pamoja na mambo mengine yaliyoonyeshwa kwenye angalizo Na. 35 la tarifa za hesabu ambayo yanaashiria uwezekano wa shirika kushindwa kuendelea na biashara.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Matatizo ya kompyuta na Teknolojia ya Mawasiliano <p>Shirika linatumia mfumo wa zamani wa Kompyuta wa "Informax" ulioanza kutumika mwaka 1993. Mfumo huu haujapata kuboreshwa tangu uzinduliwe. Hali hii imesababisha mfumo kutoa huduma kwa kiwango cha chini na kutoa taarifa zisizoaminika.</p> <p>Uhifadhi na uwezo wa kupata taarifa zinazoweza kupotea kutoka kwenye mfumo wa Kompyuta hasa upande wa kuhifadhi kumbukumbu pale patokeapo tatizo ambapo huchukua muda mrefu.</p>
2.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	<p>Madeni ya muda mrefu yasiyorudishwa</p> <p>Kama ilivyokuwa imeripotiwa kwenye ripoti zetu zilizopita, baadhi ya wanaofaidika na mikopo ya vitega uchumi hawatekelezi masharti ya mikopo. Hususani kutokulipa fungu la deni (installment)</p>

		<p>kama ilivyo kwenye ratiba/jedwali la malipo na hivyo kusababisha limbikizo la faida ambayo haijalipwa.</p> <p>Licha ya juhudi za menejimenti kufuatilia urejeshwaji wa mikopo hiyo, kwa maoni yetu baadhi ya mikopo hiyo na limbikizo la gharama ya mikopo hiyo (accumulated accrued interest) ulipwaji wake ni wa shaka</p> <p>Madeni yasiyo na dhamana (Unsecured loans) kwa Kampuni ya Makaa ya Mawe na nguvu za Umeme - Kiwira USD 7,000,000</p> <p>Mkopo wa muda mfupi wa Dola za Marekani 7,000,000 ulitolewa kwa Kampuni ya Makaa ya Mawe na Nguvu za Umeme - Kiwira ambao ulitarajiwa kulipwa baada ya miezi sita (6). Mkataba wa mkopo huo ambao ulisainiwa tarehe 10 Julai 2007 hauonyeshi kama kuna dhamana (Collateral) iliyowekwa kwa ajili ya kufidia mkopo huo endepo mdaiwa atashindwa kulipa licha ya maelezo chini ya kifungu cha 10.15 kwamba mali zote na biashara lazima ziwekewe bima. Pia ilielezwa</p>
--	--	---

			<p>kuwa mkopo huo umedhaminiwa kwa asilimia mia moja (100%) na Serikali pamoja na benki ya CRDB. Hata hivyo, hati za dhamana hizo hazikuonekana zilipoitajika kwa ukaguzi.</p> <p>Kujitoa kwa wanachama Kiasi cha wachama waliojiondoa kwenye mfuko kama kilivyoripotiwa kwenye vitabu vya shirika ni kikubwa sana. Wanachama waliojiondoa kwenye mfuko kimeongezeka na kufikia shilingi bilioni 70.7 kwa mwaka 2007/2008. Sheria ya Mfuko wa Jamii ya mwaka 1997 haionyeshi kuwa mwanachama anaweza kujitoa kwenye mfuko. Kujitoa kwa wanachama kunazuia kukua kwa mfuko na pia ni kinyume na sheria iliyoanzisha mfuko huo.</p>
3.	Bodi ya Biashara ya Nje (BET)	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Kwa ujumla imegundulika kuwa bodi haikuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.
4.	Mamlaka ya Maji safi na maji taka Tabora	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Mali za kudumu, mitambo na vifaa Sh.10,477,923,881 Hakuna tathmini iliyofanyika wakati wa kufunga vitabu kuona kama mali za kudumu, mitambo na vifaa vya Mamlaka vimepoteza thamani

			<p>yake kama inavyotakiwa na viwango vya uhasibu vya kimataifa</p> <p>Wadaiwa Sh.936,359,291</p> <p>Kiasi cha Wadaiwa kilichoonyeshwa kwenye vitabu vya Mamlaka kinazidi kile kilichoko kwenye mfumo wa ankara kwa Sh.187,548,013</p> <p>Ripoti juu ya uzingatiaji wa sheria ya Manunuzi</p> <p>Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora kwa kipindi kinachoishia tarehe 30, Juni 2008 haikuzingatia Sheria ya Manunuzi wakati wa manunuzi ya vifaa mbalimbali.</p>
5.	Benki Kuu ya Tanzania	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	<p>Angalizo Na. 42 kwenye taarifa za hesabu kuhusiana na pingamizi la kisheria linalohusu malipo yaliyofaywa na Benki kama Wakala wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.</p> <p>“Garnishee Order” iliyotolewa na Mahakama Kuu tarehe 4 Juni 2001 ilitoa amri kwa Benki Kuu kumlipa aliyetoa pingamizi kiasi cha \$ 55,099,117.66 kutoka kwenye fedha za Serikali zilizohifadhiwa na Benki kama wakala. Kutokana na kesi iliyofunguliwa na Serikali dhidi ya mdai na Benki Kuu na mazungumzo yanayoendelea</p>

			Benki haijatekeleza amri iliyotolewa na Mahakama Kuu.
6	Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	<p>Kiasi kinachodaiwa kwa M/S G. K. Hotels & Resorts</p> <p>Kipindi cha mwaka 2003/2004 Mfuko ulitoa mkopo wa shilingi milioni 535 kwa M/S G. K. Hotels & Resorts ambaye ni mpangaji kwenye kitega uchumi cha "Millenium Tower House". Bakaa ya mkopo hadi tarehe 30 Juni 2008 pamoja na riba ilikuwa shilingi milioni 722. Mdeni huyu pia anadaiwa kiasi cha sh bilioni 1.127 ambayo ni kodi ya pango hadi kufikia tarehe 30 Juni 2008. Uwezekano wa kukusanya madeni haya toka kwa mdaiwa ni mdogo, na menejimenti imejiandaa kupoteza kiasi cha shilingi bilioni 1.849 kama ilivyoonyeshwa kwenye kiangalizo Na. 16 na 20</p> <p>Kuthaminisha Mafao ya Wastaafu</p> <p>Kama inavyoonekana kwenye angalizo Na 39, kazi ya kuthaminisha Mfuko ilifanywa na Solomon Consortium kufikia tarehe 31 Disemba 2003 na tathmini hiyo ilitoa dira hadi tarehe 30, Juni</p>

		<p>2005, tarehe ambayo Mfuko ulitakiwa kubadilika toka mfuko wa Akiba ya Uzeeni na kuwa Mfuko wa Pensheni.</p> <p>Kulingana na ripoti ya mthamini, kiasi cha shilingi bilioni 107.3 zaidi kilihitajika ifikapo tarehe 30 Juni 2005 ili kuwawezesha wanachama waliopo kuwa na stahili ya kuingia kwenye mfumo wa pensheni kama watakuwa wamechangia kwa muda wa miaka 15 hadi wanapofikia muda wa kustaafu.</p> <p>Serikali ya Tanzania imeridhia kutoa kiasi chote kinachohitajika kwa mikupuo kumi kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008. Ilikezwa pia kuwa Mfuko ulitarajia kufanya tathmini ya Pili ifikapo mwaka 2008, na kutoa taarifa ya tathmini hiyo kwenye taarifa za hesabu za mwaka 2007/2008. Hata hivyo tathmini hiyo bado inaendelea.</p> <p>Malipo ya wastaafu yaliyolipwa kwa niaba ya Hazina Hesabu za Mfuko (note 20) zinaonyesha kuwa malipo ya shilingi bilioni 1.875 yalilipwa kwa wastaafu ambao walitakiwa kulipwa na Hazina</p>
--	--	--

			kwa kuwa malipo hayo yanahusisha mafao yanayotokana na ajira zao wakati wakiwa Serikali kuu. Hazina wamepitia mafaili na wamekubali kulipa kiasi cha shilingi milioni 620 na kazi ya kupitia mafaili bado inaendelea.
--	--	--	---

2.4.3 Hati Zenye Kasoro

Katika mwaka huu wa fedha, Mashirika ya Umma 15 yalipata hati zenye kasoro. Mashirika hayo na sababu za kutoa hati hizo ni kama ifuatavyo:

Na	Jina	Aina ya Hati iliyotolewa	Maelezo
1.	Kampuni ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa ya wadaiwa inajumuisha wadaiwa ambao wamekatiwa maji muda mrefu lakini bado wanapelekewa ankara za maji • Utoaji wa ankara zisizo sahihi kutokana na usomaji wa mita na ukadiriaji wa matumizi ya maji usio sahihi. • Kuna mifano ambapo Ankara hazilingani na kiasi kinachoonekana kwenye akaunti za wateja husika <p>Kwa hali hii sikuweza kuthibitisha usahihi wa maduhuli ya shilingi milioni 17,332 yaliyoripotiwa kwenye vitabu vya hesabu.</p>

2.	Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma	Hati yenye kasoro(Kipindi cha miezi sita hadi Disemba,2007)	<ul style="list-style-type: none"> • Udhaifu katika ukusanyaji wa madeni ya muda mrefu au kutaifisha mali zilizouzwa kiasi cha shilingi 7,334,721,536 licha ya ushauri uliotolewa kwenye ngazi za nyuma. • Malipo ya awali ya wanunuzi kiasi cha shilingi 6,632,693,934 yalionyeshwa kama deni badala ya kuonyeshwa kama maduhuli ya Tume. • Makusanyo yaliyoingizwa moja kwa moja benki ambayo hayakingizwa kwenye vitabu shilingi 691,217,330.64 • Kutokuwasilisha nyaraka za malipo kwa waangalizi wa mali kabla ya kubinafsishwa shilingi 1,220,300,829. • Kuchelewa kuandika mikataba ya mauzo ambako kumewaathiri wanunuzi kwa kiasi kikubwa
----	---	--	---

3.	Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dodoma	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> • Ufinyu wa Mawanda ya Ukaguzi Sera ya Mamlaka ni kutambua maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji huduma ya maji machafu kwa misingi ya Ankara zilizotumwa kwa wateja. Hata hivyo tuligundua kuwa Mamlaka inatambua maduhuli kwa misingi ya fedha taslimu zilizokusanywa kinyume na sera iliyowekwa. Hali hii ilisababisha kiasi cha shilingi 104,314,900 ambacho ni makusanyo zaidi ya kiasi kilichokuwa kwenye ankara na kilichotambuliwa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Japo marekebisho yamefanyika kwa mwaka huu wa fedha lakini tumeshindwa kujua ni kiasi gani mahesabu ya miaka iliyopita yameathiriwa na makosa haya ambayo yanaathiri pia bakaa ya kufungua mwaka. <p>Madeni ya kibiashara Kuna tofauti ya shilingi 259,576,473 kati ya leja za wadaiwa na bakaa zilizoonyeshwa kwenye orodha ya wadaiwa ya</p>
----	--	-------------------	--

			<p>tarehe 30 Juni 2008. Tofauti hii haijaweza kusuluhishwa na mamlaka, kwa hiyo tumeshindwa kujua kama kiasi kilichoonyeshwa kwenye taarifa za fedha zinawiana na zile za vitabu husika.</p> <p>Mali za kudumu</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha shilingi 187,608,534 kilichoonyeshwa kwenye taarifa za fedha za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2008 kama mali za kudumu zilizoongezwa kwa kipindi hicho hazina mchanganuo. Pia hakuna kumbukumbu zozote kama vile hati ya manunuzi zinazoonyesha aina ya mali zilizounuliwa, na haikuwezekana kuziona kwa macho. Kwa hali hii tumeshindwa kuthibisha thamani, uwepo na umiliki wa mali hizo. • Mwezi Aprili 2008 ulifanyika uthamini wa ardhi, majengo, mashine na vifaa vingine vya Mamlaka uliofanywa na Kuyenga, C.M ambaye ni mtaalam wa kuthaminisha mali aliyesajiliwa. Hata hivyo uthamini huo hauonyeshi muda wa
--	--	--	---

			<p>matumizi uliobaki kwa mali zenye thamani ya shilingi 14,420,180,000. Bila kuwepo kwa muda halisi wa matumizi uliobaki kwa mali hizo, inakuwa vigumu kuthibitisha kama kiasi cha Sh.60,458,659 kilichotolewa kama gharama ya uchakavu wa mali (depreciation) ni sahihi au la.</p> <p>Bakaa ya bidhaa/vifaa Kiasi cha Sh.644,354,870 kilichojumuishwa kwenye bakaa ya vifaa vya umeme hakikuweza kuhakikiwa ipasavyo kutokana na kukosekana kwa vigezo kama vile hati za manunuzi. Pia kulikuwa hakuna maelezo ya kutosha juu ya vigezo vilivyotumika kutoa thamani ya vifaa hivyo, na hivyo hatukuweza kuthibitisha usahihi wa kiasi kilichoripotiwa.</p> <p>Bakaa ya fedha taslimu na benki</p> <p>Kuna tofauti kati ya suluhisho</p> <p>ya benki na taarifa ya urari wa benki kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni</p>
--	--	--	---

			<p>2008 cha shilingi 10,217,778 kwenye akauti za CRDB za uendeshaji (operation) akauti kuu (main account), na akaunti ya utawala (administration account). Hatukuweza kudhibitisha kama fedha tasilimu na benki zilizoripotiwa tarehe 30 Juni 2008 zilikuwa sahihi.</p> <p>Gharama za uendeshaji</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuna tofauti kati ya leja za wateja na Urari za tarehe 30 Juni 2008 kwa malipo ya simu, vifaa vya ofisini (stationery and printing) na gharama za Mradi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa shilingi 42,873,209. Kutokana na tofauti hii, usahihi wa gharama hizo haukuweza kuthibitishwa mara moja. <p>Malipo ya shilingi milioni 29.83 hayakuwa na viambatanisho vya kutosha kama vile hati za madai na stakabadhi za malipo, na hivyo hatukuweza kuthibitisha kama malipo hayo yalifanywa kwa ajili ya shughuli za Mamlaka</p>
4	Shirika la Magazeti Tanzania	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> • Manunuzi ya vifaa vya shilingi 26,384,077 bila kuitisha zabuni kinyume na Kifungu cha 44 cha

			<p>Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake</p> <ul style="list-style-type: none"> • Ukarabati wenye mashaka wa nyumba ya kuishi wa sh. 53,920,108. Kulikuwa na ongezeko la gharama la sh.27,260,000 na mzibuni alikuwa mmoja ambaye alipitishwa na Kamati ya manunuzi na kuidhinishwa na Mhariri Mkuu. Taratibu zote za manunuzi zilikiukwa kulingana na Sheria ya Manunuzi Na 21 ya mwaka 2004 • Manunuzi ya madawa ya kuchapishia yenye mashaka sh. 1,404,785,324. • Ununuzi wa mitambo ya kompyuta yenye mashaka shilingi 13,956,444 (\$11,630.37) <p>Madeni ya muda mrefu Sh. 2,418,253,908.02</p>
5	Shirika la Utangazaji Tanzania	Hati yenye kasoro	<p>Ufinyu wa Mawanda (limitation of scope)</p> <p>Maduhuli yatokanayo na matangazo ya biashara</p> <p>Kama ilivyoripotiwa kwenye ripoti ya mwaka uliopita, Shirika la Utangazaji Tanzania linapokea maombi ya matangazo ya biashara na</p>

		<p>kutoa hati ya uthibitisho wa kurusha matangazo kabla ya kuyarusha.</p> <p>Hati za madai hutengenezwa kwa kutumia hati za uthibitisho wa kurusha matangazo ambazo zimeidhinishwa na Mkurugenzi wa Masoko.</p> <p>Iligundulika kuwa Shirika halitunzi kumbukumbu za maombi ya matangazo ya biashara yaliyopokelewa na kushugulikiwa na Hati za Uthibitisho zilizotolewa kwa kipindi hicho.</p> <p>Pia tuligundua tofauti ya shilingi 2,217,323,619 kati ya mchanganuo uliotengenezwa na Mkurugenzi wa Masoko na mchanganuo wa hati za madai zote zilizotumwa kwa wateja toka kitengo cha uhasibu kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Hakuna maelezo ya kuridhisha yaliyotolewa juu ya tofauti hiyo.</p> <p>Pia kulikuwa hakuna orodha ya vipindi na matangazo yote yaliyorushwa kwa kipindi hicho.</p> <p>Kutokana na ufinyu wa mawanda uliosababishwa na</p>
--	--	--

			<p>udhaifu wa utunzaji wa kumbukumbu na usahihi wa makusanyo ya maduhuli, tulishindwa kuthibitisha usahihi wa maduhuli ya sh. 5,420,214,926 yaliyoripotiwa kwenye taarifa za hesabu.</p> <p>Majengo, Mitambo na Vifaa Shirika liliingia mkataba na Mthamini aliyesajiliwa kwa ajili ya kuthaminisha mali zote za kudumu. Hata hivyo, mpaka tunamaliza ukaguzi, ripoti ya mwisho ya uthamini huo ilikuwa haijatolewa. Kwa hiyo, thamani ya mali za kudumu zilizoonyeshwa kwenye taarifa za hesabu haijumuishi matokeo ya uthamini uliofanywa. Kama ilivyoripotiwa kwenye ripoti ya mwaka jana, mali za kudumu, za iliyokuwa Redio Tanzania ikiwa ni pamoja na majengo, vifaa na samani hazikuingizwa kwenye taarifa ya hesabu ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2008. Pia mali zilizopo kwenye vituo mbalimbali zimepoteza thamani (impaired). Kutokana na ukubwa wa mali ambayo inaonekana kutojumuishwa kwenye mahesabu, tumeshindwa kuthibitisha</p>
--	--	--	--

		<p>usahihi wa mali iliyoripotiwa kwenye taarifa ya hesabu pamoja na gharama za uchakavu. "Letter of Credit"</p> <p>Mchanganuo unaoonyesha mwenendo wa bakaa ya akaunti ya 'letter of credit' kwa mwaka husika haukutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Bakaa ilipungua toka shilingi 775,872,275 ya tarehe 1 Julai, 2007 hadi sh 250,251,054 tarehe 30 Juni 2008. Hatukuweza kuthibitisha kama malipo yaliyofanywa kwenye akaunti ya 'letter of credit' yalikuwa halali kwa shughuli za shirika.</p> <p>Gharama za uendeshaji Malipo ya shilingi 76,646,811 hayakuwa na viambatanisho vya kutosha kama vile hati na stakabadhi za malipo, hivyo hatukuweza kuthibitisha uhalali wa malipo haya.</p> <p>Manunuzi</p> <ul style="list-style-type: none"> • Manunuzi ya shilingi bilioni 2.34 ambayo ni sawa na 49% ya malipo yote yaliyokaguliwa hayakuwa ndani ya mipaka (limits) zilizoainishwa kwenye mchanganuo wa tatu wa
--	--	--

			<p>Tangazo la Serikali (G.N) Na. 97 na 98. hii ni pamoja na manunuzi kutoainisha njia zilizotumika kutofuata taratibu za zabuni.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Manunuzi ya shilingi bilioni 1.178 ambayo ni sawa na 44% ya manunuzi yaliyokaguliwa hayakuidhinishwa na Bodi ya Dhabuni
6	Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania	Hati yenye kasoro	<p>Malipo yenye shaka</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kiasi cha sh. 1,250,000,000 kilichojumuishwa kwenye bakaa ya madai ya Mamlaka ni malipo yaliyolipwa kwa Shirika la Ndege Tanzania kwa ajili ya kusaidia usafirishaji wa Mahujai kwenda Mecca kinyume na kifungu cha 50 cha Sheria Na. 12 ya Mamlaka ya mwaka 2003. hatukuweza kujiridhisha kama malipo haya ni halali na kama yataweza kurudishwa. • Kiasi cha sh bilioni 7.13 kililipwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kwa ajili ya kukarabati kiwanja cha ndege cha Mwanza kati ya tarehe 1 Julai na tarehe 30 Juni 2008 (2007/2008)

			<p>bilioni 3.068) kinyume na kifungu cha 50 cha Sheria ya Na. 12 ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano ya mwaka 2003. Uhalali wa malipo haya haukuweza kuthibitishwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Malipo ya shilingi 151,372,212 yalilipwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani iliyotokana na manunuzi yaliyofanywa na Mamlaka kipindi cha mwaka huu wa fedha kinyume na kipengere cha tano cha Jedwali Na. 3 (Third schedule) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeka la thamani ya mwaka 1997. • Malipo ya shilingi 13,294,620 yalilipwa kwa kutumia ankara vifani, kwa hiyo hatukuweza kuthibitisha kama malipo haya yalifanywa kwa manufaa ya Mamlak. <p>Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni za Manunuzi za mwaka 2005</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mamlaka haijaanzisha kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU) kinyume na kifungu cha 34 (1) & (2) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 • Muundo wa sasa wa
--	--	--	--

			<p>Mamlaka unaonyesha kuwa kitengo cha usimamizi wa manunuzi kitaripoti kwa Mkurugenzi Mkuu.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mpango wa manunuzi wa Mamlaka haufanyiwi marekebisho kulingana na manunuzi halisi ili kuwa na ripoti ya mwezi kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 35 (o) cha Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 • Baadhi ya vifaa vilinunuliwa nje ya mpango wa manunuzi • Manunuzi ya shilingi milioni 108 ambayo ni 13% ya manunuzi yote ya mwaka hayakutangazwa kinyume na kifungu cha 61 (2) cha Sheria ya manunuzi na kanuni 80 (5) ya tangazo la Serikali Na 97 pamoja na kanuni 49 (1) -(4) ya tangazo la Serikali Na. 98 • Hakuna ushahidi unaoonyesha kama zabuni zilizoitishwa za kiasi cha shilingi milioni 113.56 zilitumwa kwa wazabuni wote walioteuliwa, na pia haikuweza kufahamika kama au la, zabuni hizo zilizingatia muda ulioainishwa kwenye
--	--	--	--

			<p>jedwali la tatu (3rd schedule) sehemu (c) ya tangazo la Serikali Na 97.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Taratibu za zabuni kwa manunuzi ya shilingi milioni 83.24 ambazo ni sawa na 10% ya manunuzi yote ya mwaka 2007/2008 hayakuidhinishwa na Bodi ya zabuni kinyume na kifungu cha 30 (a) -(g) cha Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni ya 80 (1) - (7) ya tangazo la Serikali Na 97 • Hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa zabuni zilizoshindanishwa ambazo ni 13% ya manunuzi yote zilipokelewa zikiwa zimefungwa vizuri (sealed) na kama zilifunguliwa mbele ya wahusika kwa muda uliopangwa. • Hakuna kumbukumbu za vikao vya ufunguzi wa zabuni, hivyo utoaji wa zabuni haukuwa sahihi • Wakati mwingine wajumbe wa kamati ya Uthamini (Evaluation Committee) waliwatembelea wazabuni wakati wa kuthamini zabuni zao.
--	--	--	---

			<ul style="list-style-type: none"> • Hakuna zabuni iliyotangazwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 kinyume na kanuni ya 67 (3) ya tangazo la Serikali Na. 98 na kanuni ya 97 (12) ya tangazo la Serikali Na 97 • Nyaraka za zabuni hazikuhifadhiwa kitaalam na hivyo kufanya utafutaji wa habari zinazohusiana na zabuni kuwa ngumu na ndefu. • Muundo wa Mamlaka hautoi mazingira ya Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi kufanya shughuli zao kwa uhuru kama inavyotakiwa na kifungu cha 38 cha Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004. Kukosekana kwa uimara wa kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi, baadhi ya mahitaji ya manunuzi yanapelekwa moja kwa moja kwa Bodi ya Zabuni • Hakuna ushahidi unaoonyesha kama Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) walipewa taarifa juu ya uanzishwaji wa Bodi ya Manunuzi kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 29 (1) cha
--	--	--	--

			<p>Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na nyaraka za mikataba hazikutolewa kwa Mamlaka husika kulingana na kanuni ya 116 ya tangazo la Serikali Na. 97</p> <ul style="list-style-type: none"> • Wakati mwingine kamati ya Bodi za Zabuni za muda ziliundwa kupitisha manunuzi kinyume na kanuni za manunuzi ya muda. • Hakuna ushahidi kama Afisa Masuuli aliunda Kamati ya kuhakiki na kupokea vifaa vilivyoagizwa kama inavyotakiwa na Kanuni ya 127 na 128 ya Manunuzi ya Umma ya tangazo la Serikali Na.97. • Zabuni ya kumtafuta Mshauri wa kupitia Muundo wa Mamlaka na kutathimini uwiano wa kazi ndani ya Mamlaka ilitolewa katika mazingira ya kutatanisha na hivyo kukiuka Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake. <p>Kulingana na mambo yaliyojitokeza hapo juu na uchambuzi uliofanyika,</p>
--	--	--	---

			Mamlaka imeweza kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 kwa asilimia 55 (55%).
7.	Hifadhi ya Taifa ya Tanzania (TANAPA)	Hati yenye kasoro	<p>Ufinyu wa Mawanda</p> <ul style="list-style-type: none"> Akaunti ya amana ya muda maalum <p>Menejimenti ya TANAPA haikuweza kuwapatia wakaguzi shahada zinazohusu Accounti ya Amana ya muda maalum yenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,088,801.52 kwenye benki ya Exim. Hakuna majibu yaliyopatikana toka benki kuthibitisha bakaa hiyo. Pia mazungumzo yaliyofanywa na menejimenti yanaonyesha kuwa amana mbili zenye namba EB/97/51721 za thamani ya Dola za Kimarekani 2,044,655.27 hazikuwepo kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2008. Wakaguzi pia waligundua kuwa baadhi ya hati za amana zilizotolewa na benki ya Exim hazikusainiwa na mtu wa pili aliyeidhinishwa na benki. Namba za hati zilizoletwa hazikuwa kwenye mpangilio</p>

		<p>wa kueleweka.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Gharama za kuendeleza ardhi Kiasi cha shilingi bilioni 5.9 kilijumuishwa kwenye gharama za kuendeleza ardhi ikiwa ni fidia iliyolipwa kwa wanakijiji wa Usangu lakini hakuna ushahidi kama fedha hizo zilipokelewa na wahusika. • Gharama za kutangaza utalii na kukuza mahusiano Gharama za kutangaza utalii na kukuza mahusiano zimejumuisha pia kiasi cha sh 100,000,000 zilizolipwa kwa Swagaswaga team kwa ajili ya kujenga zizi wakati wa maonyesho ya Nane Nane yaliyofanyika Dodoma. Hata hivyo fedha hizo hazikutolewa maelezo ya namna zilivyotumika. <p>Gharama za matangazo “CNN” na “Jambo Publication Limited” Manunuzi ya matangazo kwenye “CNN” hayakufuata taratibu za manunuzi. Japo kulikuwa na mkataba uliosainiwa na Mwenyekiti wa TANAPA, mambo mengine yote yanayohusu</p>
--	--	---

		<p>manunuzi yalifanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kinyume na maelekezo ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Mkataba wa matangazo na CNN kwa mwaka 2007/2008 ulikuwa wa Dola za Kimarekani 750,000. Pia TANAPA imeingia mkataba mpya na CNN wenye thamani ya Dola za Kimarekani 800,000 kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Mikataba yote miwili haionyeshi mambo yafuatayo:</p> <p>Wakati wa kutoa matangazo; Masaa ya kutangaza; Idadi ya matangazo kwa siku, wiki au mwezi; Utaratibu wa kuhakikisha kuwa matangazo yanatolewa kwa muda uliowekwa na kwa ubora unaokubalika</p> <p>●Makubaliano ya namna ya kulipa. Kwa mfano, TANAPA walifanya malipo ya shilingi 1,077,620,400 kwa mkupuo mwezi Oktoba 2007 kwa CNN. Malipo hayo hayakuambatana na uthibitisho wa kufanyika kwa matangazo. Kwa upande wa matangazo yaliyofanywa na Jambo Publication Ltd, TANAPA</p>
--	--	---

			walilipa kiasi cha Dola za Kimarekani 272,006.45 kama gharama za matangazo ambapo Dola za Kimarekani 68,373.23 ni gharama ya kutangaza kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa Heahrow (London) kwa miezi sita kuanzia Januari hadi Juni 2008 na Dola za Kimarekani 203,633.20 ni gharama ya kutangaza kwenye mabasi 100 ya mjini London. Hata hivyo mikataba ya matangazo haya haikutolewa kwa wakaguzi. Pia hati ya madai inayohusiana na matangazo hayo ina anuani ya Bodi ya Utalii ya Tanzania na hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa huduma hiyo ilitolewa
8	Shirika la Posta Tanzania	Hati yenye kasoro	Deni la sh 738,678,508 linalohusiana na mpango wa mafao ya wafanyakazi lililoonyeshwa kwenye vitabu halionyeshi thamani halisi ya deni hilo.
9	Chuo cha Uhasibu Arusha	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> Leja ya majengo, mitambo na vifaa (kiambatanisho) ya chuo ilikuwa haijatarishwa hadi tunapoandika ripoti hii, matokeo yake hatukuweza kulinganisha kiasi cha thamani na

			<p>gharama za uchakavu za vifaa hivyo kilichoonyeshwa kwenye leja kuu na kile kilichoko kwenye kiambatanisho. Kwa sababu hiyo pia hatukuweza kulinganisha bakaa sh 5,100,947,762 iliyoonyeshwa kwenye vitabu na vifaa halisi vilivyopo.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Uhakiki tulioufanya kwenye ongezeko la majengo, mitambo na vifaa katika kipindi cha mwaka husika unaonyesha baadhi ya manunuzi yaliyofanywa aidha kwa kuagiza moja kwa moja au kwa kutumia chanzo kimoja tu kabla ya kuidhinishwa na Bodi ya Manunuzi kinyume na jedwali Na. moja (First schedule) la Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2005. Mbali ya hayo vifaa vya ofisini na hosteli vya shilingi 31,175,100 na shilingi 101,749,998 kwa mpangilio, vilinunuliwa bila kuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka na pia manunuzi hayo hayakutangazwa kwenye Tangazo la Manunuzi kama inavyotakiwa na kanuni za
--	--	--	---

			<p>manunuzi ya umma za mwaka 2005</p> <ul style="list-style-type: none"> • Madeni ya wanafunzi (A/c Na. 2100/001) ya sh 207,138,504.75 yanayodaiwa toka Hazina yameonyeshwa kama madeni ya biashara. Hata hivyo kwa mara ya mwisho chuo kiliwasiliana na Hazina tarehe 17/12/2007, na tangu hapo hakuna mawasiliano yaliyofanyika na Hazina hawajajibu. Pia mchanganuo wa madeni hayo haukutolewa kwa ajili ya kuhakikiwa kwa hiyo usahihi wa madeni hayo haukuthibitishwa. • Madeni ya wanafunzi (A/c Na. 2100/002 toka wanafunzi wanaojidhamini wenyewe ya sh 288,457,700.16 (kiasi kilichokuwa kimesalia tarehe 30 juni 2008 ni sh 161,873,621) yameonyeshwa pia kama madeni ya biashara lakini hakuna mchanganuo unaoonyesha muda wa madeni hayo, kwa hiyo hatukuweza kujua ni muda gani madeni hayo yamekaa bila kukusanywa • Ada ya masomo ya shilingi 3,299,954,685.43 ambayo
--	--	--	---

			<p>inahusisha ada ya maombi na usajili hailingani na kiasi cha shilingi 3,359,500,000 ambacho kilitakiwa kukusanywa kulingana na idadi ya wanafunzi waliosajiwa. Tofauti ya shilingi 59,545,314.57 haikutolewa maelezo. Kutokana na mambo yaliyojitokeza hapo juu, usahihi wa madeni yaliyoripotiwa haukuthibitishwa.</p> <p>Chuo hakijaanzisha kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU) kama ilivyoelekezwa chini ya kifungu cha 34 cha Sheria ya manunuzi ya umma kinavyoelekeza ya mwaka 2004. Kwa sasa kuna kitengo cha manunuzi na ugavi ambacho kiko chini ya Mkurugenzi wa Fedha na Utawala.</p>
10	Chuo Kikuu cha Dar es salaam	Hati yenye kasoro	<p>Chuo kilifanya manunuzi vifaa na kazi za ujenzi zenye thamani ya shilingi 1,273,349,456 na dola za Kimarekani 300,382 kwa niaba ya vyuo vya ualimu vishiriki Dar es salaam na Mkwawa kwa mpangilio huu, bila ya kufuata taratibu za manunuzi kinyume na kanuni ya 67 na 69 ya manunuzi ya umma ya mwaka 2005</p>

11	Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> • Chuo hakitunzi rejista ya mali za kudumu wala hakikuhesabu mali hizo kwa kipindi chote cha mwaka kwa mali zisizohamishika zenye thamani ya shilingi 14,337,694,754 • Madeni ya shilingi 741,295,019 yaliyoonyeshwa kwenye vitabu yanajumuisha baadhi ya madeni ambayo yamekaa bila kulipwa kwa zaidi ya miaka 8 na hayana vielelezo vya kuthibitisha uhalali wa madeni hayo. <p>Daftari la fedha halikutunzwa vizuri na baadhi ya fedha zilizopokelewa au kulipwa kwenye daftari hazina stakabadhi za kuonyesha jinsi zilivyopokelewa au hundi zilizotumika kulipa. Vilevile usuluhisho wa bakaa ya daftari na ile ya Benki ulikuwa ni mgumu.</p>
12	Mfuko wa Pensioni ya watumishi wa Serikali	Hati yenye kasoro	Viwango vya ukaguzi vya kimataifa vya ukaguzi hususani Na. 710 (ISA 710) kinamtaka mkaguzi wa hesabu kupata ushahidi wa kutosha kama bakaa ya kufungua mwaka husika na

			<p>bakaa ya ulinganisho (comparative figure) ya mwaka uliopita zinakidhi matakwa ya viwango vya kimataifa vya kutoa taarifa za mahesabu na zinakubaliana na taarifa za ziada zilizoambatana na hesabu (disclosures) zilizoonyeshwa vipindi vya miaka iliyopita au marekebisho ya kihasibu kwenye mahesabu yaliyofanyika. Hatukuweza kuthibitisha kiasi cha bakaa ya mwanzo wa mwaka kutokana na kutokuweza kufanya upembuzi wa taarifa za mkaguzi wa miaka ya iliyopita kama viwango vya ukaguzi wa viwango vya ukaguzi wa kimataifa hususani Na. 710 kinavyotutaka.</p>
13	Mamlaka ya Maji Safi na maji Taka Lindi	Hati yenye kasoro	<p>Wateja wa maji waliokatiwa maji wanaendelea kupelekewa ankara za maji.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutoa ankara za maji ambazo sio sahihi kutokana kutokusoma mita za maji au kufanya makadirio yasio sahihi. • Ukaguzi ulibaini wateja wanaopata maji ya bomba ambao hawajawahi kupelekewa ankara za maji.

			Kumbukumbu za wateja wa maji zina majina ya baadhi ya wateja ambao hawapati maji.
14	Marine Service Co	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> • Daftari la fedha taslimu halikuwa limeandaliwa kwa ufasaha kutokana na fedha zilizopokelewa kutoka kwa wateja kutokunakiliwa kwenye daftari hilo. • Kutokukiri mapokezi ya fedha kutoka kwa wateja kwa ufasaha. <p>Kutokufanya usuluhisho wa daftari la fedha taslimu na taarifa ya benki.</p>
15	Mamlaka ya Udhibiti ya Usafiri wa Anga	Hati yenye kasoro	<ul style="list-style-type: none"> • Viwango vya ukaguzi vya kimataifa vya Ukaguzi hususani Na 710 (ISA 710) kimtaka mkaguzi wa hesabu kupata ushahidi wa kutosha kama bakaa ya kufungua mwaka husika na bakaa ya ulinganisho (comparative figure) ya mwaka uliopita zinakidhi matakwa ya viwango vya kimataifa vya kutoa taarifa za mahesabu na zinakubaliana na taarifa za ziada zilizoambatana na hesabu (disclosures) zilizoonyeshwa vipindi vya miaka iliyopita au marekebisho ya kahasibu kwenye mahesabu

			<p>yalifanyika. Hatukuweza kuthibisha kiasi cha bakaa ya mwanzo wa mwaka kutokana na kutokuweza kufanya upembuzi wa taarifa za mkaguzi wa miaka ya iliyopita kama viwango vya ukaguzi wa kimataifa hususani Na 710 kinavyotutaka Kama ilivyoonyeshwa angalizo Na. 20 la mahesabu, hapakuwepo na tozo la faida kwenye mkopo wa muda mrefu. Hata hivyo, Kipengele IV cha makubaliano ya mkopo kati ya Mamlaka na Wizara ya Fedha kinaeleza kuwa mkopo una tozo la faida ya asilimia sita 6%. Vile vile kifungu cha 4 (1) (c) kinaitaka Mamlaka kufungua benki akaunti na asilimia tano 5% ya tozo la faida kwa mwaka itumike kwa ajili ya mafunzo ya watumishi ambao wako Kitengo cha Uhasibu na wataalamu wengine wa Mamlaka. Asilimia moja 1% itakayobaki inatakiwa ilipwe in “arrears” baada ya mwaka mmoja pamoja na rejesho la kiwango cha fedha “instalment”</p>
--	--	--	--

			<p>Serikalini. Kama kifungu hiki kingetekelezwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2008, kiasi cha shilingi milioni 212 kingelipwa Wizara ya Fedha na Uchumi. Mchanganuo wa fedha hizo zinatokana na shilingi milioni 170 tozo la faida ya kipindi cha miaka iliyopita na shilingi milioni 42 zikiwa ni tozo la mwaka husika.</p>
--	--	--	---

2.4.4 Hati Mbaya na Mkaguzi Kushindwa Kutoa Maoni

Kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha, hakuna Shirika wala Taasisi ya Umma iliyopata hati mbaya wala ambapo Mkaguzi alishindwa kutoa maoni.

Nimechukua jitihada za kueleza sababu zilizopelekea kupata aina mbalimbali za hati zilizoathiri Mashirika na Taasisi za Umma ili Mashirika na Taasisi hizo ziweze kujua maeneo yenye udhaifu na kuchukua hatua kwa ajili ya kuyaboresha siku zijazo.

SURA YA TATU

MUHTASARI WA MAPENDEKEZO YA MATOKEO YA UKAGUZI WA MWAKA ULIOPITA AMBAYO HAYAJATEKELEZWA

3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za mwaka uliopita ambayo mpaka namaliza ukaguzi wa mwaka huu yalikuwa aidha hayajatekelezwa kabisa au yametekelezwa nusu, na yanahitaji angalizo la Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma.

3.1 Majibu ya Ripoti ya Mwaka Uliopita

Nimepokea majibu ya Serikali juu ya ripoti yangu ya mwaka uliopita kupitia kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa barua yenye Kumb.Na ED/AG/AUDIT/GEN/08/VOL./150 ya tarehe 4 Oktoba, 2008. Mchanganuo wa mapendekezo ya ripoti yangu kuu ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2007 ambayo hayajatekelezwa na yanahitaji angalizo zaidi ni kama ifuatavyo:

Na.	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO	MAJIBU YA MLIPAJI MKUU	MAONI
1	10.1 Maswala ya Ubinafsishaji Ofisi ya Msajili wa Hazina haikuwa imekusanya madeni yatokanayo na mauzo ya ubinafsishaji wa baadhi ya Mashirika ya Umma kutoka kwa wawekezaji. Hata hivyo, licha ya mafanikio makubwa ya ubinafsishaji baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi	Ofisi ya Msajili wa Hazina inapaswa kuhakikisha kwamba: <ul style="list-style-type: none">Hatua madhubuti za kukusanya madeni yaliyokaa muda mrefu zinachukuliwa kwa wawekezaji walioshindwa kutekeleza masharti ya	Mapendekezo yaliyotolewa yanaendana na mipango ya Serikali. Katika muundo mpya wa Wizara ya Fedha na Uchumi kuna kitengo kinachohusika na usimamizi wa utendaji wa mashirika yaliyobinafisis hwa ili	Mapendekezo hayajatekelezwa kikamilifu

	<p>nyinginezo hayajiendeshi kama ilivyokusudiwa. Baadhi ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa yamebadili malengo ya awali ya uzalishaji na mengine yameacha kabisa kujiendesha.</p>	<p>ununuzi wa mashirika hayo;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wawekezaji walioshindwa kutekeleza majukumu yao ya mikataba ya ubinafsishaji; • Mashirika na Taasisi za Umma ambazo hazijiendeshi ipasavyo zinachukuliwa na Serikali au yanauzwa tena kwa mwekezaji mwenye uwezo; • Mali za wawekezaji walioshindwa kutimiza wajibu wao zinachukuliwa na Serikali au waamriwe kulipa; • Shirika la Ukusanyaji wa madeni ya ubinafsishaji (CHC), ambalo ni mrithi wa Tume ya Rais ya Kurekebisha 	<p>kuhakikisha kuwa yanafanya biashara iliyokubaliwa kwenye mkataba wa ubinafsishaji</p>	
--	--	---	--	--

		<p>Sekta ya Mashirika ya Umma (PSRC) na LART; linashauriwa kufanya ukaguzi baada ya ubinafsishaji (post privatization audit) kwa makampuni yote yaliyobinafsishwa ili kuona kwamba mashirika hayo yanaendeshwa kulingana na makubaliano na madhumuni ya ubinafsishwaji</p>		
2.	<p>10.2 Mifumo hafifu ya teknolojia ya mawasiliano Baadhi ya Mashirika ya Umma yalikuwa na mifumo hafifu ya teknolojia ya mawasiliano. Wakati mwingine yalikuwa yanatumia mifumo iliyopitwa na wakati.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Menejimenti ya Mashirika na Taasisi za Umma husika zinapaswa kuhakikisha kuwa inaweka mifumo mipya na ya kisasa. • Mifumo ya teknolojia ya taarifa iliyopo inapaswa kuboreshwa na menejimenti za Mshirika na Taasisi za Umma. 	Hakuna jibu	Hakuna utekelezaji

3.	<p>10.3 Uandaaji wa miongozo ya Fedha na Uendeshaji Baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo hazikuwa na miongozo ya fedha na uendeshaji kama vitendea kazi muhimu katika kuhakikisha uendeshaji na shughuli za fedha zinafanyika ipasavyo.</p>	<ul style="list-style-type: none"> Menejimenti ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinapaswa kuhakikisha kuwa miongozo ya uendeshaji na ile ya fedha inaandaliwa na kutumika ipasavyo; 	Hakuna jibu	Hakuna utekelezaji
4.	<p>10.4 Utawala Bora Ilibainika pia kuwa, baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo yalikuwa na matatizo ya utawala bora kama inavyoelezwa hapa chini:-</p> <ul style="list-style-type: none"> Hazikuwa zimeunda vitengo vya Ukaguzi wa Ndani (internal audit units) wala kamati za ukaguzi (audit committees) Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani havikuwa na wafanyakazi wenye sifa; Wakuu wa vitengo vya Ukaguzi wa 	<ul style="list-style-type: none"> Menejimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinapaswa kuunda/kuanzisha vitengo madhubuti vya Ukaguzi wa Ndani ambavyo watumishi wake watakuwa na sifa zinazotakiwa na vitendea kazi bora na vya kutosha katika kutimiza wajibu wao; Wakuu wa vitengo vya Ukaguzi wa Ndani wanatakiwa 	Mapendekezo yanayolenga kuondoa mgongano wa kimaslahi unaoweza kujitokeza kwa wajumbe wa kamati za Bunge kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi linafikiriwa na Serikali	Mapendekezo hayajatekel ezwa kikamilifu

	<p>Ndani hawakuwa wakipeleka taarifa za ukaguzi kwa Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo</p> <ul style="list-style-type: none"> • Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ambavyo sio madhubuti; • Wakaguzi wa Ndani walikuwa wanafanya kazi ya ukaguzi kabla ya malipo (pre-audit); na • Baadhi ya Wabunge ni wajumbe wa baadhi ya Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo. 	<p>kutoa taarifa za ukaguzi moja kwa moja kwa Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Wajumbe wa kamati za ukaguzi kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha Sheria Na. 31 cha Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebis hwa 2004) inabidi iangaliwe upya ili iweze kuruhusu wajumbe zaidi kutoka nje ya ofisi. Hii itaiwezesha Kamati ya Ukaguzi kuwa makini zaidi katika kutoa ushauri unaofaa kwa Watendaji Wakuu; • Ili kuepuka mgongano wa kimaslahi (conflict of interest), kuhusiana na jukumu la 		
--	---	--	--	--

		usimamizi wa shughuli za Mashirika na Taasisi za Umma, Wabunge hawapaswi kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo		
5.	<p>10.5 Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi</p> <p>Tulibaini yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> Baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo hazikuwa na vitengo vya usimamizi wa ununuzi; Kutokufuata taratibu na njia bora za ununuzi kwa baadhi ya Mashirika ya Umma. Baadhi ya Mashirika ya Umma hayakuwa na bodi za zabuni; Udhaifu mkubwa ulibainika katika 	<p>Katika kutimiza utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, napendekeza yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> Elimu itolewe katika nyanja zote za ununuzi; Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ipewe mamlaka ya kutosha katika kufanya udhibiti wa kazi ya ununuzi. Kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za kesi za 	<p>Serikali itaendelea kuboresha Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ili kuboresha mapungufu yanayojitokeza katika mfumo wa manunuzi ya umma</p>	<p>Majibu hayatoshelezi na mapendekezo hayajatekel ezwa kikamilifu</p>

	<p>usimamizi wa mikataba ya ununuzi; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Vitengo vya kusimamia ununuzi vinaendeshwa na wafanyakazi wasiokuwa na sifa, ujuzi na uzoefu. 	<p>ununuzi; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Bodi za Zabuni madhubuti na Vitengo vya Usimamizi Ununuzi vinapaswa kuanzishwa au kuboreshwa. 		
6.	<p>10.6 Mashirika ya Umma yenye matatizo ya kuendelea na biashara kwa siku za usoni "Going Concern problems"</p> <p>Baadhi ya Mashirika ya Umma yamekuwa yakijiendesha kwa mtaji hasi (Negative working capital). Tatizo hili limesababisha Mashirika husika kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kulipa madeni yao hali ambayo sio nzuri kibiashara.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Juhudi zifanywe na Mashirika na Taasisi husika ili kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji; • Vitengo/ matawi ya Mashirika na Taasisi za Umma ambavyo vinajiendesha kwa hasara vinapaswa vitambuliwe na vipendekewe kufungwa, kubinafsishwa au kujiunda upya; • Mali ambazo hazitumiki na vitega uchumi ambavyo vinajiendesha bila faida vinapaswa viuzwe; • Kuboresha 	Hakuna jibu	Hakuna utekelezaji

		<p>maslahi ya wafanyakazi ili kuongeza ufanisi; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Uchambuzi yakinifu ufanyike katika kufanya maamuzi ya kuunda upya baadhi ya Mashirika ya Umma, kuangalia hali inayozuia ufanisi na kuleta hasara ili iweze kurekebisha. 		
7.	<p>10.7 Bili za Maji katika Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka</p> <p>Ukaguzi wa Mamlaka za Maji ulibaini kuwepo kwa udhaifu mkubwa katika kuandaa Ankara za maji. Hii ni pamoja na kuwepo kwa tatizo la kutumia viwango (rates) ambavyo si sahihi na kushindwa kukusanya taarifa za matumizi ya maji. Matatizo mengine ni pamoja na kushindwa kutambua wateja wao hali ambayo inasababisha</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Menejimenti ya Mamlaka za Maji husika zinapaswa kutambua wateja wao; • Kuharakisha zoezi la kuwafungia wateja mita za maji ili kuwa na mapato sahihi ya maji; • Menejimenti ya Mamlaka za Maji zinapaswa kuhakikisha kuwa ni wateja halali tu ndio wanaopeleke 	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji

	<p>kuwadai kidogo au zaidi ya matumizi halisi ya maji. Athari za udhaifu huu ni kutokuwepo na kumbukumbu sahihi na kulimbikiza madeni ambayo hayakusanyiki.</p> <p>Mbali na hayo kumekuwepo na upotevu mkubwa wa maji safi (treated water) katika kila Mamlaka za Maji ambayo ni zaidi ya kiwango kinachokubalika cha upotevu wa maji. Tatizo hili limesababisha Mamlaka nyingi za Maji kuwa na matokeo mabaya ya uendeshaji wa mamlaka zao.</p>	<p>wa bili za maji;</p> <ul style="list-style-type: none"> Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapaswa kusaidia Mamlaka za Maji katika kuboresha mifumo yao ya Ankara kwa kushauri ununuzi na uwekaji wa mifumo ya kompyuta ya utoaji Ankara “software billing package” inayofaa na itumike kwa Mamlaka zote za Maji. Hili lifanywe sambamba na mafunzo ya utumiaji wa mifumo ya kompyuta ya utoaji ankara itakayopende kezwa. 		
8.	<p>10.8 Usimamizi wa Mikataba</p> <p>Ukaguzi wa mikataba ya kisheria iliyoingiwa na baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ulibaini udhaifu mkubwa.</p>	<ul style="list-style-type: none"> Vitengo vya usimamizi wa Ununuzi na bodi za zabuni zinapaswa zihusishwe kwenye kuandaa mikataba ya ununuzi; 	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji

	<p>Udhaifu huo umesababisha kuwepo na matatizo ya kimikataba na kesi nyingi ziko mahakamani ambazo zinaweza kusababisha tozo kubwa kwa mamlaka husika.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Vitengo vya usimamizi wa Ununuzi na bodi za zabuni zinapaswa kuboreshwa ili kuweza kusimamia mikataba kikamilifu; na • Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinapaswa kutunza madaftari ya mikataba 		
9.	<p>10.9 Usimamizi wa Rasilimali</p> <p>Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo hazina hati miliki za majengo, utaratibu mbovu wa kutunza kumbukumbu, mali kupewa thamani ndogo au kubwa, kutokuthamini (non valuation) mali kwa muda mrefu na kutokufanya “impairment test” kwa kipindi kilichoshauriwa na miongozo ya kimataifa ya fedha na mali.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kumbukumbu za mali za kudumu zinazohamishi ka zinapaswa kuingizwa vitabuni, kuwekwa dhahiri kwenye hesabu za fedha na kuwa “accounted for”; • Hati miliki za majengo na mali nyinginezo zinapaswa kuhifadhiwa vizuri; • Uthamini wa mali (revaluation) unapaswa 	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji

		<p>kufanywa na “impairment test” za mali unafanywa katika muda uliopendekezwa na kukubalika na miongozo ya fedha na mali;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Menejimenti ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinapaswa kuhakikisha mara kwa mara kuwepo (physical existence) na kuwa na uhakika wa hali ya mali zao; na • Utunzaji wa kumbukumbu za mali unapaswa kuboreshwa. 		
10.	<p>10.10 Kutokurejehwa kwa mikopo llibainika kuwa kiasi kikubwa cha fedha kilichokuwa kimekopeshwa kwa wateja na baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo hakikuwa kimerejeshwa hata baada ya tarehe walizokuwa wamekubaliana.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinapaswa kuchukua hatua madhubuti ya kukusanya kiasi cha fedha ambacho hakijarejeshwa • Sera za ukopesaji 	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji

		ziangaliwe na kuboreshwa.		
11.	10.11 Kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zina mifumo hafifu ya usimamizi wa fedha. Kwa ujumla udhaifu uliobainishwa ni pamoja na kutokupeleka makato ya kisheria (statutory deductions) kwenye mamlaka husika, udhaifu katika usimamizi wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa (Debtors) na kutokulipa madeni ya wadai (Creditors) pamoja na ukosefu wa miongozo muhimu ya fedha (Financial Manuals).	<p>Kutokana na udhaifu uliotajwa hapo juu, nashauri yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Menejimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo zinapaswa kuhakikisha kuwa zinazingatia matakwa ya Sheria kwa kuwasilisha makato ya kisheria kwenye mamlaka husika na kuhakikisha mifumo ya kudhibiti fedha inafanya kazi ipasavyo. • Wadaiwa na wadai waangaliwe kwa makini ili kulinda mali za umma na kuimarisha heshima ya Shirika/Taasisi husika kwa wadau. 	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji
12.	10.13 Matokeo ya Ukaguzi Maalumu-TANESCO	<ul style="list-style-type: none"> • Sheria inayosimamia Ununuzi wa 	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji

	Wakati wa ukaguzi maalumu wa TANESCO iligundulika kwamba, mzigo mkubwa wa madeni ya TANESCO umesababishwa na mikataba mbalimbali ya ununuzi wa umeme ambayo kwa kiasi kikubwa iliingiwa bila kufuata Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake	Umma inapaswa kufuatwa wakati wa kuingia mkataba wowote unaoihusu TANESCO. • Serikali ipunguze kuingilia uendeshaji wa TANESCO ili uongozi wake uwajibike ipasavyo.		
13.	10.14 Tozo (Liquidated damages) kutoka kwa M/s Dowans Holdings Ukaguzi wa mkataba wa makubaliano wa “Power-Off Agreement” ulibaini kuwa kampuni ya kuzalisha/kufua umeme ya M/s Dowans Holdings ilishindwa kuzalisha umeme wote wa 100MW kama ilivyokuwa imeingia mkataba wa makubaliano na TANESCO.	Menejimenti ya TANESCO inapaswa kuhakikisha kuwa tozo inalipwa na M/s Dowans Holdings kwa kuchelewa kuzalisha/kufua umeme kama inavyotakiwa na kifungu cha mkataba. Endapo mlipaji atachelewa kulipa tozo hiyo, alazimike kulipa faida kwa kuchelewa kulipa fedha hizo.	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji
14.	10.17 Kuongeza kipindi cha Mkataba wa makubaliano kinyume na Sheria	Serikali inapaswa kutengua/kubatili sha/kufuta nyongeza ya muda wa	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji

	<p>Kitengo cha Makontena cha Mamlaka ya Bandari ya Tanzania kilikodishwa kwa mwendeshaji binafsi “M/s Tanzania International Container Terminal Services” tangu mwezi wa tano mwaka 2000. Mkataba wa ukodishaji ungedumu kwa kipindi cha miaka kumi kwa makubaliano ya awali. Hata hivyo, mkataba huo uliongezewa muda wa kipindi kingine cha miaka 15 kwa Nyongeza Na. 2 (Addendum) ya mkataba wa ukodishaji uliofanyika tarehe 30.12.2005 na kufanya kipindi cha mkataba wa ukodishaji kuwa miaka 25. Kwa maoni yangu kulikuwepo na ukiukaji wa taratibu na uvunjaji wa Sheria ya Ununuzi pamoja na kifungu Na. 9.1 cha Mkataba husika.</p>	<p>mkataba wa TICTS na kufanya upembuzi yakinifu wa mkataba wa kipindi cha miaka kumi ya awali kabla ya kuamua kuongeza kipindi cha Mkataba. Endapo kutakuwepo na haja ya kuongeza mkataba, Serikali inashauriwa kufuata taratibu na Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake.</p>		
--	---	--	--	--

15.	<p>Kutowasilisha makato ya kisheria Katika kipindi cha mwaka unaohusika Mashirika ya Umma 5 yalishindwa kuwasilisha makato ya kisheria yenye jumla ya Sh.29,336,119,602 kwa mamlaka husika. Kati ya kiasi hicho, makato yasiyowasilishwa (PPF, NSSF na PSPF) yalifikia Sh.23,643,858,878 wakati makato ya kodi yalifikia Sh.2,210,703,119. Zaidi ya hayo, Shirika la Posta lilishindwa kuwasilisha makato ya kisheria yenye jumla ya Sh.6,613,707 (Makato ya Bima ya wafanyakazi) na Sh.196,741,985 (Makato yanayohusu mikopo ya SACCO'S) wakati Bodi ya Biashara ya Nje (Board of Exernal Trade) imeshindwa kuwasilisha makato ya kodi ya viwanja (land Rent) yenye kiasi cha Sh.142,859,539.</p>	<p>Menejimenti za Mashirika ya Umma zinashauriwa kuhakikisha makato ya kisheria yanapelekwa kwa mamlaka husika ili kujiepusha na tozo zinazoweza kutozwa kwa Mashirika husika kwa kushindwa kuwasilisha makato ya kisheria kwa wakati unaotakiwa</p>	Hakuna majibu	Hakuna utekelezaji
-----	--	--	---------------	--------------------

3.2 Mambo Maalum Ambayo Hayajatekelezwa
 Napenda pia kutoa angalizo kwa Serikali juu ya mambo yaliyokuwepo kwenye ripoti za Mashirika na Taasisi

nyinginezo ambayo yanahitaji kutekelezwa kwa uboreshaji wa Mashirika na Taasisi zifuatazo:

3.2.1 Shirika la Posta Tanzania

Kugawa Mali na Madeni ya Lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania

Kazi ya kugawa mali za lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania (TP&TC) na Shirika la Posta (TPC) ilikuwa inaendelea na bado haijakamilika hadi tarehe 31 Disemba, 2007.

Tunashauri kwamba menejimenti ya Shirika la Posta iendelee kufuatilia toka kwa mamlaka husika ugawaji wa mali na madeni ya lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania

Kukosekana kwa Hati Miliki

Mali za Shirika zilizoripotiwa kuwa na jumla ya Sh.62,400,000 hadi tarehe 31 Disemba 2007 hazikuwa na hati miliki. Kwa kukosekana kwa hati miliki, wakaguzi hawakuweza kuthibitisha usahihi na uhalali wa umiliki wa mali hizo. Hata hivyo, ufuatiliaji wa kupata hati zilizosalia uko kwenye hatua nzuri. Orodha ya mali za Shirika ambazo hazikuwa na hati miliki inaonyesha kuwa mali hizo ziko Kondo, Muleba, Ifunda na Zanzibar.

Madai ya Wastaafu wa Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Wastaafu Wengine

Tunatambua kuwa Serikali imeahidi kutenga kiasi cha shilingi bilion 8.2 katika mwaka wa fedha 2008/2009 kwa ajili ya kulipa mafao ya waliokuwa waajiriwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uongozi wa Shirika la Posta unashauriwa uendelee kufuatilia Serikalini ahadi hiyo ili kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana kama ilivyoahidiwa.

Vilevile, kama ilivyoelezwa kwenye ripoti zetu za nyuma, mpango wa deni la mafao ya wastaafu uliandaliwa na kuingizwa vitabuni, lakini madeni hayo hayajatengewa fedha na Shirika. Hakuna michango iliyotolewa na Shirika

na kuwekwa kwa Mdhadini kisheria kwa ajili ya kulipa wanachama watakapostaafu. Matokeo yake ni Shirika kulipa mafao ya wafanyakazi wanaostaafu kwa kutumia fedha ambazo hazikutengwa kwa matumizi hayo. Zaidi ya hayo, tuliona kuwa uhasibu uliotumika kwa madai ya wastaafu haukuwa unakubaliana na sera za kahasibu (policies) na IAS 19 kwani;

- (i) Utaalam haukuwepo wa kukadiria na kujua kiasi halisi cha stahili ya kustaafu ya watumishi kwa sasa na wakati uliopita.
- (ii) Thamani ya sasa ya kiasi cha mafao yaliyoelezewa hayakuweza kujulikana kwa kuwa tathmini ya kujua thamani halisi haikutaja kiwango cha riba (interest rate).
- (iii) Thamani (actuarial) ya ongezeko au hasara zilizoonyeshwa kwenye Hesabu haikuweza kujulikana. Matokeo yake ni kuwa, deni linalohusu madai ya pensheni katika hesabu, ambalo limezidi malipo kwa kiasi cha Sh.737,678,508, halikuweza kupimwa kwa usahihi kwa kukosekana kwa hesabu zilizotayarishwa na mtaalam wa kutathimini mafao ya kustaafu (Actuarial valuer).

3.2.2 Shirika la Bima la Taifa

Matatizo ya Vifaa na Programu za Teknolojia ya Mawasiliano (Hardware and Software)

Shirika linatumia mfumo wa zamani wa Kompyuta wa "Informax" ulioanza kutumika mwaka 1993. Mfumo huu haujapata kuboreshwa tangu uzinduliwe. Hali hii imesababisha mfumo kutoa huduma kwa kiwango cha chini na kutoa taarifa zisizoaminika. Kumekuwa na tatizo la kutoweza kufanya kazi mara moja kwa mwezi hasa sehemu ya mfumo wa kutoa taarifa.

Uhifadhi na uwezo wa kupata taarifa zinazoweza kupotea kutoka kwenye mfumo wa kompyuta hasa upande wa kuhifadhi kumbukumbu pale patokeapo tatizo ambapo huchukua muda mrefu hata kwa siku tatu na kufanya kazi

nyingine zisimame au kufanyikia sehemu nyingine. Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kuweza kupata taarifa kumeleta matatizo mengi ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

- (a) Uhakiki na uwekaji wa kumbukumbu na taarifa nyingine hufanywa kwa mikono
- (b) Kanda toka kwenye matawi kwa ajili ya kutoa taarifa huhakikiwa kwa mikono
- (c) Kuingiza kanda zisizo sahihi kwenye kumpyuta

Kutenganisha utengenezaji wa taarifa kati ya Makao Makuu na Matawi (decentralisation) umesababisha matatizo mengi kama ifuatavyo:

- Taarifa zisizo kuwa sahihi kati ya makao makuu na kwenye matawi,
- Udhhibiti hafifu katika kuandaa kanda na kuzituma makao makuu,
- Udhhibiti hafifu katika kupeleka taarifa za kanda, na
- Udhhibiti hafifu katika kutunza kanda za mawasiliano makao makuu.

3.2.3 Hospitali ya Taifa Muhimbili

Wakati wa kufanya ukaguzi wa mali za Hospitali ya Taifa Muhimbili tuliona jengo moja lililojengwa ndani ya eneo la Shirika ambalo linamilikiwa na mtu binafsi.

Utawala wa Shirika ulieleza kuwa, mtu mmoja aitwaye Mr. H.A. Kiluvia aliwasiliana na Utawala wa kilichokuwa Kituo cha Afya Muhimbili ili ajenge jengo la biashara ambalo kwa sasa ndipo ilipo Benki ya NMB (National Micro Finance Bank), duka la Dawa, hotel na maduka mengine ya biashara.

Nakala ya mkataba kati ya kilichokuwa Kituo cha Afya Muhimbili na Mr. H.A. Kiluvia ulisainiwa tarehe 11 Aprili

1987. Mpangaji (H.A. Kiluvia) alitakiwa atumie jengo kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia tarehe 22 Disemba 1987.

Mkataba umeshamalizika lakini jengo hilo bado liko kwenye himaya ya Mr. H.A. Kiluvia kinyume na makubaliano ya mkataba

3.2.4 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

Mikopo Isiyorejeshwa

Kama ilivyokuwa imeripotiwa kwenye ripoti zetu zilizopita, baadhi ya wanaofaidika na mikopo ya vitega uchumi hawatekelezi masharti ya mikopo. Hususani kutokulipa fungu la deni (instalments) kama ilivyo kwenye jedwali la malipo na hivyo kusababisha limbikizo la riba ambayo haijalipwa. Mchanganuo wa mikopo hiyo ni kama ifuatavyo:

Jina la Mkopaji	Tarehe ya Mkopo	Kiasi cha Mkopo (Sh.)	Limbikizo la riba hadi tarehe 30/6/2008 (Sh)	Jumla ya mkopo na riba hadi tarehe 30/6/2008 (Sh.)	Maelezo
New K'manjaro Bazaar	03. 4.1990 26. 8.1991 na 07.09.1992	99,445,000	750,849,846	850,294,846	Hatua za Kisheria zimechukuliwa
Mbowe Hotel Ltd	10.03.1990	7,500,000	229,898,516	237,398,516	Ilikuwa ilipwe yote kufikia Disemba, 1997. Hatua za Kisheria zimechukuliwa. Shilingi milioni 50 zimelipwa.
Kagera Sugar Company Ltd	11.02.2003	12,000,000,000	5,624,290,000	17,624,290,000	Marejesho ya mkopo kuanza mwezi Septemba, 2004, makubaliano ya mkopo yalibadili-

					shwa, makubaliano mapya hayakuletwa kwa ajili ya ukaguzi
General Tyre East Africa	08.02.2005	11,610,000,000	1,892,430,000	13,502,430,000	Tarehe za marejesho ni kama ifuatavyo:- Riba (interest)- 31.12.05 Mkopo- 30.03.07 Mbali na 85% ya dhamana ya Serikali, dhamana iliyotengwa kama mapato ya baadae, ilifikia \$3,398,551.55 kwa tarehe ya makubali-ano. Hata hivyo, mbali na kiasi hicho hapo juu, \$1,465,837.60 zilifikiriwa kutokulipwa tena na kufutwa vitabuni.
KATANI LTD	06.11.2006	4,295,700,000	794,520,000	5,090,220,000	Marejesho yalitakiwa kuanza kama ifuatavyo:- Riba (Interest)- Disemba, 06 Mkopo- Disemba, 07
Continental Ventures	15.09.2005	4,063,500,000	900,322,411	4,963,822,411	Marejesho yalitakiwa kuanza kama ifuatavyo:- Riba (Interest)- Disemba, 06 Mkopo- Disemba, 07
EMUNIO Tanzania	07.10.2004	1,683,450,000	86,639,625	1,770,089,625	Marejesho yalitakiwa

Limited					kuanza kama ifuatavyo: Riba- 30.06.2006, Mkopo- 30.05.2006
Kiwira Coal & Power Company Limited	05.07.2007	8,127,000,000	840,450,000	8,967,450,000	Marejesho yalitakiwa kuanza kama ifuatavyo: Riba- Januari, 2008 Mkopo- Januari 2008
Tanzania Portland Cement Company	Novemba 2007	5,456,700,000	295,099,404	5,751,799,404	Marejesho yalitakiwa kuanza kama ifuatavyo: Riba Juni, 2008 Mkopo- Disemba, 2008
Jumla		47,343,295,000	11,414,499,802	58,757,794,802	

Licha ya juhudi za menejimenti kufuatilia urejeshwaji wa mikopo hiyo, kwa maoni yetu baadhi ya mikopo hiyo na limbikizo la riba ulipwaji wake ni wa shaka. Hii inaashiria kuwa kiasi cha mikopo hiyo kilichoripotiwa ni kikubwa kuliko inavyotakiwa ikiwa na jumla ya shilingi 58,757,794,802. Tunashauri kuwa mali zote ambazo hazizalishi zirekebishwe kama inavyotakiwa na viwango vya uhasibu vya kimataifa (IAS 39. para 59) ili kuripoti thamani halisi ya mali hizo na baadae uongozi uchukue hatua za ukusanyaji.

Dhamana ya Mikopo

Mkopo Uliotolewa kwa Benki ya Azania bila Dhamana Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ulitoa mkopo wa shilingi bilioni 4 kwa Benki ya Azania. Baada ya kupitia mkataba wa mkopo huo ambao ulisainiwa tarehe 9 Julai 2007 hatukuona kipengele kinachoonyesha kuwa mkopaji ameweka dhamana ya kufidia endapo atashindwa kulipa. Kifungu cha 2.4.1 cha mwongozo wa mfuko juu ya mikopo ya vitegauchumi kinaeleza kuwa dhamana kwa vitegauchumi vya mikopo lazima ziwe mali zisizohamishika ambazo

zinaweza kuuzika kwa haraka ili kufidia hasara endapo mkopaji atashindwa kulipa. Tunashauri uongozi kupitia upya mkopo uliotolewa kwa benki ya Azania ili kuhakikisha kuwa sera ya mikopo inafuatwa.

Mkopo Uliotolewa kwa M/s Kiwira Coal na M/s Power Co. Ltd.

Mkopo wa muda mfupi wa Dola za Kimarekani 7,000,000 ulitolewa kwa Kiwira Coal and Power Ltd ambao ungelipwa ndani ya kipindi cha miezi sita. Mkataba ambao ulisainiwa tarehe 10 Julai 2007, hauelezi bayana dhamana ya mkopo huo zaidi ya kueleza kwenye kifungu cha 10.5 kuwa majengo yote na biashara lazima yawekewe bima. Hata hivyo, hati miliki ya mali iliyowekwa dhamana haikutolewa kinyume na Kifungu cha 2.4.1 cha mwongozo wa Mfuko juu ya vitegauchumi. Pia ilielezwa kuwa mkopo ulidhaminiwa na Serikali kwa 75% na benki ya CRDB kwa 100% lakini makubaliano ya dhamana hizo hayakutolewa wakati wa ukaguzi. Mpaka tarehe 30 Juni 2008 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ulikuwa unadai riba inayofikia kiasi cha Shilingi 840,450,000 lakini si riba wala mkopo wa msingi ambao umelipwa japo muda wakurudisha mkopo ulikwishapita kwa zaidi ya miezi sita.

Mkopo Uliotolewa kwa M/s Medtech

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uliikopesha kampuni ya M/s Medtech kiasi cha Shilingi 1,525,368,425 mnamo tarehe 30 Aprili 2003 kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo ifikapo mwezi Disemba 2004. Timu ya ukaguzi iliambiwa kwamba tarehe ya kurejeshwa kwa mkopo huo ilibadilika na mdeni alitakiwa kuanza kurejesha mkopo huo kuanzia tarehe 30 Juni 2006. Hata hivyo, timu ya ukaguzi haikupatiwa mkataba wa makubaliano wa kubadilisha kipindi cha marejesho ya mkopo huo.

Zaidi ya hayo, kwa hivi sasa Mfuko unafanya mawasiliano na M/s Emunio Tanzania Ltd kama mkopaji badala ya M/s

Medtech kuhusu marejesho ya mkopo huo. Uhalali wa kisheria wa M/s Emunio Tanzania Ltd kuwa mdaiwa badala ya M/s Medtech haukuweza kufahamika kutokana na wakaguzi kutokupatiwa nyaraka za mabadiliko hayo

SURA YA NNE

USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI

4.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea usimamizi wa mapato na matumizi katika Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma ambazo pia zimeelezewa kwa undani kwenye barua za menejimenti kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Mambo ambayo yanafanana kwa Mashirika na Taasisi zote yamewekwa pamoja. Vipengele ambavyo vinajitegemea vimeelezewa chini ya vichwa vya habari kwenye Mashirika na Taasisi husika.

4.1 Usimamizi wa Matumizi

4.1.1 Malipo Yaliyofanywa kwa Wazabuni Kabla ya Huduma

Kanuni ya 122(1) chini ya kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2005 (GN.97) inaitaka Taasisi inayonunua kulipia huduma baada ya kupata huduma na kuridhishwa na ubora wa huduma hiyo. Hata hivyo ilibainika kwamba Taasisi za TANAPA, TPA, na MWAUWASA zilifanya malipo ya jumla ya Shilingi 146,024,582 kwa wazabuni mbalimbali kabla ya kupata huduma kinyume na kanuni hiyo. Uongozi wa Taasisi husika ni lazima zifuate na kuheshimu taratibu za matumizi ya fedha za umma.

4.1.2 Malipo Yenye Nyaraka Pungufu

Ukaguzi wa taarifa za hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2008 ulibaini malipo ya Shilingi 1,605,899,198 na Dola za Kimarekani 10,700 yenye nyaraka pungufu. Kanuni zinaeleza kuwa malipo yanayofanywa bila nyaraka muhimu yatajulikana kama malipo yasiyo na nyaraka kabisa (unvouched expenditure).

Mashirika na Taasisi zilizofanya malipo yenye nyaraka pungufu ni kama ifuatavyo :

Na.	Jina la Taasisi	Kiasi (sh)	Maelezo
1.	TANAPA	219,993,790 na Dola za Kimarekani 10,700	Malipo mbalimbali kwa wazabuni na watoa huduma
2.	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	466,255,884	Malipo mbalimbali kwa wazabuni waliotoa huduma TBC kipindi cha mwaka husika
3.	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma	43,700,000	Malipo yaliyofanywa kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ambayo hayana orodha na saini za walipwaji
4.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii	624,484,416	Malipo mbalimbali kwa wazabuni na watoa huduma
5.	Soko la Hisa la Dares salaam	25,948,111	Malipo kwa ajili ya posho za safari, ada za kozi, ada za michango na gharama za semina mbalimbali
6.	Shirika la Utangazaji Tanzania	525,621,221	Movement of letter of credit transactions
7.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	310,870,450	Malipo kwa wazabuni ambayo hayana hati za madaai (invoices)
8.	Mamlaka ya maji safi na maji taka - Mwanza	24,675,000	Malipo ya posho ambazo hazipo kwenye miongozo

4.1.3 Malipo Yenye Shaka

(i) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umekuwa ukilipa bonasi kwa wafanyakazi ambao wanasajili wanachama wa mfuko. Hata hivyo, shughuli zilizokuwa zikifanywa na wafanyakazi hao mpaka walipwe bonasi hazikuelezwa. Pia haikuelezwa ni kwa vipi wafanyakazi wa idara zingine kama za kompyuta, fedha na ugavi walistahili posho hizo wakati hawahusiki moja kwa moja na usajili wa wanachama. Japo tuliitisha sera inayotumika kulipa bonasi lakini sera hiyo haikutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Kutokana na utata huu, malipo ya bonasi yanayofikia Shilingi 74,357,526 yana mashaka.

(ii) Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

Tumebaini wakati wa ukaguzi kwamba kampuni ya Dowans Holdings iliwapa TANESCO hati ya malipo Na. EFD 786675 ya tarehe 17 Novemba 2006 ikitaka kurudishiwa kiasi cha Dola za Kimarekani 4,865,000 ilichotumia kama gharama za usafiri wa ndege wakati wa kusafirisha mitambo ya umeme na vifaa vingine kuja Dar es salaam.

Kulingana na maelezo ya uongozi, malipo yalifanywa baada ya timu ya muafaka kati ya Serikali na Dowans kama ilivyoandikwa kwenye muhtasari wa kikao kilichofanyika tarehe 8 hadi 15 Juni 2006. Hata hivyo, muhtasari wa kikao hicho hauielezi bayana ni nani wa kulipa gharama hizo. Hivyo, inaonekana kuwa Serikali ililipa gharama hizo kimakosa.

Menejimenti inashauriwa ichunguze uhalali wa malipo haya na kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kudai fedha hizo kama itaonekana kuwa zililipwa kimakosa.

4.1.4 Malipo ya Bima ya Majengo ya Benki Kuu ya Tanzania

Malipo yalifanywa kwa ajili ya bima ya majengo ya makao makuu ya Benki kuu ya Tanzania lakini benki inakosa ushahidi wa kutosha kama vile hati ya bima na nyaraka nyingine zinazoonyesha uhalali wa malipo hayo. Vilevile malipo yaliyotozwa na wakala wa bima yanaonekana kuwa makubwa na hakuna misingi inayoonyesha namna malipo yalivyofikiwa. Nina mashaka na makato ya bima yaliyolipwa kwa wakala kwa kuwa hayana vidhibiti vya kutosha vinavyohusiana na bima na pia inawezekana benki imelipa zaidi kutokana na kutumia viwango visivyo sahihi.

4.1.5 Malipo yaliyolipwa Zaidi ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Mkandarasi

(i) Chuo Kikuu Kishiriki cha Ualimu cha Dar es salaam Tuligundua kuwa baadhi ya wakandarasi walipewa malipo ya awali wakati wanaanza ujenzi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba yao. Malipo haya ya awali yalipunguzwa kwenye malipo yaliyofuatia. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa ilikuwa zaidi ya kiasi kilichotakiwa kulipwa kama inavyoonyeshwa hapa chini :

Maelezo	Shilingi
Hati ya madai (Certificate)	229,896,093.00
Ongeza : Malipo ya awali	<u>93,100,833.00</u>
Jumla ndogo	322,996,926.00
Toa : Makato ya malipo ya awali	<u>27,930,250.00</u>
Jumla iliyotumiwa kupata VAT	295,066,676.00
VAT 20%	<u>59,013,335.00</u>

Malipo hayo hapo juu yalifanywa kwa ESTIM Construction (T) Ltd ambapo kiasi sahihi cha VAT kilichotakiwa kukatwa ni kama ifuatavyo :

Hati ya madai (Certificate)	sh 229,896,093.00
20% VAT	sh 45,979,218.00

Kiasi kilicholipwa zaidi ni shilingi 13,034,116
(59,013,335-45,979,218) hakikutolewa maelezo ya kutosha.

4.1.6 Fidia Iliyolipwa Na TANAPA kwa Wanakijiji wa Usangu Ambayo Haikupokelewa Shilingi Bilioni 5.9

TANAPA ililipa kiasi cha shilingi bilioni 5.9 kama fidia kwa wanakijiji wa Usangu lakini hakuna ushahidi unaoonyesha kama kiasi kilicholipwa kilipokelewa na wanakijiji husika. Zaidi ya hayo, Baraza la Mawaziri kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii liliagiza TANAPA kulipa wanakijiji hao kiasi cha shilingi bilioni 4.28 kama fidia kufuatia kijiji hicho kujumuishwa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kulingana na maelekezo ya Baraza la Mawaziri, fidia hiyo ilitakiwa kulipwa kulingana na Sheria ya ardhi ya kijiji ya mwaka 1999. Hata hivyo, mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2008 TANAPA walikuwa wamelipa jumla ya shilingi bilioni 5.9 kama fidia kinyume na maagizo na hakuna ushahidi kama kiasi cha shilingi bilioni 1.62 kilicholipwa zaidi kiliidhinishwa na Baraza hilo au Bodi ya Wadhamini ya TANAPA. Bila kuwepo na ushahidi wa mapokezi ya fedha hizo, hatukuweza kuthibitisha kama kiasi kilicholipwa kilipokelewa na walengwa.

4.2 Usimamizi wa Maduhuli

Kanuni ya 78 ya kanuni za fedha za umma inataka makusanyo yote yapelekwe benki kila siku au kwa muda ambao utaonekana ni mzuri zaidi. Ukaguzi wa mkusanyo ya maduhuli na taratibu za kupeleka benki kwenye Taasisi mbalimbali umebaini ucheleweshaji wa kupeleka makusanyo benki bila maelezo ya kutosha uliofanywa na Mashirika yafuatayo:

4.2.1 Shirika la Utangazaji Tanzania

Ukaguzi wa ofisi ya fedha ya Shirika la Utangazaji Tanzania uligundua kuwa makusanyo hayapelekwi benki kwa wakati kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za fedha za Shirika hilo. Kanuni hizo zinataka makusanyo yote yapelekwe benki siku yanapokusanywa au siku inayofuata. Kinyume na kanuni zilizowekwa, ukaguzi umegundua kuwa kwa nyakati tofauti mtunza fedha amekuwa akibaki na fedha za makusanyo kwa

takribani siku 45 bila maelezo ya kutosha. Utaratibu huu unakaribisha matatizo mengi ikiwa ni pamoja na uwezekano wa fedha kuibiwa au kupotea.

4.2.2 Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania

Ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) hususan vituo vya mikoani umegundua kuwa fedha hupokelewa na makarani ambao pia huingiza fedha hizo kwenye vitabu vya fedha. Makarani hao pia hutengeza ripoti za makusanyo ya kila siku. Hata hivyo, haijulikani kama yanahakikiwa na mtu mwingine kuhakikisha usahihi wake. Vilevile ilibainika kwamba baadhi ya makusanyo yaliyofanywa na vituo hivyo yamekuwa yakichelewa kupelekwa benki kwa kipindi kinachozidi mwezi mmoja. Hii ni kinyume na sera za Mamlaka ambazo zinawataka mameneja kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanapelekwa benki mara tu baada ya kupokelewa. Ukosefu wa mfumo imara wa usimamizi wa fedha unaweza kuchangia wizi wa fedha ambazo hazijapelekwa benki.

4.2.3 Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO)

Menejimenti ya TEMDO imekuwa haipeleki makusanyo benki kwa wakati au kupeleka pungufu na kutumia kiasi kinachobaki kwa matumizi ya ofisi ya kila siku kama ifuatavyo:

Tarehe	Na ya Stakabadhi	Kiasi kilichopokelewa TEMDO	Kiasi kilichopelekwa benki	Tofauti
15.08.2007	12365	302,200	252,000	50,200
09.10.2007	12391	24,000	2,000	22,000
29.10.2008	12509	900,000	606,56	293,434
Total		1,226,200	860,566	365,634

Nasisitiza menejimenti iwe inapeleka makusanyo yote benki na kwa wakati unaotakiwa.

4.3 Hoja Maalum kwa Kila Shirika

4.3.1 Shirika la Utangazaji Tanzania

(i) Ukosekanaji wa Kumbukumbu za Ukusanyaji wa Maduhuli

Kwa ujumla Idara ya Masoko imeshindwa kuweka kumbukumbu za maombi ya matangazo ya biashara yaliyopokelewa (Broadcasting Commercial Orders). Kwa mfano idara haikutengeza mchanaganuo wa maombi ya matangazo kwa kila mwezi ambayo yaliyopokelewa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008. Pia tulibaini tofauti ya shilingi 2,217,323,619 kati ya kumbukumbu za idara ya masoko na zile za idara ya uhasibu kama ifuatavyo:

Makusanyo kulingana na kumbukumbu za Idara ya Uhasibu (Sh)	Makusanyo kulingana na Idara ya masoko (Sh)	Tofauti (Sh)
6,302,213,023	4,084,889,404	2,217,323,619

Hapakuwepo na maelezo ya kutosha kutoka kwa manajementi kuelezea tofauti zilizojitokeza kati ya taarifa zilizotolewa na Idara hizo.

Uhakiki uliofanywa kwenye muhtasari wa vikao vya bodi za wakurugenzi uligundua kuwa maombi ya matangazo na ripoti ya makusanyo havikutengenezwa na kuletwa kwa ajili ya kujadiliwa. Pia tuligundua kuwa kitengo cha kuandaa vipindi hakitoi taarifa ya vipindi na matangazo ya biashara yaliyoandaliwa. Kukosekana kwa taarifa hizo kunafanya kushindwa kubaini usahihi wa maduhuli yaliyokusanywa na Shirika kwa kipindi kilichoishia tarehe 30/6/2008.

(ii) Hati za Punguzo Zisizoidhinishwa

Katika kipindi cha ukaguzi husika, tuligundua kuwa Shirika la Utangazaji Tanzania lilitoa hati za punguzo (credit notes) za Shilingi 60,270,800 ambazo ziliingizwa kwenye leja kuu

(general ledger) bila kuthibitishwa na mtu aliyeidhinishwa na Shirika. Kulingana na kifungu cha 5.2.5.2 cha kanuni za fedha za Shirika la Utangazaji Tanzania, hati za punguzo zote lazima ziidhinishwe na Mkurugenzi wa Fedha na Ugavi au Meneja wa fedha. Hati za punguzo zilizotolewa kinyume na taratibu zinaweza kusababisha upotevu wa makusanyo na kutozingatia kanuni na taratibu za Uhasibu zilizowekwa na Shirika.

4.3.2 Ukosefu wa Usalama wa Makusanyo katika Chuo cha Ustawi wa Jamii

Kulingana na Kanuni ya 57(1) ya Kanuni za Fedha za Umma, Afisa Masuuli atawajibika kwa kuhakikisha kuwa usalama wa kutosha upo na unatumika kwa makusanyo ya maduhuli na fedha zingine za Umma. Kuhakikisha kuwa Kanuni hii inafuatwa, Afisa Maduuli anatakiwa ahakikishe kuwa ofisi ya mtunza fedha ina usalama wa kutosha. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wetu tulibaini kuwa Chuo cha Ustawi wa Jamii hakina ofisi ya mtunza fedha badala yake mtunza fedha anakaa kwenye ofisi ya uhasibu ambayo inatumikiwa na mafisa wengine ambapo anapokelea fedha tasilimu na hundi.

4.3.3 Ukosefu wa Sehemu Maalum ya Kutunzia Nyaraka katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tukuyu

Kanuni ya 151 ya Kanuni za Fedha za Umma inataka nyaraka zote zenye thamani ambazo hazijatumika zitunzwe kwenye chumba cha hazina au sanduku maalum la fedha. Uhakiki uliofanywa kwenye Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Tukuyu uligungua kuwa vitabu 30 vya makusanyo havikuwepo kwenye ofisi ya mamlaka na vingine 80 vilionekana vimeifadhiwa kwenye kabati la kawaida na kulikuwa hakuna kumbukumbu kwenye rejista ya nyaraka (counterfoil register). Ukaguzi haukuweza kubainisha mara moja kiasi cha maduhuli yaliyokusanywa kwa kutumia vitabu vilivyokosekana.

4.3.4 Shirika la Umeme Tanzania

(i) Tofauti Kwenye Kumbukumbu za Makusanyo
Wakati wa ukaguzi niligundua tofauti kati ya mapato yaliyoripotiwa kwenye ripoti ya makusanyo ya kila mwezi na kiasi kilichopo kwenye leja kuu kama ifuatavyo :

Maelezo	Michango ya Walaji Cow's	Michango ya Walaji SLO's	Mapato Mengineyo
Jumla kulingana na ripoti ya mwezi iliyotumwa makao makuu	123,378,144	355,509,564	73,173,455
Bakaa kulingana na leja kuu	233,616,208	712,362,570	68,948,057
Tofauti	109,234,064	356,853,006	4,225,398

Japo tofauti hiyo imeelezwa kuwa inatokana na makosa katika utengenezaji wa ripoti za kila mwezi, menejimenti inashauriwa kuhakikisha kuwa ripoti hizi zinatengenezwa kwa usahihi zaidi ili kutoa picha halisi ya utendaji wa kampuni.

(ii) Kuchelewa Kukusanya Madeni na Kutopeleka Hati za Madai

Iligundulika kuwa baadhi ya Taasisi za umma zina matatizo ya kukusanya maduhuli kwa wakati. Matatizo haya yanatokana na kuchelewa kutuma hati za madai kwa wateja na upungufu wa wafanyakazi katika kitengo cha mauzo. Mifano michache imeonyeshwa kwenye ripoti ya ukaguzi (Management Letter) iliyotumwa TANESCO.

(iv) Kutosoma Mita za Wateja

Tumegundua kuwa kwa mwezi Disemba 2007 mita za wateja wakubwa hazikusomwa, na hati za madai zilizopelekwa kwa wateja wafuatao zilikuwa zimekadiriwa :-

Jina	Na. ya Mteja
Tradeco Oil Industry	51036253
Agro Processiding and Allied	51036225
M/s Superstar Fowarders	51036224
M/s UCLAS	51056618

Hii ni ishara kuwa makusanyo ya mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2007 yatakuwa hayana usahihi unaotarajiwa.

(v) Ucheleweshaji wa Kupeleka Hati za Madai kwa Wateja Wapya

Tuligundua kuwa wateja wapya waliounganishiwa umeme kwa mara ya kwanza walitumiwa hati za madai baada ya miezi miwili au zaidi kama ifuatavyo :-

Mteja	Mita Na.	Tarehe ya kuungani-shwa	Hati ya madai ya kwanza
Vodacom (T) Limited	99158721	31/1/07	Haikutolewa mpaka Aprili 2008
Alpher Nuhu	13959	18/1/07	Haikutolewa mpaka Aprili 2008
Philimoni Kalokala	12140187	26/1/07	23/7/2007
Celtel (T) Limited	050801127	28/3/07	Haikutolewa mpaka Aprili 2008
Marcdonald Machange	0200672	18/1/07	28/9/2007

(vi) Kuchelewa Kusoma Mita za Wateja :

Tuligundua ucheleweshaji mkubwa wa usomaji wa mita za wateja kama ifuatavyo:

Jina la Mteja	Akaunti ya Mteja	Aina	Tarehe ya kufungiwa mita	Tarehe ya kwanza ya kusoma mita	Miezi ya kuchelewa kusoma mita
Katibu Mkuu Kiongozi	41066446	T2	04/02/2007	03/10/2007	8
Gassi Holdings Ltd	41066438	T2	25/04/2007	06/06/2007	1
Ofisi ya Magereza	41066452	T2	04/07/2007	01/09/2007	2
Derm Electricism (T) Ltd	41066451	T2	03/08/2007	04/10/2007	2
Kibo trade textiles Ltd	41066454	T2	03/08/2007	04/12/2007	4
NBC Industrial Branch	41066455	T2	03/08/2007	05/10/2007	2
National Institute for medical research	41066461	T2	15/9/2007	02/11/207	2
Coconut Fibber Manufacturing Ltd	41066476	T2	24/10/2007	06/12/2007	1
NBC Mnazi Mmoja	41066475	T2	24/10/2007	01/02/2008	3

Tatizo la kusoma mita na kuchelewa kutuma hati za madai kwa wateja (Bills) linaweza kusababisha upungufu wa Mapato ya Kampuni na usumbufu kwa wateja.

(vii) Kutuma Hati ya Madai Pungufu Kuliko Umeme Uliotumika

Ukaguzi uliofanywa kwenye utayarishaji wa hati za madai uligundua kuwa Hoteli ya Kilimanjaro Kempinski ilipelekewa madai pungufu kwa shilingi 13,120,939 (135,765 units) kwa miezi miwili mfululuzo. Tofauti hii inachangia upotevu wa mapato kunakotokana na kutowapelekea wateja madai halisi.

4.3.5 Hifadhi za Taifa Tanzania.

(i) Udhaifu katika Udhibiti wa Ada ya Kuingia Mbugani

Mchanganuo wa mwelekeo wa makusanyo ya ada ya mbugani unaonyesha kuwa makusanyo yanashuka kwa kasi licha ya ukweli kuwa kumekuwa na ongezeko la wageni wanaoingia mbugani. Ushukaji huu wa mapato umechangiwa na udhaifu katika kudhibiti makusanyo yatokanayo na wawekezaji wanaoendesha shughuli zao ndani ya hifadhi za taifa. Kwa mfano, TANAPA hawaweki kumbukumbu za watalii wanaolala kwenye hoteli zilizoko ndani ya hifadhi za taifa.

Tuliangalia rejista ya wageni inayotunzwa na TANAPA dhidi ya kumbukumbu za hoteli kwenye hifadhi ya Manyara kwa mwezi wa 11, 2008 ambapo tuligundua tofauti kubwa kati ya taarifa za pande hizo mbili kama ifuatavyo:

Tarehe	Idadi ya watalii kulingana na kumbukumbu za TANAPA	Idadi ya watalii kulingana na kumbukumbu za hoteli	Tofauti
09/11/2008	4	8	(4)
10/11/2008	0	0	0
11/11/2008	2	4	(2)
12/11/2008	6	6	0
13/11/2008	2	0	2
14/11/2008	2	12	(10)
15/11/2008	0	0	0
16/11/2008	2	6	(4)
17/11/2008	0	4	(4)
18/11/2008	2	8	(6)
19/11/2008	0	4	(4)
20/11/2008	0	0	0
21/11/2008	0	4	(4)
22/11/2008	2	2	0
23/11/2008	2	2	0

24/11/2008	3	7	(4)
25/11/2008	3	3	0
26/11/2008	0	2	(2)
27/11/2008	4	4	0
28/11/2008	0	0	0
29/11/2008	3	2	1
30/11/2008	4	8	(4)

Pia tuligundua kuwa kitengo cha Utalii na kile cha Uhasibu havitengenezi ripoti zinazoonyesha idadi ya wageni walioingia na siku walizokaa mbugani kwa lengo la kulinganisha na kumbukumbu za hoteli ili kupata usahihi wa taarifa zinazoletwa na wawekezaji ndani ya hifadhi. Tulipokea pia vibali vya tarehe 9 Januari 2009 na kugundua kuwa vibali hivi hujazwa na karani wa mlangoni sehemu inayoonyesha mahali atakapofikia mgeni husika. Udhaifu huu unatoa mwanya kwa wanaoendesha shughuli za utalii kutoa taarifa za uongo kuhusiana na mapato yaliyopatikana na hivyo kuinyima Serikali kodi stahili.

4.3.6 Mamlaka ya Bandari Tanzania

(I) Upimaji Usio Sahihi wa Mizigo kwa Ajili ya Ushuru wa Magati Kwenye Bandari za Maziwa Makuu

Ushuru wa magati unawekwa kulingana na uzito wa mizigo inayoingia na kutoka. Ukaguzi wetu uligundua kuwa mizigo iliyopitia bandari za maziwa haikupimwa yote kwa usahihi. Mizigo michache ndiyo iliyopimwa na iliyobaki ilikadiriwa isipokuwa mizigo yenye uzito maalum kama sementi, sukari n.k.

Aidha tulibaini kuwa fomu zinazotakiwa kujazwa na wenye mizigo na maafisa wa bandari hazijazwi ipasavyo, ambapo maafisa hawajazi fomu zinazowahusu (Tally sheets) badala yake wamekuwa wakijaza fomu zinazotakiwa kujazwa na wenye mizigo zinazoonyesha mizigo iliyoingia au kutoka (Inwards/Outwards Cargo Declaration forms). Menejimenti

wameeleza kuwa hali hii imechangiwa na uelewa mdogo wa wenye mizigo na upungufu wa wafanyakazi.

Kutokana na mambo yaliyojitokeza, tulishindwa kuthibitisha usahihi wa ushuru wa magati wa kiasi cha Shilingi 606,201,591 kama ilivyoonyeshwa kwenye taarifa za mahesabu.

Tunaishauri menejimenti ihakikishe kwamba mizigo yote inayoingia na kutoka inapimwa na fomu zote zinajazwa ipasavyo.

(ii) Upotevu wa Mapato Yatokanayo na Magati Binafsi Kwenye Maziwa Makuu

Kulingana na Sheria ya Bandari, Bandari zote kwenye maziwa makuu ndani ya Tanzania bara zinatakiwa kubuni vyanzo vya mapato katika maeneo yao.

Ukaguzi uliofanywa kwenye baadhi ya bandari zilizoko Mwanza na Nansio umegundua kuwa maeneo hayo yanaendesha shughuli mbalimbali ambazo zingeweza kuipatia Mamlaka ya Bandari mapato kulingana na Sheria ya Bandari lakini hakuna jitihada zilizofanywa kukusanya mapato hayo. Maeneo yaliyotembelewa ni kama ifuatavyo :

Na.	Jina la Gati	Jina la mwenye Gati	Mahali ilipo
1.	Mwaroni	City Council	Mwanza North Port
2.	Mkombozi 1	Mr. Kitana	Mwanza North Port
3.	Kamanga Ferry	Mr. Cag klaus	Mwanza North Port
4.	Kishimba	Mr. J. Kishimba	Mwanza North Port
5.	Hamo Transport	Mr. James Kisandika	Mwanza North Port
6	Nyehunge	Mr. Said Mohamed	Mwanza North Port
7.	Bijli	Mr. Bijli	Mwanza North Port
8.	Mkombozi 2	Mr. Kitana	Mwanza South Port
9.	Kamanga Ferry	Mr. Cag klaus	Nansio Port

Menejimenti inashauriwa kuhakikisha kuwa inatambua vyanzo vyote vya mapato ili kuboresha makusanyo ya Mamlaka.

4.3.7 Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania

Ukaguzi umebaini kuwa ukusanyaji wa mauzo ya gesi toka PanAfrican Energy (T) Ltd siyo wa kuridhisha. Kiasi kilichoonyeshwa kama deni analodaiwa PanAfrican Energy (T) Ltd kimekuwa kikiongezeka kwa kasi, na hii inasababisha Serikali kutopata mapato yaliyokusudiwa kwa wakati unaotakiwa.

Mchanganuo ufuatao unaonyesha kiasi ambacho kinadaiwa vihatarishi toka panAfrican Energy (T) Ltd.

Tarehe	Na. ya hati ya madai	Mauzo ya gesi	Kiasi kilicholipwa	Kiasi kilichobakia
		TZS	TZS	TZS
07/02/08	340	200,606,756	149,531,752	51,075,003
30/03/08	346	231,723,636	0	231,723,636
30/03/08	347	670,029,239	450,000,000	220,029,239
30/03/08	348	567,493,751	533,569,266	33,924,484
30/06/08	429	268,306,354	0	268,306,354
30/06/08	430	937,941,506	0	937,941,506
Jumla				1,743,000,224

SURA YA TANO

MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI

5.0 Utangulizi

Sura hii inahusu masuala ya mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye Masharika na Taasisi nyinginezo za Umma ambayo tumeona ni muhimu yaweze kuainishwa katika ripoti hii ya mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2008.

Udhibiti wa ndani ni muhimili mkuu katika Mashirika ya Umma na Taasisi zinginezo na unatakiwa kuimarishwa. Katika ukaguzi wa mashirika na Taasisi nyinginezo tumebaini mapungufu mbalimbali kama inavyoainishwa hapo chini;

5.1 Ufutaji wa Hundi Bila Kufuata Utaratibu

Kwa kawaida hundi ikibainika kuwa ina hitilafu ambayo itaifanya hundi isiweze kutumika tena kwa malipo, itabidi ifutwe kwa kuchorwa mistari miwili mbele ya uso wa hundi husika. Udhibiti huo unafanywa ili kupunguza uwezekano wa kutumika hundi hiyo vibaya endapo itapita mikononi mwa watumishi ambao si waaadilifu na kuweza kuiba fedha za shirika. Ukaguzi uliofanywa katika udhibiti wa ufutaji hundi katika mashirika mbalimbali umebainisha mapungufu yafuatayo:

(i) Chuo cha Ustawi wa Jamii

Ukaguzi uliofanyika katika ofisi ya mtunza fedha, umebaini hundi zenye thamani ya shilingi 7,761,200 ambazo zilikuwa zimekwisha sainiwa lakini zilikuwa hazijawasilishwa kwa wahusika wa malipo hayo baada ya kugundulika kuwa zilikuwa na makosa mbalimbali. Tulipofanya mahojiano na mtunza fedha (cashier) kuhusu hundi hizo, alitufahamisha kuwa hundi nyingine zilikwisha andikwa badala ya zile zenye makosa. Hayo ni mapungufu kwani hizo hundi ambazo hazikufutwa zinaweza kutumika kuchukua fedha kutoka katika akaunti ya Chuo.

(ii) Tanzania Engineering and Manufacturing Designing Organisation (TEMDO)

Katika ukaguzi wa vishina vya hundi imebainika kwamba hundi 16 zilikuwa zimefutwa. Hata hivyo ufutwaji wa hundi hizo haukufuata utaratibu wa kuchora mistari miwili mbele ya hundi hizo na kuandika neno imefutwa na badala yake katika baadhi ya hundi ufutaji uliainishwa kwa kufuta sahihi. Pia hundi zilizofutwa zote hazikuingizwa kwenye daftari la fedha la Mapato na Matumizi (Cash book) na kuandika mbele ya namba za hundi hizo neno “imefutwa”.

5.3 Kutokuandaa Usuluhisho wa Benki

Kanuni 162 ya kanuni za fedha za Umma ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 , inasisitiza kuwa lazima kufanyike usuluhisho wa benki na Daftari la Mapato na Matumizi(Cash book) kila mwezi ili kuweza kuainisha makosa mbalimbali. Katika kupitia hesabu za mashirika mbalimbali imegundulika kuwa suluhisho za benki hazifanywi na sababu za kutofanyika hazikuwekwa wazi. Baadhi ya mashirika yalifanya suluhisho za benki lakini hazikupitiwa na afisa aliyepewa dhamana kwa kazi hiyo.

Majina ya mashirika ya Umma ambayo hayakuweza kafanya suluhisho za benki ni kama ifuatavyo:

Na.	Shirika/Taasisi ya Umma.	Maelezo
1.	Mamlaka ya Kusimamia Ununuzi wa Umma.(PPRA)	Usuluhisho wa benki wa kila mwezi haupitiwi na Afisa aliyeidhinishwa kwa kazi hiyo.
2.	Baraza la Ushauri kwa Wateja wa Mamlaka ya Usimamizi wa	(i) Usuluhisho wa benki wa kila mwezi haupitiwi na Afisa aliyeidhinishwa kwa kazi hiyo. (ii) Hundi zilizochacha hazifanywi

	Mawasiliano Tanzania (TCRA)	marekebisho mapema katika vitabu vya hesabu.
3.	Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)	(i) Usuluhisho wa benki waufanyiki kwa uhakika. (ii) Usuluhisho wa Benki kwa Akaunti ya Maduhuli haufanyiki kwa benki zilizopo NBC na CRDB. (NBC Akaunti namba. 022103000156 and CRDB Akaunti namba. 01J1043011104). (iii)Usuluhisho wa fedha ambazo hazijafika benki unaonyesha kuwa kuna risiti ambazo zimeingizwa mara mbili kiasi cha shilingi 71,096,331 ambazo hazijasahihishwa.
4.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania. (TCAA)	Usuluhisho wa benki hasa wa akaunti ya maduhuli unaonyesha kwamba msimamizi wa kitengo cha usuluhisho wa benki hapitii kazi yake na kujiridhisha kama imefanywa vizuri kwa kuwa hakuna sehemu yeyote anayosaini. Baadhi ya Suluhisho za benki zilizokwishaufanywa zinaonyesha kuwa hazikutayarishwa vizuri na menejimenti haijafanya uchunguzi wowote kuhusu sababu za mapungufu hayo. bakaa za benki zilizotumika kwenye usuluhisho wa Benki zinatofautiana na taarifa za benki.

Kwa kutofanyika usuluhisho wa benki kila mwezi makosa kati ya taarifa za benki na matumizi (Cash book) hayawezi kugundulika kiurahisi na kushughulikiwa mapema. Mapungufu yaliyojitokeza katika mashirika mbalimbali kama niliyoyaainisha hapo juu inaonyesha kwamba ni matatizo yanayojirudia katika mashirika mengi na Taasisi

za Umma hivyo ni vizuri yakawekewa mkazo wa kuyarekebisha.

5.4 Usimamizi Dhaifu katika Makusanyo ya Fedha Taslimu NSSF

Ukaguzi uliofanyika katika michango ya waajiri ya kila mwezi umeonesha kwamba michango inapelekwa kwenye mfuko kwa kupitia benki au kwa fedha taslim. Michango hiyo ya kila mwezi huwa inaambatanishwa na fomu ya NSSF namba 15 ambayo inaonyesha taarifa za mwajiri na taarifa za mfanyakazi husika ambazo zinahusisha taarifa za mshahara pamoja na michango yake ya kila mwezi. Michango hiyo ya kila mwezi inadhibitiwa kwa utaratibu wa kuikatia stakabadhi za kukiri mapokezi. Usuluhisho huwa unafanywa kati ya mkusanyaji wa michango na Mtunza fedha kwa kuandaa taarifa fupi ya makusanyo na taarifa za kupeleka fedha benki.

Hata hivyo, ukaguzi umegundua mapungufu katika kupokea michango katika tawi la Morogoro kuwa mashine ya kuhesabia noti haifanyi kazi vizuri na kuweza kugundua noti ambazo ni bandia. Kwa mfano tarehe 4 Januari, 2008 mashine ilishindwa kugundua noti mbili bandia za shilingi elfu kumi kila moja kwa maana hiyo basi kama mapungufu hayo yasiporekebishwa yanaweza kuleta hitilafu katika makusanyo ya mapato ya shirika.

5.5 Mapungufu Yaliyoonekana Katika Usambazaji wa Hundi.

Mashirika na Taasisi za umma wanatakiwa kuwa na udhibiti wa utoaji wa hundi kwa wahusika wa malipo mbalimbali kwa kuwa na kitabu cha kutolea hundi ambacho kitaonyesha taarifa mbalimbali za hundi husika kama vile jina la mlipwaji, namba ya hundi, kiasi cha malipo na tarehe ya kuchukua hundi. Udhibiti huu unafanywa kwa ajili ya kuzuia hundi zisitolewe kwa wasio wahusika.

Wakati wa ukaguzi tumeweza kugundua baadhi ya mapungufu katika baadhi ya mashirika ya umma pamoja na

kuwa wanavyo vitabu vya kutolea hundi lakini bado hundi zilitolewa bila kusainiwa na mlipwaji kama ninavyoainisha bapo chini

Na.	Shirika	Nambaya Hundi	Kiasi (Sh.)
1.	TBC	35	318,905,190
2.	NSSF	Mbalimbali (various)	1,579,832,604
Jumla			1,898,737,794

5.6 Mapungufu Katika Mgawanyo wa Kazi

Mgawanyo wa kazi ni muhimu sana kudhibiti na kuzuia makosa au mapungufu mbalimbali kwa kutumia wafanyakazi wenyewe katika mzunguko wa kazi. Mgawanyo wa kazi unasaidia mfanyakazi mmoja kukagua kazi ya mfanyakazi mwenzake na pia mfanyakazi mmoja hana nafasi ya kupitisha malipo yeyote bila kupitiwa na mwingine. Wakati wa Ukaguzi tumegundua kuwa baadhi ya mashirika ya Umma hayana utaratibu wa mgawanyo wa kazi katika idara mbalimbali kama inavyoainishwa katika mifano hii hapo chini;

Shirika	Maelezo
Mamlaka za Bandari.	Idara ya fedha katika bandari za Mwanza, Kigoma, Kyela na mamlaka za bandari za nchi kavu, tumebainisha kwamba zina upungufu mkubwa wa mgawanyo wa kazi haswa katika kitengo cha uhasibu ambavyo vina upungufu wa wafanyakazi hivyo kusababisha kazi ambazo zilitakiwa kufanywa na wahasibu badala yake zinafanywa na wafanyakazi wa kada nyingine ambao hawana taaluma ya uhasibu na ambao hawawezi kutenganisha kati ya huduma zitolewazo na uandaaji wa vitabu.
Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga	Fedha taslimu hukusanywa na makarani / wahasibu katika vituo

Tanzania (TCAA)	mbalimbali na kukatiwa stakabadhi na hatimaye kuzipeleka benki. Lakini hatimaye wahasibu hao hao ndiyo wanaoingiza stakabadhi kwenye vitabu vya fedha kinyume na taratibu za fedha.
-----------------	---

5.7 Usuluhisho wa Benki Umeonyesha Mapokezi ya Fedha Ambayo Hayaonekani Benki - DAWASCO

Katika usuluhisho wa benki katika akaunti namba 900 ya CRDB na vitabu vya fedha kwa kipindi kilichoishia mwezi Juni 2008 ilibainika kuwa kulikuwa na hundi za muda mrefu zenye thamani ya shilingi 14,084,688 ambazo zilipokelewa kutoka kwa wateja mbalimbali lakini hazikuingia kwenye akaunti. Mchanganuo unaonyesha muda ambao fedha hizo hazikuingizwa kwenye akaunti ni kama ifuatavyo:

Muda ambao hundi zimekaa bila kuingia kwenye akaunti hadi tarehe 30 Juni 2008.	Kiasi Sh.
Miezi 3 hadi miezi 6	3,181,535
Miezi 6 hadi miezi 12	6,166,613
Zaidi ya miezi 12	4,736,540
Jumla	14,084,688

Kuna uwezekano mkubwa wa kuonyesha bakaa ya vitabu vya fedha ambayo si sahihi na pia zinaweza kusababisha hundi kuchacha. Imebainika kuwa masahihisho yalikuwa yamefanywa kwenye vitabu vya hesabu ili kufuta kiasi hicho cha fedha na bakaa za wateja kusahihishwa lakini kumekuwa na ucheleweshaji wa kufanya marekebisho hayo bila kuwa na sababu za msingi.

Mapungufu hayo machache ambayo yameainishwa katika uhibititi wa ndani, unaonyesha kuwa uongozi wa mashirika mbalimbali hautilii mkazo taratibu zote za usimamizi wa fedha ili kuweza kulinda mali za umma.

SURA YA SITA

TATHMINI YA UTENDAJI

6.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia Tathimini ya Utendaji katika Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo. Mashirika mengi ya Umma yameanzishwa na kupewa majukumu ya usimamizi wa raslimali za Umma na mengine kutoa huduma kwenye jamii ya Watanzania.

Hata hivyo, imebainika kuwa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo hayafanyi vizuri katika utendaji wake.

6.1 Mambo Muhimu Yanayochangia Kurudisha Nyuma Utendaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

Mambo mbalimbali yamechangia mashirika mengi ya Umma na Taasisi nyinginezo kutofanya vizuri.

- (i) Urasimu katika kutoa miongozo na ushauri wa kisheria kwa wizara husika.
- (ii) Sheria dhaifu na mfumo wa sheria ambazo zinatawala shughuli mbalimbali za Mashirika ya Umma,
- (iii) Usimamizi mdogo wa kutowajibika kwa ofisi ya Msajili Hazina, wizara mama, na bodi za Wakurugenzi.
- (iv) Kutokuwa na utamaduni wa Ujasiriamali, uongozi usio imara na upungufu wa utaalumu kwenye nyanja mbalimbali.
- (v) Muundo wa utendaji kazi na mifumo mbalimbali inapangwa bila kuzingatia malengo ya Shirika.
- (vi) Mapungufu katika kupanga majukumu, kupanga mahitaji ya fedha na jinsi ya kudhibiti matumizi ya fedha ambao unasababishwa na kutokuwa na watumishi wenye utaalumu wa kutosha, uwajibikaji na uwazi.

(vii) Mapungufu katika utaratibu wa manunuzi na utunzaji wa vifaa vya ofisi.

6.2 Utendaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo Katika Mwaka Husika wa Ukaguzi.

Utendaji wa mashirika ya Umma umepimwa kwa kuzingatia thamani ya utendaji halisi na uwezo wa kifedha wa shirika.

Tathimini ya utendaji halisi wa mashirika unazingatia uwezo wa mashirika wa kufikia malengo na mambo mbalimbali ambayo yataonekana ni muhimu kuyatolea taarifa, lakini upimaji wa uwezo wa kifedha wa shirika unapimwa kwa kuangalia faida au hasara inayopatikana katika mwaka husika.

Zaidi ya hayo, uwezo wa kifedha katika mashirika unaangaliwa pia kwa kuzingatia pia faida au hasara iliyokuwepo miaka ya nyuma katika vitabu hadi tarehe 30 Septemba 2007, 31 Disemba 2007 and 30 Juni 2008 kwa mashirika yote yanayofunga hesabu katika miaka ya fedha kulingana na tarehe nilizoainisha.

Katika kipindi husika cha ukaguzi, tathmini ya ufanisi wa uendeshaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ulipimwa kwa kutumia vigezo vya hesabu yaani faida na hasara iliyopatikana katika shirika husika.

Ifuatayo ni utendaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo:

Taasisi	Faida kwa mwaka wa fedha Sh.	Hasara kwa mwaka wa fedha Sh.
Mamlaka za Maji	370,711,085	1,389,362,740
Bodi za Uangalizi	21,691,610,790	9,553,098,603
Vyuo vya Elimu ya juu	5,276,073,929	2,685,539,545
<i>Mashirika ya Umma</i>	118,051,293,661	83,357,566,164
Taasisi za Serikali	34,785,531,601	3,278,104,002
Jumla	180,175,221,066	100,263,671,054

6.3 Limbikizo la Faida au Hasara

Katika mwaka husika, msimamo wa kifedha katika Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ulipimwa kwa kuangalia limbikizo la faida au hasara iliyopatikana wakati wote wa uendeshaji wa Taasisi husika.

Yafuatayo ni mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ambayo yalikuwa na limbikizo la faida au hasara katika vitabu vyao vya hesabu:

Shirika/Taasisi	Limbikizo la Faida	Limbikizo la Hasara
Mamlaka za maji	1,211,251,749	5,570,304,655
Bodi za uangalizi	89,672,168,700	7,546,402,387
Vyuo vya Elimu ya juu	19,823,100,853	2,837,074,266
Mashirika ya Umma	602,377,355,008	31,212,057,177
Taasisi za Serikali	172,921,611,576	4,580,535,456
Jumla	883,168,413,619	51,746,373,941

Kutokana mchanganuo huu hapo juu, Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo yanaongoza kwa kuwa na limbikizo kubwa la faida na mamlaka za maji zinaongoza kwa kuwa na limbikizo dogo la faida. Hatua za haraka zichukuliwe ili kukabiliana na hali hiyo katika mamlaka za maji.

6.4 Matokeo na Mapendekezo Maalum ya Ukaguzi.

6.4.1 Mapungufu katika Uendeshaji wa Shirika la Umeme Tanzania.

Katika ukaguzi wa uendeshaji wa Shirika la Umeme Tanzania kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2007 tuliweza kugundua mambo yafuatayo ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho ya haraka ili kuongeza ufanisi katika shirika hili.

- Maduhuli yaliyokusanywa na Shirika la Umeme-Tanzania hadi mwisho wa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2007, kiasi cha shilingi bilioni 5 zilibakishwa Songas Ltd kwa ajili ya kuwekeza katika kampuni hiyo. Hata hivyo ufanisi wa kampuni hiyo ni wenye kutia shaka kwani inaendelea kupata hasara kiasi cha dola za Kimarekani 4,935,000 kwa mwaka.
- Ukaguzi wa utekelezaji wa mkataba wa Kununua umeme kutoka SONGAS wa TANESCO na SONGAS Ltd umegundua kuwa TANESCO ana haki ya kimkataba ya kutathmini gharama za awali za mradi ili kujua uhalali wake na zitumike kama kigezo cha kulipa 'capacity charges'. Ukaguzi umegundua kuwa tathmini hiyo haijafanyika na hivyo TANESCO imeendelea kulipa 'capacity charges' za Dola Million tano (USD 5,000,000) kwa mwezi kwa kuangalia makadirio ambayo yametolewa na Songas Ltd. Ni mtazamo wetu kuwa gharama zinazolipwa na TANESCO sio sahihi kwa sababu tathmini haijafanyika. Tunapendekeza Uongozi wa TANESCO uchukue hatua za haraka kufanya tathmini ili kujua gharama halisi ambayo TANESCO anasitahili kulipa SONGAS Ltd.
- Kampuni ya Richmond Development ililipwa malipo ya awali kiasi cha dola za Kimarekani 30,696,598 ikiwa ni asilimia 35% ya mapato ili waweze kukamilisha taratibu za benki katika Benki ya Biashara. Muda wa kurejesha fedha hizo ni miezi 24 hata hivyo kuanzia mwezi Novemba 2007 kiasi kilichokuwa kimerejeshwa ni dola za Kimarekani 7,674,186 na limebaki deni la dola za Kimarekani 23,022,412. Hata hivyo inafahamika kuwa mkataba kati ya shirika la umeme na Richmond (M/S DOWANS) ulivunjwa tarehe 1 Agosti 2008 kabla ya Shirika la Umeme halijakamilisha kulipwa fedha zote.
- Shirika la Umeme-Tanzania kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita limekuwa likilipa mapato yake yote kwa zaidi ya asilimia 90% kwa makampuni ya IPTL na Songas.

6.4.2 Mapungufu Yaliyojitokeza Katika Ukaguzi wa Mamlaka za Maji.

Imebainika kwamba, sehemu kubwa za Mamlaka ya maji safi na maji taka zinasambaza maji kwa kutumia mfumo ambao ni wa zamani sana. Hali hiyo inachangia maji mengi kupotea yakiwa njiani, uunganishaji mabomba kwa njia ya udanganyifu, utoaji wa ankara za maji ambao kwa muda mrefu unaonekana kuwa siyo sahihi na utaratibu mbaya wa kukusanya maduhuli ambao unachangia mapato kuwa madogo ikilinganishwa na gharama halisi zinazotumika kwa ajili yaumeme kama inavyoainishwa hapa chini.

- (i) Maduhuli ya maji yanayopotea na kiasi cha chini ya kiwango cha mapato kwa shilingi kinatumika kwa matumizi ya umeme.

Maji ambayo yanapotea bure DUWASA ni asilimia 40% hiki ni zaidi ya kiwango cha wastani ambacho ni asilimia 31.8% na gharama za umeme za DUWASA ni zaidi ya kiwango cha kawaida kilichowekwa na DUWASA na kwa sasa sh 1 ya maduhuli inatumika kwa ajili ya kulipia gharama za umeme ambayo ni chini ya kiwango kilichowekwa. Uongozi unatakiwa uwe na udhibiti wa matumizi ya gharama za umeme. Mapato ya mamlaka za maji yameongezeka kwa 1% wakati matumizi yameongezeka kwa 14% kuanzia mwaka wa fedha uliopita.

- (ii) Wateja Waliofungiwa Mita za Maji, Utoaji wa Bili za Maji na Maduhuli.

Mfumo wa utoaji bili katika Mamlaka ya Maji Tanga (TAWASA) unafanyika bila utaratibu mzuri kiasi kwamba kila mtumishi katika kitengo cha kutoa bili ana uwezo wa kuzifanyia bili marekebisho na marekebisho mengi hayana viambatanisho sahihi kama vile barua ya mteja akilalamikia kuhusu bili yake ambayo imeidhinishwa na meneja au kiongozi mwingine yeyote ambaye amepewa madaraka na meneja kuidhinisha barua mbalimbali za wateja na baadhi ya wateja hawana mita. Kwa utaratibu huu si rahisi

kumwajibisha mtumishi yeyote kama kutatokea tatizo lolote katika ukusanyaji wa maduhuli. Inashauriwa kwamba marekebisho yote ya ankara lazima yawe yameambatanishwa na barua ya mteja ambayo imeidhinishwa na Meneja Mkuu au Meneja Biashara kwa pamoja na Meneja wa Fedha kwa niaba ya Meneja Mkuu.

(iii) Usomaji wa Mita za Maji Usio Sahihi

Maduhuli yanayotokana na maji safi na maji taka katika DAWASCO yanachangiwa na bili ambazo zinatumiwa kwa wateja katika mwaka husika. Mamlaka ya maji imerithi idadi ya wateja ambayo iliandaliwa na mmiliki aliyepita ambaye ni City Water Services Limited. Idadi ya wateja iliyorithiwa ina mapungufu yafuatayo:

- Utayarishaji na utoaji wa ankara za maji ambazo si sahihi kwa sababu ya kutosomwa mita kwa usahihi na makadirio ya matumizi ya maji kwa wale ambao hawana mita. Usomaji usio sahihi wa mita unachangiwa na mita zilizoharibiwa au mbovu na uwezo wa mita kushindwa kurekodi vizuri matumizi ya maji kutokana na msukumo mdogo wa maji katika mfumo wa kusambaza maji ambao unajitokeza mara kwa mara.
- Makosa machache yamejitokeza katika mwaka husika kuwa wateja wameunganishwa maji lakini hawapelekewi bili za maji.
- Ukaguzi umeonyesha kuwa katika mwaka husika wa ukaguzi, mita zilizosomwa hazina uhusiano na akaunti mbalimbali za wateja waliosajiliwa. Hii inaashiria kwamba kuna maduhuli ambayo hayako kwenye vitabu vya mamlaka lakini thamani yake haifahamiki.

(iv) Kushindwa Kufikia Malengo Muhimu Ambayo Yameainishwa Katika Mkataba Kati ya DAWASCO na DAWASA

DAWASCO ilitakiwa kufikia mwelekeo wa utendaji kazi na malengo ukaguzi ulibaini makuu yaliyokubalika kati ya shirika la maji safi na maji taka (DAWASA) na DAWASCO kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya ukodishaji yaliyosainiwa tarehe 2 Septemba 2005 kama yaliyorekebisha tarehe 12 Disemba 2005.

Katika kupitia mwelekeo wa utendaji na mwelekeo wa malengo, ukaguzi ulibaini kuwa katika mwaka husika malengo muhimu ambayo yameainishwa katika jedwali hapo chini haya kuweza kufikiwa na shirika la Maji safi na maji taka.

(v) Malengo Muhimu Ambayo Hayakufikiwa na Shirika la Maji Taka na Maji Safi (DAWASCO)

Malengo muhimu	Units	Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka 3	Mwaka 4	Mwaka 5	Kufikiwa Kwa malengo 30 Juni 2008	Maoni
Na. Kifungu								
1. Kufungiwa mita wateja	Na.	14,475	16,500	16,500	16,500	17,500	8,570	hayakufikiwa
2. Wateja wapya	Na.	12,500	30,500	27,000	10,500	5,000	9,844	hayakufikiwa
3. Malengo ya makusanyo	Sh. 'million	1,700	2,300	3,100	3,700	3,750	1,619	hayakufikiwa

Hii inaashiria kuwa kifungu namba 38.4 cha mkataba hakikufuatwa na itachangia adhabu ambayo ni sawa na 0.5% ya makusanyo ya kila wiki au baada ya tarehe ya mwisho kufikiwa. Kwa maana hiyo basi, adhabu ya jumla ya shilingi

millioni 121 imekadiriwa na kuonyeshwa kwenye hesabu za mwaka. Kwa mwaka wa nyuma adhabu ilikuwa shilingi milioni 74. Zaidi ya hayo, uhakika wa shirika kuendelea kufanya vizuri unatia shaka kwa kutofikia malengo ya msingi ambayo imechangia maduhuli na mapato ya shirika kushuka na hatimaye ile hatari ya kushindwa kufikia kulipa mikopo na madeni mengineyo ya shirika yanapotakiwa kulipwa katika siku za baadaye.

6.5 Benki Kuu ya Tanzania.

6.5.1 Mpango wa Benki Kuu ya Tanzania Kutafuta Kampuni ya Ushauri ili Kupata Hali Halisi ya Madeni ya Nje ya EPA.

Malimbikizo ya madeni ya nje (EPA) ni moja la matukio yaliyojitokeza katika Taasisi kubwa ya fedha ya Serikali. Ili kuepukana na tukio hilo tena na mengine yanayofanana na hilo katika siku zijazo, mamlaka husika zimechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwalazimisha watu waliohusika kuiba fedha hizo kuzirejesha na baadaye hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

Hata hivyo, kupitia upembuzi wa madeni ya EPA na taratibu zake ni muhimu sana ili kubaini kama kuna mianya mingine ya udanganyifu katika kushughulikia suala hili la malipo ya madeni ya nje. Tumeishauri Benki Kuu iongeze jitihada za kuingia mkataba na kampuni ya ushauri ili iweze kufanyia kazi mapungufu yote yaliyoainishwa katika ripoti maalumu ya uchunguzi. Zaidi ya hayo, tunashauri Serikali ifanye mapitio pia katika sehemu nyingine ambazo zimeonyesha kuwa zina mapungufu kama vile msaada wa kuagiza bidhaa nje ya nchi “Commodity Import Support Fund”, ili kuziba mianya ya udanganyifu katika siku zijazo kwa watu wachache kuweza kupata nafasi ya kujinufaisha na fedha za Umma isivyo halali.

6.5.2 Benki Kuu Kutokuwa na Sera Rasmi ya Kudhibiti Fedha Haramu.

Katika mwaka 2006 Tanzania ilipitisha sheria ya kudhibiti fedha haramu ili kuweka utaratibu mzuri wa kukinga na kuzuia mzunguko wa fedha haramu, kutoa taarifa za fedha haramu na kuanzisha kitengo cha uchunguzi (Financial Intelligence Unit), Pamoja na kuanzishwa kwa Kamati ya Taifa ya kushughulikia fedha haramu na mambo mengine yanayohusiana, kulingana na Sheria ya kudhibiti mwaka 2006 na kanuni zilizotolewa 2007. Benki Kuu ya Tanzania inamajukumu mawili ambayo ni kudhibiti na kutoa taarifa.

Hata hivyo, Benki kuu haina sera madhubuti na taratibu za kudhibiti mzunguko wa fedha haramu. Pia, Benki Kuu haina miongozo ambayo inaweza ikatumika katika Idara mbalimbali kama vile Idara ya huduma za kibenki, Idara ya mambo ya nje, matawi ya benki, watumishi, Amana za Serikali na amana mbalimbali.

Hii inaashiria kwamba, kwa kutokuwepo mfumo wa sera ya ndani kuhusu udhibiti wa fedha haramu katika idara mbalimbali za benki inaweza kusababisha Benki Kuu kushindwa kutimiza malengo yake muhimu. Kwa hiyo basi, Benki Kuu inashauriwa kuwa na sera na taratibu ambazo zitashughulikia udhibiti wa fedha haramu hapa nchini.

6.6 Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA)

6.6.1 Kuanzisha na Kuendeleza Sheria za Kisekta

EWURA ni Mamlaka iliyoanzishwa kisheria na inahusika na usimamizi wa kiufundi na kiuchumi katika kudhibiti shughuli za umeme, mafuta, Gesi asilia na Taasisi za Maji Tanzania. Kazi muhimu za EWURA ni pamoja na kutoa leseni, kupitia bei za bidhaa mbali mbali na kuzifanyia marekebisho kulingana na hali ya soko, kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa sheria ya viwango kama inafuatwa kama vile usalama, ubora, afya na mazingira yanayomzunguka mfanyabiashara.

Katika mwaka husika, Taasisi iliweza kutunga Sheria na kuzipitisha kama vile Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 na Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008. Kwa hiyo basi, ni muhimu Sheria hizo mbili za Taasisi ziweze kupitishwa na kuunganishwa na Sheria iliyopo ya EWURA ili kuiwezesha Taasisi hiyo kuweza kutimiza majukumu yake kisheria kama zilivyoidhinishwa. Pamoja na hayo, EWURA inatakiwa iimarishe ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ikiwa ni moja ya kazi zake kuu.

6.7. Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma

6.7.1 Kumekuwa na Taarifa Finyu Zinazotolewa kwa Mamlaka na Mashirika Kuhusu Taratibu za Manunuzi.

Taarifa za manunuzi kutoka katika Taasisi mbalimbali zinazopelekwa katika mamlaka hiyo ni finyu sana kama inavyoainishwa hapo chini.

- Taasisi 22 kati ya 350 ziliwasilisha mpango wao wa manunuzi wa mwaka katika mamlaka hiyo katika mwaka husika
- Asilimia 26 ya Wizara yaliweza kuwasilisha taarifa za zabuni kwa mamlaka husika.
- Asilimia 18 ya Serikali za Mitaa zimeweza kuwasilisha taarifa za zabuni zao kwenye mamlaka husika.
- Asilimia 46 ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ziliweza kuwasilisha taarifa zao za zabuni kwa mamlaka husika.
- Taarifa za mikataba zilizowasilishwa kwenye Mamlaka ya kudhibiti Ununuzi wa Umma ni sawa na asilimia 62 ya zabuni zote zilizotangazwa.

Haikuthibitika kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi wa Umma (PPRA) imekuwa ikipeleka taarifa kwa Taasisi za Umma ambazo hazifuati taratibu na sheria zilizowekwa, kwa kuwasisitizia maeneo gani yamekiuka taratibu kuanzia wanapoandaa taarifa ya manunuzi ya mwaka hadi wanapotangaza zabuni na mikataba.

Hii inathibitisha kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma haitimizi majukumu yake vizuri kwa kufuatilia kwa karibu Taasisi za Umma zote na kwa kutokuwajulisha mapungufu yaliyojitokeza. Taasisi nyingi za Umma zinadhani kuwa utaratibu wa kupeleka taarifa kwenye Mamlaka hauna ulazima sana kwao na siyo muhimu.

Utawala wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma unatakiwa kufuatilia kwa karibu kama taratibu za manunuzi zinafuatwa na kuwajulisha Taasisi husika mapungufu yote yaliyojitokeza katika taarifa zilizowasilishwa kwenye Mamlaka.

6.8 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)

6.8.1 Fedha za Wafadhili Zinatumika Chini ya Kiwango.

Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) limekuwa likipata fedha kutoka kwa Wafadhili mbali mbali kwa ajili shughuli za maendeleo kama vile kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi na kuandaa mafunzo kuhusu afya kwenye nyanja mbalimbali kwa mfano kufanya utafiti kuhusu “biodiversity health”. Hata hivyo, fedha zinazotolewa na wafadhili hazikutumika kwa kiwango kinachotakiwa. Hadi mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2008 jumla ya shilingi milioni 126.3 ambazo zilitoka kwa Wafadhili hazikuweza kutumika kwa mafunzo kwa miaka mitatu sasa . Orodha ya wafadhili ni kama ifuatavyo:

Na.	Mfadhili	Mwaka alioweka fedha	Kiasi cha Fedha (Sh.)
1.	Mac Arthur Foundation	1996	51,006,321
2.	Chuo Kikuu cha Queensland	2004	21,772,750
3.	Wizara ya Maliasili na Utalii	2004	13,510,081
4.	Baraza la Hifadhi ya Mazingira	2004	10,781,000
5.	Chuo kikuu cha Greenwich	2004	8,285,691
6.	Tanzania Promotion	2004	7,533,151

	Services.		
7.	KRCD	2004	7,000,000
8.	T.W.P.F	2004	6,450,790
	Jumla		126,339,785

Kwa kutokutumika kwa kiasi hicho cha fedha, malengo ya matumizi ya hizo fedha hayakuweza kufikiwa na inapelekea kupunguza imani ya wafadhili kwa TANAPA na kuweza kupunguza misaada ya miradi ya maendeleo. Uongozi wa TANAPA unawajibika kutumia misaada ya Wafadhili kwa wakati na kwa malengo yaliyokusudiwa.

6.8.2 Ucheleweshaji au Kutotekelezwa kwa Miradi ya Maendeleo.

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa baadhi ya miradi ya maendeleo aidha ilichelewa kutekelezwa au haikutekelezwa kabisa.

Katika miradi michache ya maendeleo tuliyopitia yenye thamani ya shilingi 1,980,912,829 imeonekana haijakamilika katika mwaka husika kama inavyoainishwa kwenye jedwali hapo chini:-

Na	Jina la mradi	Mbuga	Bajeti	Kiasa halisi	Utekelezaji	Maoni
1.	Ujenzi wa nyumba ya CPW - Soronera	Serengeti	88,000,000	-	haujaanza	Mchakato wa zabuni haujakamiliika
2.	Ujenzi wa ukumbi wa starehe - Seronera	Serengeti	141,200,000	-	Haujaanza	Mchakato wa zabuni haujakamiliika
3.	Uwekaji wa mabomba ya maji umbali wa km.22 - Naabi	Serengeti	684,788,208	-	Haujaanza	Mchakato wa zabuni haujakamiliika
4.	Ujenzi wa nyumba	Serengeti	220,000,000	-	Haujaanza	Mchakato wa zabuni

	ya kufikia wageni.					haujakami lika
5.	Samani za ofisi kwa ajili CPW	Serengeti	13,929,000	-	Haujaanza	Ukarabati wa ofisi ya Mhifadhi Mkuu haujakami lika.
6.	Nyumba ya watumishi Mvave.	Mbuga ya Sadani	45,000,000	29,811,240		Ujenzi wa nyumba Umesimama
7.	Ununuzi wa gari Landcruiser station wagon kwa ajili CPW	Rubondo Island	86,000,000	-	Gari haijanunuliwa	Gari linatakiwa linunuliwe na makao makuu
8.	Ujenzi wa nyumba ya watumishi wawili. Makao makuu ya mbuga.	Tarangire	158,211,343	-	Haijakami lika	Mchakato wa zabuni na uteuzi umekamili ka
9.	Nyumba ya mtumishi -Kuro	Trangire	93,784,278	-	Haujaanza	Mchakato wa zabuni na uteuzi umekamili ka
10	Gharama za kuunganisha umeme.	Tarangire	450,000,000	-	Haujaanza	Fedha zimerejeshwa TANAPA makao makuu kwa marekebisho.
Jumla			1,980,912,829			

Ucheleweshaji wa kukamilisha miradi ya maendeleo kunaashiria kutokuwepo kwa wataalamu wa kuweza kufanya kazi kwa haraka na ufanisi. Uongozi wa Idara ya Wanyama Pori unashauriwa kuwa na wataalamu wa kusimamia miradi inayoanzishwa.

6.9 Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi Serikalini (GEPF)

6.9.1 Mfumo wa Uhasibu wa Oracle Haufanyi Kazi Ipasavyo.

Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi Serikalini (GEPF) unatumia mfumo wa uhasibu uitwao Oracle katika kuandaa hesabu zake. Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika tumeweza kubaini kuwa Mfumo huo hautumiki kikamilifu katika kuandaa hesabu za Mfuko na badala yake wanatumia excel spreadsheets. Mfumo huo wa uhasibu wa Oracle umenunuliwa katika mwaka 2005/2006 na umeanza kufanya kazi mwezi Februari 2007. Mfumo huo haukuweza kufanyiwa utafiti wa awali ili kuweza kubaini ni jinsi gani unavyoweza kufanya kazi. Madhumuni ya kununua mfumo huo wa uhasibu ilikuwa kuongeza ufanisi katika kutayarisha hesabu na kupunguza kazi ambazo zinafanywa kwa mkono.

Kwa kutokufanya kazi vizuri kwa mfumo huo wa uhasibu wa Oracle, umepelekea taarifa zote zilizohitajika kwa ukaguzi kuwasilishwa kwa kutumia Excel spreadsheets.

6.10 Shirika la Utangazaji Tanzania

6.10.1 Mapungufu Katika Kufuatilia Vipindi, Matangazo ya Biashara na Kusaini Mkataba.

Shirika la Utangazaji Tanzania halijaweka utaratibu wa kufuatilia vipindi na matangazo ya biashara yanayofanywa na Shirika.

Kufuatilia vipindi na matangazo ya biashara kutauwezesha uongozi wa Shirika kijiridhisha kuwa vipindi vyote vilivyopangwa na matangazo yote ya biashara yanafanyika kwa utaratibu na kwa matakwa ya mkataba na wateja wanapewa ankara zao.

Pia, Shirika la Utangazaji halijasaini mikataba na wateja wa nje ya nchi. Katika mwaka husika, Shirika la Utangazaji lilitoa huduma za matangazo kwa makampuni kwa mkopo

bila kuingia nao mkataba na bila kufuata taratibu za kisheria za kusaini mkataba. Mawasiliano yote kati ya makampuni hayo na Shirika yalifanywa kwa njia ya mtandao.

Matangazo ya kibiashara yanafanyika bila kuwa na Broadcasting Confirmation Orders (BCOs) kinyume na taaratibu zilizoainishwa kifungu 5.2.4.3 cha muongozo wa fedha (Accounting Manual)

Hali hiyo inaweza kusababisha kupungua kwa mapato ya Shirika kwa kushindwa kutoa ankara za madai kwa vipindi mbalimbali na matangazo ya biashara, na ikatokea mteja mojawapo akawa si mwaminifu inakuwa si rahisi kumfuatilia kwa sababu ya kutokuwa na kumbukumbu za wateja waliorushiwa vipindi na matangazo mbalimbali. Pia vipindi vya matangazo ya biashara yanaweza kurushwa bila idhini ya uongozi wa Shirika.

Mikataba yote inatakiwa isainiwe kati ya Shirika la Utangazaji na wateja kwa huduma zote zinazotolewa na shirika.

Menejimenti ya shirika inatakiwa kuhakikisha kuwa BCOs zinatayarishwa kwa matangazo yote ya biashara yanayofanyika na kuepusha matangazo yanayorushwa hewani bila ya kuwa na BCO.

6.11 Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

6.11.1 Kitengo cha Makontena Kilichokodishwa Hakifanyi Kazi Ipasavyo.

Mamlaka ya Bandari Tanzania imekodishwa kitengo cha makontena kwa kampuni binafsi iitwayo Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) kuanzia mwezi Mei mwaka 2000. Mkataba wa awali ulikuwa ni wa kipindi cha miaka 10, hata hivyo mwishoni mwa mwaka 2005, mkataba huo wa ukodishaji

uliongezewa muda na kuwa miaka 15 kwa utaratibu wa Adenda No.2.

Hata hivyo katika kutathmini utendaji katika kipindi kilichoishia tarehe 31.1.2007, Mamlaka ya Bandari ilibaini kwamba mwendeshaji ameshindwa kufanya kazi kama ilivyo katika makubaliano ya mkataba na kwa chini ya kiwango kwa 25% na ikaamua kuandika barua ya kutaka kusitisha mkataba kwa mujibu wa kifungu namba 7.4.2 (2) cha mkataba wa ukodishaji.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo Serikalini, kamati ya usuluhisho iliteuliwa ili pande zote zikutane na kupitia upya mkataba lakini mwendeshaji alikataa na kamati ikarejesha suala hilo tena Serikalini kwa maamuzi.

Tatizo kubwa katika kitengo cha makontena ni mlundikano unaochangiwa na uhaba wa mitambo ya kupakua makontena. Kubwa zaidi muendeshaji kushindwa kuwekeza katika mitambo ya kisasa ya kupakua na kupakuwa makontena.

Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari inashauriwa kwamba mkataba wa ukodishaji unatakiwa kusitishwa, mara tu baada ya kuona huduma zinazotolewa ni hafifu. Kwa kuzingatia ongezeko kubwa la makontena, mamlaka ya bandari iweke utaratibu wa kuruhusu waendeshaji wengine kushughulikia makontena badala ya kumtegemea TICTS peke yake.

6.11.2 Msongamano Katika Bandari ya Dar es Salaam

Sehemu ya kupakulia makontena katika bandari ya Dar es salaam inakabiliwa na changamoto nyingi, kati ya hizo kubwa zaidi ni ongezeko kubwa la mizigo ikiwa ni nje ya uwezo wa kawaida wa bandari, muda mrefu zaidi wa kushughulikia makontena, meli kukaa kwa muda mrefu kabla kupakua mizigo na utendaji kazi usioridhisha.

Hata hivyo, Bandari ya Dar es Salaam imechukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na matatizo hayo;

- Kuongeza utumiaji wa Bandari ya nchi kavu Ubungo.
- Kuongeza upana wa eneo la bandari kwa kubomoa majengo ya kuhifadhia mizigo (warehouses) ambayo yalikuwa hayatumiki.
- Kufanya kazi kwa masaa 24.
- Kutumia eneo la kukodi lililopo nje ya bandari.
- Kujenga maghorofa ya kuegeshea magari na
- Eneo la ziada limenunuliwa sehemu ya Kurasini kwa shughuli za bandari.

Kwa sasa mlundikano katika bandari ya Dar es Salaam ni mkubwa zaidi katika mizigo ya kawaida haswa katika eneo la yadi ya magari pia makontena ambayo bado yapo katika sehemu ya kupokelea mizigo. Pamoja na juhudi zote hizo zinazofanywa na Mamlaka ya Bandari ya Dar es Salaam ya kupunguza msongamano, bado hali ni mbaya na tatizo la mlundikano wa mizigo bado lipo.

Hii inamaanisha kwamba pamoja na juhudi zote zilizofanywa na Mamlaka ya Bandari hazikuweza kutoa matokeo yaliyokusudiwa.

Uongozi wa bandari unatakiwa kuongeza juhudi zaidi ili kupunguza msongamano bandarini.

6.12 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

6.12.1 Uwekezaji Usio na Tija -Matinje

Wakati wa kutembelea miradi inayomilikiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa , tulibaini kuwa mitambo iliyowekwa katika kampuni ya Matinje Gold haifanyi kazi na imekwishaanza kuwa na kutu.

6.12.2 Uwekezaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa Katika Kampuni Washirika.

Hesabu za M/s Siemens (T) LTD kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2006 zinaonyesha kwamba mtaji ambao unatakiwa ugawanywe kwa wamiliki wa hisa

ilikuwa ni shilingi 280,904,000. Hii inamaanisha kwamba 20% ambazo ni hisa za Shirika la Maendeleo linatakiwa lipate mgawo wake wa shilingi 56,180,800 ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichowekezwa ambacho ni shilingi 80,000,000 kama inavyoonyeshwa katika vitabu vya hesabu vya M/s Siemens (T) Ltd.

Hesabu za hivi karibuni za Ms Ace Audit & Expertise Ltd kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2004. Hesabu hizi zinaonyesha kuwa na limbikizo la hasara ya shilingi 132,061,256 hadi tarehe 31 Disemba, 2004. Matokeo yake kampuni ilikuwa na mtaji wenye hasara wa shilingi 78,061,256. Hii inaashiria kwamba asilimia 30% ya hisa zinazomilikiwa na shirika la maendeleo lina gawio la hasara la shilingi 23,418,377 ikilinganishwa kiwango kilichowekezwa cha shilingi 15,000,000 ambacho kilioneshwa kwenye hesabu.

Zaidi ya hayo, tumeelezwa kwamba toka Shirika lianze kuwekeza halijawahi kupata gawio la faida katika kampuni yeyote ambayo shirika limewekeza.

Kwa maelezo hayo hapo juu, fedha zilizowekezwa kwenye makampuni hayo zimepungua thamani na uwezekano wa kurudishiwa fedha hizo toka katika makampuni hayo ni mdogo sana.

6.13 Shirika la Bima la Taifa Linakabiliwa na Madai ya Muda Mrefu

Kutokana na kifungu namba 109 cha sheria ya Bima ya mwaka 1996 kinaeleza kuwa kila mwenye Shirika la Bima anatakiwa kulipa madai anayoyapokea kutoka kwa wateja wake ndani ya siku 60 tokea siku aliyopokea madai hayo. Kama mwenye shirika atashindwa kulipa madai ya mteja wake kwa muda uliokubalika anatakiwa aombe kibali kwa Kamishna wa Bima kwa ajili ya kuongezewa muda wa kulipa deni husika na Kamishna anaweza kutoa muda wa ziada na katika kipindi hicho ni lazima deni liwe limekwishalipwa.

Katika kufuatilia madeni ya bima ya muda mrefu imebainika kwamba kiasi cha shilingi bilioni 9.6 ambazo zimebaki bila kulipwa kwa muda mrefu hayakupata kibali cha Kamishna. Hata hivyo, kwa vile shirika limekuwa na mtaji mdogo wa kujiendesha imekuwa vigumu sana kwa shirika kuweza kutekeleza matakwa ya kifungu cha sheria namba 109 kilichoainishwa hapo juu. Mchanganuo wa madeni ya nyuma kulingana na muda hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2007 ni kama ifuatavyo:-

Mwaka uliopitishwa deni.	Kiasi (Sh.)
1992 - 2000	8,093,319,197
2001	7,241,683
2002	415,254,400
2003	28,910,548
2004	225,362,521
2005	222,238,511
2006	195,755,806
2007	387,289,890
JUMLA	9,575,372,556

Kwa kuzingatia hali halisi ya shirika, ni vigumu sana madeni hayo kulipwa.

SURA YA SABA

UTEKELEZAJI WA SHERIA ZA MANUNUZI

7.0 Utangulizi

Tanzania imefanya mabadiliko makubwa ya sheria za manunuzi na kupelekea kuanzishwa kwa sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 ambayo imeanzishwa na Mamlaka ya kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA). Ili kuhakikisha manunuzi yanafuata taratibu katika Tanzania, kifungu namba 44 (2) cha sheria ya manunuzi kinamtaka mkaguzi wa Taasisi yeyote ya umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama taratibu zote za manunuzi zimefuatwa katika Taasisi husika.

Vilevile, kanuni ya 31 ya kanuni za manunuzi ya Umma (Bidhaa, Ujenzi, Huduma zisizo za kiushauri na uuzaji wa mali za Umma kwa zabuni), inamtaka mkaguzi wa Hesabu wa Taasisi ya umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama manunuzi yanefuata taratibu za kuitisha zabuni na katika ushindani na ununuzi au uuzaji unatakiwa kuidhinishwa kwanza na bodi ya zabuni.

Kwa kuzingatia mamlaka tuliyopewa katika vifungu vya sheria vilivyo ainishwa hapo juu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu imepitia taratibu zote za manunuzi katika mamlaka mbalimbali za umma katika ukaguzi wake wa kawaida kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Katika ukaguzi kwa vipindi kwa mwaka huo husika tumeweza kugundua mapungufu mbalimbali ambayo tumeona ni bora yaingizwe katika ripoti hii ya mwaka. Mojawapo ya mapungufu hayo ni kutokuwepo kwa vitengo vya manunuzi katika mashirika yote yaliyokaguliwa, utaratibu mzima wa manunuzi unategemea sana mamlaka za juu katika kutoa maamuzi, kutokuwepo kwa mpango wa manunuzi, uteuzi wa watumishi ambao hawajasomea mambo ya manunuzi kuwa makatibu wa vikao vya Bodi za Zabuni, kutokuiarifu Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) kuhusu uteuzi wa wajumbe wa zabuni, utendaji dhaifu wa Bodi za

Zabuni, taarifa za manunuzi hazikutangazwa na mapungufu mengine ya manunuzi kama yalivyoainishwa hapa chini:-

7.1 Matokeo ya Ukaguzi kwa Ujumla

7.1.1 Kutokuwepo kwa Kamati ya Manunuzi

Kifungu 34 cha sheria ya manunuzi, 2004 kinaitaka Taasisi yeyote ya Umma kuwa na kitengo cha manunuzi na iwe na wajumbe wanaotakiwa kulingana na sheria. Katika kufuatilia kama kifungu hicho cha sheria kinafuatwa, tumeweza kugundua mapungufu ambayo wakurugenzi wa mamlaka mbali mbali za umma hawakuweza kuanzisha kitengo cha manunuzi kama inaavyotakiwa kufanya hivyo na sheria ya manunuzi. Mapungufu hayo yanaonekana katika baadhi ya mashirikailivyoainishwa hapo chini:

SHIRIKA/ TAASISI
Shirika la Hifadhi za Tanzania
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Mwanza
National Council of Technical Education
Benki Kuu ya Tanzania
Chuo cha Ustawi wa Jamii
Taasisi ya Elimu Tanzania
Shirika la Utangazaji Tanzania
Bodi ya Korosho -Tanzania
Mamlaka ya kudhibiti Mawasiliano (TCRA)

7.1.2 Kutokuwa na Mpango wa Manunuzi

Kifungu 45 cha sheria ya manunuzi (PPA), 2004 kinasema kuwa kila Taasisi ya Umma inatakiwa iwe na mpango mzuri wa manunuzi kwa mwaka mzima ili kuzuia manunuzi ya dharura pia wanatakiwa kuzingatia kununua vifaa vyenye ubora na kwa wakati na kwa bei nafuu. Pia Taasisi zote za Umma zinatakiwa kupunguza gharama za manunuzi kwa kufuata taratibu za manunuzi na kwa kufuata mipango ya manunuzi pamoja na mipango wa matumizi.

Hata hivyo, katika kipindi husika cha ukaguzi, baadhi ya mashirika ya Umma tuliyoyapitia hayakuwa na mipango ya manunuzi na manunuzi yote yalifanyika pale tu kulipotokea mahitaji ya manunuzi na kutumia mgawanyo wa ununuzi katika mafungu ili kushinda matumizi ya njia husika ya manunuzi.

Kwa mfano:-

Shirika la Hifadhi za Taifa
Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Mwanza
Benki kuu ya Tanzania
Chuo cha Ustawi wa Jamii
Taasisi ya Elimu Tanzania
Bodi ya Korosho -Tanzania

7.1.3 Utendaji wa Bodi za Zabuni

Katika Taasisi mbalimbali Wakurugenzi wameanzisha Bodi za Zabuni kama ilivyoainishwa kwenye kifungu namba 28(1) & (4) cha sheria za manunuzi ya mwaka 2004. Hata hivyo mapungufu yafuatayo yameonekana katika utaratibu mzima wa uteuzi na kazi za Bodi za Zabuni kama ifuatavyo:

Uteuzi wa Bodi za Zabuni haukufanywa na Wakurugenzi Wakuu na badala yake ulifanywa na maafisa wengine waliowateua kufanya kazi hiyo kinyume na kanuni ya 33 (2) (a) ya sheria manunuzi ya mwaka 2004. Wakati wa Ukaguzi hatukuweza kubaini kama Mamlaka ya kudhibiti wa manunuzi ya Umma (PPRA) haikujulishwa kuhusu uanzishwaji wa Bodi za Zabuni kama inavyotakiwa katika kifungu 29 (1) cha sheria za manunuzi cha mwaka 2004. Pia imebainika kuwa kuna mapungufu makubwa katika utoaji wa zabuni na maamuzi yanayotolewa yanaonyesha wazi kuwa Bodi ya Zabuni hazifahamu kazi zake na mamlaka yake kulingana na kifungu 30 & 32 cha Sheria ya Manunuzi cha mwaka 2004. Kwa kuzingatia sheria zabuni zote zinapitiwa kwa pamoja na kuchagua mshindi ambaye ameonyesha kuwa na huduma nzuri na gharama nafuu.

Zaidi ya hayo, imebainika kwamba baadhi ya makatibu wa Bodi za Zabuni hawana taaaluma ya mambo ya manunuzi na siyo wakuu wa kitengo cha manunuzi ambayo ni kinyume na taratibu zilizoainishwa katika sehemu ya 2 (C) ya jedwali la pili lilotengenezwa chini ya kifungu 28(2). Pia kuna baadhi ya wajumbe wa Bodi za Zabuni kushindwa kuhudhuria vikao vya Zabuni kwa zaidi ya mara tatu mfululizo bila kuwa na sababu za msingi na hawachukuliwi hatua za kisheria.

7.1.4 Kutokuwepo na Mipaka ya Kazi Kati ya Mihimili Mikuu Kwenye Michakato ya Manunuzi.

Kifungu cha 38 cha sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 kinaainisha kwamba Mkurugenzi Mkuu, Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi, Idara za watumiaji na Kamati inayofanya tathmini ya manunuzi zinatakiwa zifanye kazi kwa uhuru katika kutimiza majukumu yao ya kisheria bila muingiliano. Hata hivyo, imebainika kwamba miundo mingi ya ofisi katika mashirika mbalimbali ya Umma inaonyesha kwamba kitengo cha Manunuzi vinasimamiwa na Idara za watumiaji kama vile Idara ya Fedha na Utawala au Idara ya utumishi na utawala na kupelekea kupunguza uhuru wa kitengo cha manunuzi kinyume na sheria.

Kwa kuongezea, kuna muingiliano katika kufuata taratibu za kazi za Wakurugenzi Wakuu wa mashirika na Wenyeviti wa na wajumbe wa Bodi za zabuni. Imebainika kwamba wenyeviti wa Bodi ya zabuni au wajumbe wa Bodi ndiyo wanaosaini mikataba mbalimbali ya ununuzi kinyume na kanuni ya 33(3) ya G.N.Na.97 ambacho kinazuia Mkurugenzi Mkuu kukaimisha madaraka yake kwa wajumbe wa Bodi za Zabuni na Kitengo cha Manunuzi.

Imebainika kuwa katika Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano, Katibu wa Bodi ya Zabuni (the Supplies and Logistics Officer) kiutendaji anaripoti kwa Mkurugenzi wa usimamizi wa raslimali za shirika “Director of Corporate Resources Management” ambaye ni mwenyikiti wa bodi ya zabuni.

Hali hiyo, inapunguza uhuru wa kitengo cha manunuzi. Jambo jingine lilijitokeza ni kwamba maombi ya manunuzi kutoka katika Idara mbalimbali hayapitii kwa Afisa Ugavi ila yanapelekwa moja kwa moja kwenye kikao cha Bodi za Zabuni na Taarifa ya uthamini inapelekwa moja kwa moja kwenye Bodi ya zabuni na kamati ya Uthamini kabla haijapitiwa kwanza kwenye kitengo cha ununuzi

7.1.5 Uteuzi wa Kamati ya Tathimini ya Zabuni

Kanuni ya manunuzi namba 90(1) inayataka Mashirika yote ya Umma na Taasisi nyinginezo kuanzisha Kamati za kutathimini ya Zabuni ambazo zinatakiwa ziwe na wajumbe si chini ya watatu na wasiozidi watano. Hata hiyo imebainika kwamba kuna baadhi ya kamati zilikuwa na wajumbe zaidi ya watano kinyume na kifungu cha sheria kilichoainishwa hapo juu. Pia taarifa za Kamati ya tathmini ya zabuni hazina sahihi za wajumbe husika wa kamati hiyo. Kwa kuongezea, tumebaini kuwa mapendekezo ya kuteuliwa wajumbe wa kamati ya tathmini ya zabuni yamefanywa na kitengo cha manunuzi bila kuthibitishwa na Mkurugenzi Mkuu na badala yake yaliidhinishwa na wakuu wa Idara kama vile Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala kinyume na kifungu 37(2) cha sheria za manunuzi ya mwaka 2004.

7.1.6 Manunuzi Yaliyofanywa Bila Ushindani

Ukaguzi uliofanywa katika mwaka husika kuhusu taratibu za manunuzi, ulibaini kwamba manunuzi mbalimbali yamefanywa bila kufuata taratibu za ushindani kama inavyoelezwa katika kifungu namba 59 cha sheria za manunuzi cha mwaka 2004. Sheria ya manunuzi inasema kuwa Taasisi zote za Umma zinatakiwa kufanya manunuzi ya vifaa, na huduma au mauzo yanatakiwa waitishe zabuni za ushindani. Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa nukuu za bei (quotations) zilitumwa kwa wauzaji na watoa huduma ambao wameidhinishwa kutoa huduma na haikuthibitika kwamba waliidhinishwa katika kipindi husika

kama inavyoainishwa kwenye jedwali la tatu, sehemu (C) G.N. Na.97.

Pia, hakukuwa na ushahidi kama manunuzi yalifanyika kwa ushindani kwani hapakuwa na ushahidi kwamba bahasha zilizofunguliwa mbele ya Kamati ya manunuzi na kwa kipindi kilichopangwa kwa sababu hakukuwa na kumbukumbu zozote zilizotunzwa na Bodi ya Zabuni.

7.1.7 Manunuzi Yaliyofanywa bila Kutangazwa kwa Zabuni.

Ukaguzi umebainisha mapungufu makubwa katika utangazaji wa zabuni na katika mwaka wa fedha 2007/2008 manunuzi mbalimbali yamefanyika na Mashirika ya Umma bila kutangaza zabuni. Mifano michache inaainishwa katika Jedwali hapo chini:

Shirika	Zabuni ambazo hazikutangazwa
Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Zabuni ya huduma ya Afya aliyopewa AAR Health Servicer (T) Limited yenye thamani ya shilingi 75,670,000 na zabuni kwa ajili ya kutunza kumbukumbu elektroniki za Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) yenye thamani ya shilingi 32,380,000 hazikutangazwa.
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	Mfuko ulifanya manunuzi ya gari lenye thamani ya shilingi 120,000,000.
Chuo cha Ustawi wa Jamii	Manunuzi mbalimbali yenye thamani ya shilingi 107,610,800 yalifanyika bila kuitisha zabuni

7.1.8 Uundwaji wa Bodi za Zabuni Usiofuata Kanuni

Katika kupitia uundwaji wa Bodi za Zabuni mbalimbali imebainika kwamba Bodi nyingi za zabuni zimeundwa kwa idadi ndogo ya wajumbe ikilinganishwa idadi ya wajumbe

iliyoainishwa katika kifungu Na. 28 (2) cha sheria manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Kuna baadhi ya Mashirika imebainika kwamba wawakilishi mbalimbali wa mabaraza ya wafanyakazi wameteuliwa kuingia bodi za zabuni kwa nafasi zao. Pia baadhi ya Bodi zilikuwa na wajumbe chini ya idadi inayotakiwa kisheria. Kwa mfano:- Chuo cha Ustawi wa Jamii wajumbe wa Bodi ya zabuni walikuwa saba na Benki Kuu mjumbe wa TUICO aliteuliwa kwenye bodi ya zabuni kwa nafasi yake.

7.2 Matokeo ya Ukaguzi Maalumu

7.2.1 Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mkanganyiko kwenye Zabuni ya kupitia Muundo wa Mamlaka, kutathmini utendaji kazi na ngazi mbalimbali za mishahara.

Katika kupitia taratibu za zabuni mbalimbali tumebaini kwamba zabuni iliyoitishwa ya kupitia muundo, kutathmini utendaji kazi na upitiaji wa ngazi mbalimbali za mishahara, awali kabisa ilitangazwa tarehe 16,17 na 20 za mwezi wa Agosti 2007 ambapo PricewaterhouseCoopers (PWC) walionekana kushinda zabuni hiyo tarehe 28/1/2008 baada ya kupata alama 87.75 ingawaje uteuzi huo unapingana na maamuzi ya kamati ya kutathmini ambayo ilimteua Ernest &Young ambaye alipata alama 87.80. Hatimaye PWC na uongozi wa TCRA ulianza majadiliano tarehe 5/2/2008 na walikubaliana kuingia mkataba. Bodi ya zabuni iliidhinisha makubaliano hayo tarehe 6/2/2008 na kuridhia kuwa PWC apewe mkataba kwa thamani ya shilingi 59,879,040 kwa ajili ya kazi hiyo. Hata hivyo mkataba huo haukusainiwa na PWC na hakuna ushahidi wowote wa maandishi ulioonyesha kuwa makubaliano na PWC yalibadilishwa na uongozi pia hakuna ushahidi kuwa Bodi ya zabuni ilifuta zabuni hiyo.

Zabuni hiyo ilitangazwa tena ambapo waliokuwa washindi kwenye zabuni ya awali walizuiliwa kushiriki na zabuni hiyo

hatimaye kutolewa kwa kampuni ya Transport Resources Centre Limited (TRCL) Kampuni ambayo ilionekana kuwa haifai katika mchakato wa awali kabisa wa Zabuni ndiyo iliyoteuliwa kama imeshinda na kuzizidi kampuni nyingine kumi na moja (11) ambazo zilionekana zina ubora kulingana na dodoso za kikao cha Bodi ya zabuni kilichokaa tarehe 4/6/2008. Katika hali ambayo si ya kawaida Mkurugenzi Mkuu aliteua Bodi ya muda ya manunuzi na kampuni hiyo ya TRCL ikapata zabuni hiyo tarehe 27/6/2008 kwa kupendekezwa na Mwenyekiti wa Bodi hiyo ya muda na kuidhinishiwa na Mkurugenzi Mkuu. Bodi hiyo ya muda ilikuwa na wajumbe watatu ambao wanakaimu ukuu wa Idara tofauti na kuteuliwa kwa ajili ya kupitisha zabuni hiyo tu.

Katika kupitia taarifa mbalimbali ambazo ziliwasilishwa na kampuni iliyoshinda Zabuni hiyo (Transport Resources Centre Limited) imebainika kuwa hakukuwa na mabadiliko makubwa ya maamuzi kati ya wataalamu waliopitia zabuni ya mwanzo na zabuni iliyorudiwa kuhusu uchambuzi wa kampuni hiyo. Katika Zabuni iliyorudiwa inaonyesha kuwa kampuni iliyoshinda ilikuwa na washauri wawili (Consultants) walitoa taarifa za uongo kuwa wamefanya kazi na kampuni hiyo kwa zaidi ya miezi kumi na mbili na kwa kiasi kikubwa alama ziliongezeka kwa ajili hiyo, pia imebainika kuwa Mtaalamu wa Ushauri Mkuu (Principal Consultant) wa kampuni iliyoshinda zabuni pia alikuwa mjumbe wa kamati ya kupitisha zabuni ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) na suala hilo halikuwekwa wazi wakati wa kupitisha mapendekezo ingawaje kulikuwa na maoni (comment) kutoka kwa mjumbe mmoja wa bodi ya zabuni. Suala hili halikuweza kufanyiwa kazi kuhusu mjumbe wa kupitisha zabuni wa TCRA pia ni mshauri mkuu wa kampuni iliyoshinda zabuni na kupata suluhisho la tatizo hilo. Tumeona mchakato mzima wa zabuni haukuwa na uwazi na ukweli na kwa kiwango kikubwa umechangia uvunjaji wa sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake ambazo zinaitaka

Mamlaka kuunda tume huru kuchunguza utoaji huo wa zabuni na hatua sahihi zichukuliwe.

7.2.2 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

Ununuzi Wenye Kutia Shaka wa Huduma ya Ulinzi Kutoka kwa Alliance Day and Night Limited

Katika mwaka husika wa Ukaguzi, mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulinunua huduma ya ulinzi kwa ajili ya kulinda ofisi zake zilizopo nchi nzima. Matokeo ya tathmini ya kamati ya manunuzi iliyowasilishwa kwa Bodi ya Zabuni katika kikao chake kilichokaa tarehe 13 Augusti 2007 kilipendekeza washindi kwa maeneo na kampuni ya Alliance Security ilishindania maeneo yafuatayo kama inavyoonyesha kwenye Jedwali.

Mkoa	Loti Na.	Mzabuni	Matokeo ya tathmini
Arusha (ofisi 2)	5	Pentagon Security	1
		<i>Alliance day and Night</i>	2
Kilimanjaro (Ofisi 5)	7	Bullwark	3
		Pentagon	1
		<i>Alliance day and Night</i>	2
Tabora (maeneo 2)	9	Aliance day and night	1
Dodoma (maeneo 2)	10	Bulwark security	2
		Alliance day and Night	1
Singida (maeneo 2)	11	Panic system	1
		<i>Alliance day and Night</i>	2
		Real security	3

Katika mchakato wa kuteuwa washindi wa kila eneo la ulinzi katika kikao chake cha Bodi ya Zabuni kilichofanyika tarehe 13 Augusti 2007 Bodi ya zabuni ilielekeza Idara ya Ulinzi kufanya uchunguzi (vetting) na kuteua washindi watatu kwa kila eneo kwa ajili maamuzi. Taarifa ya uchunguzi iliyofanywa na Idara ya Ulinzi na kusainiwa na Mkuu wa Idara hiyo (Chief Security Manager) ilitoa maoni ambayo ni tofauti na yaliyotolewa na kamati ya kutathmini

zabuni kwa kutumia vigezo tofauti na kuiteua kampuni ya Ulinzi ya Alliance Day and Night Security Guard Limited yenye sanduku la Posta 305 Tabora kutoa huduma za ulinzi katika maeneo ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora, Dodoma, Mwanga Same, Tarakea, Hai, Everest Chines restaurant, Nzega rest house kuanzia 31/10/2007 mpaka tarehe 31/10/2009.

Hata hivyo, uhalali wa kuteua kampuni hiyo na kuwapa maeneo mengi zaidi badala ya kampuni zilizopendekezwa na kamati ya kutathmini zabuni hazikuweza kufahamika mara moja. Muingiliano wa mchakato mzima wa manunuzi kati ya kamati ya kutathmini na Idara ya Ulinzi haijajulikana chanzo chake na hali hiyo inaashiria ukiukwaji mkubwa wa sheria za manunuzi na uchunguzi wa kina unahitajika ili kuthibitika kwamba uteuzi huo ulikuwa huru na wa haki.

Pia imebainika kwamba taarifa za zabuni za kampuni ya Alliance Security haikuandaliwa kulingana na muundo ulitolewa na (PPRA) ambayo inaonyesha ni jinsi gani kampuni iliweza kushinda. Hata hivyo kampuni hiyo haifanyi vizuri katika baadhi ya maeneo iliyopangiwa kulinda. Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unashauriwa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu utoaji wa zabuni hiyo ya ulinzi na kuchukua hatua zinazostahili .

7.2.3 Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA)

TANAPA ilisaini mkataba wa kupatiwa huduma ya utangazaji kupitia shirika la CNN na Jambo Publications ingawa mchakato mzima wa manunuzi ulifanywa na Wizara. Mikataba husika ilisainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Tanzania na mwenyekiti wa Bodi ya Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) wakati huo Kanali Mstaafu wa jeshi Emmanuel S. Balele kwa kipindi hicho lakini mchakato mzima wa kupata huduma hiyo ulifanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kinyume na taratibu za sheria za manunuzi za mwaka 2004. Mkataba huo wa matangazo na

CNN kwa mwaka wa fedha 2007/2008 ulikuwa wa thamani ya Dola za Kimarekani 750,000. Baadaye Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) ilisaini mkataba mpya wa Dola za Kimarekani 800,000 kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kwa ajili ya huduma ya matangazo. Mikataba yote hiyo miwili haikuonyesha muda wa matangazo hayo kama yanatolewa kwa siku ,kwa wiki au kwa mwezi na kwa muda gani ili kuweza kufuatilia kama matangazo hayo yanatolewa kwa wakati na kwa kiwango kulingana na makubaliano ya malipo. Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) mnamo mwezi Octoba 2007 ililipa malipo ya jumla ya Shilingi 1,077,620,400 kwa CNN. Malipo hayo hayakuambatanishwa na vithibitisho vya kufanyika matangazo au viambatanisho vyovyote vinavyoonyesha kuwa matangazo hayo yalirushwa hewani na CNN. Kuhusu kutangaza matangazo kwa kupitia Jambo Publications Ltd, London, Hifadhi ya Taifa - Tanzania ililipa jumla Dola za Kimarekani 272,006.45 ikiwa ni ada ya kutoa huduma ya matangazo kwa miezi sita kuanzia Januari 2008 hadi Juni 2008. Matangazo yaliyofanyika katika uwanja wa ndege wa Heathrow Terminal 4 uliopo London yaligharimu Dola za Kimarekani 68,373.23 ambapo huduma ya matangazo kupitia mabasi 100 ya mjini London yaligharimu Dola za Kimarekani 203,633.20. Mikataba ya matangazo hayo haikuweza kupatikana kwa ukaguzi. Hata hivyo, ankara ya malipo ya tarehe 18/12/2007 kuhusiana na malipo yaliyofanyika ilikuwa na anwani ya Bodi ya Utalii Tanzania ingawaje malipo yalifanywa na Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA). Pamoja na hayo, hapakuwa na ushahidi wowote ulionyesha kwamba matangazo hayo yalifanyika. Kwa maoni yangu ingawaje nia ya matangazo hayo ilikuwa nzuri na kwa manufaa kwa taifa, utaratibu uliotumika haukuwa sahihi na hivyo kufanya upatikanaji wa thamani ya fedha kwa huduma zilizotolewa kuwa mashakani.

7.2.4 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

Zabuni Yenye Kutia Shaka Iliyotolewa Kwa Njia ya Mtandao

Shirika la Utangazaji Tanzania limeingia makubaliano na kampuni ya WiA kwa ajili ya kutoa huduma ya Internet kuanzia mwezi Disemba 2007 bila kufuata taratibu za zabuni ikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba mwezi Juni 2008 baada ya miezi sita kupita. Shirika la Utangazaji lilitumia nukuu za bei (quotations) katika kupata huduma hiyo mwezi Juni 2008 kwa makampuni ya WiA, TANSAT na Startel (T). Hata hivyo katika hali isiyo ya kawaida zabuni ilitolewa kwa kampuni ya WiA na makampuni mengine yakawa yameshindwa.

Pamoja nakuwa kampuni ya WiA ilonekana kunukuu bei ya juu kuliko wazabuni wengine, kamati ya tathmini ilifanya mazungumzo na kampuni ya WiA ili kupunguza gharama ya huduma hiyo kutoka shilingi 172,000,000 bei ambayo ilionekana awali kwenye nukuu za bei za kampuni ya WiA na kuwa shilingi 60,000,000 ambayo inakaribiana sana na bei zilizokuliwa na wale wazabuni washindani. Hata hivyo nyaraka mbalimbali zilizohusika na mkataba hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi.

Tarehe 23/7/2007 Bodi ya Zabuni iliamua kuitumia kampuni ya P Squared Limited ya Uingereza bila kushindanishwa (single source procurement) kwa ajili ya kuboresha vituo vya radio vya lengo jipya la BH, PRT na kituo cha kurushia matangazo ya televisheni kilichopo Mikocheni kwa mkataba wa Paundi za Kiingereza 53,212 na ulisainiwa tarehe 11/10/2007. Hata hivyo imebainika kwamba dondoo za kikao cha zabuni cha tarehe 26/11/2007 zilionyesha kwamba makampuni matano (5) yalialikwa kuleta nukuu za bei na makampuni matatu yaliweza kuleta nukuu zao. Mkurugenzi Mkuu aliagiza Bodi ya Zabuni kutoendelea na mchakato wa kuchagua mzabuni hadi hapo P Squared Ltd atakapoleta nukuu yake.

Tarehe 5/2/2008 Bodi ya Zabuni iliamua kumpatia zabuni P Squered Ltd kwa maelezo kwamba kampuni zile 3 za awali zilikuwa na gharama kubwa zaidi. Lakini nukuu zilizowasilishwa zilionekana kuwa na gharama ndogo kuliko ile ya P Squered ambazo zilikuwa dola za Kimarekani 51,383 hadi Dola za Kimarekani 71,630 ikilinganishwa na gharama za P Squared za pauni za Kiingereza 53,212 ambazo ni sawa na shilingi 126,000,000.

Haikuweza kufahamika mara moja umuhimu wa kuanza mchakato wa Zabuni wakati mkataba ulikwishasainiwa na malipo yalikuwafanyika tarehe 1/11/2007. Wazabuni wengine walienguliwa kwa madai kuwa gharama zao zilikuwa ni za juu zaidi ingawaje kampuni ya P Squared ndiyo iliyokuwa na gharama kubwa zaidi .

7.2.5 Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

Zabuni kwa Ajili ya Ujenzi wa Yadi Kutunzia Makontena Shilingi 4,165,666,875

Ukaguzi uliofanyika katika mkataba ulioingiwa kati ya Mamlaka za Bandari Tanzania na M/s Tangerm Ltd ya Dar es Salaam yenye ubia na kampuni ya M/s Techno Combine Construction Ltd kwa ujenzi wa yadi kutunzia makontena katika eneo la Ex-TANESCO kwa kutumia consolidated system kwa gharama ya shilingi 4,165,666,875. Mkataba huo umeonyesha mapungufu yafuatayo;

Na.	Kipengele	Mapungufu
1.	Mkataba wa kusawazisha eneo	Kazi ya kusawazisha Yadi iliyopo eneo EX-PCMC na EX-TANESCO mkataba huo alipewa CHIKO, Hata hivyo haikuweza kufahimika uhusiano uliopo wa kazi hiyo na mkataba wa awali wa ujenzi wa yadi iliyopo EX-TANESCO. Gharama ya awali ya mkataba imefanyiwa mabadiliko kwa 56.7% yaani kutoka shilingi 245,850,000

		hadi shilingi 385,319,000 pia baada ya kufuatilia BOQ imebainika kwamba kazi ya kuchimba (excavation) imebadilika kutoka mita 20,800 hadi mita 49,923
2.	Makubadiliano ya ubia	Kamati ya kutathmini zabuni ilishauri kazi hiyo ifanywe kwa ubia kati ya kampuni ya M/s Tangerm LTD ya Dar es Salam na M/s Techno Combine Construction LTD kwa gharama ya shilingi 2,184,046,000 (bila kujumuisha VAT). Haikuweza kufahamika ni kwa vipi mkataba huo uliingiwa kwa ubia.
3.	Muda wa kumaliza kazi	Ingawaje makubaliano ya muda wa kazi ni siku 45 na ndiyo yaliyopelekea kutoa kazi kwa kampuni hiyo bila kushindanisha kampuni nyingine, ingawaje muda huo pia ni zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa na kamati ya manunuzi. Hata hivyo muda wa kazi uliongezwa tena kutoka tarehe 29/5/2008 hadi tarehe 18/7/2008, na pia uliongezwa siku 43 hadi tarehe 25/9/2008 na kufanya jumla ya siku 133.
4.	Hali halisi ya mradi na thamani ya fedha zilizotumika	Ukaguzi wa mradi uliofanywa tarehe 9/10/2008 imebaini kuwa Mkandarasi alikuwa hajamaliza kazi na hali hiyo inaashiria kwamba muda wa nyongeza ulikuwa unatolewa bila kuzingatia hali halisi ya utendaji kazi. Zaidi ya hayo inaonekana kwamba mradi huo wa shilingi 4.17 bilioni haukuzingatia thamani ya fedha kwa kukamilisha kazi kwa wakati na ubora unaotakiwa. Tunashauri ufanyike uchunguzi wa kina kuhusiana na mradi huu.

Kwa maoni yangu kuwa Mamlaka za Bandari Tanzania ingeweza kupata mkandarasi ambaye angeweza kufanya kazi kwa ubora, ufanisi na kwa bei nafuu kama wangeshinganisha wazabuni.

Ili kujiridhisha kuwa gharama za mradi zilizolipwa na Mamlaka za Bandari Tanzania zinawiana na gharama ya kazi iliyofanyika, itabidi uongozi wa mamlaka za Bandari ufanye tathmini ya mradi au ufanyike uchunguzi na wakitaalamu ili kubaini kama gharama za huo mradi ni sahihi.

Zaidi ya hayo kushindwa kwa mkandarasi kumaliza kazi kwa wakati, mkataba huo unatakiwa ufanyiwe tathmini ili kuweza kubaini ni kiasi gani cha fedha kama adhabu kinachotakiwa kulipwa na mkandarasi kwa kuchelewesha kumaliza kazi.

SURA YA NANE

USIMAMIZI WA MIKATABA

8.0 Utangulizi

Sura hii inahusu uchambuzi wa mambo ya kisheria na usimamizi wa mikataba ambayo tumeona ni muhimu kutolewa taarifa kama zilivyojitokeza katika taarifa za kaguzi za mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Ukaguzi wa mikataba ulifanywa sambamba na ukaguzi wa kawaida wa hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kama ilivyoainishwa kwenye kufungu 26 (e) cha Sheria ya Ukaguzi Na.11 ya mwaka 2008.

Sheria ya Ununuzi Na.21 ya mwaka 2004 pamoja na kanuni zake za mwaka 2005 inatoa tafsiri ya mkataba kama makubaliano kati ya Shirika na mzabuni au mkandarasi au mnunuzi wa kifaa, mtoaji vifaa au utoaji wa huduma au uuzaji wa vifaa vya Umma. Nadharia zinafafanua kuwa mkataba ni makubaliano baina ya watu wawili au zaidi wakikubaliana na kufanya kwa pamoja jambo kwa mujibu wa sheria. Ni makubaliano yanayowafunga kisheria wote wawili au zaidi ya hapo au Mashirika yaliyo na haki ya kufanya kazi kwa pamoja.

Katika Ukaguzi wetu tulibaini kuwepo na udhaifu katika uingiaji na utekelezaji wa mikataba kama inavyoainishwa kwenye aya zifuatavyo:-

8.1 Mkataba wa Kununua Umeme Kati ya TANESCO na SONGAS

Ukaguzi wa utekelezaji wa mkataba wa kununua umeme kati ya TANESCO na SONGAS Ltd umebaini kuwa TANESCO ina haki ya kimkataba ya kutathmini gharama za awali za mradi ili kujua uhalali wake na zitumike kama msingi wa kulipa mrahaba (capacity charges). Ukaguzi umegundua

kuwa tathmini hiyo haijafanyika na hivyo TANESCO imeendelea kulipa mrahaba wa Dola Million tano (USD 5,000,000) kwa mwezi kwa kuangalia makadirio ambayo yametolewa na Songas Ltd. Ni mtazamo wetu kuwa gharama zinazolipwa na TANESCO sio sahihi kwa sababu tathmini haijafanyika. Tunapendekeza Uongozi wa TANESCO uchukue hatua za haraka kufanya tathmini ili kujua gharama halisi ambayo TANESCO inastahili kulipa SONGAS Ltd.

8.2 Udhaifu Katika Utekelezaji wa Mkataba wa Uendelezaji wa Dar es Salaam Water Front - Shs.433,837,547 - Mamlaka ya Bandari Tanzania

Ukaguzi wa mchakato wa manunuzi na utekelezaji wa mkataba kati ya Mamlaka ya Bandari na M/s CPCS Consultants kwa ajili ya uendelezaji wa Dar es Salaam Water Front kwa gharama ya shilingi 433,837,547 umebaini mapungufu kama ifuatavyo:-

Na.	Pungufu	Maelezo ya kina ya Ukaguzi
1.	Kukosekana taarifa ya tathmini ya kuonyesha nia ya kushiriki katika zabuni.	Hapakuwepo na taarifa ya tathmini badala yake bodi ya zabuni ilipokea ripoti iliyoandaliwa na idara ya manunuzi kinyume na taratibu za manunuzi. Ripoti hiyo ilitumika kufanya maamuzi ya kumpata mkandarasi.
2.	Ununuzi ambao haukushindanishwa kinyume na taratibu	Mkurugenzi wa huduma za ugavi na ununuzi aliomba bodi ya zabuni kuidhinisha na kumpitisha mzabuni M/s CPCS Consultants bila kumshindanisha kinyume na kanuni na.35 G.N 98 ya sheria ya manunuzi.

3.	Zabuni ya kumpata mshauri wa mradi haikutangazwa.	Kulikuwa na uvunjwaji wa kanuni Na.112 (4) (G.N 98) ya sheria za manunuzi ambapo zilitumika barua kualika kampuni mbali mbali kuleta naombi yao kuonyesha uwezo wa kifedha badala ya kutangazwa wazi.
----	---	---

8.3 Mkataba wa Huduma ya Ulinzi Kati ya M/S Gema Security na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Upembuzi wa kina wa mchakato wa manunuzi na mkataba ulioingiwa na pande mbili tajwa hapo juu ulibaini mapungufu yafuatayo:-

- Mzabuni alichaguliwa kwa kigezo kimoja cha bei ndogo na kuacha vigezo vingine muhimu katika kutathmini zabuni.
- Mkataba haukuwa na muhuri wala chapa kinyume na utaratibu.
- Kumekuwa na vitendo vingi vya wizi kwenye maeneo yanayolindwa na kampuni ya M/s Gema Security, pamoja na uongozi wa mamlaka kufahamu kuhusu vitendo hivi, hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kurekebisha hali hiyo.
- Mkataba haukuweka wazi idadi ya walinzi wanaohitajika lindoni hivyo kupelekea madai kubadilika kila mwezi na kuleta wasiwasi juu ya malipo yaliyofanywa dhidi ya kampuni hiyo kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

	Idadi ya walinzi kwa mwezi			
	Ndani	Nje	"Estate"	Jumla
Februari	70	40	48	158
Machi	59	44	48	151
Aprili	-	121	48	169
Jumla	477	205	144	

- Kumetokea kutokuelewana kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya M/s Gema Security kuhusu idadi ya walinzi wanaotakiwa lindoni, na hakuna jitihada zozote zilizofanywa na menejimenti ya bandari kuhakikisha hali ya kutoelewana inatatuliwa mapema.
- Mkandarasi (Gema Security) ameshindwa kutimiza masharti ya kifungu Na. 3.0 cha mkataba kinachotaka kuwepo lindoni walinzi wenye silaha, mbwa, magari na pikipiki.
- Kulionekana kuwepo madai hewa ambapo hati za madai zilizowasilishwa na Gema zilipunguzwa kwa kiwango cha asilimia hamsini: Mfano madai ya Shilingi 245,280,000 yalipunguzwa hadi kufikia Shilingi 195,690,000.

8.4 Udhaifu Katika Mikataba-Bandari ya Dar es Salaam

Ukaguzi uliofanyika Mamlaka ya Bandari tawi la Dar es Salaam ulibaini mapungufu katika mikataba ifuatayo:-

1.	Mkataba wa kutoa huduma za usafi wa akina mama “Female Sanitary Service” kwa mwaka wa fedha 2006/2007 iliyotolewa na Bradys Quality Service kwa gharama ya shilingi 9,000 kwa debe la taka kwa mwezi.
2.	Mkataba wa kutoa huduma ya bustani zinazotolewa na Property Market Consult - shilingi 107,916,000
3.	Mkataba wa kukodi magari kwa gharama ya shilingi 267,060,000 kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia tarehe 27 Aprili 2007 mpaka tarehe 11 Aprili,2008 uliongezwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2008
4.	Mkataba wa “Block Staking Operations of Bagged Cargo” Bandari ya Dar es Salaam kwa mwaka wa fedha 2006/2007

Katika upembuzi wa mikataba hiyo hapo juu tuligundua mapungufu yafuatayo:-

Kukosekana kwa Uhalali wa Mikataba Inayotambuliwa Kisheria.

- Hapakuwepo na mikataba inayotambuliwa kisheria bali kulikuwepo na makubaliano tu ambayo hata hivyo hayakusainiwa na pande zote mbili. Makubaliano hayo yaliongezwa kwa muda mrefu kuliko muda ule wa awali. Hali hii pia ilijitokeza katika mikataba katika bandari ya Tanga.

(ii) Tathmini ya Utendaji wa Watoa Huduma

Katika tathmini ya utendaji wa watoa huduma waliotajwa hapo juu, tulibaini kuwepo mapungufu ambayo pamoja na kujulikana kwa uongozi wa Bandari hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kurekebisha hali hiyo. Kwa mfano mtoa huduma ya usafi wa akina mama “Female Sanitary Service” aliongezewa muda japokuwa alikuwa ameonyesha mapungufu katika utendaji wake.

(iii) Kukosekana kwa Kifungu Kinachohusu Malipo kwa Kutokumaliza Kazi kwa Muda Uliokubalika Kimkataba

Mkataba kati ya Bradys Quality Service na bandari Dar es salaam kwa ajili ya kutoa huduma ya usafi wa akina mama “Female Sanitary Service” na mkataba wa “Block Staking Operations of Bagged Cargo” katika bandari ya Dar es Salaam kwa mwaka 2006/2007 haikuwa na vifungu vinavyozungumzia malipo ya kuchelewa kumaliza kazi kwa muda uliokubalika kimkataba.

(iv) **Kutokuwa na Msimamo Wakati wa Kutathmini Zabuni.**

Tuligundua kuwa katika mojawapo ya kigezo kilichotumika kuwaondoa baadhi ya wazabuni katika zabuni za kuhudumia bustani ni pamoja na kuwa na leseni ambazo zinaonyesha kuwa wanatoa huduma ya usafi badala ya kuhudumia bustani. Hata hivyo, Mzabuni aliyeshinda zabuni hii alionekana kuwa na leseni ya kufundisha namna ya kuthaminisha majengo na sio kuhudumia bustani.

(v) **Mkataba Haukuweka Wazi Kuhusu Idadi ya Vifaa Vitakavyotolewa.**

Katika mkataba wa kutoa huduma ya usafi kwa akina mama kwa mwaka wa fedha 2006/2007 bei ilikuwa shilingi 9,000 kwa debe la uchafu kwa mwezi. Hata hivyo idadi ya madebe yanayohitajika kwa mwezi haikujulikana hivyo kutoa mwanya kwa mzabuni kuweza kucheza na idadi ya debe atakavyo.

(vi) **Kubadilishwa kwa Bei ya Zabuni Bila Sababu Maalumu.**

Bei ya zabuni kwenye ununuzi wa huduma ya kutengeneza bustani katika bandari ya Dar es Salaam ilirekebisha kwa kiwango cha shilingi 1,216,000 kutoka shilingi 7,777,000 hadi kufikia shilingi 8,993,000 kwa mwezi bila kuwepo sababu za kutosha kufanya hivyo.

8.5 Udhaifu Katika Mkataba wa Pango Kati ya Bandari ya Kigoma na M/s Gravimports SpI

Ukaguzi uliofanyika katika bandari ya kigoma umebaini kwamba kazi ya kupakia na kupakuwa mizigo bandarini imekodishwa na inaendeshwa na kampuni binafsi ijulikanayo kama M/s Gravimports SPL ya Burundi ikiwa na ubia na kampuni ya MUAPI ya Tanzania kwa gharama ya

pango ya mwaka ya Dola za Kimarekani 200,000 kuanzia 1/1/2008 kwa kupindi cha miaka mitano.

Hata hivyo ukaguzi umebaini mapungufu yafuatayo:

- Mkataba ulisainiwa Makao Makuu na hapakuwepo na maelekezo yoyote kwa menejimenti ya bandari ya Kigoma juu ya usimamizi na utekelezaji, hivyo uongozi wa bandari ya Kigoma ulionekana kutojua vifungu vingi vya utekelezaji wa mkataba huo.
- Tulibaini kuwa wafanyakazi wa bandari Kigoma hawana uwezo wa kujua kazi zinazofanywa na mkandarasi, hivyo hati za madai hutengenezwa kutokana na taarifa zinazotolewa na mkandarasi bila kuzihakiki na kujua ukweli wake.
- Hati ya dhamana “performance bond” ya dola za Kimarekani 500,000 iliyotakiwa kutolewa na mkandarasi, ilichelewa kutolewa kwa kipindi cha miezi sita ambapo ilitolewa tarehe 30/6/2008 badala ya tarehe 1/1/2008.
- Mkandarasi alitakiwa kuchukua bima ya dola za Kimarekani milioni tano (5), lakini wakati wa ukaguzi hatukupata ushahidi wowote kama bima hiyo ipo kama inavyotakiwa kwenye mkataba.
- Kodi ya pango ya mwaka ilichelewa kwa kipindi cha miezi saba bila kilipwa ambapo dola za Kimarekani 200,000 zilipwa tarehe 7/8/08 badala ya kulipwa ndani ya siku tisini (90) toka tarehe ya kuingiwa mkataba ambayo ni tarehe 1/1/2008. Tunapendekeza uongozi wa bandari Makao Makuu uwe na utaratibu wa kushirikisha viongozi wa vituo watakaosimamia utekelezaji wa mikataba ili kuleta utendaji ulio bora.

8.5 Mkataba wa Bima wa Ujenzi wa Majengo Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania

Ukaguzi wa mkataba wa bima ya ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania ulibaini mapungufu kwenye mkataba huo kama ifuatavyo:-

- (i) **Kukosekana kwa Dhamana ya Bima.**
Kati ya jumla ya premiums za Dola za Kimarekani 6,302,823.42 ambazo Benki imelipa kwa wakala wa bima kati ya tarehe 20 February 2003 mpaka 24 July 2007, Benki imeweza kupata dhamana zenye thamani ya Dola Kimarekani 2,478,388 pekee na kuacha sehemu kubwa ya bima hizo kutokuwa na dhamana badala yake Benki ina barua tu kutoka kwa wakala.

Pia katika kipindi kati ya tarehe 20 February 2003 mpaka 24 July 2007, kulikuwepo mabadiliko ya kuongeza dhamana, gharama na kampuni za bima ambazo nazo hazikuidhinishwa na mamlaka husika, hata hivyo mabadiliko hayo nayo hayakuambatana na dhamana kama ilivyotakiwa kwenye mkataba.

- (ii) **Gharama za Bima Zilizozidi Kiwango**
Malipo ya gharama za bima katika mkataba wa awali zilikubaliwa kuwa kiwango cha asilimia 0.45 kwa “Contractors All Risk-Main”. Hata hiyo, mabadiliko yaliyofanyika kwenye mkataba huo yalipelekea Benki kulipa gharama kubwa zaidi kwa kiwango cha asilimia 0.91% mpaka asilimia 0.96% bila kupata idhini ya mamlaka husika.
Tulibaini pia kiwango cha gharama za bima kwa “Contractors All Risk-public liability” awamu ya kwanza (I) ilikubaliwa kuwa asilimia 0.175% sawa na Dola za Kimarekani 26,250, lakini gharama halisi iliyoonekana kwenye mkataba ni Dola za Kimarekani 130,550 na kupelekea kuwepo na ziada ya Dola za Kimarekani 104,300. Tulishindwa kujua sababu zilizopelekea pande zote mbili kusaini mkataba wenye tofauti hii kubwa. Vilevile, Benki Kuu ililipa Dola za Kimarekani 679,500 kwa wakala wa bima hata hivyo hapakuwa na maelezo ya kutosha kuhusu ukubwa wa gharama zilizolipwa kimakosa kwa ziada ya Dola za Kimarekani 267,550.

Mkataba wa awamu ya pili (II) ulitoa kikomo cha thamani ya bima kuwa Dola za Kimarekani 20,000,000 itakayogharimu Dola za Kimarekani 1,798,888 zitakazolipwa na Benki. Kwa kipindi chote cha ujenzi kwa kiwango cha asilimia 16. Kiwango hiki kinaonekana kuwa kikubwa bila sababu.

Hata hivyo pamoja na kukubaliana kiwango hicho hapo juu, Wakala wa Bima alileta madai yenye thamani ya Dola za Kimarekani 3,182,471.50 na hatimaye Benki kulipa madai hayo ambayo hayakuwapo kwenye makubaliano ya awali hivyo kufanya Benki kulipa ziada ya Dola za Kimarekani 1,383,583.5.

Vilevile, tulibaini kuwa gharama za bima katika mkataba wa awamu ya pili (II) zilikokotolewa kwenye thamani ya jengo badala ya kutumia kikomo kilichowekwa awali ambacho ni Dola za Kimarekani 20,000,000 hii ilifanyika kinyume na makubaliano ya mkataba.

(iii) **Kuingia Mikataba Miwili Inayofanana.**

“Public liability risk”: Wakati mkandarasi ilitakiwa kuweka aina hii ya bima kama ilivyo kwenye kifungu Na. 18 na 19 cha mkataba wa ujenzi, Benki nayo iliingia mkataba na wakala wa bima na kulipa fedha kwa ajili ya bima hiyo hiyo. Hata hivyo pamoja na kugundua suala hili Benki Kuu haijaweza kudai kurudishwa gharama za ziada kama ilivyokubaliwa kwenye kifungu Na. 19(3) cha mkataba.

“Damage to property risk”: kifungu Na. 18 na 19 cha mkataba wa ujenzi kinamtaka mkandarasi pia kuweka bima ya kuingia mali. Benki nayo ilinunua bima kama hiyo kutoka kwa wakala wa bima ambayo inaonyesha kuingia gharama mara mbili kwa bima ya aina moja.

(iv) **Sababu za Benki Kununua Bima Hazikupatikana**

Pamoja na kwamba benki ilipata ushauri wa kitalaamu katika kununua bima hizi. Tumbaki na maswali ambayo hayakupata majibu ya kutosha kama ifuatavyo:-

- Je benki ilifaidika nini kwa kuwakatia bima wataalamu washauri ambao ni M/s Architect WEBB Uronu, M/s Design & Services; M/s Inter-Consult, na M/s Tan Consult kwa ajili ya kazi zao za kitalaamu?
- Pia je kulikuwa na haja gani kwa Benki Kuu kukatia bima kampuni hizo badala ya kuziacha zikate zenyewe?

(v) Taarifa Zinazokinzana Kwenye Maktaba wa Bima Awamu ya Pili (II)

Taarifa zinazokinzana zilitolewa kwa uongozi wa benki. Kwa mfano wakala wa bima aliiandikia Benki Kuu kuwa awamu ya pili ya bima inapatikana Ulaya, Amerika na Afrika Kusini na alisisitiza kuwa hakuna kampuni hapa nchini inayoweza kutoa huduma kama hiyo ya bima. Taarifa hii iliongezewa uzito na Meneja wa mradi wa Benki Kuu ambapo alishauri uongozi kwamba bima hii ichukuliwe Afrika Kusini.

Hata hivyo tuligundua kuwa huduma hiyo ilichukuliwa hapa nchini kwenye kampuni ya M/s Alliance Insurance Corporation Limited na hivyo kuleta shaka juu ya taarifa zilizotolewa awali.

(vi) Taarifa Zinazokinzana Kuhusu Kampuni ya Bima
Awali bima ilionekana imekatwa kwenye kampuni ijulikanayo kama M/s Nova Risks Partners Ltd ya Afrika kusini na nyingine kuchukuliwa kwenye kampuni ya M/s Alliance Insurance Corporation Ltd ya Tanzania, lakini madai na malipo yalitoka kwenye kampuni zingine ambazo hazikuainishwa kwenye mkataba: Kwa mfano

- Ankara yenye nambari 6458 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 441,916 ilitoka kwa M/s Scintilla Insurance Company ya Afrika kusini na siyo M/s Nova Risks Partners Ltd.

- Ankara nyingine nambari 6459 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 432,000 ilitoka kwa M/s Santam Insurance Company ya Afrika Kusini kampuni ambayo haikuainishwa kwenye mkataba.
- Vilevile, ankara nambari 402706 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,028,903 ilitoka kwa M/s Scintilla Insurance Company ya Afrika Kusini.

Kutokana na taarifa zilizokinzana tunachukulia suala hili kuwa na mazingira ya utata na wasiwasi. Hivyo tunashauri Benki Kuu ianze kufanya uchunguzi wa suala hili na ichukue hatua zinazostahili ikiwa ni pamoja na kurejeshewa hela zitakazokuwa zimelipwa zaidi.

8.7 Usimamizi Mzuri Unahitajika Kwenye Sehemu Iliyobaki ya Mkataba wa Ujenzi wa Majengo ya Makao Makuu ya Benki Kuu.

Upembuzi wa mkataba wa ujenzi kati ya Group Five Building East (PTY) Limited na Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa majengo ya Makao Makuu yaliyopo mtaa wa Mirambo Dar es Salaam ulibaini mapungufu yafuatayo:

- Mkataba wa awali ulisainiwa tarehe 25 Juni 2002.
- Makubaliano ya gharama za ujenzi kwenye mkataba ilikuwa Dola za Kimarekani 73,600,000.
- Tarehe ya kuanza kwa ujenzi haikuonyeshwa
- Tarehe ya kumaliza ujenzi pia haikuonyeshwa
- Kifungu Na.13 cha mkataba kinaeleza kuwa “gharama za ujenzi haziruhusiwi kubadilishwa kwa namna yoyote ile. Hata hivyo Benki Kuu haikuheshimu kifungu hicho na hivyo kuruhusu mabadiliko ya gharama za ujenzi huo kuongezeka na kufikia dola za Kimarekani 284,671,000 kufikia tarehe 30 Juni 2008

Kubadilika Bei ya Ujenzi

Kwa Mfano Hati ya madai Na. 32 ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani 12,071,804.67 ikijumuisha Dola za

Kimarekani 6,517,230 zilizotajwa kuwa gharama za “prolongation” kwa ajili ya muda wa nyongeza na Dola za Kimarekani 71,500 zikiwa ni dhamana ya bima iliyolipwa na mkandarasi. Malipo haya hayakuwa na vielelezo vya kutosha kuonyesha makubaliano ya malipo kati ya benki na Mkandasi.

Jedwali A 15 (i) la majedwali ya masharti ya ujenzi linaeleza kuwa Mkandarasi amejumuisha kwenye gharama za awali za ujenzi thamani sawa na asilimia 5.39% ya gharama zote kwa ajili ya kufidia mabadiliko ya bei ya awali kwa kazi iliyopimwa awali.

Kifungu Na. 32 cha mkataba kinachoeleza mabadiliko ya gharama za ujenzi, kimefutwa kwa kalamu ya mkono bila kutolewa sababu maalumu ya kufanya hivyo. Kanuni Na.43 ya Sheria ya manunuzi (G.N Na. 97) inakataza kufutwa au kufanya marekebisho ya mkataba baada ya kusainiwa na pande zote mbili.

Pia kanuni Na. 44 inaeleza kuwa mabadiliko yoyote ya bei ya manunuzi lazima yapitiwe na kuidhinishwa na bodi ya zabuni.

Lakini mpaka tunamaliza ukaguzi mwezi Novemba 2008, hapakuwepo ushahidi wa kuonyesha kuwa madiliko yaliyofanywa kwenye bei yaliidhinishwa na bodi ya zabuni.

8.8 Usimamizi wa Gharama za Ushauri Katika Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Benki Kuu

Sambamba na mkataba wa ujenzi kuna mikataba ya ushauri majenzi (Quantity Surveyor) ya WEBB Uronu & Partners, Project Planning Consultants, Design and Services (Limited), na Tan Consult Limited.

Washauri hawa walitakiwa kutoa huduma zao kulingana na sheria za Tanzania za ubunifu na kusanifu majenzi yaani “The Architects and Quantity Surveyors Ordinance - By Laws 1950 (as revised in 1972)” Hata hivyo, jedwali la

malipo ya washauri lililombatanishwa kwenye mkataba linaonyesha namna ya kuwalipa washauri kama inavyooneka kwenye kifungu Na. 60 hapa chini;

- i) Kama bei ya mkataba itazidi paundi 2,000 watalipwa asilimia 5.
- ii) Kama bei ya mkataba haizidi paundi 2,000 watalipwa asilimia 10 kwa ujenzi unaogharimu paundi 250, na itashuka hadi kufikia asilimia 6 kwa ujenzi unaokaribia kugharimu paundi 2,000.
- iii) Asilimia hizi zinaweza kupunguzwa hadi kufikia asilimia 5 kwa kazi kubwa inayojirudia lakini kama hakuna kazi inayojirudia zitaendelea kutumia zile za awali kwa kazi isiyozidi paundi 2,000.
- iv) Kama kutakuwa na majengo mawili yenye sura sawa yanayojengwa kwa wakati mmoja na yako sehemu moja yakiwa kwenye mkataba mmoja malipo yatakuwa asilimia 6 ya gharama za jengo la kwanza na asimilia 3 kwa jengo jingine.

Gharama kwenye mkataba wa awali wa Group Five East (PTY) Limited uliosainiwa Mwezi Juni 2002 zilikuwa Dola za Kimarekani 73,600,000; na jumla ya malipo mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2008 yalikuwa yamefikia Dola za Kimarekani 284,671,176 sawa na shilingi 335,991,987,901. Mchanganuo wa malipo hadi tarehe 30 Juni 2008 kwa washauri ilikuwa kama ifuatavyo:

Jina la mkandarasi/mshauri	Malipo bado June 2008 Shs	Asilimia iliyokokotolewa kulinganisha na bei ya mkandarasi.
Design and Services Limited	39,801,670,160.36	11.85%
WEBB Uronu & Partners	24,349,296,705.35	7.25%
Inter Consult Ltd	8,921,404,091.60	2.66%
Tan Consult Ltd	5,991,508,081.47	1.78%

Malipo kwa Design and Services Ltd na WEBB Uronu & Partners yalikuwa juu ya viwango vilivyokubaliwa awali. Menejimenti ya Benki Kuu ilishindwa kudhibitisha sababu za kufanya malipo hayo kinyume na makubaliano. Tunashauri uongozi kutazama upya masharti hayo ili kuepuka kulipa gharama zaidi na hatua zichukuliwe kwa wahusika.

8.9 Utekelezaji wa Mkataba Wenye Shaka Mradi wa Mawasilano ya Kompyuta (ICT)-NSSF

Ukaguzi katika Mkataba ulioingiwa kati ya NSSF na M/s Micro Software Systems (T) LTD kwa ajili ya ushauri, kujenga mifumo ya kompyuta ya “oracle e-business suite applications and core fund management system” on 29/10/2004, iligundua mapungufu yafuatayo:

- Muda wa kumaliza kazi hiyo awali ulipangwa kuwa miezi 18 kuanzia tarehe 1/11/2004 hadi Aprili, 2006, uongozi uliamua kuwekeza zaidi na kupunguza muda wa kumaliza kazi kuwa miezi 12 badala ya 18 iliyopangwa awali. Hata hivyo NSSF kwa barua yake yenye kumb Na.NSSF/HQ/C.03/514/Vol.III/15 ilikuwa imepita miezi 24 bila mkandarasi kumaliza kazi yake. Hii inatupa wasiwasi juu ya maamuzi yaliyofanywa na uongozi kama yalizingatia thamani ya fedha kwenye mradi huu.
- Mkataba ulisainiwa tarehe 29/10/2004 ulionekana kuwa na tofauti katika bei ya kununua leseni ya Oracle ambapo mkataba uliandikwa kwa tarakimu dola za Kimarekani 512,000 lakini kwa maneno ulisomeka kuwa dola “laki tano elfu kumi na mbili na mia sita kumi na nane tu” yaani (512,618).
- Tarehe 12/9/2006 NSSF walilipa kwa ajili ya sehemu ya mradi wa Oracle “payroll systems” kiasi cha shilingi 24,390,000 yaani (USD 18,000@1355/-). Hata hivyo, mkataba ulikuwa hauruhusu kulipa sehemu tu bali kulipia mradi mzima.

- Mfumo uliokuwepo yaani “core system design” ulilazimika kuboreshwa ili kutatua matatizo katika kuhifadhi kumbukumbu (data) na hivyo kubadilisha tarehe ya kumaliza kazi kutoka 19/9/2006 hadi tarehe 8/10/06 bila kuzingatia muda wa awali ambao ulikuwa Aprili 2006. Hali hii inaonyesha kutokuwepo kwa upembuzi yakinifu wakati mradi huu unaanza.
- Tulibaini kuwa hapakuwepo na uhusiano mzuri kati ya pande mbili za mkataba pale NSSF ilipoandika barua kwenda kwa mkandarasi tarehe 7/11/2006 ikilalamikia kucheleweshwa kumalizika kwa ujenzi wa mradi.
- Mkurugenzi wa teknolojia ya habari alimwandikia barua Mkurugenzi Mkuu tarehe 8/9/2006 akimshauri kuidhinisha malipo kwa mkandarasi bila kuzingatia malalamiko na ushauri uliotolewa na watumiaji.
- Malipo kwenye mkataba hayakujumuisha kodi ambazo zilitakiwa kulipwa hapa nchini, hivyo kumsaidia mkandarasi akwepe kulipa kodi ambazo alistahili kulipa hapa nchini.
- Leseni ya kubuni na kujenga mfumo wa “core fund management system” haijaachwa kwa NSSF hivyo kuhatarasha utendaji wa NSSF kama ikitokea mfumo kushindwa kufanya kazi.
- Uhusiano wa makampuni yaliyooneka kwenye utekelezaji wa mradi yakiwa ni M/s Arowana Consulting Group ya Bangalore-India, Macro soft systems LLC ya Muscat Oman na Macro soft Systems (T) Limited ya Dar es salaam hukujulikana hivyo kuleta mashaka juu ya uhalali wake.

8.10 Mkataba Mbovu wa Uuzwaji wa Nyumba za NSSF Zilizopo Eneo la ADA - Estate Kinondoni

NSSF walinunua majengo na eneo lenye ukubwa wa ekari 4.6 kwenye kiwanja Na. 80/1 na Na. 90/2 vilivyopo eneo la ADA - Estate Kinondoni tarehe 6 Disemba 2000 kutoka TAZARA kwa gharama ya shilingi bilioni 1.4.

Mpango wa kuendeleza eneo hili ulianza mwaka 2002 kwa ajili ya kujenga majengo ya kuuza, na NSSF walianza kujenga majengo nane yenye ghorofa nne kila moja mwaka 2004 na kumaliza kujenga mwaka 2006 kwa gharama ya shilingi 5,940,805,946.00.

Mchakato wa kuuza ghorofa hizo ulianza kwa kutangaza zabuni kwenye gazeti la the “Express” la tarehe 02 hadi 08 Novemba, 2006 na tarehe 10 Januari 2007 zabuni ilitolewa kwa kampuni ijulikanayo kwa jina la M/s Seven Anchors Properties and Services Company limited

Ukaguzi wetu kwenye nyaraka zilizowasilishwa zinazohusu mauzo ya ghorofa hizo umegundua mapungufu yafuatayo:-

(a) Tathmini ya Zabuni

Hatukupata nakala halisi ya taarifa ya tathmini kwa sababu ilikuwa imechukuliwa na TAKUKURU. Hata hivyo kifani cha taarifa hiyo kilichopatikana hakikuwa na tarehe hivyo kuleta mashaka kama tathmini ilifanyika kama inavyotakiwa na kifungu Na. 33 cha Sheria ya manunuzi, 2004

(b) Muundo wa Kamati ya Tathmini

Tathmini ya zabuni hii ilifanywa na wajumbe sita kinyume na kanuni Na.90 (1) ya Sheria ya manunuzi, 2004 inayotaka wajumbe wa kamati hii wasipungue watatu na wasizidi watano. Vilevile, kamati ya tathmini iliteuliwa na Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala badala ya kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kama inavyotakiwa na kifungu Na.33 (e) cha Sheria ya manunuzi, 2004.

(c) Daftari la Kusajili Mahudhurio ya Kikao cha Zabuni

Kikao cha kufungua zabuni kinahitaji kuwepo na daftari la mahudhurio likiwa imesainiwa na pande zote yaani mwakilishi wa NSSF na mwakilishi wa wazabuni ambayo linasimama kama kielelezo

kwamba ufunguzi ilifanyika kwa uwazi halikupatikana wakati wa ukaguzi.

Vilevile, nyaraka zote za zabuni zilizowasilishwa hazikuweza kusomeka kwa sababu zimeharibiwa na maji hivyo taarifa muhimu kama vile majina ya wazabuni, na bei zao hazikupatikana. Kanuni Na. 19 (5) G.N. 97 ya Sheria ya manunuzi inatamka wazi kuwa taarifa zote zinazohusu zabuni zihifadhiwe kwa kipindi cha miaka mitano baada ya kumalizika kwa mikataba au shughuli za manunuzi ili zitumiwe na Waziri wa fedha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, au Mamlaka zinginezo. Hivyo NSSF imevunja kanuni hiyo hapo juu.

(d) Kuidhinisha Mauzo ya Nyumba Hizo

Bodi ya wadhamini katika kikao chake cha 37 kilichofanyika tarehe 18 Disemba, 2006 iliidhinisha kumuuzia mzabuni aliyetajwa hapo juu badala ya zabuni hiyo kuidhinishwa na bodi ya zabuni kama inavyoelekezwa na kifungu Na. 30 (d) cha Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004.

(e) Uzoefu wa Kampuni Iliyopewa Zabuni

Kampuni ya Seven Anchors Properties and Services Company limited, iliyonunua nyumba hizo ilisajiliwa tarehe 11 Oktoba 2006 ikiwa ni wiki tatu kabla ya kutangazwa kwa zabuni ya kuuzwa nyumba hizo tarehe 02 Novemba 2006. Ni maoni yetu kuwa NSSF haikuzingatia kigezo cha uzoefu wa kampuni kwenye biashara. Mambo haya hapo juu yanaleta shaka kwamba inawezekana kampuni hiyo iliundwa mahususi kwa ajili ya kununua nyumba hizo.

(f) Mkataba wa Mauzo

Mkataba pamoja na mambo mengine ulikuwa na vipengele muhimu kama ifuatavyo:

- i) Bei ya kununua nyumba itakuwa Dola za Kimarekani 6,510,000 sawa na Shilingi 8,550,234,000
- ii) Mnunuzi alitakiwa kulipa asilimia 10 ya bei ya kununulia kabla ya siku 15 toka tarehe ya kukubaliwa kununua yaani tarehe 10 Januari 2007 na kiasi kinachosalia kitalipwa ndani ya siku 90 kutoka tarehe hiyo hapo juu.
- iii) Gharama zote za kubadilisha umiliki toka kwa muuzaji kwenda kwa mnunuzi zitalipwa na mnunuzi.
- iv) Gharama zote za ulinzi, Bima na usafi zitalipwa na mnunuzi toka siku ya kulipa asilimia kumi.

Hata hivyo, ukaguzi uligundua mapungufu yafuatayo kwenye usimamizi wa mkataba huu:

➤ **Tofauti ya Tarehe za Kusaini Mkataba Kati ya Mnunuzi na Muuzaji**

Mkataba wa mauzo uliosainiwa tarehe 2 Oktoba 2007 na mnunuzi na kusainiwa na NSSF tarehe 4 Oktoba 2007. Tunautazama mkataba kama ulisainiwa bila pande mbili kuwa pamoja na mashahidi hivyo kuleta utata juu tarehe halisi ya mkataba. Vilevile mkataba ulisainiwa na Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji kinyume na kifungu Na. 33 (h) cha Sheria ya manunuzi, 2004 kinachomtaka Mkurugenzi Mkuu kusaini mikataba yote kwa niaba ya NSSF.

➤ **Kucheleweshwa kwa Malipo ya Awali.**

Malipo ya awali ya dola za Kimarekani 100,000 yalipokelewa tarehe 16 Aprili 2007 ikiwa ni miezi 3 baada ya kukubaliwa kununua, badala ya siku 15 kama

ilivyokuwa kwenye mkataba. Pia fedha ambazo zililipwa hazikuwa sawa na asilimia kumi (10%) ya bei ya kuuzia ambayo ilitakiwa kuwa dola za Kimarekani 651,000. Malipo hayo ya dola za Kimarekani 100,000 yalifanywa kupitia cheki Na. 487000454 ya tarehe 14 Aprili 2007 iliyotolewa na Mashreq Bank (Tawi la Zabeel) ya S.L.P 1250 Dubai, UAE. Pia tarehe 14 Mei 2007 Benki hiyo ililipa fedha zingine Dola za Kimarekani 551,000 kwa cheki Na.487000625.

Pamoja na kwamba mnunuzi hakuzingatia kifungu cha kulipa asilimia kumi (10%) ya bei ya kununulia ndani ya siku 15, hatukuweza kujua kama kulikuwa na chembe ya fedha haramu, hivyo kuongeza wasiwasi juu ya uhalali wa mauzo ya nyumba hizo.

➤ **Gharama za Kutunza Majengo**

Mkataba ulikuwa wazi kuwa gharama zote zitokanazo na usafi, ulinzi, na bima zitaanza kulipwa na mnunuzi baada tu ya kulipa asilimia kumi (10%) ya bei ya kununulia. Hata hivyo, NSSF waliendelea kulipa gharama zote baada ya tarehe 14 Mei 2007 mpaka tarehe ya kukabidhi majengo hayo yaani Oktoba 2008.

➤ **Kutozingatia Vipengele vya Malipo**

Mkataba uliweka wazi kuwa baada ya kulipwa kwa malipo ya awali ya asilimia kumi (10%) ya bei ya kununulia, asilimia tisini (90) inayobaki italipwa ndani ya siku 90 kutoka tarehe ya kukubaliwa kununua majengo hayo ambayo ilikuwa tarehe 1/11/2007. Hata hivyo ilimchukuwa mnunuzi takribani miezi kumi na saba (17) kabla hajalipa sehemu hiyo ya madai Septemba, 2008 hivyo kusababisha hasara ambayo haikujulikana kwa haraka kutokana na mabadiliko ya thamani ya fedha. Hatukuweza kujua sababu za NSSF kutositisha mkataba huu pamoja na madhaifu yote yaliyojitokeza. Tunapendekeza uchunguzi wa kina ufanyike ili kujua uhalali wa mauzo ya majengo haya.

8.11 Mauzo ya Jengo la Club Oasis bila Kufuata Utaratibu-NSSF

Kwa mwaka wa fedha tuliokagua NSSF waliuza jengo lake lililoko kiwanja Na. 489-517 block “J”, eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, kwa bei ya shilingi milioni 600 kwa kampuni ya M/s TILE FRESH Limited ya Dar es Salaam. Majengo hayo awali yalinunuliwa kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) tarehe 7 Augosti, 2003 kwa gharama ya shilingi 350,000,000 na kukabidhiwa kwa NSSF tarehe 30 Juni, 2004.

Ukaguzi wa nyaraka zilizohusika kuuza jengo hilo umebaini mapungufu yafuatayo:

- (a) **Kubadilishwa kwa Jina la Mnunuzi**
Uongozi wa NSSF ulikubali kubadilishwa jina kutoka kwa Dr. Hawa Sinare kwenda kwenye Kampuni ya M/s Tile fresh Limited, bila kupata idhini ya Bodi ya wadhamini.
Kampuni ya M/s Tile Fresh Limited ilisajiliwa tarehe 22 Disemba, 2004, siku ambayo Bodi ya Wakurugenzi iliidhisha kuuzwa kwa majengo hayo, hivyo kuleta wasiwasi kama kampuni hiyo iliundwa makusudi kwa ajili ya kununua majengo hayo.
- (b) **Majengo Hayakuuzwa kwa Njia ya Ushindani**
Hatukuweza kujua sababu za NSSF kutokuuza majengo hayo kwa ushindani kama inavyotakiwa na kifungu Na.59 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004 pamoja na kuwepo ukweli kuwa majengo hayo yalinunuliwa kwa ushindani kutoka TIB.

Dr.Hawa Sinare mnamo tarehe 10 Novemba 2004 kupitia kampuni nyingine ya M/s EPITOME Advocates ya Dar es Salaam alionyesha nia ya kununua majengo hayo bila mwaliko wowote, na NSSF mnamo tarehe 27 Disemba 2004. Uuzaji wa majengo hayo, ni jambo ambalo linatia shaka namna taarifa za kuuzwa

zilizyomfikia mnunuzi ukizingatia NSSF haikuwa na nia ya kuuza majengo hayo hapo awali.

- (c) **Kuchelewa Kukamilisha Mkataba wa Mauzo.**
Mkataba wa mauzo ulisainiwa tarehe 29 Ockoba 2007, ikiwa ni miaka mitatu tangu makubaliano ya awali ya kuuziana nyumba hiyo yaliyofanyika tarehe 27 Disemba 2004. Hatukupata sababu za kuridhisha zilizofanya NSSF kuuendelea kujikita kwenye mazungumzo ya muda mrefu kiasi hicho wakati uwezekano wa kuuza nyumba hiyo kwa ushindani ulikuwepo. NSSF wamepata hasara ya kushuka kwa thamani ya fedha kwani shilingi 600,000,000 ya mwaka 2004 sio sawa na shilingi 600,000,000 za mwaka 2007.
- (d) **Namna ya Kulipa na Kukabidhi Majengo Hayo**
Mkataba wa mauzo uliosainiwa tarehe 29 Oktoba 2007 ulikuwa wazi kwamba NSSF ilitakiwa kukabidhi majengo ndani ya siku 60 baada ya kusainiwa mkataba, lakini kabla ya malipo hayajafanyika ambayo ni shilingi milioni 600. Kwa upande mwingine mnunuzi alitakiwa kulipa ndani ya siku 7 baada ya kukabidhiwa majengo. Hati ya makabidhiano ilisainiwa tarehe 16 Novemba 2007 lakini dhamana ya malipo iliyotolewa na Benki ya CRDB ilipokelewa tarehe 10 Juni 2008 ikiwa ni zaidi ya miezi saba tangu tarehe ya kukabidhiwa.

Pamoja na mambo yote hapo juu, mpaka sasa suala la kuhamisha umiliki wa majengo hayo bado halijakamilika. Tunadhani kwamba mkataba huu sio sahihi na hivyo tunaomba uongozi uangulie uwezekano wa kusitisha mkataba huu na kuanza nyumba hiyo kwa ushindani.

8.12 Gharama za Nyongeza Kwenye Mkataba Bila Kuidhinishwa na Mhandisi Mshauri na Bodi ya Zabuni Shilingi Milioni 194

Shirika la Utangazaji Tanzania lilimpa mkandarasi Thompson Broadcasting and Media Limited ya Ufaransa jumla ya Euro 114,225 sawa na shilingi milioni 194 ikiwa ni gharama za nyongeza kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa vituo saba vya kurushia matangazo iliyotokana na kubadilika kwa hali ya udogo kwenye sehemu husika. Hata hivyo, malipo hayo hayakuidhinishwa na mhandisi mshauri wa mradi wala bodi ya zabuni japokuwa kulikuwa na ushauri kutoka kwa uongozi kuhusu nia ya kufanya hivyo.

8.13 Upungufu Katika Kusimamia Mikataba ya Kukodisha Mabweni katika Chuo cha Ustawi wa Jamii

Chuo kilikodisha nyumba sita kwa ajili ya mabweni ya wanafunzi wa chuo hicho kwa mwaka wa masomo 2007/2008 na kulipa shilingi 69,490,000. Makubaliano yalikuwa kwamba chuo kilipe gharama zote kisha wanafunzi watarejesha gharama hizo. Hata hivyo, kati ya fedha zilizolipwa jumla shilingi 36,650,000 hazikurejeshwa na wanafunzi kwani walikataa kuhamia kwenye mabweni hayo na hivyo kusababisha hasara ya kiasi hicho kwa chuo.

8.14 Mkataba Mbovu Kati ya Chuo cha Ustawi wa Jamii na Mobitel (MIC) TZ Limited

Chuo cha Ustawi wa Jamii kiliingia mkataba wa kukodisha eneo la ardhi la mita 20 x 30 kwa ajili ya kuweka mnara wa simu kwa kipindi cha miaka ishirini kwa kodi ya Dola za Kimarekani 6,000 kwa mwaka kwa kampuni ya Mobitel (MIC) TZ Limited kuanzia tarehe 5 Mei, 1998. Mobitel waliendeleza eneo kwa kujenga mnara na kibanda ambavyo vinatumika mpaka sasa. Mapungufu yafuatyo yalijitokeza kwenye mkataba huo:-

- **Kutokuwepo Kifungu Kinachoruhusu Mabadiliko ya Bei**

Kodi ya dola za Kimarekani 6,000 kwa mwaka kwa muda wa miaka ishirini ni ndogo ukizingatia kushuka kwa thamani ya fedha kila siku. Tunadhani kulikuwa na haja ya mkataba huo kutazamwa upya ili kuendana na hali halisi ya mabadiliko ya thamani ya fedha.

- **Kutokuwepo Kifungu Kinachoweka Wazi Hatima ya Kibanda na Mnara Baada ya Kipindi cha Mkataba Kumalizika**

Kampuni ya Mobitel walijenga kibanda na mnara katika ardhi inayomilikwa na chuo. Hata hivyo, hapakuwepo na kifungu chochote kwenye mkataba kinachoelekeza kuhusu umiliki au uondoaji wa kibanda pamoja na mnara baada ya mkataba kuisha.

- **Kutokamilika kwa Mkataba Husika**

Chuo kilisaini mkataba na kupeleka kwa Mobitel kwa ajili ya kusaini ili mkataba huo ukamilike ambapo chuo kiliikumbusha kampuni ya Mobitel kurudisha mkataba huo kwa barua yenye kumb.Na NSWTI/AGC/M.32/17 ya tarehe 19 Oktoba, 1998 baada ya kusainiwa. Hata hivyo, kampuni ya mobitel ilijibu kwamba mkataba wa awali umepotea na kuomba wapelekewe nakala nyingine. Pamoja na kupelekewa nakala nyingine, Mobitel hawakuwahi kusaini mkataba huo mpaka sasa na kufanya mnara huo kujengwa isivyo halali. Ukaguzi pia ulibaini kuwa kampuni ya Mobitel haijalipa kodi kwa vipindi viwili mfululizo yaani mwaka 2007/08 na 2008/09.

8.15 Mkataba Ulioisha Muda Wake Kati ya Serikali na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine

Katika ukaguzi wa mkataba kati ya Chuo Kikuu cha Sokoine na Serikali kwa ajili ya ukodishaji wa chuo cha misitu kilichopo Olmotonyi Arusha, imebainika kuwa

mkataba wa awali wa miaka kumi (10) uliosainiwa mwaka 1997 na umeisha muda wake mwezi Juni mwaka 2007 na mpaka sasa hakuna mkataba mpya ambao umekwishasainiwa. Tunashauri uongozi wa chuo ufanye jitihada kuhakikisha kuwa wanaingia mkataba na Serikali ili kuepusha matatizo yanayoweza kujitokeza endapo mgogoro utatokea.

SURA YA TISA

USIMAMIZI WA RASILIMALI

9.0 Utangulizi

Usimamizi wa raslimali ni mfumo unaojitosheleza wa namna ya kudhibiti raslimali za Shirika au Taasisi kwa utendaji ulio bora kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kutoa huduma bora kwa jamii. Raslimali zinawakilisha utajiri unaomilikiwa na Shirika au Taasisi na hivyo kuhitaji usimamizi wa umakini na wa hali ya juu.

Kinyume na matarajio ya ukaguzi, katika mwaka wa fedha 2007/2008 kulionekana mapungufu katika usimamizi wa mali za kudumu na zisizo za kudumu. Matatizo yaliyojitokeza kwa kupindi tulichokagua ambayo tunadhani ni muhimu kuyatolea taarifa ni kama ifuatavyo:-

9.1 Uwekaji Mbovu wa Kumbukumbu na Kukosekana Bima kwa Rasilimali

Raslimali ziligundulika kutoingizwa kwenye daftari la mali za kudumu kama inavyotakiwa na miongozo ya ndani ya utawala wa Mashirika ya Umma. Pia raslimali za kudumu hazikukatiwa bima ili kuzikinga na athari zinazoweza kutokea. Mfano wa Mashirika yaliyokutwa na mapungufu hayo ni kama ifuatavyo:-

Na.	Taasisi	mapungufu
1.	TCRA	Mamlaka haina daftari la mali za kudumu. Mali za kudumu hazijafanyiwa tathmini kwa muda mrefu.
2.	PPRA	Mali za kudumu hazina bima. Daftari la mali za kudumu halina taarifa muhimu kama mahali ilipo, nambari ya utambuzi, jumla ya gharama za uchakavu na thamani halisi ya mali.

		Mali za kudumu hazihesabiwi mara kwa mara.
3.	DUWASA	Mamlaka haina daftari la mali za kudumu.
4.	TBC	Shirika halina daftari la mali za kudumu.
5.	CDA	Mali za kudumu hazina bima. Mamlaka haina daftari la mali za kudumu.
6.	IRUWASA	Mali za kudumu hazina bima.
7.	Mbeya UWSA	Mali za kudumu hazina bima.
8.	TAFORI	Mali za kudumu hazina bima.
9.	NEMC	Mali za kudumu hazina bima.
10.	TPA	Hakuna daftari la mali za kudumu zilizopo kituo cha Mwanza.
11.	LUWASA	Mali za kudumu hazina bima.
12.	TSHTDA	Mali za kudumu hazina bima.
13.	DIT	Mali za kudumu hazina bima.

9.2 Umiliki wa Rasilimali

Ukaguzi wa umiliki wa rasimali kwenye mashirika ya umma umegundua yafuatayo:-

- 9.2.1 Kukosekana kwa Kadi za Umiliki wa Magari na Pikipiki.
Magari na pikipiki za Mamlaka ya Maji Mbeya yaligundulika kutokuwa na kadi za umiliki. Maelezo yaliyotolewa na uongozi kwamba magari hayo na pikipiki yaliletwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na.	Aina ya pikipiki	Gharama awali	Thamani halisi
STJ 689	TOYOTA	10,988,550	294,972
STH 1505	ISUZU LORRY	6,073,600	398,039
STJ 6059	ISUZU PICKUP	10,240,000	671,089
STG 379	HONDA	1,703,593	56,022
STJ 379	HONDA	1,500,000	49,327
ST 381	HONDA	1,677,200	55,154
		32,182,943	1,524,603

Na.	Aina ya ghari	Thamani
DFP 1308	Toyota Land Cruiser (St. Wagon)	59,601,134
DFP 1309	Toyota Hilux Double Cabin	11,264,075
DFP 1310	Toyota Hilux Double Cabin	11,264,075
Jumla		82,129,284

9.2.2 Kukosekana kwa Kadi za Umiliki -TAFORI

Pia Taasisi ya utafiti wa Misitu haina umiliki halali wa mali zifuatazo:-

Aina	Na.	Jina la mmiliki	Maoni
Pikipiki	TZL 1683	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Pikipiki	TZL 1684	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Pikipiki	TZL 1685	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Pikipiki	TZL 1686	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	Imesajiliwa DFP 4544
Pikipiki	TZL 1681	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	Imesajiliwa DFP 4545
Pikipiki	TZL 1682	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	Imesajiliwa DFP 4543
Gari	SU 34567	Utafiti wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Gari	SU 34574	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Gari	SU 34573	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Gari	SU 34572	Mradi wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Gari	SU 34569	TAFORI Box 1854 Dar es Salaam	
Gari	SU 34570	Utafiti wa Misitu S.L.P 292 Morogoro	
Gari	SU 34571	TAFORI OFI AGROFOREST PROJECT, Box 1854 Morogoro	

9.2.3 Magari ya Benki Kuu Yamesajiliwa kwa Namba Binafsi.

Tulipokuwa tunakagua mali za Benki kuu ya Tanzania tulingundua magari matatu yakiwa na usajili wa namba za binafsi.

S/N	Aina ya gari na namba ya usajili
1.	Toyota Land Cruiser VX T.312 ALH
2.	Toyota Land Cruiser VX T.288 ALH
3.	Toyota Land Cruiser T658 AHM

9.2.4 Umiliki wa Kiwanja Na. 21-Tabora na Bodi ya Tumbaku

Upembuzi wa mali zinazomilikiwa na bodi ya tumbaku umegundua kuwa Bodi ina hati miliki Na. 12155 iliyotolewa mwaka 1957 kwa muda wa miaka 99 kumiliki kiwanja Na. 21 kilichopo Tabora Mjini. Tulingudua pia kiwanja hicho hakipo kwenye vitabu vya Bodi kwa sababu inasemekana kilirudishwa Serikalini. Ushahidi kuthibitisha taarifa hizo haukupatikana hivyo kuleta shaka juu ya umiliki wake.

9.2.5 Kukosekana kwa Hatimiliki

Ukaguzi uligundua kukosekana kwa hatimiliki za viwanja katika mashirika mbali kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Na.	Taasisi	Na. ya kiwanja
1.	Bodi ya Korosho Tanzania	16
2.	CDA-Dodoma	40
3.	Mamlaka ya Maji Iringa	4
4.	Mamlaka ya Maji- mbeya	10
5.	Mamlaka ya Maji Arusha	4
6.	Mamlaka ya Maji Musoma	8
7.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	7
8.	Benki Kuu ya Tanzania	Kitalu Na. 28A

		Zanziba.
9.	VETA-Plots	3
10.	Taasisi ya Elimu Tanzania	5
11.	Soko la Kariakoo - Mbezi house	1
12.	Tanzania Small Holders Tea Development Agency	16
13.	Chuo cha Uhasibu Arusha	1
14.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii	9
15.	Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT)	11
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi	8

9.2.6 Mgogoro wa Kiwanja Na. 250 Block 'T' Barabara Kenyatta-Mwanza- NSSF

NSSF walinunua Kiwanja Na. 250 block 'T' tarehe 10 Septemba 2005 kutoka kwa Kassim Omari wa S. L. P. 327 Mwanza ikiwa ni nyongeza ya kiwanja Na. 254 block "T" kwa ajili ya kujenga jengo la kibiashara lijulikanalo kama "NSSF Commercial Complex" Mwanza.

Kabla ya kumlipa Kassimu, NSSF waliamua kuthaminisha kiwanja hicho na Mthamini alitoa makadirio ya kiasi cha shilingi 29,800,000, Kassim Omari alidai kiasi cha shilingi 14,000,000 ikiwa ni gharama za nyongeza za kuendeleza kiwanja hicho na NSSF hatimaye walilipa kiasi cha shilingi 43,800,000 tarehe 10 Septemba 2005 bila kusaini mkataba wa makabidhiano ya fedha.

Baada ya NSSF kuendeleza na kumaliza kujenga jengo hilo, Kassim Omari aliibuka baada ya miaka mitatu akidai kuwa kiasi cha fedha alicholipwa ni nusu ya kiwanja, hivyo anaomba kulipwa kiasi kama kile cha mwanzo kama ilivyoonekana kwenye barua yake ya tarehe 18 Machi 2008.

Hivyo pande mbili hizi wameingia kwenye mgogoro ambao ulikuwa haujaisha hadi tunafanya ukaguzi mwezi Disemba, 2008.

9.3 Utunzaji wa Vifaa.

Utunzaji wa vifaa na udhibiti wa vifaa lazima uzingatie kanuni na matakwa ya kitalaamu ambayo yanakubalika. Pamoja na kwamba eneo hili halikufanyiwa ukaguzi wa kina, lakini katika ukaguzi umegundua baadhi ya udhaifu katika utunzaji vifaa ikiwa ni pamoja na kutokuwepo na stoo za hadhi, bidhaa kutokuingizwa vitabuni, kutokuhesabu mali mwisho wa mwaka, kutowaalika wakaguzi wa nje wakati wa kuhesabu mali, na kutotoa maelekezo namna ya kuhesabu mali.

9.4 Rasilimali Zisizopimika Ambazo Hazitumiki na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine

Ukaguzi wa mali zisizopimika za Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ulibaini kuwepo kwa mali ambazo ni ‘Kovis Documentation Software’ na ‘5ACL Version 8 Auditing Software’ yenye thamani ya shilingi milioni 33 zilizonunuliwa mwaka 2004 na 2005. Mali hizo hazikuwahi kutumika tangu zinunuliwe. Vilevile, ukaguzi ulibaini kwamba leseni za mali hizo hazijalipiwa kwa muda mrefu kiasi cha Dola za Kimarekani 18,000 na hivyo kufungiwa kuzitumia. Hali hiyo hapo juu inaashiria kuwa mali hizo zilinunuliwa bila kuwa na mipango endelevu ya kuzitumia.

9.5 Udhaifu katika Kusimamia Upangaji wa Nyumba za Wafanyakazi- Chuo cha Ustawi wa Jamii.

Mikataba ya upangaji ya wafanyakazi Chuoni hapo imebainika kuwa mikataba mingi iliisha muda wake bila kuongezwa kama inavyotakiwa katika kipengele mojawapo cha mkataba. Pia mikataba mingine ilichukua muda wa zaidi ya miaka sita bila kuongezwa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

Na.	Jina la Mpangaji	Kitalu	Mwisho wa Mkataba	Tarehe kuhuhishwa
1.	Esther D. Kapteni	C-1	15.8.2001	1.7.2007
2.	D.T. Luhanga	B-4	6.1.2006	1.7.2007
3.	Tully Msirikali	B-3	Dec. 2001	1.7.2007
4.	Nkwame Ibrahim	B-8	10.3.2003	1.7.2007

5.	Dr. Lawrence Vitto	B-7	1.7.2004	Hakuna mkataba mpya
6.	Zeno Ngowi	D-8	1.3.2007	Hakuna mkataba mpya
7.	Myung Chin Song	B-1	Jan, 2003	Hakuna mkataba mpya
8.	Thomas D. Kasilila	B-6	1.3.2004	Hakuna mkataba mpya

9.6 Serikali Haijalipa Gharama za Kiwanja cha TPA

Mnamo mwaka 1996, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilinunua kiwanja Na. 2459/35 kilichopo mtaa wa Shaaban Robert na Garden Avenue kwa gharama ya shilingi 362,995,415 kwa ajili ya kujenga jengo la kitega uchumi. Hata hivyo, mradi huu haukuanza mara moja kwa sababu mbalimbali.

Wakati mamlaka ikijipanga kuanza ujenzi huo, Serikali iligawa kiwanja hicho kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa bila kuirejeshea Mamlaka ya Bandari fedha walizotumia kununua kiwanja hicho. Gharama zilizolipwa na Mamlaka ya Bandari ni kama ifuatavyo:-

	Shilingi
Gharama ya ununuzi tarehe 04.02.1997	362,692,440
Gharama za kutathmini	302,975
Total	362,995,415

Tuliarifiwa kuwa Mamlaka ya Bandari imepeleka madai hayo Serikalini lakini mpaka sasa hakuna majibu.

9.7 Masurufu, Mikopo, na Kodi za Pango

Taasisi zinazoendeshwa kwa mfumo wa “accrual” zinatakiwa kuwa na mikakati madhubuti kuhakikisha kuwa fedha zilizotolewa kwa wateja au watumishi zinakusanywa kwa wakati ili kuwezesha utendaji ulioboreka. Lakini ukaguzi wa hesabu za mashirika umebaini mapungufu kwenye udhibiti wa masurufu, mikopo, na kodi za pango kama ifuatavyo:-

9.7.1 Masurufu ya Muda Mrefu Ambayo Hayajarejeshwa
Sh.17,629,973,487

Ukaguzi wa hesabu za mashirika mbalimbali umebaini kuwepo kwa masurufu ambayo hayajarejeshwa yenye thamani ya Shilingi 17,629,973,487 kama ifuatavyo:-

Na.	Taasisi	Maelezo	Thamani Shs.
1.	MUWASA	Masurufu ya muda mrefu	332,465,008
2.	DAWASCO	Masurufu ya muda mrefu	432,427,750
3.	MNH	Masurufu ya muda mrefu	141, 442,424
4.	TANESCO	Masurufu ya muda mrefu	285,602,774
5.	Mbeya UWASA	Masurufu ya muda mrefu	827,448,990
6.	NIP	Masurufu ya muda mrefu	97,961,943
7.	TCRA	Masurufu ya muda mrefu	9,285,082, 678
8.	LUWASA	Masurufu ya muda mrefu	107,678,623
9.	NIC	Masurufu ya muda mrefu	1,291,145,642
10	TEA	Masurufu ya muda mrefu	64,270,000
11.	Reli Assets Holding	Masurufu ya muda mrefu	4,742,216,436
12.	NSSF	Masurufu ya muda mrefu	22,231,219
Jumla			17,629,973,487

9.7.2 Masurufu Yasiyorejeshwa Kutoka kwa Wafanyakazi Walioacha Kazi Sh.79,657,529

Katika shirika la hifadhi ya jamii na Benki ya Posta Tanzania kuligundulika kuwepo kwa masurufu na mikopo kwa waliokuwa wafanyakazi wa mashirika hayo ambao wameacha kazi na kuacha madeni yenye thamani kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Na.	Taasisi	Maelezo	Thamani Shs.
1.	NSSF	Masurufu na mkopo wa watumishi	54,350,499
2.	TPB	Masurufu na mkopo wa watumishi	25,307,030
Jumla			79,657,529

9.7.3 Kodi za Pango Zisizolipika Kutoka Waliokuwa Wapangaji wa Nyumba za NSSF- Sh. 1,133,446,161

Uchambuzi wa mahesabu ya NSSF imebaini kuwepo madeni yenye thamani hiyo hapo juu ikiwa ni madeni ya waliokuwa wapangaji wa nyumba za Shirika hilo. Hapakuwepo na ushahidi kujua jitihada zinazofanywa ili kukusanya fedha hizo hapo juu ambayo yamekuwa chechefu kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja.

9.8 Kukaa na Fedha za Wafadhili bila Kuzitumia kwa Muda Mrefu-TANAPA - Sh. 126.3 milioni

TANAPA walipokea fedha kutoka kwa wahisani kwa ajili ya kutekeleza shughuli maalumu ikiwa ni pamoja na kufundisha watumishi na shughuli zingine za afya.

Hata hivyo tulibaini kuwa fedha hizo ziliwekwa bila kutumika kwa muda mrefu na kufanya shughuli zilizopangwa kutotekelezwa. Kwa mfano kulikuwa na fedha za mafunzo jumla shilingi milioni 126.3 kutoka kwa wahisani hadi kufikia tarehe 30 Juni 2008 ambazo hazikutumika kwa zaidi ya miaka mitatu.

9.9 Udhaifu katika Kusimamia Mikopo Iliyotolewa na Benki Kuu.

Ili Kusaidia ukuaji wa kilimo na kuongeza usafirishaji wa bidhaa za ndani na nje ya nchi Serikali iliamua kuanzisha huduma ya kusadia kampuni za ndani zenye sifa kupata mikopo kwenye benki ya biashara iliyoteuliwa ili kutoa mikopo hiyo. Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa na mfuko wa dhamana ambapo baadae Serikali ilitoa “Treasury Special Bonds” kwa ajili ya madhumuni hayo.

Kwa sasa kuna kampuni sita (kampuni nne zikiwa za kusafirisha maua nje ya nchi, moja kwenye kilimo cha mboga na nyingine kwa ajili ya ufugaji wa kuuza mazao ya wanyama nje ya nchi) yalifaidika na mikopo hiyo. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalionekana kwenye utekelezaji wa mpango mkakati huo.

Mkataba wa kutekeleza mpango huu kati ya Benki Kuu na Benki ya Uwekezaji (TIB) ulisainiwa mwezi Mei 2008 wakati utekelezaji wa mpango huu ulianza mwaka 2006. Hii ina maana ya kuwa utekelezaji huo ulianza bila kuwepo na makubaliano ya pande mbili.

Pamoja na kuwa benki teule zilitekeleza mpango huu chini ya udhamini wa benki kuu yaani, Benki ya biashara hazitapata hasara endapo mteja atashindwa kulipa, hapakuwepo na mpango wa Benki Kuu kuchukua tahadhari kama kukinga athari zinazoweza kujitokeza. Kwa mfano, kwa sasa Benki Kuu haina taarifa muhimu za utendaji wa kampuni ambazo zimejiingiza kwenye mpango huu. Taarifa kama hesabu zilizokaguliwa ni muhimu kuiwezesha benki kuwajua wakopaji.

9.10 Kukusanya Mikopo Kutoka kwa Wateja wa Benki ya Posta Tanzania

Ukusanyaji wa madeni katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi ulikuwa sio wa kuridhisha. Sehemu kubwa ya mikopo

iliyokuwa imetolewa kwa wateja ilikuwa haijarejeshwa hadi kufikia mwisho wa kipindi ambacho walitakiwa kurejesha. Hii ina maana kwamba wakopaji walikuwa hawalipi madeni kama ilivyokubaliwa. Tuligundua kuwa hali ya madeni ambayo ni chechefu hadi tarehe 31 Disemba 2007, yalikuwa shilingi 647,760,329 na madeni yaliyofutwa kwa mwaka yalikuwa shilingi 1,777,846,427. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na benki za kutumia dalali kudai madeni ikiwa ni pamoja na kushikilia mali za wakopaji dalili za kurejeshwa kwa mikopo hiyo bado sio nzuri.

Mfano wa mikopo ambayo hailipiki ni kama ufuatavyo:

Jina la Mkopaji	Tarehe ya mkataba	Thamani ya Mkopo	Tarehe ya kurejesha	Salio 31.12.2007
Mkopo wa biashara		Sh.		Sh.
Metro Julius Reuben Mbiduka	28.09.2005	13,887,717	28.10.2007	4,757,541
Susan Ernest Kisanji	16.12.2003	17,468,926	16.12.2005	4,398,461
Valerian Faustin Tesha	04.08.2006	8,000,000	04.09.2007	4,946,449
Pili Hamisi Mwamba	27.08.2004	7,000,000	27.08.2005	4,589,764
EM Trucking Co.Ltd	16.08.2005	30,000,000	16.11.2005	9,420,598
Rochoice Engineering Works Ltd	31.12.2003	41,206,954	28.09.2006	18,293,575
Thomas Mjewa Oswald	15.10.2003	6,086,332	15.04.2005	3,874,425
Jonat Hussein Msuya	17.08.2005	10,000,000	17.08.2007	6,814,780
Aisha Leonard Mhina	16.09.2005	10,000,000	16.09.2007	3,753,150
Laurential	31.08.2005	10,000,000	31.08.2007	4,330,356

Michael Mvungi				
Medson Andrea Sanga	31.01.2002	15,125,000	08.02.2004	5,803,546
Isaka Juma Mseme	11.03.2004	14,427,778	11.03.2006	3,790,040
Malongoza Hesaya Godson	30.06.2003	8,200,000	30.12.2004	5,762,608
Makala Idi Makala	30.06.2003	8,100,000	30.12.2004	7,729,464
Samweli Frank Samweli	30.06.2003	11,200,000	30.12.2005	8,470,460
Nicolaus Wilson Mushi	29.09.2003	8,462,671	29.09.2005	5,792,068

9.11 Tuhuma za Wizi wa Kughushi Uliofanywa na Wafanyakazi wa TPB

Bakaa ya fedha za tuhuma za wizi wa kughushi uliokuwa umefanywa na watumishi wa Benki ya Posta Tanzania iliyokuwa imejumuishwa na mapato mbalimbali ya baadae (sundry receivables) imeongezeka kutoka shilingi 95,748,037 kufikia tarehe 31 Disemba, 2006 hadi shilingi 152,724,256 Disemba, 2007. Tuliambiwa kuwa Benki ilipeleka madai ya bima ya shilingi 95,748,037 kwa Shirika la Bima ya Taifa kwa ajili ya wizi huo wa kughushi uliofanywa na wafanyakazi wa benki kipindi cha miaka iliyopita na nyongeza ya madai inayofikia shilingi 26,340,000 ilipelekwa shirika la bima katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31/12/2007.

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini kuwa, mnamo mwezi Machi 2008 Shirika la Bima lilithibitisha kuwa litarejesha shilingi 20,203,837 na asilimia 70% ya fedha hizi ambazo ni shilingi 14,142,686 zilishalipwa kupitia cheki Na.171519 ya tarehe 19/3/2008. Benki ilidai na kupata shilingi 5,000,000 kutoka

mafao ya Dafrosa Mushi aliyekuwa ameachishwa kazi mwezi Machi 2008. Hadi tunamaliza ukaguzi mwezi Machi 2008 madai ya bima kwa wizi wa kughushi uliokuwa umefanywa na watumishi wa Benki ya Posta Tanzania ya kiasi cha shilingi 30,636,219 yalikuwa hayajalipwa na Shirika la Bima na kiasi kilichotakiwa kurejeshwa na Shirika la Bima mbali na madai hayo ya muda mrefu ya kiasi cha shilingi 96,884,200 kilikuwa bado hakijathibishwa

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini kuwa mchanganuo wa umri wa madeni na orodha ya watumishi waliokuwa wamehusika na wizi wa kughushi haikuwa imeandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Pia hapakuwepo na tengo la madeni chechefu lililokuwa limetengwa kwenye hesabu kwa ajili ya deni lilotajwa hapo juu, kwa hiyo, wakaguzi hawakuweza kujiridhisha kwa uhakika kuhusu ukusanyaji wa fedha zilizotajwa hapo juu.

9.12 Usimamizi wa Uwekezaji

Uwekezaji katika maeneo mengine ni changamoto ambazo ni muhimu na zinahitaji mipango mikakati madhubuti kama mtu analenga kupata faida au kufikia lengo alilokuwa amelikusudia. Upembuzi wa uwekezaji katika sehemu mbalimbali kunakofanywa na baadhi ya mashirika ya umma ulibaini baadhi ya mapungufu kama yalivyoorodheshwa hapo chini:-

9.12.1 Jitihada Pungufu Katika Kusimamia Mkataba wa Kuchangia Gesi na Panafrican Energy (T) Company Limited

Upembuzi wa mikataba mbalimbali ya kuchangia gesi (PSAs) iliyokuwa imeingiwa kati ya Serikali na TPDC kwa upande mmoja na makampuni mbalimbali kama vile SONGAS Tanzania Limited na PanAfrican Energy (T) Company Limited kwa upande mwingine ulibaini kuwa ndani ya mkataba kulikuwepo na kipengele kilichokuwa kinazitaka kampuni za uzalishaji kurejesha asilimia 75 ya

gharama zake kutokana na mauzo ya gesi kabla ya kugawana faida. Kampuni ya PanAfrican Energy (T) Company Limited ilikuwa inarejesha gharama za uzalishaji asilimia 75 kabla ya kugawana faida. Ili kuwa na uhakika wa gharama halisi kampuni ilizotumia, TPDC lazima ijiridhishe yenyewe na uhalali wa gharama zilizodaiwa kwa kufanya ukaguzi wa gharama zilizotumika na kampuni ya uzalishaji umeme kwa mujibu wa kipengele Na. 21.2 cha PSA kati ya Serikali, TPDC na PSA.

Kitengo cha ndani cha ukaguzi cha TPDC kinatakiwa kipewe jukumu la kufanya uhakiki wa gharama zilizoingiwa na kampuni na ili kuhakikisha jukumu hilo linatekelezwa, kitengo kinatakiwa kutumia utaalumu wa wataalamu kutoka idara nyingine za TPDC. Tulibaini kuwa kitengo hakikuwahi kutekeleza jukumu hilo na kwa hiyo kampuni ya kuzalisha umeme inarejesha gharama zake kwa tarakimu ambazo hazijahakikiwa na TPDC. Katika hali hii Serikali inaonekana kuwa nje ya udhibiti wa gharama za makampuni yanayozalisha umeme ambayo ni msingi muhimu wa kugawana faida kwa pande zote mbili.

9.12.2 Uwekezaji wa TANESCO Katika Kampuni ya SONGAS Limited Shilingi Bilioni 5

Kutokana na hesabu zilizokaguliwa za kampuni ya SONGAS Limited kwa mwaka ulioishi tarehe 31/12/2007 kampuni baada ya kodi ilipata hasara ya USD 4,935,000. Zaidi ya hayo, jumla ya madeni yalizidi jumla ya rasilimali kwa dola za Kimarekani 3,478,000 ikiashiria kwamba uwezo wa kampuni kuendelea kufanya biashara uko mashakani. Hata hivyo mapato yanayozalishwa na TANESCO yanaendelea kushikiliwa na SONGAS Limited kwa uwekezaji wa baadae. Jumla ya kiasi kilichokuwa kimeshikiliwa hadi Disemba 2007 kilikuwa shilingi bilioni 5.

Kutokana na matatizo ya kifedha inayoikumba kampuni ya SONGAS Limited, kiasi kinachoshikiliwa kinaweza kuwa hatarini kurejeshwa. Badala ya kiasi cha fedha kuendelea

kushikiliwa na SONGAS, TANESCO ingeweza kuwekeza kiasi hicho kwenye sehemu yenye faida.

9.12.3 Kutokuwapo na Taarifa za Nyumba za NDC

Ukaguzi ulibaini kuwa nyumba zilizokuwa imepewa Shirika la NDC kati ya miaka ya 1967 na 1970 hazikuwa zimejumuishwa kwenye jedwali la nyumba za shirika na pia hapakuwepo na mapato ya kodi ya pango iliyokuwa imekusanywa kutoka vitega uchumi (nyumba) hizi, japokuwa shirika lilikuwa na hati miliki. Orodha ya nyumba hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kitalu Na.529 Msasani Penusula yenye hati miliki Na. 186216/57
- Kitalu Na.528 Msasani Penusula yenye hati miliki Na. 186216/58
- Kitalu Na.523 Msasani Penusula yenye hati miliki Na. 186216/47

Kutokuingizwa taarifa za nyumba hizi kwenye jedwali la nyumba za Shirika kunaweza kusababisha upotevu wa nyumba hizi bila menejimenti kujua.

9.12.4 Kuwekeza Kwenye Miradi Isiyokuwa na Tija

Sehemu ya 62 ya Sheria ya NSSF Na.28. ya mwaka 1997 inaipa nguvu bodi ya wadhamini ya NSSF kuwekeza kwenye miradi yenye tija. Upembuzi wa mikataba ulibaini kuwa kiasi kikubwa cha fedha kilikuwa kimekopeshwa kwenye makampuni mbalimbali ambayo ilikuwa haina tija kiuchumi na kibiashara kama inavyotakiwa na sehemu ya sheria iliyotajwa hapo juu. Zaidi ya hayo, kipengele Na.5.4 cha Sera ya mfuko wa uwekezaji ya mwaka 2007, inataka mfuko kuachana na kuwekeza kwenye miradi ambayo haina tija. Hata hivyo, ifuatayo ni orodha ya mikopo ambayo imebainika kutokuwa na tija na ambayo NSSF haijafikia uamuzi wa kuachana nayo kama inavyotakiwa kisheria:-

NA	MKOPAJI	MAPUNGUFU
1.	Kilimanjaro Bazaar - Sh 105 M at 31% p.a (1990,1991,1992)	Mkopaji alishinda kesi baada ya NSSF kumshitaki mkopaji aliyeshindwa kulipa deni na baadaye NSSF iliamriwa kulipa Sh.600 milioni. NSSF ilikata rufaa tarehe 27/2/2007 na hadi Aprili 2008 kesi ilikuwa haijaanza kusikilizwa.
2.	Mbowe Hotels Limited - Sh 15 M at 31% p.a and 12% p.a (1994,1999)	Mkopaji alishindwa kulipa na mfuko ulilazimika kumshitaki ambapo kesi haijaisha.
3.	Emunio Tanzania Limited- USD 1.86 M at 8% p.a USD (2004)	Mkopaji alishindwa kulipwa na baadaye ilibainika kuwa kampuni ipo kwenye mchakato wa kujiunda upya na mazungumzo na mwekezaji yalikuwa yakiendelea ambapo hisa ambazo zingelipwa na muwekezaji zingetumika kulipa mkopo wa NSSF.
4.	Ubungo Plaza Limited (UPL) - Sh 1,284.2 M at 10% p.a (2004)	Utaratibu wa kurejesha mkopo ulibadilishwa kwa kuzingatia hali ya kifedha ya mkopaji na sasa mkopo utarejeshwa mwezi Machi 2010.
5.	Kagera Sugar Company Limited- Sh 12 Billions at 10% p.a (2004,2005)	Mkopaji ameshindwa kulipa faida ya tozo la mkopo wake na matokeo yake faida ya tozo la mkopo limefikia kiasi cha Sh.5,624.29 milioni kufikia tarehe 30 Mei 2008. Serikali ilipendekeza mkopaji asamehewe faida ya tozo la mkopo kwa asilimia 55

		Mkopaji akakubali kusamehewa na bakaa iliyobaki kuwa "Capitalized"
6.	General Tyre East Africa - USD 10 M at 6% p.a (2005)	Notisi ya kushindwa kulipa deni imetumwa kwa mkopaji.
7.	Continental Ventures(T) Limited - USD 3.5 Millions (2005)	Mkopwaji ameshindwa kutimiza wajibu wake.
8.	Katani limited- USD 3.7 Millions (2006)	Mkopaji ameshindwa kulipa mkopo wake.
9.	Kiwira Coal & Power Company Limited - Sh USD 7 M (2007)	Mkopwaji ameshindwa kurejesha mkopo kwa mujibu wa mkataba.

Menejimenti ya NSSF haizingatii Sehemu Na. 5.4 ya sera ya uwekezaji ya mfuko ya mwaka 2007 pamoja na Sheria ya Mfuko Na.28 ya mwaka 1997.

9.12.5 Uwekezaji Katika Hisa za Kawaida Zisizokuwa na Mapato -NSSF Sh.62,785,093,300

Upembuzi wa vitega uchumi ulibaini kuwa NSSF imewekeza kwenye makampuni mbalimbali kwa njia ya hisa za kawaida na hakuna ushaidi kuwa hivi karibuni NSSF itapata gawiwo kutoka kwenye makampuni hayo. Historia inaonyesha kuwa hakuna gawiwo limewahi kutolewa na makampuni hayo. Kwa ujumla, kuwekeza kwenye makampuni hayo kumbainika hauna tija. Orodha ya makampuni husika ni kama ifuatavyo:-

Jina la Kampuni	Bakaa 30/6/08-Sh.	Maelezo
Tanzania Oxygen Ltd	13,200,000	Hakuna tamko la gawiwo
Tanzania Housing Bank	495,280,000	Liko chini ya muflisi
1 st Adili Bank Corp Ltd	3,152,024,742	Mkopo huu ni

		utata mtupu
CDC Mbeya Cement	1,152,024,742	Hakuna tamko la gawiwo
Ubungo Plaza	9,817,038,702	Hakuna tamko la gawiwo
TANRE Share	1,000,000,000	Hakuna tamko la gawiwo
HEPZ (Quality Group) Share	47,156,025,113	Hakuna tamko la gawiwo
PPL Pension Properties	3,500,000	Hakuna tamko la gawiwo
Jumla	62,789,093,299	

Mifano hii michache inayoashiria udhaifu wa uwekezaji wa NSSF inapaswa ichukuliwe kwa uzito maalum. Hii ni kwa sababu ukifanya mchanganuo wa mikopo ambayo imetolewa kwa makampuni ya watu mbalimbali, karibu ya mikopo yote imethibitika kutokurejeshwa. Mbaya zaidi inapelekea menejimenti ya Mfuko kuhangaika na kesi nyingi zilizopo mahakamani. Ili kuhakikisha usalama wa fedha za wanachama wa mfuko, NSSF inapaswa kupembua taratibu za uwekezaji na idara ya uwekezaji ya shirika kuhakikisha kwamba fedha za wanachama zinatumiwa vizuri na siyo kuziwekeza kwenye miradi ambayo haina tija.

9.12.6 Mkataba wa Kubadilishana Madeni Kati ya Shirika la Bima na Serikali.

Katika miaka iliyopita Serikali ililikopesha Shirika la Bima la Taifa kwa ajili ya kulipa madeni ya haraka na ilipofika mwanzoni mwa mwaka huu kiasi cha shilingi 4,428,674,047 kilionekana ndiyo bakaa ya Deni.

Katika kikao cha Bodi cha 185 kilichofanyika tarehe 10/7/2007, kilitoa taarifa kwamba Serikali inafikiria kufuta deni lake la shilingi bilioni 4.4 ambalo ililikopesha Shirika la Bima mwaka 2005 kununua Chuo cha Bima kilichopo Mikocheni chenye thamani ya shilingi

2,873,118,900 na kulifuta deni lililobaki la shilingi 1,555,555,146.

Makubaliano hayo ya kubadilishana deni hilo yalisainiwa mwezi Novemba, 2007 kati ya Wizara ya Fedha na Shirika la Bima la Taifa. Baada ya hapo Serikali ikawa imekinunua Chuo hicho kwa thamani ya shilingi 2,873,118,900 na kulingana na makubaliano ya mkopo ikawa kuna bakaa ya shilingi 1,555,555,146 ambayo haijarejeshwa.

Hata hivyo, kulingana na maelezo ya menejimenti, walisema kuwa makubaliano yaliyofikiwa na Serikali ya kubadilishana deni hilo kwa kununua chuo cha Bima ambacho kilifanyiwa tathmini upya kwa shilingi 4,015,000,000 na kubaki bakaa ya deni ya shilingi 413,674,047. Makubaliano hayo mapya hayakutekelezwa na hakuna uthibitisho wa maandishi uliopatikana lakini taarifa hizo zimeweza kuonekana kwenye hesabu za shirika kinyume na taratibu za uhasibu.

9.13 Uhamishishaji wa Deni la Mkopo la NSSF Wenye Kutia Shaka Kutoka M/s Meditech Kwenda M/s Emunio Tanzania Limited

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulitoa mkopo wa shilingi 1,525,368,425 kwa M/s Meditech tarehe 30 Aprili 2003 na makubaliano ya muda wa malipo ulikuwa mwezi Disemba 2004. Baadaye ilifahamika kwamba muda wa kuanza kulipa mkopo ulibadilishwa na kuwa tarehe 30 Juni 2006. Makubaliano ya kubadilisha muda mpya wa kuanza kulipa mkopo hayakuweza kupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

Mawasiliano ya karibuni yaliyofanywa na Mfuko kuhusu mkopo imeonekana yakifanywa na M/s Emunio Tanzania Limited kama ndiye mkopaji. Utaratibu wa kisheria wa kuhamisha mkopo kutoka kwa M/s Meditech Ltd kwenda

kwa M/s Emunio Tanzania Ltd haukuweza kujulikana kwa kuwa hakukua na nyaraka zozote zilizowasilishwa kwa Ukaguzi kuhusiana na suala hilo.

Uhamisho huo wa deni kutoka M/s Meditech kwenda M/s Emunio Tanzania Limited ambayo ni moja kati ya makampuni sugu ya ulipaji madeni na iko katika mchakato wa kubadilisha umiliki (katika aya yenye kichwa cha habari kisemacho utoaji mikopo katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) hauna tija kibiashara na kiuchumi) hali hii inaashiria hatari kuhusiana na mchakato mzima wa mkopo na hasara iliyo mbele.

9.14 Malipo Yenye Kutia Shaka ya NIC-UK Loyds Akaunti Namba 0954286 - Dola za Kimarekani 75,213 kwa Benki ya Posta

Ukaguzi ulibaini malipo yaliyofanyika katika akaunti ya benki namba 095428 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 75,213 tarehe 24 Agosti 2007 lakini katika usuluhisho wa benki ikabainika kwamba malipo hayo yalilipwa kimakosa na benki. Ilibainika pia kuwa malipo hayo yalifanywa na Benki kwa maelekezo na idhini ya Meneja Mkuu wa Shirika na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala tarehe 24 Agosti 2007.

Menejimenti ilipingana na maelezo ya benki kwa barua ya tarehe 7 Novemba 2007 iliyokuwa na maelezo kwamba haijawahi kutoa maelekezo yeyote kuhusiana na malipo hayo na benki inawajibika kwa hasara hiyo na inatakiwa irejeshe fedha hizo haraka kwenye akaunti ya Shirika hilo.

Menejimenti ya Shirika imefanya juhudi ya kurejeshewa fedha na hatimaye mwezi Julai 2008 (wakati tunafanya Ukaguzi) , taarifa ya benki ilionyesha Shirika limeingiziwa fedha kwenye akaunti yake kutoka Lloyds kiasi cha Dola za Kimarekani 78,825.96. Hata hivyo hapakuwa na taarifa zozote zilizotolewa na benki kuhusiana na fedha zilizoingia kwenye akaunti lakini ikaonekana ni marejesho ya fedha zilizoibiwa.

Ingawaje malipo hayo yalionekana dhahiri ni ya kugushi lakini hakuna ushahidi wowote uliopatikana ulioonyesha kuwa Menejimenti ilitoa taarifa kwa mamlaka husika kwa ajili ya uchunguzi na hatua za kisheria kuchukuliwa .

9.15 Mapungufu Yaliyobainika Katika Kutekeleza Mkataba wa Makubaliano wa Uwakala Kati ya TPB na TPC

Utekelezaji wa mkataba wa makubaliano ya uwakala kati ya Benki ya Posta na Shirika la Posta Tanzania ulibainika kuwa na mapungufu. Baadhi ya mapungufu hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) **Amana Zaidi kwenye Shirika la Posta Tanzania**
Mapato ya baadaye (receivables) yaliyokuwa yameonyeshwa kwenye hesabu za mwaka ulioshia tarehe 31/12/2007 yalikuwa shilingi 6,538,475,000 ambazo zilijumuisha amana zaidi za Shirika la Posta Tanzania. Mchanganuo wa kiasi cha amana zaidi cha shilingi 1,534,283,000 ni kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:-

Akaunti Na.	Maelezo ya Akaunti	31.12.2007 Sh.	31.12.2006 Sh.
190420001	TPC Excess Deposits (Current Balance)	1,410,112,574	1,361,063,193
190420004	TPC Excess Old Balance	<u>124,170,395</u>	<u>98,054,641</u>
Jumla		<u>1,534,282,969</u>	<u>1,459,117,834</u>

Shirika la Posta Tanzania ni wakala wa Benki ya Posta Tanzania. Shirika la Posta Tanzania lina wajibu wa kukusanya amana za wateja wa Benki ya Posta Tanzania pamoja na kulipa wateja wa benki hiyo kwa niaba ya Benki ya Posta. Shirika la Posta Tanzania linatakiwa kutuma amana za wateja Benki ya Posta baada kutoa fedha ilizolipa

wateja wa benki wa posta. Amana zaidi zinatakiwa zitumwe kwenye akaunti ya makusanyo ya mkoa ndani ya wiki mbili toka tarehe ya kukusanya amana hizo.

Hata hivyo ilibainika kuwa, bakaa ya deni toka Shirika la Posta mwishoni mwa mwaka ilikuwa ni kubwa ikiashiria kwamba Shirika la Posta Tanzania halikuwa likituma amana zaidi za wateja kwa mujibu wa mkataba. Taarifa hizo hapo juu zinaonyesha kuwa bakaa ya amana zaidi za wateja wa Benki ya Posta zilizokuwa zimeshikiliwa na Shirika la Posta Tanzania ziliongezeka kwa shilingi 75,165,135 kutoka shilingi 1,459,117,834 kufikia tarehe 31 Disemba 2006 na shilingi 1,534,282,969 kufikia tarehe 31 Disemba 2007. Hii inaonyesha kuwa hakuna juhudi zilizofanywa na menejimenti ya Benki ya Posta Tanzania kuhakikisha amana za wateja zaidi zinapokelewa kutoka shirika la Posta Tanzania.

Zaidi ya hayo mchanganuo wa umri wa bakaa ya deni haukutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Kutokulipwa amana zaidi za wateja wa TPB kutoka kwa TPC zinapunguza uwezo wa kifedha wa Benki ya posta Tanzania na hivyo kuipelekea benki kuwa na upungufu wa fedha usio wa lazima.

(ii) Wizi wa Kughushi Uliofanywa na Watumishi wa Shirika la Posta

Upembuzi ulibaini kuwa fedha zilizotolewa (withdraws) na watumishi wa Shirika la Posta uliongezeka kutoka shilingi 44,947,400 mwaka 2006 nakufikia shilingi 47,443,500 mwaka 2007 bakaa iliyotajwa hapo juu inajumuisha kiasi cha fedha shilingi 3,666,600 ambazo kwa muda mrefu zilikuwa kwenye mgogoro na Shirika la Posta Tanzania tangu mwaka 2002 na kiasi kilichobaki cha shilingi 43,776,900 kilikuwa hakijafanyiwa usuluhisho na Shirika la Posta Tanzania au Benki ya Posta haikuthibitisha kufanya usuluhisho huo. Pia, hapakuwepo na tengo la deni chechefu lililokuwa limefanywa kwenye mahesabu kutokana na wizi wa kughushi wa fedha za kutoa (withdraws) licha ya bakaa

kuthibitishwa kutokurejeshwa na kiasi cha fedha hizo kuwa kwenye mgogoro kwa miaka mingi.

Kutokana na yaliyoelezwa hapo juu ukaguzi haukuweza kubaini kiasi halisi na uwezekano wa marejesho ya fedha zilizoibwa na watumishi wa shirika la Posta kinachofikia shilingi 47,443,500 kilichoonyeshwa kwenye hesabu za mwaka husika .

SURA YA KUMI

USIMAMIZI WA RASLIMALI WATU

10. Utangulizi

Matokea ya kaguzi mbalimbali zilizofanyika kwa mwaka wa fedha 2007/2008 yameonyesha mapungufu katika kusimamia raslimali Watu. Tulibaini ajira zisizofuata taratibu za ajira, utunzaji mbovu wa kumbukumbu za wafanyakazi, upungufu wa wafanyakazi, wafanyakazi kutokuwa na mikataba, upendeleo katika ajira, na kutolipwa kwa makato kwenye mifuko ya pensheni na matumizi mabaya ya wataalamu.

Madhara ya mapungufu hayo hapo juu ni pamoja na kuacha kazi kwa wafanyakazi, wafanyakazi kukosa ari ya kufanya kazi na kukosekana ufanisi. Maelezo ya kina ya matatizo hayo hapo juu yanatolewa kama ifuatavyo:-

10.1 Utunzaji Mbovu wa Kumbukumbu za Wafanyakazi.

Ukaguzi wa mafaili ya wafanyakazi uligundua kuwa kumbukumbu muhimu za wafanyakazi hazikuwekwa kama inavyotakiwa. Kumbukumbu kama vile mikataba ya ajira, nakala za vyeti, barua za ajira, taarifa za kupandishwa vyeo, uhamisho, ongezeko la mishahara n.k hazikutunzwa vizuri kama inayoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Na.	Taasisi	Mapungufu.
1.	TANAPA	Kati ya mafaili 75 ya wafanyakazi tuliyoangalia, mafaili 10 ndiyo yalikuwa na kumbukumbu za kutosha.
2.	Chuo cha Ustawi wa jamaa	Kumbukumbu za wafanyakazi wa mkataba hazikuwepo.
3.	NSSF	Mikataba ya ajira, nakala za vyeti, barua za ajira, taarifa za kupandishwa vyeo, uhamisho ongezeko la mishara n.k hazikuwepo.

10.2 Kupima Utendaji Kazi wa Wafanyakazi

Mashirika mengi yalionekana kukosa mifumo mizuri ya kupima utendaji wa wafanyakazi wao, hivyo kupelekea kutojua ubora na ufanisi wa kazi za wafanyakazi. Pia kuna baadhi ya mashirika yaliyokuwa na mifumo ya kutathmini utendaji ambayo haijaweza kutumika ipasavyo.

10.3 Mapungufu Katika Usimamizi wa Mikataba ya Ajira Sheria ya Ajira Na. 6 ya Mwaka, 2004 inamtaka mwajiri kuweka mikataba ya ajira yenye taarifa zifuatazo:-

- Jina, Umri, Jinsia,
- Mahali alipoajiriwa,
- Kazi atakayofanya,
- tarehe ya kuanza kazi,
- Masaa ya kazi,
- Mshahara na mafao mengine na namna ya yatavyolipwa.

Hata hivyo, kwa mwaka huo, Mashirika ya Umma yaligundulika kutokuwa na mikataba na wafanyakazi wake kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

Na.	Taasisi	Mapungufu
1.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni 2008 Mamlaka ya Bandari iliajiri wafanyakazi 127 kwa mkataba wa muda kati ya miezi sita (6) na miaka mitatu (3). Hata hiyo, mikataba yote haikuambatana na taarifa zingine kama inavyotakiwa kisheria.
2.	Shirika la Utangazajia Tanzania.	TBC ilimwajiri meneja mmoja mwezi Disemba 2006 bila kuwa na mkataba wa ajira kinyume na kifungu Na. 7.7 cha kanuni za utumishi wa shirika hilo.
3.	DAWASCO	Hapakuwepo na mkataba wa afisa mmoja aliyeajiriwa kwa kipindi cha mkataba.

10.4 Upungufu wa Wafanyakazi Katika Baadhi ya Mashirika

Katika kaguzi za miundo ya mashirika ilibainika, kuwepo matatizo ya upungufu wa wafanyakazi katika miundo hiyo

ambapo tunaona kuwa malengo ya mashirika yanaweza yasifikwiwe kwa sababu ya ukosefu wa muundo hiyo. Vilevile, mgawanyo wa kazi katika sehemu zingine ulikuwa mgumu kwa sababu ya upungufu wa wafanyakazi na hivyo kupunguza ufanisi katika utendaji na uimarishwaji wa muundo wa ndani kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Shirika	Idara	Upungufu
Shirika la Tija Tanzania	Utumishi	Nafasi 2 za wakurugenzi zipo wazi. Mkurugenzi wa mafunzo na mkrugenzi wa utumishi na utawala.
Shirika la Hifadhi za Taifa	Utumishi	Nafasi 7 za mameneja zipo wazi.
NSSF-(Ofisi ya Wilaya ya Geita)	Uhasibu	Kuna mhasibu mmoja tu anayeshughulikia masuala yote ya kahasibu hivyo kufanya udhibiti wa mfumo wa ndani kushindwa kufanya kazi vizuri.
UDSM (Chuo cha uandishi wa habari na mawasilano ya umma)	Uhasibu	Kitengo cha uhasibu kina mtu mmoja tu.
TEMDO	-Ubunifu, na Teknolojia -Mkurugenzi mkuu -Uhasibu	Nafasi ya mkurugenzi mkuu iko wazi, mkuu wa kitengo cha ubunifu na mhasibu ziko wazi pia.

10.5 Uhamisho wa Aliyekuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala kwa Nia ya Kumshusha Daraja.

Ukaguzi uliofanyika kwenye usimamizi rasimali watu umegundua mapungufu yafuatayo kwenye uhamisho wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala - NSSF.

Bodi ya Wadhamini Katika Kikao chake cha tarehe 22/2/2005 iliidhinisha mapendekezo ya uongozi kuhusu kumhamisha aliyekuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala kwenda mkoa wa Kilimanjaro kuwa meneja wa ofisi ya mkoa. Kifungu cha 3.2.2 kanuni za utumishi za shirika, Bodi ndio yenye mamlaka ya kumteua mkurugenzi hivyo, uongozi wa NSSF kupendekeza kutengua uteuzi wa mkurugenzi haikuwa sahihi. Barua ya uhamisho ilijumuisha Sharti la kuwekwa mkurugenzi huyo kwenye majaribio ya kipindi cha miezi sita na baada ya hapo anaweza kuthibitishwa kazini, na kwamba mshahara atakao lipwa utakuwa ule wa mkurugenzi.

Mkurugenzi huyo alianza kulalamika kuwa ameonewa kwa kuandika barua kwa Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, tarehe 28/6/05, 22/7/05 na 29/7/05, na Mkurugenzi mkuu alimjibu kuwa anachukulia suala hilo kama limefungwa na halihitaji malumbano zaidi. Vilevile Mkurugenzi Mkuu kupitia barua Na. NSSF/C/PF/778/103, alimtishia mlalamikaji kuwa atamchukulia hatua za kinidhamu endapo ataendelea kulalamika, bila kutatua tatizo la mlalamika.

- Mnamo tarehe 8/3/2006 mlalamikaji alimwandikia mwenyekiti wa Bodi akimweleza kuwa hajatendewa haki, lakini hata hivyo mwenyekiti wa bodi hakumjibu hadi baada ya miezi kumi na nane (18) ndipo alipomjibu akimweleza kuwa kweli anakiri kuwepo na matatizo wakati wa uhamisho wake na kukiri kulifanyia kazi suala lake, lakini mpaka sasa suala hili bado halijapatiwa ufumbuzi.

10.6 Ajira ya Mkurugenzi na Utumishi na Utawala Asiyekuwa na Sifa

Baada ya kuhamishwa kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala kama ilivyoonekana kwenye aya hiyo hapo juu, Bodi ya Wadhamini katika kikao chake cha 33 kilichofanyika mwezi, 2005 ilimwajiri Mkurugenzi mpya kwenye nafasi iliyoachwa wazi na Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala aliyehamishiwa Kilimanjaro. Mkurugenzi mpya

alipewa mkataba wa miaka mitatu Kuanzia Septemba 2005. Hata hivyo, kulingana na kanuni za utumishi za NSSF imebainika kuwa Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala anatakiwa kuwa na cheti cha stashahada ya uzamili na uzoefu wa miaka saba katika nafasi kama hiyo. Hata hivyo Mkurugenzi aliyeajiriwa hakuwa na sifa za kuajiriwa kwani hana cheti cha uzamili kwani upembuzi wa mafaili yake haukupata vyeti kuthibitisha kuwa alikuwa na sifa za kutosha na uzoefu wa miaka saba katika kazi hiyo.

10.7 Kutokuzingatia Sheria za Ajira

Wakati wa ukaguzi tuligundua kuwepo kwa uvunjwaji wa sheria za ajira ambapo ajira zilifanyika bila kufuata taratibu zilizowekwa, mfano wa baadhi ya mapungufu hayo ni pamoja kuajiri watu ambao hawajafikisha sifa na uzoefu wa kutosha kushika nafasi walizopewa, kuajiri watu bila kutangaza nafasi hizo. Pia kulikuwa na wafanyakazi walioajiriwa wakiwa na umri mkubwa kuliko kawaida. Pia kulikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi walioacha kazi kwa mwaka husika. Matatizo hayo yalitokea kwenye mashirika ya NSSF, TSN na TPA.

10.8 Matumizi Mabaya ya Wataalamu - NSSF

UKaguzi wa usimamizi rasimali watu uliofanyika katika shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) uligundua kuwepo kwa matumizi mabaya wa wataalamu ambapo wafanyakazi walionekana kupangiwa kazi ambazo hawajasomea. Kwa mfano kuna mfanyakazi mwenye taaluma ya juu ya Uhasibu (CPA) amepangiwa idara ya ulinzi kama mlinzi mwandamizi. Pia kuna mfanyakazi mwingine mwenye sifa hiyo hiyo alipangwa masijala bila sababu za msingi.

10.9 Kutowasilisha Makato ya Kisheria

Ukaguzi umegundua kuwa baadhi ya mashirika yamekuwa yakifanya makato ya kisheria kama vile kodi ya mapato, michango ya pensheni na SACCOS bila kuziwasilisha kwenye mamlaka husika kinyume na Sheria za nchi. Vilevile

mashirika yalizimika kulipa tozo ambazo zingepukika endapo michango hiyo na kodi hizo zingewasilishwa mapema. Hadi tarehe 30 Juni 2008, Shirika la posta lilikuwa na makato ambayo yanayokaribia jumla ya shilingi 1,503,492,491.

SURA YA KUMI NA MOJA

UTAWALA BORA

11.0 Utangulizi

Utawala bora unahamasisha ulazima wa Mashirika ya Umma kuwa na sera bora za kusimamia raslimali. Katika kuhakikisha usimamizi bora wa raslimali, Shirika linahitaji kuwa na taratibu ambazo zitalifanya kuwa na udhibiti madhubuti ambao utaondoa kama sio kupunguza udanganyifu, wizi, uzembe na utendaji wa kazi usiokuwa tija.

Shirika linapaswa kujipanga na kuandaa mipangilio ambayo itahimiza uwazi na mifumo ya ndani madhubuti. Hivyo, muundo wa Shirika unapaswa uwezeshe katika kujipima; kwa mfano kuanzishwa kwa vitengo vya ndani vya ukaguzi, bodi ya zabuni, vitengo vya kusimamia manunuzi, kamati za ukaguzi pamoja na kuhakikisha kuwa kunakuwepo ukaguzi wa ndani ulio huru.

Zaidi ya hayo, Mashirika yanatakiwa kuwa na maadili ya kazi, mpango wa huduma kwa jamii, mpango wa Shirika, bajeti za mwaka sambamba na bodi za wakurugenzi makini kwa ajili ya kufanya maamuzi makubwa na makini ya Shirika.

Madhumuni ya utawala bora katika undeshaji kazi za kila siku ni kwa shirika husika kuwajibika kikamilifu na kutimiza matakwa na matarajio ya wadau kiuchumi na kijamii.

Kwa hivyo, sura hii inaeleza kwa ufupi udhaifu uliobainika wakati wa kaguzi za Mashirika ya Umma unaohusu mambo ya utawala bora ambayo yalionekana ni muhimu kuyaweka bayana ndani ya sura hii ya taarifa ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

11.1. Upembuzi wa Utendaji wa Vitengo vya Ndani vya Ukaguzi Pamoja na Miundo ya Bodi za Wakurugenzi

Na	Shirika	Mapungufu
1.	TCRA	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa na hapakuwepo na ushahidi kuwa taratibu za kihesabu na za manunuzi zilifuatwa. Mamlaka iliingia mkataba na M/s TAC Associates tarehe 16 Februari 2008 kufanya kazi ya ukaguzi wa ndani kwa gharama ya malipo ya Shilingi 13,200,000 kwa mwaka lakini hapakuwepo na taarifa za ukaguzi wa ndani zilitolewa kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka 2007/2008.
2.	TBC	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
3.	MUWASA	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
4.	TUWSA	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
5.	NEEC	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakikuwa kikifanya kazi katika mwaka 2007/2008.
6.	DIB	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
7.	BUWASA	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
8.	LUWASA	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
9.	TUWSA	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
10.	TSN	Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakijaanzishwa
11.	BoT	Gavana wa benki Kuu, ambaye pia ni Afisa Mtendaji Mkuu, ni mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi. Pia Manaibu watatu wa Gavana ni wajumbe wa Bodi (na kutokana na Sehemu ya 9(2) cha Sheria ya Benki

		Kuu ya mwaka 2006, mmoja wao ni Naibu Mwenyekiti). Menejimenti imechukua asilimia 44 ya wajumbe wa Bodi.
12.	Soko la Kariakoo	Bodi ya wakurugenzi ilivunjwa mwaka 2000 kwa madai ya kutofanya kazi kimakini na kikamilifu; kwa hivyo shirika linafanya kazi chini ya Bodi ya Ushauri iliyoteuliwa na Jiji la Dar es Salaam tangu wakati huo. Bodi ya Ushauri ya Soko la Kariakoo inaundwa zaidi na wakuu wa Idara wa Jiji la Dar es Salaam bila ya kuwa na muda maalumu wa ujumbe au muda wa Bodi. Mwenendo huu hauendani na Sheria iliyolanzisha Soko la Kariakoo ya Mwaka 1974.
13.	Bodi ya Biashara za Nje	Bodi ya wakurugenzi iliendelea kuwepo ofisini hata baada ya kwisha kwa muda wake tarehe 29 Machi 2007 na Bodi mpya iliteuliwa mnamo tarehe 8 Januari 2009 ikichelewa kuanza kazi kwa miaka miwili. Kuchelewa kwa kuanzisha Bodi ya Wakurugenzi kuliipelekea bodi kufanya mikutano minne isiyokuwa ya kisheria.
14.	COSOTA	Uchelewashaji wa kuteua Bodi ya Wakurugenzi Mpya kulisababisha maamuzi muhimu ya uendeshaji wa Shirika ya muda mrefu kutokufanyika kwa kipindi hicho.
15.	NACTE	Muda wa baraza la Uongozi uliisha mnamo tarehe 18 Septemba 2007, lakini uteuzi wa baraza jipya ulichelewa kufanywa hadi Julai 2008 hivyo baraza lilijiendesha bila ya kudhibitiwa. Kitengo cha ndani cha Ukaguzi kinasimamiwa na kuendeshwa na mtu mmoja tu, ambaye ni mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani (CIA) ambaye pia anajishuhulisha na kazi za kila siku za

		kufanya ukaguzi wa awali wa malipo (pre-audit) kabla hayajalipwa, na hivyo kutia dosari uhuru wa Kitengo hicho.
16.	NSSF	Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini anatoa huduma za uwakili kwa Mfuko kupitia kampuni yake ya Sheria. Katika mwaka 2007/2008 Shilingi 20,880,000 zililipwa kwa Kampuni hiyo kwa kuendesha kesi ya wafanyakazi wawili waliokuwa watumishi wa NSSF. Kuna ushahidi wa kutosha wa mgongano wa kimaslahi na uwezekano wa kufanya hila ya kupata kazi hiyo na hata kushawishi kiwango cha malipo.

Baadhi ya Wakaguzi wa Ndani wa Mashirika ya Umma, wanafanya kazi ya kukagua malipo katika hatua za awali kabla hayajalipwa (pre-audit); na hivyo kuwa sehemu ya waidhinishao malipo. Mfano Mamlaka ya bandari Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania. Pia kulikuwepo na baadhi ya wakaguzi wa ndani kuwa wajumbe wa bodi za zabuni hivyo kupelekea kutia dosari uhuru wa wakaguzi wa ndani kutokana na mgongano wa kimaslahi.

11.2 Upembuzi wa Bodi za Wakurugenzi

Kutodhibitiwa kwa Marupurupu ya Bodi za Wakurugenzi Bodi za Wakurugenzi ni vyombo vya juu vyenye majukumu ya kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma kwa kutumia madaraka ya kisheria zilizopewa bodi katika kutekeleza majukumu yake ya kiusimamizi. Na kwa kutambua kuwa wajumbe wa Bodi hizo ndio waandaaji wa sera wakiwa na madaraka ya kuachisha kazi watumishi ikiwa ni pamoja na kujipangia marupurupu yao; ni dhahiri kuwa watajipangia marupurupu makubwa, na menejimenti ya mashirika husika kutokuwa na mamlaka ya kukataa mapendekezo ya marupurupu hayo.

Tukirudi na kukumbuka miaka ya nyuma wakati ilipokuwepo Kamati teule ya Mashirika ya Umma “Standing Committee of Public Organisations” (SCOPO) ambapo moja ya kazi zake ilikuwa kuidhinisha ada za wakurugenzi na marupurupu mengineyo, na kufanya ile dhana ya “check and balance” kufanya kazi kwa uwazi kuonekana umuhimu wake.

Matokeo ya upembuzi yakinifu wa ada ya wakaguzi umeonyesha kuwa kumekuwepo na hali ya kufanana karibu ya Mashirika yote ya Umma hapa Tanzania. Posho wanazojilipa Wakurugenzi wa Bodi ikiwemo, posho za vikao, usafiri, ada ya wakurugenzi ni kubwa sana ukilinganisha na hali ya uchumi ya Tanzania. Posho hizi zinatofautiana kati ya Shirika moja na lingine kutegemeana na uwezo wa kifedha na uwezo wa kujiendesha kwa faida kwa Shirika husika. Kwa maoni yangu baadhi ya marupurupu wanayojilipa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi ni ya juu sana.

Kutowajibika kwa Bodi za Wakurugenzi

Mkutano wa uwajibikaji katika Mashirika ya Umma uliofanyika tarehe 23 na 24 Januari, 2009 hususani kupembua utendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Shirika la Umme na Ugavi Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania, kampuni ya Maji Dar es Salaam, TANROADS na Shirika la Ndege Tanzania ulibaini kuwa utendaji wa Bodi za Wakurugenzi ni wa mashaka na hakuna juhudi zozote za kupima utendaji kazi wake. Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika ya Umma wamekuwa wakiendelea na kuzitumikia Bodi zao hata mara baada ya muda wake kuisha kisheria na wakati mwingine wanateuliwa kuendelea kuziendesha Bodi hata kama utendaji kazi wao hauridhishi na umekuwa ukipungua muda hadi muda.

Kwa maoni yangu na kwa kuzingatia maazimio ya Mkutano wa uwajibikaji katika Mashirika ya Umma iliazimiwa kuwa:

- kuna haja ya kuwapa nguvu ya kisheria wakurugenzi wa bodi katika suala zima la kuwateua watendaji wakuu wa mashirika wanayoyasimamia badala ya Rais wa Jamhuri

ya Mungano. Rais abakiwe na jukumu la kuwateua wenyeviti wa bodi za wakurugenzi.

- Serikali itapaswa kuingia mkataba wa kiutendaji na bodi za wakurugenzi za Mashirika ya Umma na kupanga malengo ambayo watatakiwa kuyatekeleza wakati wa kipindi cha kuitumikia bodi. Malengo hayo yatakuwa wazi kwa Umma na yatatumika kuipima bodi na kufanya uamuzi wa bodi kuendelea na kipindi kingine cha miaka mitatu. Kwa hali hiyo, bodi zitatakiwa kusaini mkataba wa kiutendaji na watendaji wakuu wa mashirika yao, ambao pia watawasaini mkataba wa kiutendaji na wasaidizi wao na pia wasaidizi wao watawasaini mkataba wa kiutendaji na wafanyakazi walioko chini yao.

11.3 Udhaifu Uliobainika Katika Upembuzi wa Kamati za Ukaguzi

Na	Shirika	Mapungufu
1.	TBC	Kamati ilikutana mara moja mwaka 2007/2008
2.	CDA	Kamati haikuwa na mjumbe aliyekuwa na ujuzi wa kiasibu.
3.	NEMC	Kamati ilikutana mara mbili tu kwa mwaka wakati inatakiwa kukutana mara nne kulingana na sheria ya fedha Na. 32
4.	MUWSA	Kamati ilikutana mara moja mwaka 2007/2008
5.	BUWASA	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
6.	IAE	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
7.	LUWASA	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
8.	Mwl. Nyerere Memorial Academy	Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi ni miongoni mwa watendaji wa Chuo, hivyo kushindwa kufanya maamuzi na kazi za kamati kwa uhuru na kwa ufanisi.
9.	MWAUWASA	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
10.	ISW	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
11.	TPDC	Hakuna Kamati ya Ukaguzi

12.	IAA	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
13.	DIB	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
14.	DIT	Hakuna Kamati ya Ukaguzi
15.	MUWSA	Kamati ilikutana mara moja mwaka 2007/2008
16.	TUWASA	Mtendaji mkuu ambaye kwa mujibu ya cheo chake ni katibu wa bodi ya wakurugenzi, pia ni katibu wa kamati ya Ukaguzi ambayo inapaswa kutoa taarifa kwa bodi ya wakurugenzi
17.	NACTE	Hakuna Kamati ya Ukaguzi

11.4. Wabunge Waliotumikia Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni 2008

Dhana ya kutenganisha majukumu ya mihimili mitatu, Serikali, Bunge na Mahakama ilikuwa kuhakikisha kazi zinafanywa kwa misingi iliyowekwa na kukubalika. Kinyume na dhana hii, ilibainika kuwa asilimia 30 ya wajumbe wa bodi za Mashirika ya Umma 13 ni wabunge wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hali hiyo, jukumu la kazi ya bunge ya kusimamia utendaji kazi za Serikali kwa kuzingatia kanuni za utawala bora umeingia dosari.

Kutokana na udhaifu ulioelezwa hapo juu, Mkutano wa Uwajibikaji katika Mashirika ya Umma uliofanyika tarehe 23 na 24 Januari, 2009 uliazimia na kuitaka Serikali kuhakikisha Wabunge hawateuliwi kuwa wajumbe wa bodi za Mashirika ya Umma.

Jedwali hili hapa chini, linaloonyesha kiasi cha Wabunge waliopo kwenye Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma.

Na	Shirika	Idadi ya wajumbe	Idadi ya Wabunge	Idadi ya wasio wabunge	% ya Wabunge
1.	Bodi ya Pamba Tanzania	9	5	4	56
2.	Kiwanda cha Mbolea Tanzania	7	2	5	29
3.	Bodi ya Korosho Tanzania	9	3	6	33
4.	Mamlaka ya Eneo la Hifadhi Ngorongoro	14	5	9	36
5.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania	6	1	5	17
6.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania	5	1	4	20
7.	Chuo Kikuu cha Mzumbe	17	3	14	18
8.	Makumbusho ya Taifa	11	3	8	27
9.	Bodi ya Chai Tanzania	8	3	5	38
10.	Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC)	5	2	3	40
11.	Bodi ya Sukari Tanzania	8	2	6	25
12.	Bodi ya Bahati nasibu Tanzania	6	2	4	33
13.	Kampuni ya Huduma za Bahari Ltd	6	2	4	33
	Jumla	111	34	77	
	Asilimia	100%	30%	70%	

Pia, ilibainika kuwa maafisa wawili wa ngazi ya juu Serikalini na mmoja kutoka sekta binafsi ni wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi nyingi. Kutokana na ukweli kwamba kazi ya wajumbe wa Bodi za wakurugenzi ni kujitoa kiakili na muda katika kuendesha bodi hizo, ni dhahiri kuwa wajumbe hao watahindwa kuchangia kikamilifu maendeleo ya Mashirika wanayoyatumikia. Mchanganuo wa wajumbe hao na bodi wanazozitumikia ni kama ifuatavyo:

Na	Mjumbe wa Bodi	Shirika
1.	P/Secretary	UDSM, DAWASCO, Chuo Kikuu Mzumbe, NSSF, NBMM n.k.
2.	Mtumishi wa Ngazi ya Juu Serikalini	CHC, RAH, Shirika la Bima la Taifa, Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, n.k
3.	Mtu Binafsi	Chuo Kikuu cha Ardhi, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Bodi ya Biashara ya Nje Tanzania, PPF n.k.

Hii ni kinyume na matakwa ya Sehemu ya 12 ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 1992 inayotaka mjumbe wa bodi asiteuliwe kutumikia bodi zaidi ya tatu. Kuhakikisha uteuzi unafanywa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, kila mapendekezo ya uteuzi wa wajumbe wa bodi yatumwe kwa Msajili wa Hazina kama inavyotakiwa na Sehemu ya 12 (2) ya Sheria ya makampuni iliyotajwa hapo juu.

11.5 Muungiliano wa Maamuzi Katika Mashirika ya Umma

Utoaji wa maamuzi katika Mashirika ya Umma umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Mosi, maamuzi yanayofanywa na Menejimenti za Mashirika husika katika shughuli zake za kila siku, kwa lugha nyingine yakiwa yanafahamika kama maamuzi ya kiutendaji. Maamuzi haya utekelezaji wake ni wa muda mfupi kati ya siku, miezi hadi mwaka mmoja. Hatua ya pili ya maamuzi ni yale maamuzi ambayo ni makubwa na ambayo utekelezaji wake unahitaji muda mrefu na fedha nyingi. Utekelezaji wa maamuzi haya ni kati ya miaka mitatu hadi mitano na kuendelea. Maamuzi haya huwa yanafanywa na Bodi ya Wakurugenzi ya shirika husika.

Kwa vile Mashirika ya Umma yanajitegemea kisheria, kwa hivyo chombo cha mwisho cha kufanya maamuzi iwe ni Bodi za Wakurugenzi ambazo zitawajibika kwa kutokutekeleza majukumu yake kwa umakini.

Licha ya hayo, Mashirika mengine kama vile bodi za Udhibiti, Wizara mama n.k, zinaweza kutoa ushauri tu lakini usichukuliwe kama ndio maamuzi ya mwisho kuhusiana na utendaji wa kazi za kila siku au za muda mrefu za mashirika.

Hata hivyo, ilibainika kuwa Serikali iliingilia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania katika kufanya maamuzi yake ya muda mfupi na muda mrefu. Suala hili, ilihusisha Wizara ya Maliasili na Utalii kuamuru TANAPA kulipa kiasi kikubwa cha fedha na kuingia mkataba bila ya kufuata taratibu zilizoanishwa kwenye Sheria ya Manunuzi.

11.6 Majukumu ya Msajili wa Hazina Katika Kusimamia Mashirika ya Umma

Kama ilivyoainishwa katika Tamko la Msajili wa Hazina Cap. 418 na Sehemu ya 6 ya Sheria ya Makampuni Na 16 ya 1983, kazi ya Msajili wa Hazina ni pamoja na:

- Kusimamia shughuli za uendeshaji wa Mashirika ya Umma pamoja kufanya upembuzi yakinifu wa raslimali za Serikali kwa Mashirika yote ambayo Umma wa Tanzania una maslahi.
- Kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu uanzishwaji wa Shirika la Umma na kulipatia raslimali kwa ajili ya kujiendesha.
- Kufanya upembuzi yakinifu wa utendaji wa kifedha wa Mashirika ya Umma akiwa na lengo la kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kama kuunganisha au kuvunja Shirika la Umma au kuimarisha utendaji wa Shirika husika.
- Kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeteuliwa kuwa mjumbe wa bodi zaidi ya bodi za wakurugenzi tatu kwa wakati mmoja isipokuwa pale ambapo anatakiwa kisheria kuwa mjumbe wa bodi zaidi ya tatu kwa wakati mmoja.

11.7 Kutokuwapo na Sheria ya Kuanzisha Kamati za Ukaguzi katika Mashirika ya Umma

Ukaguzi wa baadhi ya Mashirika ya Umma ulibaini kuwa kuna baadhi ya taratibu mbalimbali zinazotumiwa katika kuanzisha Kamati za Ukaguzi. Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (ilizorekebishwa 2004) inaeleza uanzishaji wa Kamati za Ukaguzi katika Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali na Mikoa. Sheria hii haielezi uanzishaji wa Kamati za Ukaguzi katika Mashirika ya Umma na hivyo Mashirika ya Umma hayalazimiki kuanzisha Kamati za Ukaguzi.

Pia, muundo wa kamati ulioelezwa kwenye Kanuni Na. 31 ya Kanuni za fedha za Mwaka 2001 inawataka wajumbe wa kamati za ukaguzi wawe maafisa wa ngazi za juu wa Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali na Mikoa wakati ambapo Mashirika ya Umma yameanzisha Kamati za Ukaguzi kwa kufuata misingi ya utawala bora. Hata hivyo imebainika kuwa baadhi ya mashirika ya Umma yaliamua kuanzisha Kamati za Ukaguzi kwa kufuata matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma mwaka 2001 na kupelekea kuwapo na mkanganyiko katika kufanya tathmini ya mashirika haya.

Kutokana na hali ya mkanganyiko iliyoelezwa hapo juu, Msajili wa Hazina anapaswa kutoa muongozo kwa Mashirika ya Umma kuhusu utaratibu wa kuanzisha Kamati za Ukaguzi madhubuti ili kuwa na lugha moja na taratibu sawa katika uanzishaji wa kamati hizo.

SURA YA KUMI NA MBILI

MATOKEO YA UBINAFSISHAJI

12.0 Utangulizi

Mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990s) Serikali iliamua kutojikusisha na uendeshaji wa Mashirika ya Umma na kuyabinafsisha baadhi ya Mashirika hayo. Serikali iliamua kujikusisha zaidi na jukumu la udhibiti, na kuacha shughuli za kibiashara mikononi mwa sekta binafsi. Uamuzi huu ulisababishwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utendaji mbovu uliophelekea Mashirika hayo kujiendesha kwa hasara. Siyo Mashirika yote yalibinafsishwa, baadhi yalitengwa kwa ajili ya kubinafsishwa lakini baadae yakaruhusiwa kuendelea na biashara. Serikali iliamua kuyaunda upya na yakaanza kutoa huduma kwa umma wa watanzania kama ilivyokuwa hapo awali.

Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ulianza mwaka 1993. Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilipewa jukumu la kusimamia shughuli nzima ya ubinafsishaji. Hata hivyo Tume ivunjwa rasmi tarehe 31 Disemba 2007 baada ya kubinafsisha sehemu kubwa ya Mashirika ya Umma yaliyokuwa yametengwa kwa ajili ya ubinafsishaji. Tarehe 1 Januari 2008 akiba ya bidhaa/vifaa/raslimali iliyokuwa imesalia ya Mashirika ya Umma 34 zikiwa katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji zilihamishiwa kwa Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC).

Tarehe hiyo hiyo, Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) lilikabidhiwa jukumu la kufanya kazi za iliyokuwa SIMU 2000 Ltd. Miongoni mwa kazi zilizokuwa zimeachwa na SIMU 2000 Ltd zilikuwa ni pamoja na usimamiaji na uuzaji rasimali za iliyokuwa TTCL na kuchukua raslimali za pensheni kwa ajili ya kulipia madeni ya mafao ya iliyokuwa Shirika la Posta na Mawasiliano la Afrika Mashariki pamoja na kuchukua jukumu la kusimamia na kuendesha kesi zote za madai zilizokuwa Mahakamani.

Kabla ya hapo Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) lilikuwa limerithi kazi zilizokuwa zimeachwa na “Loans and Advance Realisation Trust (LART) na Shirika Hodhi la Raslimali za lilokuwa Shirika la Ndege (ATHCO).

Sura hii inaelezea kwa kifupi mambo ambayo ni muhimu kuufahamisha Umma yaliyotolewa kutoka taarifa za mbalimbali za Ukaguzi, taarifa ya mwaka ya Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC), taarifa ya SIMU 2000 Ltd na taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2008.

Taarifa ya Msajili wa Hazina ni muhimu sana katika sura hii kwa kuwa yeye ndiye msimamizi wa hisa za Serikali katika Mashirika ya Umma.

12.1 Hali ya Mashirika ya Umma

Kufikia tarehe ya maandalizi ya taarifa hii, Mashirika ya Umma hai 164 yalikuwa yametambulika na mengine 43 ambayo yalikuwa kwenye hatua mbalimbali aidha kufunga shughuli zake, kubinafsishwa, kuundwa upya au kufilisiwa.

Upembuzi wa taarifa ya mwaka ya Msajili wa Hazina ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2008 ulibaini kuwa Mashirika ya Umma kumi na mawili (12) ambayo yalikuwa kwenye mchakato wa ubinafsishaji, Mashirika kumi na manne (14) yalikuwa hayafanyi kazi, Mashirika kumi na mawili (12) yalikuwa yako kwenye mchakato wa kufilisiwa, Mashirika Manne (4) yalikuwa kwenye mchakato wa kuundwa upya na Shirika moja lilikuwa kwenye mchakato wa kufungwa. Kwa ujumla Serikali imewekeza hisa na rastimali zenye thamani ya Shilingi 246,666,172,379. Kwa kifupi Mashirika hayo ni kama yalivyoonyeshwa kwenye Jedwali hapo Chini.

Na	Maelezo	No	Jumla ya Raslimali Sh
1.	Mchakato wa ubinafsishaji	12	91,900,617,960
2.	Hayafanyi kazi	14	85,905,745,060
3.	Mchakato wa kufilisiwa	12	10,691,271,115
4.	Mchakato wa kuundwa upya	4	70,859,227,000
5.	Mchakato wa kufungwa	1	(12,506,598,308)
Total		43	246,666,172,379

12.2 Mashirika ya Umma Ambayo Yako Kwenye Mchakato wa Ubinafsishaji

Kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina na taarifa ya mwaka ya Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) mashirika ya Umma kumi na mawili (12) yalikuwa kwenye mchakato wa kubinafsishwa. Upembuzi wa taarifa zilizotajwa hapo umeonyesha kuwa Serikali ilikuwa imewekeza raslimali zenye thamani ya Shilingi 83,783,258,959 katika mashirika hayo ikiwa ni hisa na raslimali nyingine. Mashirika ya Umma ambayo yako kwenye mchakato wa ubinafsishaji ni kama yafuatavyo:

Na	Shirika	Ukaguzi wa mwisho	Jumla Shilingi	Umiliki wa Serikali %	Maelezo
1.	Shirika la Ndege Tanzania	30-Jun 2008	18,034,359,000	100	Mchakato wa ubinafsishaji
2.	Kiwanda cha Matairi Afrika Mashariki	30 Jun 05	(8,942,000,000)	74	Limetengwa kwa ajili ya kuuzwa
3.	Kampuni ya Maji Songwe				Haliko kwenye taarifa ya Msajili wa Hazina
4.	Loji ya Mbuga ya Wanyama Mikumi	30-Jun 96	1	100	Mchakato wa ubinafsishaji

5.	Morogoro Leather Goods				Haliko kwenye taarifa ya Msajili wa Hazina
6.	Kitara Holding ground				Haliko kwenye taarifa ya Msajili wa Hazina
7.	BP (T) Ltd	31 Dec 07	48,566,000,000	50	Mchakato wa mauzo ya hisa za Serikali za ubia na BP
8.	NBC (T) ltd	31 Dec 07	32,370,000,000	30	Mchakato wa mauzo ya hisa za Serikali za ubia na NBC(T) Ltd.
9.	Datel Tanzania Limited	31-Dec-05	-323,000	35	Mchakato wa ubinafsishaji
10.	Tembo Chipboards Ltd.	31-Dec-94	975,000,000	80	Mchakato wa ubinafsishaji
11.	Usafiri Dar-Es-Salaam (UDA)	30-Jun-06	846,631,959	49	Litabinafsish wa hivi karibuni
12.	Tembo Chipboards Ltd.	31-Dec-94	975,000,000	80	Mchakato wa ubinafsishaji
Jumla			91,900,617,960		

Serikali inapaswa kuharakisha mchakato wa ubinafsishaji wa Mashirika yaliyotajwa hapo juu.

12.3 Mashirika ya Umma Ambayo Hayafanyi Kazi

Kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina Mashirika ya Umma kumi na nne (14) yalikuwa hayafanyi kazi. Upembuzi wa taarifa ya Msajili wa Hazina imeonyesha kuwa Serikali ilikuwa imewekeza rasimali zenye thamani ya Shilingi

85,905,745,060 katika mashirika hayo ikiwa ni hisa na raslimali nyingine. Mashirika ya Umma ambayo hayafanyi kazi ni kama yafuatavyo:

Na	Shirika	Ukaguzi wa mwisho	Jumla Shs	Umiliki wa Serikali %	Maelezo
1.	Kisarawe Brick Factory (KIBRICO)	31-12-2003	-144,065,000	30	Halifanyi kazi. Mchakato wa kuuza hisa za Serikali
2.	Kilimanjaro Machine Tools	31-12-89	-652,989,944	100	Halifanyi kazi. Raslimali zilihamishiwa NDC ili kundeleza kanda ya uuzaji bidhaa nje ya nchi.
3.	SIMU 2000 Ltd	31-12-06	43,346,350	100	Limeacha kufanya kazi rasmi tarehe 30/6/06, na kuhamishiwa CHC mwezi Mei, 2007.
4.	Loans Advances Realization Trust (LART)	30-06-06	1,575,250,000	100	Limeacha kufanya kazi rasmi tarehe 30/6/06, na kuhamishiwa CHC mwezi Mei, 2007
5.	Mikumi Wildlife Lodges	30-06-96	1.	100	Halifanyi kazi
6.	MMT - Mang'ula	31-12-87	191,355,469	100	Halifanyi kazi Lilibinafsishwa na PSRC. Liko kwenye hatua ya kukabidhiwa kwa mwekezaji mpya (St. Mary International Schools)

7.	National Milling Corporation	30-06-94	14,511,600	100	Halifanyi kazi.
8.	Nyanza Glass Works	30-Juni-00	7,710,570,174	100	Halifanyi kazi. Lilikabidhiwa kwa NDC na PSRC mwezi Machi 2007.
9.	PEHCOL	30-Juni-00	4,601,072,024	100	Halifanyi kazi
10.	Public Sector Reform Commission (PSRC)	31-12-2007	69,716,733,159	100	Halifanyi kazi
11.	Tanzania Automobile Manufacturing Company (TAMCO)	31-12-99	2,532,882,162	100	Halifanyi kazi. Raslimali ziliamishwa NDC ili kundeza kanda ya uuzaji bidhaa nje ya nchi.
12.	Tanzania Fishing Company (TAFICO)	30-6-94	266,129,065	100	Halifanyi kazi
13.	TeleShop Co. Limited	31-Dec-02	50,950,000	49	Halifanyi kazi
Jumla			85,905,745,060		

12.4 Mashirika ya Umma Ambayo Yako Kwenye Mchakato wa Kufilisiwa

Upembuzi wa taarifa ya Msajili wa Hazina umebaini kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yalikuwa kwenye mchakato wa kufilisiwa. Haya ni yale mashirika ambayo hayawezi kulipa madeni yake ya muda mfupi bila ya kuuza raslimali zake za muda mrefu. Kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina Serikali imewekeza hisa na raslimali zenye thamani ya Shilingi 10,691,261,115 kwenye mashirika hayo kumi na mawili. Mashirika ya Umma ambayo yako kwenye Mchakato wa kufilisiwa ni kama yafuatavyo:

Na	Shirika	Ukaguzi wa mwisho	Jumla ya thamani ya raslimali za Serikali	Umiliki wa Serikali %
1.	Basuto Farm	30-Sep-02	644,449,423	100
2.	BHESCO	30-Jun-01	104,285,208	100
3	Gidagamowd	30-Sep-98	239,723,885	100
4.	Imara Wood Products	31-Dec-91	194,300,000	100
5.	Kiltimbers Co Ltd	31-Dec-90	69,093,720	100
6.	Mulbadaw Farm	30-Sep-98	902,699,681	100
7.	Murjanda Farm	30-Sep-98	461,940,530	100
8.	National Shipping Co. Ltd	30-Jun-99	6,320,069,245	100
9.	Setchet Company	30-Sep-00	1,010,576,396	100
10	Tanga -RTC	30-Jun-01	126,152,332	100
11	Tanzania Elimu Supplies	30-Jun-94	347,400,197	100
12.	Tanzania Motor Services Company (TMSC)	30-Sept-98	270,570,498	100
Jumla			10,691,261,115	

12.5 Mashirika ya Umma Ambayo Yako Kwenye Mchakato wa Kuundwa Upya

Shirika huundwa upya mara baada ya kushindwa kuendesha shughuli zake za kila siku na kushindwa kulipa madeni yake ya muda mfupi na muda mrefu. Hii ni njia nzuri ya kuokoa shirika kabla ya kufikia hatua ya kufilisiwa. Kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina Serikali imewekeza hisa na raslimali zenye thamani ya Shilingi 70,859,227,000 kwenye mashirika hayo nne. Mashirika ya Umma ambayo yako kwenye Mchakato wa kuundwa upya ni kama yafuatavyo:

Na	Shirika	Ukaguzi wa mwisho	Jumla ya thamani ya raslimali za Serikali Shs	Umiliki wa Serikali %	Maelezo
1.	Shirika la Taifa la Bima	31 Des 2007	55,448,880,000	100	Mchakato wa Kuundwa upya
2.	Shirika la Migodi Tanzania	31 Des 2007	297,658,671	100	Kuwa wakala wa Serikali
3.	Bodi ya Mbegu za Pamba Tanzania	30-Jun-06	9,069,370,881.00	100	Kurekebish wa kuwa Bodi ya Udhibiti
4.	Benki ya Posta Tanzania	31-Des-06	5,859,227,000.00	45.3	Mchakato wa Kuundwa upya
Jumla			70,859,227,000		

12.6 Shirika la Umma Ambalo Liko Kwenye Mchakato wa Kufungwa

Upembuzi wa taarifa ya Msajili wa Hazina ulibaini kuwa "Tanzania Hotels Investment Co. Ltd (TAH) haliwezi kulipa madeni yake ya muda mfupi au ya muda mrefu na liko kwenye mchakato wa kufungwa. Tanzania Hotels Investment Co.Ltd (TAH) shirika linalomilikiwa asilimia mia moja na Serikali limekuwa likijiendesha kwa mtaji hasi ya shilingi 12, 506,598,308 kama ilivyonakiliwa kwenye taarifa ya Msajili wa Hazina. Kampuni tanzu zote za shirika hili zilishabinafsishwa na Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC).

12.7 Wadeni wa Siku Nyingi na Malipo ya Awali Sh. 7,424,072,923

Upembuzi wa taarifa ya mwaka ya PSRC ulibaini wadaiwa wa siku nyingi wenye jumla ya deni la shilingi

7,424,072,923. Uthibitisho wa deni ulifanyika kwa kuwaandikia baadhi ya wadaiwa 27 katika kuthibitisha deni wanalodaiwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2007 ambapo ni wadaiwa 9 tu ndio waliojibu.

Hata hivyo, kati ya wadaiwa tisa (9) waliojibu, wanne (4) kati yao hawakukubaliana na kiasi walichokuwa wakidaiwa kwa madai kuwa taarifa za tume zilikuwa sio sahihi na zilikuwa ni zaidi ya deni wanalodaiwa. Jumla ya deni lilodaiwa kuwa ni zaidi ya deni ni shilingi 2,498,518. Hii ina maana kuwa bakaa ya wadaiwa haikuwa sahihi.

12.8 Amana za Wanunuzi Zisizokuwa na Vielelezo Sh.6,746,157,339

Mizania ya hesabu ya PSRC ya tarehe 31 Disemba 2007 ilikuwa na amana za wanunuzi wa Mashirika ya Umma yaliyokuwa yamebinafsishwa. Mashirika hayo yalikuwa na mauzo ya rasimali za umma zipatazo shilingi 8,448,452,749 kutoka kwa wenye dhamana 316. Upembuzi wa taarifa za wenye amana 211 zenye thamani ya shilingi 7,203,502,344 ulibaini kuwa shilingi 6,632,693,934 za wanunuzi wenye amana 208 zilinakiliwa kama wadai badala ya makusanyo ya fedha taslimu bila ya kuonyesha mapato yaliyopatikana kutoka kwa wanunuzi hao. Mchanganuo ufuatao unaonyesha wanunuzi wenye amana:

Maelezo	Namba	Kiasi cha Amana Sh.
Bei ya manunuzi iliyolipwa yote	129	2,367,402,616
Bei ya manunuzi ambayo haijaonyeshwa	8	2,398,400,000
Wadaiwa wa siku nyingi	62	1,396,580,301
Fedha zilizolipwa zaidi ya bei ya manunuzi	9	12,966,017
Zinazosubiri idhini ya Serikali	3	570,808,410

Amana za wanunuzi zikinakiliwa vibaya husababisha “overstatement” kwa wadai PSRC na “understatement” ya mapato kutoka kwa Mashirika yaliyobinafsishwa. Kunakili vibaya kunaweza kupelekea wizi unaotokea kwa njia ya kughushi. Hapakuwepo na marekebisho ya kutambua mapato hususani kwa wenye amana ambao wamelipa fedha kamili za manunuzi ya mashirika ya umma wala wale waliolipa zaidi ya bei ya manunuzi.

12.9 Gharama za Ubinafsishaji Ambazo Hazikuwa na Mikataba Sh.1,248,681,919

Upembuzi wa gharama za ubinafsishaji zilizotumika ulibaini malipo ya shilingi 1,248,681,919 ambazo hazikuwa na nyaraka za mikataba. Mpaka wakati wa kuandika taarifa hii ya ukaguzi nyaraka hizo zilikuwa hazijapatikana na hivyo usahihi wa malipo yaliyotajwa hapo juu haukuweza kuthibitishwa.

12.10 Tathmini na Usimamizi Baada ya Ubinafsishwaji.

Kutokana na taarifa ya utendaji ya Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2007 ubinafsishaji wa mashirika sita (6) ulikuwa umekamilika. Ubinafsishwaji wa mashirika umekamilika vizuri lakini matokeo au utendaji wa mashirika hayo limebakia suala kubwa la kujiuliza. Hata hivyo Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC), limeweza kuandaa sera ya usimamizi na tathmini baada ya ubinafsishaji. Sera hiyo ni dira ambayo itatumika kutoa utaratibu mzima wa kusimamia na kufanya tathmini ya raslimali zilizobinafsishwa. Pia sera hiyo itawezesha kufanya mchanganuo wa matokeo ya utendaji wa mashirika hayo baada ya ubinafsishaji.

Katika kutekeleza sera ya ufuatiliaji na usimamizi wa Mashirika na raslimali za Umma baada ya ubinafsishaji, Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) lilikuwa limepanga kufanya tathmini ya Mashirika 40 yaliyobinafsishwa, hata hivyo liliweza kufanya tathmini ya mashirika 20 tu kufikia tarehe 31 Disemba 2008.

SURA YA KUMI NA TATU

MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU

13.0 Utangulizi

Sehemu ya 35 (2) (3) ya Sheria ya Fedha Na. 6. ya 2001 (iliyorekebisha 2004) na iliyobadilishwa na Sehemu ya 36 (1) ya Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 inampa nguvu za kisheria Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi Maalumu. Sheria inasema wazi kuwa pale ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaona kuna haja ya kulitaarifu Bunge la Jamhuri ya Muungano kuhusu matumizi ya raslimali za Umma, afanye hivyo bila kuchelewa, ataandaa taarifa ya ukaguzi maalumu kuhusiana na mambo hayo na kupeleka taarifa ya ukaguzi huo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Kutokana na jukumu hilo alilopewa kisheria, kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi maalumu katika mashirika ya umma matatu; ambayo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Moshi (MUWSA). Hata hivyo, ukaguzi maalumu wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haujakamilika hivyo taarifa yake haijajumuishwa kwenye sura hii.

13.1 Ukaguzi Maalumu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA)

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipokea barua yenye Kumb. SHC/1.50/1/12 ya tarehe 31 Julai 2008 ikieleza tuhuma za matumizi mabaya ya fedha na raslimali za umma katika Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA). Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliombwa kufanya ukaguzi maalumu ili kubaini ukweli wa tuhuma hizo. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikubali kufanya ukaguzi huo maalumu na kugundua mambo yafuatayo.

13.2 Matokeo ya Ukaguzi na Mapendekezo

13.2.1 Mapungufu ya Miongozo ya Uendeshaji wa Mamlaka

Tulibaini kuwa mamlaka ilikuwa ikitumia muongozo uliokuwa umeandaliwa na M/s Delloite & Touch Tohmatsu Emerging Market Ltd utumike kwa ajili ya kuanzishwa kwa mamlaka na misingi ya miongozo ya fedha, sheria za watumishi na sheria za kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za mamlaka. Hata hivyo, taratibu na miongozo hiyo ilikuwa na mapungufu makubwa na ilikuwa imepitwa na wakati.

Kwa ujumla muongozo huo ulikuwa unatumika kama sehemu kuu ya kunukuu sheria zote za malipo, sheria za utumishi na sheria nyinginezo za uendeshaji wakati ambapo sheria na miongozo hiyo ilitakiwa kuandaliwa na kutunzwa tofauti. Muongozo huo ulikuwa na mapungufu mengi kutokana na ukweli kwamba haukuandaliwa utumike kama unavyotumika. Muongozo huo uliandaliwa kama kielelezo cha kuanzisha mamlaka, na baadaye ilitakiwa iandaliwe miongozo mingine tofauti ya uendeshaji na kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ili itumike katika kuendesha shughuli za kila siku za mamlaka hiyo.

Mpangilio wa Mafunzo, Semina na Mikutano Nje ya Nchi Ambayo Haikutekelezwa

Mamlaka ilitumia muongozo uliokuwa umeandaliwa na mshauri mtaalamu M/s Delloite & Touch Tohmatsu Emerging Market Ltd ikishirikiana na LeoBoef Lamb Greene na MacRacw National Economic Research Associates ambao unatoa muongozo wa mafunzo yanayohitajika kwa mamlaka ya udhibiti. Uchambuzi wa muongozo huo ulifanywa ili kubaini ni kwa kiwango gani ambacho mamlaka ilikuwa imetumia muongozo huo katika kuendesha shughuli za mafunzo. Muongozo pamoja na mambo mengine unaelekeza mpango wa mafunzo na semina zifanyike ndani na nje ya nchi.

Mwongozo wa mafunzo unaitaka mamlaka kuchuja mapendekezo ya mpango wa elimu kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi wake. Hata hivyo, mamlaka iliendesha shughuli zote za mafunzo bila kujali mahitaji ya mafunzo kwa watumishi. Mafunzo yamefanywa bila kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo. Kwa hiyo, inawezekana mamlaka imeingia gharama za mafunzo kwa mafunzo ambayo hayahitajiki kutokana na kutokuwepo na tathmini ya mahitaji ya mafunzo.

Zaidi ya hayo mwongozo unaitaka mamlaka kutumia mafunzo ya wakufunzi (Training of the trainers approach) ambapo wafanyakazi wachache na wajumbe wa bodi wangeweza kufundishwa na baadae kutumia ujuzi walioupata kufundisha wengine, na kwa hiyo gharama za mafunzo zingepungua. Kwa vile hapakuwepo na watumishi na wajumbe wa Bodi ambao walikuwa wamehudhuria mafunzo kwa ajili ya kuwafundisha wenzao kutokana na mpango wa elimu uliopo, mamlaka iliendesha shughuli zote za mafunzo bila kufuata matakwa ya muongozo wa mafunzo na kuingia gharama ambazo zingeweza kuepukika.

13.3 Wajibu wa Bodi ya Wakurugenzi na Waziri Mwenye Dhamana Kuhusu Bajeti ya Mamlaka

Wajibu wa bodi ya wakurugenzi na Waziri katika kupitisha bajeti na bajeti nyongeza ya mamlaka unadosari kubwa. Sehemu ya 49(1) na (2) ya Sheria ya EWURA ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2002) inaitaka mamlaka kuandaa bajeti na kuituma kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa taarifa. Hivyo, bajeti ya nyongeza nayo inatakiwa pia kupelekwa kwa Waziri kwa taarifa. Kinyume na mujibu wa Sheria bajeti ya nyongeza katika mwaka husika haikutumwa kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa taarifa.

Pamoja na nia njema ya kuifanya mamlaka kuwa na madaraka na Taasisi yenye ufanisi bora duniani, jukumu la bodi ya wakurugenzi kuhusu kupitisha bajeti linapaswa

kuwekwa wazi kulingana na yaliyojitokeza na kwa kuzingatia matakwa ya utawala bora.

13.4 Malipo ya “Arrears” ya Posho ya Kujikimu Sh.62,760,288

Ilibainika kuwa jumla ya shilingi 62,760,288 zililipwa kwa wafanyakazi na wajumbe wa bodi mwezi Disemba mwaka 2007 kama malipo ya “Arrears” ya kujikimu. Malipo ya “Arrears” ya posho za kujikimu yalitokana na kurekebishwa kwa aina ya fedha za kigeni zitakazotumika kulipia posho ya kujikimu kutoka dola za Kimarekani kwenda Euro ambapo malipo ya awali yalikuwa yamelipwa kwa dola za Kimarekani. Kibali cha kulipa malipo hayo kilitolewa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji tarehe 19 Novemba 2007 ambacho kilihusu malipo yaliyolipwa kuanzia Julai 2007, hadi mwezi Novemba 2007. Kwa maoni yetu hii ni kinyume na taratibu zinazohusu malipo ya posho ya kujikimu kwa sababu watumishi na wajumbe wa bodi walikuwa wamesharudi kutoka safari, kwa hiyo haikuwepo sababu yoyote ya kimsingi ya kulipa posho ya kujikimu “restrospectively”. Zaidi ya hayo, kwa kuwa EWURA ni Taasisi ya Serikali inapaswa kufuata (inabanwa) miongozo inayotolewa na Katibu Mkuu Utumishi na Msajili wa Hazina juu ya malipo ya posho ya kujikimu. Kwa hiyo, mtu anaweza kushangaa kwamba kibali kilichotolewa na Waziri cha kurekebisha aina ya fedha za kulipia posho ya kujikimu kutoka dola za Kimarekani kwenda Euro ni sahihi.

13.5.1 Tozo Dogo kwa Petroli Iliyochanganywa Mafuta ya Taa/Maji

Katika kipindi cha mwaka 2007/08 jumla ya sampuli 237 petroli /dizeli zilifanyiwa uchunguzi. Ilibainika kuwa sampuli 138 kati ya hizo 237 zilikuwa zimechanganywa na mafuta ya taa/maji ambayo ni sawa na asilimia 58 ya sampuli yote. Ilibainika kuwa tabia ya kuchanganya mafuta ya taa/maji na petroli/ dizeli inasababishwa na:-

- Kodi mafuta ya taa ni ndogo na pia mafuta ya taa yana msamaha wa kodi wa shilingi 400 kwa lita ambacho ni

kichocheo kinachowafanya wafanyabiashara wasio waaminifu kuchukua wasaa huo kukwepa kulipa kodi kwa kuchanganya mafuta ya taa/maji na petroli/dizeli.

- Kiasi cha chini na cha juu cha tozo kwa wafanyabiashara ambao siyo waaminifu ni shilingi 1,000,000 na shilingi 3,000,000 kwa siku kwa kuchelewa kulipa tozo baada ya kupewa taarifa ya kulipa.

Tunaona kwamba kutokana na hali ya uchumi wetu kwa sasa, tozo wanalopewa wafanyabiashara ambao siyo waaminifu ni dogo sana ambalo halitoshi kuwavunja moyo wa kuendelea na tabia hiyo ya kuchanganya petroli na mafuta ya taa/maji.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa mamlaka imepewa nguvu za kisheria kutoza tozo isiyozidi shilingi 3,000,000 au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa mtu yeyote anayechanganya petroli na mafuta ya taa/maji kwa mujibu ya sehemu ya 42(1) ya sheria ya EWURA. Hata hivyo mamlaka imeonekana kutokutumia sheria iliyotajwa hapo juu kuwatoza wafanyabiashara ambao siyo waaminifu. Hii inaonyesha kwamba tozo inayotozwa inashawishi hali hiyo kuendelea, kwa mfano kama mfanyabiashara akichukua lita 39,000 za mafuta ya taa akichanganya na lita 61,000 za dizeli atapata lita 100,000 za mafuta machafu, ambazo akiziuza atapata faida halisi ya shilingi 15,600,000 kama hatakatwa na watumishi wa EWURA. Hata hivyo kama mfanyabiashara huyo atakamatwa na watumishi wa EWURA atalipa tozo ya shilingi 3,000,000 ambapo atabakiwa na faida halisi ya shilingi 12,600,000.

Kwa hali hii, tabia ya kuchanganya petroli na mafuta ya taa/maji itaendelea hadi hapo EWURA itakapo

chukua hatua kali ikiwa ni tozo ya shilingi 3,000,000 na kifungo cha miaka mitano kwa pamoja.

13.6 Gharama za Malazi Nje ya Nchi Sh.171,175,219

Jumla ya shilingi 171,175,219 zilitumika kwa ajili ya gharama ya malazi kwa wafanyakazi na wajumbe wa bodi ya mamlaka ya EWURA walipokuwa wamesafiri kikazi nje ya nchi.

Posho ya kujikimu inayolipwa kwa mtumishi/mjumbe wa bodi kwa safari za kikazi ni kwa ajili ya kulipia gharama zote (yaani gharama za malazi na mlo). Kwa maana hiyo, jumla ya fedha shilingi 171,175,219 zinaonekana zimelipwa isivyo sahihi na ni malipo mara mbili.

Manejimenti ilidai kuwa kiwango cha sasa cha posho ya kujikimu kinacholipwa Euro.300 kwa watumishi wengine na Euro.350 kwa wajumbe wa bodi ikiwa ni pamoja na gharama za malazi ziliidhinishwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Hata hivyo, barua iliyoomba idhini ya kubadilisha viwango vya posho ya kujikimu kutoka Dola za Kimarekani 300 kuwa Euro 300 kwa wafanyakazi wengine na kutoka dola za Kimarekani 350 kuwa Euro 350 kwa wajumbe wa bodi haikuonyesha kwamba viwango vya posho ya kujikimu vilikuwa vilipwe sambamba na gharama za malazi.

Mahojiano na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Umwagiliaji, yalithibitisha kuwa Wizara iliidhinisha viwango vya posho ya kujikimu ikiwa inafahamu kuwa viwango hivyo ni gharama zote za kusafiri kama zilivyo taratibu za Serikali.

Kwa hali hiyo, kiasi chote kilicholipwa kama gharama za malazi kinaonekana kuwa gharama mara mbili.

13.7 Ukaguzi Maalum MUWSA

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipokea barua yenye Kumb. Na. MUWSA/MU/5/VOL III/194 ya tarehe 9/7/2008 kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi ikimuomba kufanya ukaguzi maalum katika Idara ya Ugavi ya Mamlaka hiyo kwa ajili ya kubaini ukubwa wa upotevu wa mali ya stoo ulitokea katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30/06/2008.

13.8 Yatokanayo na Ukaguzi Maalum

Kutokana na Ukaguzi maalum tuligundua upotevu wa mali za stoo zenye thamani ya shilingi 98,957,617. Hii ilitokana na upembuzi wa akiba ya bidhaa/vifaa kwa baadhi ya vifaa kwa mujibu wa hadidu rejea ambapo uligundulika upotevu huo.

SURA YA KUMI NA NNE

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

14.0 Utangulizi

Kutokana na udhaifu uliobainika katika kaguzi za Mashirika ya Umma pamoja na hoja za ukaguzi zilizoandikwa katika sura za awali za ripoti hii ninazo sababu za kutosha za kuhitimisha na kutoa mapendekezo kwa Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za mashirika husika.

Sura hii inahusu hitimisho na mapendekezo kwa mambo muhimu yaliyobainika na kaguzi ambayo yanahitaji kuangaliwa na Serikali na Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti husika za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo. Mapendekezo haya yanatolewa kulingana na mamlaka niliyopewa chini ya kifungu Na. 34 cha Sheria ya fedha za Umma Na. 6 ya 2001 (iliyorekebisha 2004) na kubadilishwa na Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya 2008 kwa madhumuni ya kuzuia na kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyokuwa na tija, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya umma na kuzuia hasara zinazotokana na uzembe, wizi, udanganyifu, na kugushi fedha na matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Baada ya kukagua na kuhitimisha kaguzi za hesabu za fedha za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kwa kipindi cha ripoti hii na kwa kutumia mamlaka niliyopewa, yafuatayo ni hitimisho na mapendekezo.

14.1 Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Mwaka Uliopita

Kulikuwepo na mambo muhimu ambayo yalibainika na kaguzi za mwaka uliopita ambayo yalitolewa mapendekezo. Baadhi ya mapendekezo hayakutekelezwa kikamilifu na mapendekezo mengine hayakutekelezwa kabisa kama yalivyoonyeshwa kwa kifupi katika sura ya tatu ya taarifa hii.

Mapendekezo

Serikali, Bodi za wakurugenzi na watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuongeza juhudi zaidi katika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya kaguzi za mwaka uliopita ambayo hayakutekelezwa yanatekelezwa kwa wakati ili kuongeza kasi ya ufanisi ya utendaji na kufikia lengo la kitaifa la “Millennium Development Goals”.

14.2 Usimamizi wa Mapato na Matumizi

14.2.1 Usimamizi wa Mapato

Katika kaguzi zetu za usimamizi wa mapato tulibaini baadhi ya Mashirika ya Umma ambayo yalikuwa na mifumo hafifu ya kusimamia mapato ambapo ilipelekea kutokuandaa kwa wakati bili za wateja, kuchelewa kukusanya mapato, kutokuwa na taarifa sahihi na kamilifu za mapato pamoja na kutokuwa na udhibiti wa makusanyo ya mapato.

Mapendekezo

Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa ankara za madai zinaandaliwa na kupelekwa kwa wateja kwa wakati, mapato sahihi yanakusanywa na kuandikwa kwa usahihi kwenye vitabu vya mahesabu na kuimarisha udhibiti wa mapato katika kuondoa mianya yote ya ubadhirifu wa fedha za Umma.

14.2.2 Usimamizi wa Matumizi

Kwa upande mwingine, katika kaguzi zetu za usimamizi wa matumizi ya fedha iligundulika kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yalikuwa na mifumo hafifu wa kudhibiti matumizi ya fedha ambayo ilipelekea baadhi ya malipo kufanywa bila idhini ya maafisa wenye dhamana na malipo mengine kufanywa bila kuwa na nyaraka sahihi.

Mapendekezo

Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa malipo

yanaidhinishwa na maafisa wenye dhamana na nyaraka husika zinaambatanishwa pamoja na hati za malipo ambapo itapelekea kuimarisha usimamizi wa matumizi katika Mashirika ya Umma.

Pamoja na hayo, mahitimisho na mapendekezo yetu ya jumla yanasisitizwa na mifano halisi ifuatayo:

- (i) **Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)**
Jumla ya Dola za Kimarekani 4,865,000 zililipwa kwa Mkandarasi M/s Dowans ikiwa ni gharama ya kukodi ndege maalumu kwa ajili ya kusafirisha vifaa vya kuzalishia umeme kuja Dar es Salaam bila ya kuwa na kifungu kwenye mkataba kinachoruhusu malipo ya aina hiyo na malipo hayo kufanywa bila idhini ya wenye dhamana.

Mapendekezo

Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania linapaswa kutoa maelezo ya uhalali wa malipo hayo ya Dola za Kimarekani 4,865,000 zilizolipwa kwa M/s Dowans kwa ajili ya kukodisha ndege maalumu kusafirishia mashine za kuzalishia umeme kuja Dar es Salaam bila ya kuwa na kifungu kwenye mkataba kinachoruhusu malipo hayo na malipo hayo kufanywa bila idhini ya wenye dhamana.

- (ii) **Benki Kuu ya Tanzania (BoT)**
Benki kuu ya Tanzania ililipa jumla ya shilingi bilioni 7.3 kwa wakala wa bima ikiwa ni “Insurance Premium” kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya makao makuu ya benki hiyo bila ya kuwapo kwa nyaraka sahihi zinazojitosheleza na viambatisho muhimu.

Mapendekezo

Menejimenti ya Benki Kuu Tanzania inapaswa kufanya uchunguzi wa mazingira iliyopelekea jumla ya Shilingi bilioni 7.3 kulipwa kwa wakala wa bima ikiwa ni

“Insurance Premium” kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya makao makuu ya benki hiyo bila ya kuwapo kwa nyaraka sahihi zinazojitosheleza na viambatisho muhimu, ikiwa na lengo la kuwawajibisha maofisa wanaohusika kuidhinisha malipo hayo na kuzuia malipo ya aina hiyo kujirudia hapo baadae.

(iii) Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

Ukaguzi wa mapato yanayotokana na mizigo inayoingia na kusafirishwa na bandari za maziwa uligundua upotevu wa mapato yatokanayo na “Jetties” binafsi. Iligundulika kuwa mizigo inayopitia bandari za maziwa makuu haipimwi ipasavyo. Ni sampuli ndogo tu ya mizigo mikubwa huwa inapimwa. Fomu zilizokuwa zikitumika kuhakiki uzito wa mizigo hazikuwa zikijazwa kikamilifu na kwa ufasaha.

Zaidi ya hayo, upotevu mkubwa wa mapato yatokanayo na “Jetties” binafsi katika bandari za maziwa makuu ulitokana na shughuli nyingi ambazo zingeweza kuingizia Mamlaka ya Bandari mapato kutokutozwa gharama za bandari ikiwa ni pamoja na mapato kutokukusanywa kusini na mashariki mwa bandari za Mwanza na Nansio.

Mapendekezo

- Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari ya Mwanza na Nansio inapaswa kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na “Jetties” binafsi yanatozwa na kukusanywa kusini na mashariki mwa bandari ya Mwanza na Nansio.
- Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari Makao Makuu Dar es Salaam inapaswa kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya mapato vinatambulika na mapato yote yanakusanywa.

14.3 Kupitia Mifumo ya Ndani ya Udhibiti

Katika kaguzi za mifumo ya ndani ya udhibiti iligundulika kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yalikuwa na mifumo iliyokuwa na mapungufu kama yalivyoelezwa hapo chini:

- Utunzaji mbovu wa hundi zilizokuwa zimeandikwa kimakosa (Cancelled cheques) ambazo zingeweza kutumiwa na watumishi ambao sio waaminifu kulipa malipo ambayo hayajaidhinishwa.
- Baadhi ya Mashirika ya Umma hayakuwa yakifanya usuluhisho wa kibenki. Hii iliongeza athari za kushindwa kugundua kwa wakati makosa ya malipo ya fedha taslimu yasiyokuwa ya kawaida. Mbali na hayo, malipo yasiyokuwa ya uhalali katika taarifa (statement) ya benki na daftari la fedha taslimu yanaweza kulipwa bila kugundulika.

Mapendekezo

- Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa ina mifumo thabiti ya ndani ya udhibiti na inatumika ipasavyo.
- Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa hundi zilizoandikwa kimakosa (Cancelled Cheques) zinatunzwa mahali salama kuepuka kutumiwa vibaya na watumishi wabadhirifu na zinatakiwa kuhifadhiwa kwa uhakiki wa ukaguzi.

14.4 Kupitia Utendaji wa Kazi

Katika upembuzi wa utendaji wa kazi katika baadhi ya Mashirika ya Umma iligundulika kuwa kuna changamoto zinazokabili utendaji kazi wa Mashirika ya Umma. Baadhi ya changamoto zinayoyikumba Mashirika ya Umma ni pamoja na mlolongo katika kutekeleza miongozo, kutokuwa na ushauri wa kisheria kwa mashirika husika, Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokuwa huru ambayo bado inafanya kazi chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi kinyume na tamko la kuanzishwa kwake. Hii ni pamoja na mashirika hayo kutokuwa na mawazo ya kibunifu na pia kutokuwa na menejimenti bora zenye utaalamu unaotakiwa. Hii

inachangiwa na Wizara mama zinazosimamia na kutathmini utendaji na uendeshaji wa mashirika ya umma kutokuwa makini.

Mapendekezo

- Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanatakiwa kujenga utamaduni wa ujasiriamali, kuajiri menejimenti bora na zenye utaalamu unaotakiwa kwenye shirika husika.
- Pia, Wizara mama zinapaswa kujenga uwezo wa ndani ili kuweza kusimamia na kufanya tathmini ya utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Wizara hizo.
- Msajili wa Hazina anapaswa kuimarisha ofisi yake katika suala zima la usimamizi wa Mashirika ya Umma.
- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inapaswa kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi wake katika suala zima la kuingia katika mikataba ya kisheria na suala zima la usimamizi wa mikataba.
- Mawaziri wenye dhamana wanapaswa kuhakikisha Mashirika ya Umma yaliyoko chini yao yanaendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.
- Msajili wa Hazina anapaswa kuhakikisha kuwa mashirika yanaajiri watumishi wenye sifa zinazotakiwa na shirika husika.
- Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka zinapaswa kuhakikisha zinawatambua wateja wake na kuharakisha kazi ya kuwafungia mita kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na mauzo ya maji.
- Menejimenti ya Benki Kuu ya Tanzania inapaswa kuandaa sera na miongozo ya kushughulikia fedha haramu na kudhibiti fedha zinazoweza ugaidi.
- Menejimenti ya Shirika la Utangazaji inapaswa kuhakikisha kuwa maombi ya matangazo ya kibiashara (BCOs) yanaandaliwa kwa matangazo yote yanayofanywa na hakuna tangazo litakalorushwa hewani bila ya maombi kutoka kwa mteja.
- Menejimenti ya Mamlaka ya Bandari inapaswa kuzingatia kifungu Na. 7.4.2 (2) cha mkataba wa ukodishaji na

kuendelea kuishawishi Serikali kuvunja mkataba na TICTS wa ukodishaji kwa misingi ya utendaji kazi mbovu wa mkodishaji ili kuruhusu mwendeshaji mwingine kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

14.5 Kuzingatia Sheria ya Manunuzi

- Mashirika ya Umma yanapaswa kufuata na kuonyesha utendaji bora katika manunuzi ya vifaa, huduma na kazi za ujenzi ili kuhakikisha matokeo ya kazi yanalingana na thamani ya fedha zilizotumika. Pia, Watendaji Wakuu wanapaswa kuendelea kuboresha na kuweka mifumo ya ununuzi katika kuhakikisha suala zima la thamani ya fedha linazingatiwa.
- Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inapaswa kufanya uchunguzi maalumu katika mamlaka ya kudhibiti Mawasiliano (TCRA) kuhusu zabuni ya kutathimi muundo, na kazi na ngazi za mishahara (Organisation review, job evaluation, na job grading) ambayo awali ilitangazwa tarehe 16, 17 na 20 Agosti 2007 na kuingia mkataba tarehe 28 Januari 2008 kinyume na mapendekezo ya Kamati ya Tathmini.
- Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inapaswa kufanya uchunguzi na kujiridhisha kuwa uwazi na taratibu za manunuzi zilifuatwa na Menejimenti ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika mchakato mzima wa kutathimi na kuingia mkataba wa huduma za ulinzi na kampuni ya M/s Alliance Day and Night Limited.
- Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) inapaswa kufanya uchunguzi maalumu katika Shirika la Utangazaji Tanzania kuhusu zabuni mbili za kuongeza ubora wa Studio ya Redio katika jengo jipya la BH, PRT na “Scoop News Studio” liliko TVT Mikocheni kwa gharama ya paundi 53,212 na kutoa huduma ya mtandao kwa gharama ya shilingi 172,000,000 aliyopewa Mzabuni M/s P Square Ltd ya Uingereza na M/s WiA Company Ltd”.

- Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania inapaswa kufanya uchunguzi maalumu kuhusu mkataba wa pamoja (joint venture) kati ya M/s Tangerm Ltd ya Dar es Salaam na M/s Techno Combine Construction Ltd kwa ajili ya ujenzi wa “container staking yard” katika sehemu lilokuwa jengo la TANESCO kwa gharama ya shilingi 4,165,666,875.

14.6 Usimamizi wa Mikataba

Upembuzi wa mikataba iliyokuwa imengiwa kati ya makampuni binafsi na Mashirika ya Umma ulibaini baadhi ya mikataba mibovu na ambayo haikuwa ya kisheria. Mikataba iliyopembuliwa na kubainika kuwa na mapungufu ni ile iliyokuwa imeingiwa na shirika la TANESCO, BoT na NSSF. Kutokana na upembuzi wa mikataba hiyo yafuatayo ni mapendekezo:-

Mapendekezo

- Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania inapaswa bila kuchelewa kupitia upya makubaliano ya mradi wa SONGAS na kubaini gharama halisi zitakazopaswa kulipwa.
- Menejimenti ya Benki Kuu inapaswa kupitia Mkataba uliopo wa kuendeleza majengo ya makao makuu ya benki hiyo ili kubaini kama bado makubaliano hayo ni halali na benki imejilinda na vihatarishi vya mkataba. Upembuzi pia ufanyike katika mkataba wa “Sub - contractor and consulting engineers”. Upembuzi uzingatie pia kuweka gharama na muda wa kumaliza kazi ya ujenzi. Kwa vile benki itaendelea kuwa na wakandarasi kama vile usimamizi wa majengo na wale wa kuendeleza teknolojia ya mawasiliano inapaswa kufikiria na kuunda mbinu bora za usimamizi wa miradi inayoendelea.
- Menejimenti ya Benki ya Tanzania inapaswa kufanya uchunguzi huru kuhusu malipo ya Bima ya ujenzi wa majengo ya makao makuu ya BoT na kuchukua hatua

sahihi ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha zilizolipwa kama bima (Premiums).

- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kuthibitisha endapo thamani ya fedha ilipatikana wakati wa kutekeleza, mradi wa kompyuta wa “Oracle e-business Suite Application and Core Fund Management System Project” kwa kuunda tume ya kufanya uchunguzi.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kufanya uchunguzi wa mapungufu yote yaliyojitokeza wakati wa kuuza nyumba za shirika zilizokuwa “ADA - Estate Kinondoni” kwa lengo la kubaini uhalali wa zoezi zima la kuuza nyumba hizo. Hatua zinapaswa kuchukuliwa kwa watumishi waliohusika na kusimamia makubaliano na mkataba huo endapo itabanika kulikuwepo na uzembe katika uuzaji wa nyumba hizo.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kuthibitisha kuwa thamani ya fedha ilipatikana katika kuuza majengo ya Club Oasis au vinginevyo kuunda tume huru ya kuchunguza uhalali wa mauzo ya club hiyo.

14.7 Utunzaji Rasilimali

Serikali inapaswa kuiwezesha Wizara ya Fedha na Uchumi kuanzisha kitengo maalumu ambacho kitashughulikia na kutathmini hisa za Umma. Kuna umuhimu wa kitengo hicho ukizingatia hali ya sasa ya mapato hasi (negative return) yanayopatikana kutokana na uwekezaji wa hisa za Serikali. Pindi mradi utakapoangaliwa na kugundulika una faida, Serikali itapaswa kuingiza fedha kwenye miradi hiyo yenye faida kubwa.

14.8 Utawala Bora

Utawala bora unahamasisha ulazima wa Mashirika ya Umma kuwa na sera bora za kusimamia rasilimali. Katika kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali, shirika linahitaji kuwa na mlolongo wa taratibu ambazo zitalifanya kuwa na vidhibiti madhubuti ambavyo vitaondoa kama sio kupunguza udanganyifu, wizi, uzembe na utendaji wa kazi usiokuwa makini. Shirika linapaswa kujipanga na kuandaa mipangilio ambayo itahimiza uwazi na mifumo ya ndani

madhubuti. Hivyo, muundo wa Shirika unapaswa uwezeshe katika kujipima.

Madhumuni ya utawala bora katika undeshaji kazi za kila siku ni kwa shirika husika kuwajibika kikamilifu na kutimiza matakwa na matarajio ya wadau kiuchumi na kijamii. Zaidi ya hayo, Mashirika yanatakiwa kuwa na maadili ya kazi, mpango wa huduma kwa jamii, bajeti za mwaka sambamba za bodi ya wakurugenzi makini kwa ajili ya kufanya maamuzi makubwa na mazito ya Shirika.

Tulibaini kuwa baadhi ya mamlaka za juu za Serikali zilikuwa zinaingilia utendaji kazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo katika kufanya maamuzi makubwa ya kiutendaji. Kwa mfano, TANAPA ilipokea maagizo Kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii kuingia mkataba na CNN na Jambo Publication Ltd bila kufuata taratibu za manunuzi. Haikufahamika mara moja kwa Wakaguzi ni kwa kiasi gani Bodi ya Wadhamini na Menejimenti ya TANAPA ilihusishwa katika kufanya maamuzi haya makubwa mbali na kutekeleza maagizo ya Wizara. Zaidi ya hayo, tulishindwa kuelewa Wizara inatumia Sheria ipi kuamuru TANAPA kuingia mkataba bila kuzingatia matakwa ya utawala bora.

Mapendekezo

- Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Tanzania anapaswa kufikiria kupanua majukumu ya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma (POAC) katika kuhakikisha kuwa inasimamia hesabu za Mashirika na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa. Pia kuna haja ya kuendelea kuiboresha kamati ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.
- Serikali inapaswa kuingia mkataba wa kiutendaji na wakurugenzi wa bodi na kuandaa malengo ambayo yatatakiwa kutekelezwa katika kipindi cha bodi ikiwa madarakani na ambayo yatakuwa wazi. Kwa hali hiyo bodi ya wakurugenzi nayo itapaswa kuingia mkataba wa kiutendaji na watendaji wakuu wa mashirika ya umma

ambao pia watatakiwa kuingia mkataba wa kiutendaji na wasaidizi wao.

- Bodi za wakurugenzi wa mashirika ya umma zinapaswa kuhakikisha watendaji wakuu wa mashirika ya umma wanawajibika zaidi kwa matokeo ya utendaji kazi wao. Bodi za wakurugenzi zipewe mamlaka zaidi ya kuingia mikataba ya kiutendaji (performance contract) na viongozi wa Juu wa mashirika ya umma baada ya kuainisha malengo ya mwaka ambayo watatakiwa kuwajibika. Malengo ambayo watendaji wakuu watatakiwa kuwajibika yanatakiwa yawe wazi. Kwa hali hiyo kuna haja kuangalia uwezekano wa watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma kuteuliwa na Bodi za Wakurugenzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa na wajibu wa kuteuwa wenye viti wa Bodi za Wakurugenzi.
- Kwa vile Bunge ni chombo cha juu kinachowawakilisha wananchi na kinachosimamia utendaji wa kazi wa Mashirika ya Umma kupitia Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma (POAC), na ili kuepuka mgongano wa kimaslahi, napendekeza kuwa wabunge wasiwe wajumbe wa Bodi za wakurugenzi za Mashirika ya Umma kama ilivyoazimiwa na mkutano wa uwajibikaji wa Mashirika ya Umma uliofanyika Januari 2009.
- Kwa kuzingatia mapendekezo niliyoyatoa kwenye taarifa yangu ya mwaka 2007 kwamba kuongezwa kwa muda wa TICTS haukuwa sahihi, kutoka mwaka 2010 hadi mwaka 2025, mkataba umalizike kama ilivyokuwa kwenye mkataba wa awali. Mamlaka ya Bandari Tanzania inapaswa iendelee kujibadilisha yenyewe kama ilivyoainishwa kwenye mpango mkakati wake na kwa mujibu wa Sheria ya Bandari ya mwaka 2004. Mkutano wa Uwajibikaji uliazimia kuwa mkataba wa TICTS na Mamlaka ya Bandari Tanzania usitishwe rasmi ili aweze kupatikana mwendeshaji mwingine ambaye ana uwezo wa kuendesha shughuli za kontena kwa ufanisi zaidi.
- Menejimenti ya Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO) inapaswa kuhakikisha kuwa linafua umeme

kulingana na mpango nyongeza katika muda uliopangwa na pia kutengeneza mtandao wa kusambaza umeme kupeleka katika vituo vilivyokusudiwa.

- Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuligawa mara mbili Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania; ambapo shirika moja litashughulika na shughuli za kibiashara na la pili lishughulike na utoaji wa leseni, kufanya ukaguzi na kufanya kazi zaidi za udhibiti. Kwa kipindi cha muda mfupi shirika la TPDC litahitaji kuwezesha kimtaji (ambapo inawezekana kwa gawiwo la mgao linalopata kutokana na mkataba wa gesi uliopo) ili kuliwezesha kutimiza majukumu yake.
- Menejimenti ya Shirika la Maji Dar es Salaam (DAWASCO) inapaswa kuwekeza kwenye uchimbaji wa maji ardhini ili yatumike kwa eneo kubwa la Jiji la Dar es Salaam ambalo halina maji. Pia, Shirika liangalie uwezekano wa kupitia upya ankara za maji ili kuiwezesha DAWASCO kulipa gharama zake za uendeshaji. Ankara za maji zirekebishwe kulingana na mfumuko wa bei.
- Wakala wa barabara Tanzania (TANROADs) inapaswa kuhakikisha kuwa inachukua hatua madhubuti kujua kwa nini gharama za utengenezaji wa barabara hapa Tanzania ni kubwa sana ukilinganisha na sehemu nyingine za bara letu la Afrika. Pamoja na kubaini kifanyike kitu gani ili kuweza kupunguza gharama hizo na kuangalia faida isiyo ya kawaida wanayopata makandarasi wa ujenzi wa barabara.
- Shirika la ndege la Tanzania (ATCL) linapaswa kuhakikisha kuwa uamuzi wowote utakaofanywa kutokana na mazungumzo yanayoendelea kuhusu ushirikiano wa pamoja (joint venture) uzingatie matakwa ya watumiaji wa ndege. Kama watumiaji wa ndege watapata huduma bora, nafuu na za kuaminika, basi soko la usafiri wa anga halina budi kuwa huria. Pia, Shirika la ndege Tanzania, bila kuchelewa linapaswa kuthibitisha kuridhia kwake kwa maamuzi ya YAMAUSSOUKRO ambayo Tanzania inapaswa kuridhia.

- Bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Maji na Nishati (EWURA) inapaswa kujikita katika kuendeleza uwezo wa mamlaka ili kuweza kutoa hudhuma bora. Pia, mshikamano na upendo baina ya wafanyakazi, uongozi wa EWURA na Bodi ya Wakurugenzi ni muhimu sana kwa kila mmoja kutimiza majukumu yake yatakayopelekea kuboresha utendaji kazi wa EWURA. Kuboresha utendaji kazi wa EWURA utategemea dira madhubuti ya Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi na wafanyakazi walio makini.
- Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kufanya maamuzi yanayohusu TANAPA kwa kuishirikisha Bodi na Menejimenti ya TANAPA pamoja na Msajili wa Hazina ambaye ni mmiliki wa Mashirika yote ya Umma kwa niaba ya Serikali. Zaidi ya hayo, TANAPA inapaswa kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya 2004 pamoja na Kanuni zake.

14.9 Ukaguzi Maalum EWURA

Wakati wa ukaguzi maalum hatukuweza kubaini upotevu wa moja kwa moja wa fedha za Mamlaka ya Udhhibiti wa Maji na Nishati EWURA. Hata hivyo kulikuwepo na matatizo katika Menejimenti ya EWURA na mpango mzima wa kujiendeleza kielimu kupitia mafunzo, mikutano nje ya nchi ikijumuisha:-

- Kulikuwepo utata kati ya majukumu ya bodi ya Wakurugenzi na Waziri mwenye dhamana juu ya uidhinishaji wa bajeti ya awali ya mamlaka na bajeti ya nyongeza.
- Wajumbe wa bodi na watumishi walihudhuria mafunzo ya nje ya nchi walilipwa mara mbili ambapo walilipwa posho ya kujikimu na wakati huo huo kulipiwa gharama za malazi.
- Mamlaka ya Uthibiti wa Maji na Nishati EWURA haifanyi juhudi kubwa katika kuondoa tatizo la kuchanganya petroli/dizeli na mafuta ya taa/maji.

- Uchanganyaji petroli/diseli na mafuta ya taa /maji ni mbinu mojawapo ya kukwepa ulipaji wa kodi.

Mapendekezo

- Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa fedha zilizolipwa zaidi kwa wakurugenzi wa bodi na watumishi wa EWURA zinarejeshwa kwenye akaunti husika.
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapaswa kuhakikisha kuwa safari za mafunzo nje ya nchi kwa wajumbe wa bodi na watumishi wa EWURA zinapangwa kikamilifu na fedha za kugharamia mafunzo hayo zitolewe kulingana na gharama halisi za mafunzo.
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapaswa kuhakikisha kuwa safari za mafunzo nje ya nchi kwa wajumbe wa bodi na watumishi wa EWURA zinafanywa wakati kuna haja ya mafunzo hayo na thamani ya fedha iwe kipaumbele.
- Orodha ya wafanyabiasha wasio waaminifu ambao wanachanganya petroli/dizeli na mafuta ya taa/maji inapelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kurejesha mapato yaliyopotea kwa njia ya kusamehewa kodi ya mafuta ya taa ambayo baadaye yalitumika kuchanganywa na dizeli.

14.10 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Upembuzi wa usimamizi wa rasilimali watu ulibaini upungufu mkubwa katika baadhi ya mashirika ya umma ikitokana na kutokuwa na mamlaka ya udhibiti ambayo ingedhibiti shughuli za mashirika ya umma kama ilivyokuwa inafanya Tume ya Usimamizi wa Mashirika ya Umma (SCOPO) kabla ya kuvunjwa kwake. Upembuzi umebaini kuwa baadhi ya mashirika hayatunzi taarifa za waajiriwa, wanaajiri watumishi bila kutumia taratibu za ushindani na uwazi, wanaajiri watumishi wasiokuwa na

sifa, kutokuwepo na mfumo wa wazi wa kuwapima watumishi, upungufu wa watumishi na watumishi wenye sifa kutokupangiwa kazi walizosomea.

Mapendekezo

- Serikali inapaswa kuanzisha mamlaka madhubuti ambayo itakuwa na majukumu ya kudhibiti utendaji na uendeshaji wa mashirika ya umma katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika kutoa huduma nzuri kwa jamii.
- Kutokana na mapungufu yaliyojitokeza kwenye kaguzi, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma zinapaswa kuimarisha Idara za Utumishi na kuhakikisha kwamba taarifa za watumishi zinatunzwa vizuri, ajira za wafanyakazi zinapaswa kuwa wazi na kwa ushindani ili shirika husika liweze kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa.
- Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanapaswa kuboresha mfumo wa kutathmini utendaji wa watumishi katika kufikia malengo ya shirika husika.
- Bodi ya wadhamini ya NSSF inapaswa kurejea maamuzi yake ya awali ya kumuhamisha Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa zamani na taratibu zilizotumika kumpata na kumuajiri Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa sasa. Kwa maoni yangu taratibu zilizotumika katika kumuhamisha Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa zamani na kumuajiri Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa sasa ulikuwa na mapungufu makubwa na haukuwa wazi.
- Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wanapaswa kutuma kwa wakati makato yote ya kisheria kwa mamlaka husika kama ilivyoelezwa katika sheria husika.
- Raslimali watu ni raslimali muhimu ya shirika kwa hiyo watendaji wakuu wa mashirika ya umma wanapaswa kuhakikisha kwamba usimamizi wa raslimali watu

unapewa kipaumbele ili kuweza kufikia malengo ya shirika husika.

14.11 Tatizo la Uchumi wa Dunia

Dunia kwa sasa inakabiliwa na matatizo ya kiuchumi ambayo imezikumba baadhi ya nchi tajiri duniani ikiwemo Marekani. Matatizo haya yamejitokeza mara tu baada ya bei za chakula na mafuta kupanda mwaka 2008. Matatizo ya sasa ya kiuchumi yanaweza yakaathiri kwa kiasi kikubwa vita dhidi ya kuondoa umasikini Tanzania.

Japokuwa Tanzania haijakumbwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la sasa la Dunia la kiuchumi, ni kiasi cha muda tu kabla Tanzania haijakumbwa na tatizo hili. Hivyo basi, watanania tusibweteke kuwa tatizo hili ni la nchi tajiri duniani. Hii ni kwasababu uchumi wa nchi yetu unategemea kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi nyingine. Kwa mfano, msaada wa kifedha tunaopata kutoka kwa wahisani unaweza ukapungua kwa miaka ijayo na uhusiano wetu wa kibiashara na nchi nyingine pia ukadhurika.

Zaidi ya hayo, kwa vile tatizo la uchumi wa duniani limezikumba nchi tajiri kwa kiasi kikubwa, mauzo ya bidhaa zetu nchi za nje na huduma nyingine kama za utalii zitapungua na hivyo kudhuru pato la Taifa. Changamoto hizi za kiuchumi zinahitaji juhudi za pamoja za kitaifa na tunahitaji kuanza kuchukua hatua na kuwa tayari kwa changamoto hizi.

Mapendekezo

Serikali ya Tanzania na Mashirika yake yanapaswa;

- Kuhakikisha kuwa vyanzo vya ndani vya rasilmali - kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi unahitajika, kuziba mianya ya ukwepaji kulipa mapato ya kodi hususani mafuta ya magari na mitambo, misamaha ya kodi na mengineyo kama vile kupanua wigo wa kodi na kuboresha mfumo wa kodi ili kuhimiza ulipaji wa kodi.

- Kubana matumizi - Serikali inapaswa kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima kama vile ilivyoamua kupunguza manunuzi ya magari ya kifahari na kupunguza gharama za semina. Pia, matumizi ya kawaida yanaweza kusimamiwa ili mapato yanayokusanywa yatumike kwenye shughuli za maendeleo.
- Kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali zetu - matumizi ya raslimali yanapaswa yapewe kipaumbele katika kuhakikisha watanzania wananufaika na raslimali zao.
- Kutumia fursa zilizopo - Serikali inaweza kuangalia wasaha ambao haujatumika na kuutumia katika kukuza uchumi kwa manufaa ya watanzania wote. Maeneo hayo ni kama vile:- kuimarisha huduma za bandari ili majirani zetu waweze kuvutiwa na huduma hizo, kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuboresha sekta ya uvuvi.

14.12 Kukabiliana na Vihatarishi (risk management)

Vihatarishi ni uwezekano wa shughuli za shirika kuathirika kutokana na mambo mbalimbali kama vile teknolojia, kiuchumi, kisiasa, kifedha, huduma za jamii na undeshaji na kutokea kwake kuna madhara makubwa kwa Serikali na mashirika yake.

Kwa upande mwingine kukabiliana na vihatarishi kunahitaji utaratibu ulioratibiwa katika kutambua, kuchanganua, kutathmini na kuchukua hatua madhubuti katika kudhibiti utokeaji wa athari hizo.

Inajumuisha utaratibu ulioratibika katika kutathmini na baadaye kutafuta mikakati ya kuondokana na vihatarishi. Utaratibu huu unajumuisha mpango mzima wa kutambua, kuchanganua, kutathmini vihatarishi na kukabiliana nazo. Serikali na mashirika yake yanakabiliwa na vihatarishi vya ndani na vya nje ambapo zinahitaji kutambuliwa na kukabiliana nazo.

Kwa hivyo, kuna ulazima wa Serikali kuandaa mpango mkakati, madhubuti na kuendeleza mifumo katika kukuza akili ya uelewa wa vihatarishi vikuu inayokabiliana nayo.

Mapendekezo

Serikali na mashirika yake yanapaswa kuifahamu na kuelewa dhana nzima ya kukabiliana na vihatarishi. Mashirika ya Umma yanapaswa kuandaa mkakati wa kutathmini vihatarishi, na kuandaa mafunzo ya hali ya juu katika suala zima la kukabiliana na vihatarishi. Katika kufanya hivyo yafuatayo yanapaswa kushughulikiwa:-

- Sera za kukabiliana na vihatarishi na faida zake zinapaswa kufahamika na watumishi wote.
- Watendaji wakuu wa mashirika ya umma wanapaswa kumiliki, kuwezesha, kuendeleza ufahamu na kuongoza katika dhana nzima za kukabiliana na vihatarishi.
- Utaratibu na mazoea ya shirika unapaswa kuwezesha na kuendeleza mawazo mazuri ya kupambana na vihatarishi ambavyo vinaweza kuzuia uendeshaji wa shirika.
- Dhana ya kukabiliana na vihatarishi inapaswa kueleweka katika utawala mzima wa Serikali na mashirika yake.
- Dhana ya kukabiliana na vihatarishi inapaswa kwenda sambamba na matarajio na malengo ya shirika husika.
- Vihatarishi vinavyotokana na uendeshaji wa mashirika vinapaswa kufanyiwa tathmini na kukabiliana nazo; na
- Inajumuisha usimamizi, upembuzi na inaweza kuhusisha majadiliano muhimu na wadau wengine katika kubuni mbinu za kukabiliana na vihatarishi.

VIAMBATISHO

Kiambatisho I

Mwenendo/Mtiririko wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo kwa Miaka Mitatu Iliyopita.

Bodi za Udhibiti				
Na	Jina la Bodi	2007/08	2006/07	2005/06
1.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu Majenzi.	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
2.	Bodi ya Biashara ya Nje (BET)	Hati inayoridhisha yenye msisitizo.	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
3.	Bodi ya Korosho - Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
4.	Bodi ya Bima za Amana	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
5.	Mamlaka ya Kudhibiti Nishati na Maji (EWURA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Ilikuwa haijaanzishwa
6.	Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
7.	Bodi ya Bahati na Sibuni Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
8.	Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
9.	Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (NBMM).	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
10.	Tume ya Rais ya Kurekebisha Sekta ya Mashirika ya Umma (PSRC)	Hati yenye kasoro (Hesabu za miezi sita Dis 2007)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

11.	Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Ilikuwa haijaanzishwa
12.	Bodi ya Sukari Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
13.	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
14.	Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano (TCRA)	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
(c)	Bodi ya Pamba Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
15.	Bodi ya Chai Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati yenye kasoro	Hati yenye Shaka
(d)	Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
(e)	Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
16.	Bodi ya Pareto ya Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka				
Na.	Jina la Mamlaka	2007/08	2006/07	2005/06
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Arusha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
2.	Shirika la Maji Safi na Maji Taka la Dar es Salaam	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Singida	Hati inayoridhisha	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro

4.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Dodoma	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Iringa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Lindi	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati yenye kasoro
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Mbeya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Moshi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Musoma	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Mwanza	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Shinyanga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Tabora	Hati inayoridhisha yenye msisitizo.	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

13.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Tanga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
14.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Bukoba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
15.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Sumbawanga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Babati	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Parastatal				
Na.	Jina la Shirika	2007/08	2006/07	2005/06
1.	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye kasoro
2.	Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
3.	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
4.	Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
5.	Shirika la Bima (NIC)	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro

6.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
7.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
8.	Mfuko wa Mafao wa Mashirika ya Umma (PPF)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
9.	SIMU 2000 LIMITED	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
10.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
11.	Shirika la Ugavi na Umeme Tanzania (TANESCO)	Hati inayoridhisha	Kushindwa kutoa maoni	Hati inayoridhisha
12.	Shirika la utafiti na maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
13.	Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
14.	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (TEMDO)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

15.	Kiwanda cha Mbolea TFC	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
16.	Benki ya Raslimali Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
17.	Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
18.	Shirika la Posta Tanzania	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro
19.	Benki ya Posta Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
20.	Kampuni ya Kusimamia Raslimali za Shirika la Reli Tanzania.	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
21.	Twiga Bancorp Limited	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	
22.	Shirika la Reli Tanzania	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati inayoridhisha yenye msisitizo
23.	Shirika la Utangazaji Tanzania TBC	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro	Lilikuwa halijaanzishwa
24.	Benki Kuu ya Tanzania	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati inayoridhisha yenye msisitizo
25.	Marine Service Company	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro
26.	Kampuni ya Ranchi za	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

	Taifa (NARCO)			
27.	Shirika la maendeleo ya viwanda Vidogo SIDO	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
28.	Mfuko wa Pensheni ya watumishi Serikalini GEPF.	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
29.	Shirika la Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
30.	NHC/PPF/IP S Co. Ltd	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
31.	Ubungo Plaza Co. Ltd	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Taasisi za Serikali				
Na	Jina la Taasisi	2007/08	2006/07	2005/06
1.	Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
2.	Mamlaka ya Masoko ya Hisa na (CMS)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
3.	Shirika la Tija la Taifa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
4.	Mamlaka ya Udhibiti wa Anga Tanzania.	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
5.	Baraza la Taifa la Teknolojia ya Elimu (NACTE)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

6.	Baraza la Taifa Uwezesaji Kiuchumi (NEEC)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
7.	Baraza la Taifa Usimamizi wa Mazingira (NEMC)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
8.	Makumbusho ya Taifa Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
9.	Taasisi ya Taifa ya Sukari	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
10.	Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
11.	Shirika la Magazeti Tanzania (TSN)	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
12.	Taasisi wa Umoja wa Vipande (UTT)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
13.	Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
14.	Benki ya Shirika la Twiga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
15.	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wadogo wadogo wa Chai Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha
16.	Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
17.	Taasisi ya Takwimu Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

18.	Taasisi ya Elimu Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
19.	Shirika la Huduma ya Maktaba Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
20.	Tume ya kudhibiti ushindani wa kibiashara	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Ilikuwa haijaanzishwa
21.	Baraza la Taifa la Mitihani	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
22.	Kituo cha uwekezaji Tanzania	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
23.	Baraza la Taifa la Michezo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania				
S/N	Jina la Chuo	2007/08	2006/07	2005/06
1.	Chuo Kikuu cha Ardhi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
2.	Chuo cha Teknolojia Dar es salaam	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
3.	Chuo cha Mabaharia Dar es Salaam	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
4.	Chuo cha Uhasibu Arusha	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
5.	Chuo cha Elimu ya Watu Wazima	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
6.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
7.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya Muhimbili	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro

8.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
9.	Chuo Kikuu cha Mzumbe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
10.	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Hati yenye kasoro	Hati yenye kasoro	Hati inayoridhisha
11.	Chuo cha Ustawi wa Jamii	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
12.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Kiambatisho 2

Ukaguzi wa Mashirika ya Umma Ambao Unaendelea Hadi Kufikia Machi, 2009

Vyuo vya Elimu ya Juu				
Na	Jina la Chuo	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Chuo cha Elimu ya Biashara Education (CBE)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mkutano wa kuhitimisha ukaguzi unasubiriwa
2.	Chuo Kikuu Kishiriki Cha Ushirika na Mafunzo ya Biashara (MUCCOBS)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Kazi ya ukaguzi inaendelea
3.	Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Kazi ya ukaguzi inaendelea
4.	Chuo Kikuu cha Dodoma	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mkutano wa kuhitimisha ukaguzi unasubiriwa
5.	Chu cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Kazi ya ukaguzi inaendelea
6.	Chuo cha Maendeleo ya Mipango Miji	30.06.2008	M/s TAC Associates	Hatua ya kuandaa ripoti
7.	Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji RUBADA	30.06.2008	M/s OREFCO	Kazi ya ukaguzi inaendelea
8.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	30.06.2008	M/s Global Accountancy	Kazi ya ukaguzi inaendelea
9.	Chuo cha Waandishi wa Habari Tanzania (TSJ)	30.06.2008	M/s Global Accountancy	Kazi ya ukaguzi inaendelea

Bodi za Udhibiti				
Na	Jina la Bodi	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hatua ya kuandaa ripoti

2.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafishaji Ardhini na Baharini (SUMATRA)	30.06.2007	M/s TAC Associates	Hatua ya kuandaa ripoti
3.	Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB)	30.06.2007	M/s Shayo and Co	Kazi ya ukaguzi inaendelea

Taasisi ya Serikali				
Na	Jina la Taasisi	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	30.06.2007	M/s TAC Associates	Mahesabu yamepokelewa. Mchakato wa makubaliano ya ada ya ukaguzi unaendelea
2.	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania (TFNC)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mahesabu yamepokelewa. Mchakato wa Makubaliano ya ada ya ukaguzi unaendelea
3.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	30.06.2007	M/s TAC Associates	Mkutano wa kuhitimisha ukaguzi unasubiriwa
4.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)	30.06.2008	M/s Ernst & Young	Mkutano wa kuhitimisha ukaguzi unasubiriwa
5.	Idara ya Usimamizi wa Amana	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	Kazi ya ukaguzi inaendelea
6.	Taasisi ya Mbegu za Pamba Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	Kazi ya ukaguzi inaendelea
7.	Tume ya Pamoja ya Fedha	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea

8.	Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Pori Tanzania (TAWIRI)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mahesabu yamepokelewa. Mchakato wa makubaliano ya ada ya ukaguzi unaendelea
9.	Tume ya sayansi na Teknolojia Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea
10.	Tume ya ya Taifa ya Mipango ya Ardhi Tanzania (NLPC)	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea
11.	Jumuiya ya Ushirika Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hatua ya kuandaa ripoti
12.	Soko mla Hisa Dar es Salaam	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mahesabu yamepokelewa. Mchakato wa makubaliano ya ada ya ukaguzi unaendelea
13.	Mamlaka ya Elimu Kibaha	30.06.2008	M/s ATEKAY	Hatua za mwisho ya kutoa ripoti
14.	Marine Park Institute	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea

Parastatal				
Na	Jina la Shirika	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Sirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mahesabu yamepokelewa . Mchakato wa makubaliano ya ada ya ukaguzi unaendelea
2.	Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA)	30.06.2008	M/s TAC Associates	Kazi ya ukaguzi inaendelea
3.	Shirika la Masoko Kariakoo	30.06.2008	M/s TAC Associates	Kazi ya ukaguzi inaendelea

4.	Sirika la Nyumba la Taifa (NHC)	30.06.2008	M/s PWC	Mawasiliano yanaendelea
5.	COASCO	30.06.2008	M/s TAC Associates	Mahesabu yamepokelewa . Mchakato wamMakubalia no ya ada ya ukaguzi unaendelea
6.	Taasisi ya Idara ya Madawa (MSD)	30.06.2008	M/s DCDM	Hatua ya kuandaa ripoti
7.	Shirika la Mawasiliano Tanzania		M/s PWC	Kazi ya ukaguzi inaendelea
8.	Mfuko wa Pensheni ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)	30.06.2008	M/s PWC	Kazi ya ukaguzi inaendelea
9.	Shirika la Ndege Tanzania	30.06.2008	M/s PWC	Kazi ya ukaguzi inaendelea
10.	Shirika la Nguvu za Atomiki Tanzania	30.06.2008	M/s Y.H. Malundo	Kazi ya ukaguzi inaendelea

Mamlaka za Maji				
Na	Jina la Mamlaka	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)	30.06.2008	M/s PWC	Kazi ya ukaguzi inaendelea
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Mtwara	30.06.2008	M/s TAC Associates	Hatua ya kuandaa ripoti
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Kigoma/Ujiji	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Makambako	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Mbinga	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea

6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Njombe	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Kazi ya ukaguzi inaendelea
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Songea	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hatua za mwisho ya kutoa ripoti
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Morogoro	30.06.2008	M/s ATEKAY	Hatua za mwisho ya kutoa ripoti

Hesabu za Mashirika ya Umma Ambazo Hazikuwa Zimewasilishwa Kwa Ajili ya Ukaguzi Hadi Kufikia Machi 2009

1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Kyela	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Mpanda	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Tukuyu	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
4.	Shirika la Taifa la Mionzi Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
5.	Mamlaka ya Maji Safi na maji taka ya Mji wa Korogwe	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa

Vyuo vya Elimu ya Juu				
Na.	Jina la Chuo	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa	30.06.2008	M/s Haron & Co	Hesabu hasijawasilishwa
2.	Chuo cha Uhasibu Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
3.	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa

Bodi za Udhibiti				
Na	Jina la Bodi	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Bodi ya Usajili ya Wakandara	30.06.2008	TAC Associates	Hesabu hasijawasilishwa
2.	Baraza la Taifa la (NCC)	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
3.	TPRI	30.06.2007	M/s TAC Associates	Hesabu hasijawasilishwa
4.	Bodi ya Katani Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa

Parastatal				
Na	Jina la Shirika	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Taasisi ya Taifa ya Mionzi Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa

Taasisi za Serikali				
Na.	Jina la Taasisi	Mwaka Unaisha	Mkaguzi	Maelezo
1.	Tropical Pesticides Research Institute	30.06.2008	M/s TAC Associates	Hesabu hasijawasilishwa
2.	TAFORI	30.06.2008	M/s COASCO	Hesabu hasijawasilishwa
3.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa	30.06.2008	M/s TAC Associates	Hesabu hasijawasilishwa

	Madawa			
4.	Baraza la Michezo Tanzania	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa
5.	CARMATEC	30.06.2008	M/s Amas Associates	Hesabu hasijawasilishwa
6.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu ya National (NBS)	30.06.2008	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu	Hesabu hasijawasilishwa